Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Thelathini na Sita - Tarehe 29 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISLAAM ISSA KHATIBU):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwaka 2002/2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Revenue Authority for the Year 2002/2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation* kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Consolidated Holding Corporation for the Year ended 31st December, 2003).*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 335

**Barabara za Vijijini Songwe**

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. PAUL E. NTWINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara nchini kote zinatengenezwa sasa na kwa kuwa Vijiji vya Magamba, Itindi, Nahalyongo Kata ya Galula, Mpona, Malangali, Iyovyo - Kata ya Totowe na Vijiji vya Mheza Manda, Isanzu - Kata ya Namkukwe havina mawasiliano ya barabara jambo linalowafanya Wananchi wa maeneo hayo wateseke sana kwa kukosa mawasiliano hayo kwenye Wilaya na Mkoa:-

(a) Je, ni lini ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo utapatikana?

(b) Je, kwa nini Serikali isitekeleze ahadi yake ya kuitengeneza barabara hiyo kidogo kidogo kama ambavyo imekuwa ikiahidi mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika Kata za Galula, Totowe na Namkukwe, vinaunganishwa na barabara ya Galula hadi Namkukwe yenye urefu wa km. 56. Barabara hii ni ya Mkoa na hivyo inahudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kati ya km. 56 za barabara ya Galula hadi Namkukwe ni kilomita sita tu za mwanzo ndizo ziko katika hali ya kufanyiwa matengenezo *(Routine Maintenance),* sehemu iliyobaki ya kilomita 50 zimeharibiwa na mafuriko ya Ziwa Rukwa na Mto Songwe hivyo hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999, Serikali kupitia Ofisi iliyokuwa ya Mhandisi wa Ujenzi wa Mkoa wa Mbeya, ilipendekeza barabara hiyo itafutiwe *alignment* itakayoonekana inafaa zaidi ya ile ya awali ambayo itapita Vijiji vya Ilembo, Maganga, Malangali, Mheza hadi Namkukwe (yaani itapitia kila Kata katika Tarafa ya Songwe). Gharama halisi ya kujenga barabara hiyo mpya kwa kiwango cha changarawe na yenye urefu wa km. 57 ilikadiriwa kuwa jumla ya Sh. 16 bilioni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mbeya, itatoa kiasi cha zaidi ya jumla ya Sh. 50.0

milioni kutoka Mfuko wa Dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Aidha, kutokana na barabara hiyo kuwa kwenye ukanda wa ardhi chepechepe na kwa vile imeandaliwa *alignment* nyingine ni vizuri tuvute subira ili zipatikane fedha za kutosha za kufanya upembuzi yakinifu kufahamu gharama halisi kwa kila kipande ndipo matengenezo ya vipande vidogo vidogo yaanze kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. Kwa njia hii ufumbuzi wa kudumu wa mawasiliano ya barabara utapatikana.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii imekuwa ni kikwazo kikubwa cha usafirishaji katika eneo la Namkukwe na Wananchi wamekuwa wakiipigia sana kelele; na kwa kuwa kila siku majibu yamekuwa ni gharama kubwa za kuijenga hiyo barabara kwa kupitia chini karibu na Ziwa Rukwa; je, Waziri haoni kuwa ingewezekana hii barabara ikapitishwa juu kidogo ya Ziwa ili gharama hizo ziweze kupungua?

Kwa kuwa kumekuwa na ahadi ya kutoa kidogo kidogo fedha za kutengeneza hii barabara. Sasa Waziri anasemaje, hatuwezi tukaanza kutengeneza kidogo ili tuimalize?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, lazima nikiri kwamba, Mheshimiwa Paul Ntwina, amekuwa akiifuatilia barabara hii sana kiasi kwamba, tumeshajibu zaidi ya mara tatu hapa Bungeni kuhusu barabara hii. Ukweli umebaki ule ule kwamba, ufinyu wa bajeti ndio unaosababisha barabara hizi zisitengenezwe. Kwa hiyo, juu ya suala kwamba kila wakati tunasema gharama ni kubwa, tunasema hali halisi kwamba, gharama ni kubwa ya kutengeneza barabara hii.

Pili, je haiwezekani tukapata *alignment* mpya? Bahati mbaya Mheshimiwa Paul Ntwina, alikuwa hajaingia wakati najibu. Nilisema kabisa kwamba, imekadiriwa mwaka 1999 ilipimwa kutengeneza *alignment* mpya barabara hii ili isipite kule inapoona ipite sasa hivi. Nayo itagharimu shilingi 16 bilioni. Nimekubali hapa katika jibu kwamba, tutaanza kutengeneza barabara hii tukipata fedha kidogo kidogo ili iweze kupitika. Mwaka huu tumeitengea fedha ili kufanya sehemu nyingine zipitike.

Na. 336

**Ubinafsishaji wa Kiwanda cha *Mbeya Textile Limited***

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, lengo mojawapo la kukibinafsisha Kiwanda cha *Mbeya Textile* lilikuwa ni kukiwezesha kiwanda kuzalisha kwa tija na kuongeza ajira kwa wafanyakazi mbalimbali:-

(a) Je, mpaka sasa kiwanda kimetoa ajira mpya kwa watu wangapi?

(b) Je, kiwanda kimefikia hatua gani kiufanisi hadi kufikia mwaka 2004?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (k.n.y. WAZIRI WA NCII, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati Kiwanda cha Nguo cha Mbeya kinabinafsishwa tarehe 1 Julai, 1999, kilikuwa na wafanyakazi 310, kati ya hao mwekezaji mpya aliwachukua asilimia 80 sawa na wafanyakazi 248. Idadi ya wafanyakazi imeongezeka hadi kufikia 600 mpaka sasa. Kwa hiyo, ajira mpya ni wafanyakazi 352.

(b) Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Nguo cha Mbeya kimefikia uzalishaji wa asilimia 55 ya uwezo wake mpaka sasa. Kabla ya kubinafsisha, Kiwanda kilikuwa kinazalisha kwa wastani wa asilimia 11 ya uwezo wake *(Installed Capacity)* hasa kutokana na ukosefu wa mitaji *(Working Capital).* Hali hii ilikilazimisha kiwanda kufungwa na wafanyakazi wote kulazimika kupelekwa likizo isiyokuwa na malipo *(Leave Without Pay).*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la Kiwanda cha *Mbeya Textile Limited* kwa sasa, ni upungufu wa pamba (malighafi). Hii inatokana kwa Serikali kusimamisha kilimo cha pamba katika Wilaya ya Chunya na sehemu nyingine za Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Kiwanda unalazimika kuagiza pamba kwa gharama kubwa kutoka katika Kanda ya Ziwa na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji kiwandani.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa tatizo kubwa ambalo linakwamisha ufanisi katika kiwanda hiki imekuwa ni kutopatikana kwa pamba. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwaruhusu watu wa Chunya na maeneo mengine kulima pamba aina ya *BT* ambayo haishambuliwi na funza mwekundu ili iwe utatuzi kwa ajili ya kiwanda hiki? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa kiwanda hiki uwezo wake ilikuwa ni kuajiri watu 2,000 jambo ambalo lingetusaidia sana Mbeya katika kuhakikisha kwamba tunaupiga vita umaskini. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kumwondolea huyu mwekezaji kodi zote ili aweze kuhimili matatizo hayo ambayo chanzo chake ni Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilipiga marufuku kilimo cha pamba katika Mkoa wa Mbeya na Mikoa ya Kusini kutokana na *red boll* ambayo ilishambulia pamba ambayo ilikuwa inalimwa Kanda ya Ziwa vilevile.

Mheshimiwa Spika, kabla Serikali haijaruhusu kilimo cha pamba, inabidi kufanya utafiti kujua kwamba, hiyo aina ya pamba aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, haitashambuliwa na mdudu huyo wa *red boll.* Kwa maana hiyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, tarehe 1 Agosti, 2004, wataalamu wa Wizara ya Kilimo na wadau wote wa Kanda ya Ziwa, watakuwa hapa kwa ajili ya Mkutano Dodoma na hivi tunavyoongea tayari wamekwishawasili kuongelea suala hilo na kutazama uwezekano kama itakubalika kuwaruhusu kuanza kulima pamba katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina uwezo wa kumwondolea kodi zote mwekezaji wa Kiwanda cha Mbeya. Lakini tumekwenda kutazama tunataka kwanza awekeze kama alivyokubaliana katika Mikataba yake ya mwanzo. Kwanza, mashine alizosema atazitengeneza atawekeza, awekeze kwanza, kwa sasa hivi wamefikia dola 600,000 mpaka 700,000 kwa mashine kwa ajili ya *tie and dye.*

Lakini tunataka amalize utengenezaji wake. Pindi atakapomaliza, Serikali itakuwa tayari kumfikiria na mawazo yake au mapendekezo yake ayalete katika *Steering Committee* ambayo italitazama suala hili kwa makini kabisa.

Na. 337

**Mgogoro wa Gereza la Mng'aro na Vijiji vya Mng'aro/Mazinde**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa umekuwepo mgogoro kati ya Gereza la Mng'aro na Vijiji vya Mng'aro/Mazinde Kata ya Mng'aro Tarafa ya Umba, Jimboni Mlalo; na kwa kuwa pamoja na jitihada za kushughulikia mgogoro huo bado hali haijabadilika:-

(a) Je, hivi tatizo la msingi katika mgogoro huo ni nini?

(b) Je, ni kwa nini mgogoro huo unaendelea kuchukua muda mrefu kiasi hicho bila kutatuliwa?

(c) Je, kama amani ikivunjika kutokana na kutotatuliwa kwa migogoro ya namna hiyo nani alaumiwe?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Gereza la Mng'aro lilianzishwa mwaka 1976 kwa ajili ya kurekebisha wafungwa kwa kuwafundisha kilimo cha umwagiliaji cha zao la mpunga. Eneo hilo lilikabidhiwa kwa Jeshi la Magereza na Wizara ya Kilimo. Alama zinazoendelea kulitambulisha eneo hilo ni matuta yaliyojengwa kabla ya kukabidhiwa

kwa Jeshi la Magereza. Kimsingi hakuna mgogoro mkubwa wa ardhi kati ya Gereza na Wananchi wa Vijiji vya Mazinde, Mng'aro na vingine vinavyolizunguka eneo la Gereza kwa kuwa Wananchi wengi wanafahamu mipaka halisi ya eneo la Gereza. Tatizo lililopo linatokana na Wananchi wachache wanaoingia eneo la Gereza kwa maslahi yao binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo hili lililopo linachukua muda mrefu kutatuliwa kutokana na Serikali kukosa fedha za kugharamia kupimwa kwa eneo hili. Hata hivyo, Serikali imepanga kulipima eneo hili katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 ambapo taratibu za kisheria za umiliki zitakamilishwa ili kuondoa visingizio vya uvamizi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa utamaduni wa Watanzania, hatutegemei kutokea mifarakano itakayopelekea kuvunjika kwa amani kati ya Gereza la Mng'aro na Vijiji vinavyozunguka Gereza kwa kuwa hivi sasa kuna ushirikiano mzuri katika masuala yote ya kijamii.

Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana katika kuwaelimisha Wananchi wa Vijiji vinavyopakana na Gereza, waheshimu mipaka ya Gereza iliyopo wakati tunajiandaa na zoezi la upimaji.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza.

Mimi ndio Mbunge wa Mlalo, ninayetokea katika eneo linalozungumzwa. Mgogoro huo ninaufahamu pengine zaidi kuliko Mheshimiwa Waziri anavyoufahamu. Nasema hakuna mpaka unaoonekana. Wakati Viongozi wa Wilaya wanapokwenda eneo hilo kujaribu kusuluhisha mgogoro huo, kinachotokea wanakwenda kwa Viongozi wa Magereza na wanamaliza wenyewe bila Viongozi wa Kijiji na Vijiji vile vinavyohusika. Kwa hiyo, nasema mgogoro bado upo ni vizuri Serikali ijiandae kuumaliza.

Pili, kwa kuwa yametokea malalamiko mengi ya namna hii hapa ndani ya Bunge kwamba, Wananchi wa Vijiji mbalimbali wanaopakana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama huwa na migogoro ya mipaka. Kama tunavyojua, vyombo hivi vinalinda nchi yetu, vinalinda uhuru wetu, vinalinda Wananchi na mali zao. Hivi Serikali haioni kwamba haipendezi Wananchi kugongana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa nini jambo hili lisimalizwe nchi nzima mara moja? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nadhani mtazamo unaweza kutofautiana kwa uhusiano mkubwa kati ya mgogoro au tatizo lililopo. Mheshimiwa Kagonji pengine kama alivyosema yeye ndiyo anayeishi na Wananchi kule. Kule mtazamo wao kwamba mgogoro ni mkubwa sana. Lakini kwa upande wetu ambapo tunajua kwamba waliovamia mpaka sasa hivi ni Wananchi 20 kati ya Wananchi wengi wanaozunguka eneo lile tunaona si mkubwa sana.

Ndiyo maana nikasema kwamba, huenda uwe mkubwa au mdogo lakini maadamu tuna utaratibu sasa wa kwenda kulipima lile eneo, tatizo litamalizika.

Napenda nimhakikishie pia kwenye swali lake la pili kwamba katika hotuba yetu ya bajeti tulielezea mpango wetu wa kuyapima maeneo yote ya Magereza. Kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hata ya Polisi ambayo yana migogoro ya hapa na pale, zoezi hilo limeanza na linaendelea kwa lengo la kumaliza kabisa hiyo migongano baina ya Wananchi na Serikali ambayo kweli haipendezi.

Na. 338

**Mmomonyoko wa Maadili Katika Jamii**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, jamii inakabiliwa na wimbi kubwa la mmomonyoko wa maadili unaoambatana na ukiukwaji wa mila na desturi zetu; na kwa kuwa ili kujenga jamii iliyo bora ni lazima kuwepo na sheria za kulinda mila na desturi hizo:-

(a) Je, ipo sheria inayosimamia mavazi yanayopingana na mila na desturi zetu?

(b) Je, kwa wanaume kusuka nywele ni utamaduni wetu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna sheria mahsusi ambayo imewekwa kusimamia na kudhibiti mavazi yanayopingana na mila na desturi zetu. Lakini zipo sheria ambazo zinalinda maadili ya Taifa katika maeneo maalum kama ifuatavyo: Sheria ya Sinema na Michezo Jukwaani Na. 4 ya mwaka 1976, inampa madaraka Waziri kutunga kanuni za kudhibiti filamu na michezo ya jukwaani kwa kuzingatia mila, desturi, itikadi na maadili yetu ikiwa ni pamoja na mavazi. Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984, inampa Waziri uwezo wa kuweka utaratibu wa kudhibiti vikundi vya sanaa za maonyesho kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mavazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ingawa si utamaduni wa Watanzania wote kwa wanaume kusuka nywele, zipo jamii nchini mwetu ambazo zina desturi hiyo kama ifuatavyo: Katika jamii ya Wamasai, vijana wa kiume ndio husuka nywele, wasichana na akinamama watu wazima hawasuki nywele. Katika jamii ya Wasukuma tabia ya wanaume kusuka nywele sawa na wanawake iko kwa vijana, hasa wasanii, ikiwa ni kivutio kimojawapo katika shughuli zao za kisanii wanaita *"Shingaa"*. Tabia hizi zipo katika mambo mengi kwa mfano, sisi Wahehe huchanja chale, wenzetu Wazaramo na Warufiji hatukuwafundisha, lakini wao wanachanja makubwa zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana iko mifano mingine zaidi na hiyo niliyoitaja na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo wanaifahamu lakini nilidhani hiyo inatosha kama mfano. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Waziri, alisema kuwa hakuna sheria mahsusi ya mavazi, lakini kuna udhibiti wa mavazi hususan katika nyanja tofauti, alivyosema katika majukwaa yetu. Lakini mbona kuna wanenguaji wanacheza uchi katika shughuli za michezo na hakuna sheria ambayo inawabana kudhibiti hali hii. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa hili anasemaje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, si sahihi sana kusema wanacheza bila kuvaa nguo. Ukiangalia wanavaa nguo za namna fulani. Kama Waheshimiwa Wabunge, mmeangalia miaka ya hivi karibuni, mtakuwa mmeona mabadiliko katika vikundi vya sanaa kuna mabadiliko. Kwa sababu wataalamu wa Wizara yangu, wanakwenda kuongea nao na kuwashauri vizuri zaidi juu ya namna ya kufanya hii michezo ya jukwaani. Lakini kama Baba wa Taifa alivyowahi kushauri, wewe ukiona mwanamke amevaa vazi lisilopendeza au fupi mno, basi wewe tazama pembeni. Kama utatazama pembeni watabadilika haraka sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimwia Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Je, haoni kwamba kwa mavazi ambayo yanaonyeshwa katika majukwaa hivi sasa yanayovaliwa yanachochea UKIMWI au yanachochea kuongeza idadi ya UKIMWI?

**SPIKA:** Hilo ni jepesi. Mheshimiwa Waziri lijibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, namshauri sana Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, azingatie ule ushauri wangu. Hicho unachofikiri kinachochea, ukitazama pembeni hivi, utakuta mabadiliko mazuri tu. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 339

**Mafunzo ya Kompyuta kwa Shule za Sekondari**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa, elimu katika Shule za Sekondari haiwezi kuwa kamili katika kuhimili ushindani kwenye ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia kama wanafunzi hawatapatiwa mafunzo ya msingi ya kompyuta:-

(a) Je, Serikali inatoa msimamo gani inapoendelea kupuuzia kuanzishwa mafunzo ya kompyuta katika shule zote za sekondari nchini?

(b) Je, hadi kufikia mwaka 2004 ni shule ngapi za sekondari zinazofundisha masomo ya kompyuta?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fungu la fedha kuanzia bajeti ya mwaka 2004/2005 ili kuzipatia vifaa vya kompyuta na umeme wa gridi Sekondari za Kizaga, Ndago na Shelui, zilizoko katika Wilaya ya Iramba kwani shule hizo zote zipo karibu sana na ulikopita umeme wa Gridi ya Taifa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nikijibu swali Na. 161 la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mkunge wa Viti Maalum, katika Mkutano wa 14 wa Bunge hili, Serikali inatambua umuhimu wa kufundisha somo la kompyuta katika shule zote za sekondari. Kikwazo ni gharama na maandalizi yanayotakiwa yafanywe vizuri kabla ya kuanza kufundisha somo hilo, likiwemo tatizo la kutokuwepo umeme katika shule nyingi za sekondari. Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), imeshaandaa mitaala ya kufundishia somo la kompyuta katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Wizara yangu iko mbioni kuanza kufundisha somo la Kompyuta katika Vyuo vya Elimu ya Ualimu vyote 34, kwa lengo la kila anayefuzu katika vyuo hivyo awe na ujuzi wa kompyuta wa kawaida. Baada ya kuwa na Walimu wa aina hiyo, ndipo tutaweza kuanza ufundishaji wa somo hilo katika shule zetu zote kwa kuanzia pale ambapo upo umeme na Mwalimu mwenye ujuzi huo. Kwa mara nyingine niwashukuru Serikali ya Sweden wanaotusaidia katika kuandaa mpango huo wa kuanzisha *computer lapse* katika vituo vyetu vyote 34 vya ualimu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2004, somo la kompyuta linafundishwa na kutahiniwa katika Shule za Sekondari 13. Hata hivyo, zipo shule nyingine za sekondari zinazofundisha somo la kompyuta ingawa si kwa lengo la kutahiniwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mpango wa MMES 2004 - 2005, itatoa ruzuku ya kukamilishia Ujenzi wa Madarasa, Nyumba za Walimu na kusaidia ujenzi wa Maabara, Maktaba na Hosteli pale inapohitajika. Sehemu ya ruzuku hiyo inaweza kutumika kufunga nyaya ya umeme na kuvuta umeme ufike shuleni pale ambapo umeme wa Gridi ya Taifa tayari unatumika katika eneo hilo. Aidha, Wakuu wa Shule zote za Serikali za Sekondari ambao shule zao ziko karibu na maeneo ambayo umeme wa Gridi ya Taifa unatumika, wanatakiwa walete Wizarani maombi ya fedha ya kuingiza umeme katika shule zao pamoja na Nyumba zote za Walimu *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, Mheshimiwa Waziri atatamka ni mwaka gani mashule yote ya sekondari na vyuo vyote hapa nchini vitakuwa vinafundishwa au vina vifaa vya kompyuta kusudi elimu iendane na wakati wa utandawazi?

(ii) Kwa kuwa Chuo cha Ualimu cha Kinampanda Wilaya ya Iramba kilianzishwa tangu kumalizika kwa vita ya pili ya dunia. Je, Mheshimiwa Waziri, hawezi kukienzi chuo hiki kwa kukipa vifaa na uwezo wa kufundisha somo la kompyuta? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kwamba, je, naweza kutamka ni mwaka gani shule zote na vyuo vyote vitaweza kuwa na kompyuta? Jibu ni kwamba, kwa sasa hivi siwezi kutamka. Isipokuwa kama nilivyosema, kwanza tumeamua kwamba namna nzuri ya kufanya jambo hili la ufundishaji wa kompyuta ni lazima tuanze na walimu. Kwa hiyo, tunategemea kuanzia *intake* ijayo, yaani ya mwaka 2005 ya walimu watarajali, yaani wale wanaokwenda kusomea ualimu, tutakuwa na *labs* za kompyuta na walimu katika vyuo vyote vya ualimu 34.

Kwa hiyo, tutaanza kutoa kila mwaka na baada ya hapo walimu ambao wana ujuzi wa kawaida wa kutumia kompyuta na kuweza kwenda kufundisha wanafunzi. Naamini huo ni mwanzo mzuri. Tutakapoona tumekuwa na kiasi kizuri cha walimu ndipo tutakuwa na mpango wa kuanza kufundisha katika shule zote, lakini tutaanza kwa kadri tunavyowapata walimu na tunavyoweza kuandaa vifaa vya kufundishia na kuwepo kwa umeme katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kutupa kipande cha historia kwamba, Chuo cha Ualimu cha Kinampanda kilianzishwa mara baada ya Vita Kuu ya Pili, kwa hiyo, ni cha siku nyingi sana. Je, naweza kukienzi chuo hicho?

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, kwa sababu ni miongoni mwa vile vyuo 34, tunategemea kuanzia mwaka 2005, tutakuwa na *computer labs* katika vyuo vyote kikiwemo cha Kinampanda. Kwa hiyo, ndiyo njia ya kukienzi. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kitendo cha kuagizia kompyuta zenye thamani ya karibu Shilingi milioni 300 nje ya utaratibu kimezorotesha sana kuendeleza somo hili la kompyuta. Je, Waziri anaweza kutueleza ni hatua gani anazozichukua kuhakikisha zile kompyuta mbovu zilizoagizwa na ambazo hazikufika mashuleni zitafidiwa ili kuwawezesha wanafunzi kupata somo la kompyuta? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu zangu, jambo hili linashughulikiwa na mojawapo ya Kamati za Kudumu za Bunge, nafikiri ni Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi. Hawajaleta taarifa hapa Bungeni. Kwa hiyo, pengine kama kumbukumbu yangu ni sahihi, kanuni zetu zinasema

jambo ambalo liko mbele ya Kamati, tuache kwanza lifike kwenye Bunge ndipo tunapoweza kulizungumzia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kumbukumbu zako ni sahihi kabisa

Na. 340

**Mradi wa Barabara - Wino**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k. n. y. MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI)** aliuliza: -

Kwa kuwa Mradi wa Barabara ya Wino - Ifinga Kata ya Matumbi ulianza vizuri hadi barabara hiyo mpya ifike Ifinga na kwa kuwa kazi iliyobaki ilikuwa ni kusawazisha milima, kujenga makingamaji na kufukia makalvati vizuri na kwa kuwa tangu mwaka 2000 barabara hiyo inapigwa danadana kati ya *TANROADS* na *District Engineer: -*

(a) Je, mradi huo unahitaji nguvu kubwa kiasi gani ambacho *District Engineer* hawezi kuifanya?

(b) Je, Serikali kwa upande wa Wizara ya Ujenzi haiwezi ikamaliza kazi iliyosalia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Wino - Ifinga yenye urefu wa kilometa 46.9 ni barabara ya Wilaya inayosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Barabara hii ilifunguliwa kwa kukata milima na kuweka baadhi ya makalvati. Barabara hii inahitajika kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Kutokana na makisio yaliyofanywa na Mhandisi wa Wilaya ya Songea, mradi wa ujenzi wa barabara hii unahitaji kiasi cha Sh.376,036,722/30/= ili kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe na kuifanya iweze kupitika kipindi chote cha mwaka.

Aidha, katika kutambua umuhimu wa barabara hii kwa Wananchi wa Ifinga na Vijiji vya njiani, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara ya Ujenzi imetenga jumla ya Shilingi milioni 70 kwa ajili ya kukarabati barabara hii kutoka Mfuko wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Songea, ielekeze nguvu zake katika barabara hii ili fedha iliyotengwa na Wizara yangu iweze kutoa matunda yatakayoonekana.

Na. 341

**Ujenzi wa Barabara ya Mwanza - Shinyanga**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza: -

Kwa kuwa ni muda mrefu umepita tangu barabara ya kutoka Mwanza hadi Shinyanga itangazwe kuanza kujengwa, lakini bado ujenzi haujaanza na kwa kuwa tenda inatangazwa ya kujenga barabara toka Shinyanga - Nzega na Tinde - Isaka: -

(a) Je, ni lini barabara ya Shinyanga - Nzega na Tinde - Isaka itaanza kujengwa?

(b) Je, itagharimu fedha kiasi gani hadi kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ilula (mpakani mwa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga) - Shinyanga Mjini - Tinde - Nzega na Tinde - Isaka yenye urefu wa kilometa 270 iko chini ya ufadhili wa *European Union* kwa jumla ya Shilingi bilioni 59 na zimetolewa. Zabuni za ujenzi wa barabara hii ziliitishwa mwezi Desemba, 2001 na kupokelewa tarehe 11 Aprili, 2002. Zabuni na kandarasi zimegawanywa katika makundi mawili *(lots),* ambazo ni za sehemu ya barabara ya Ilula - Shinyanga - Tinde *(lot 1)* na Nzega - Tinde - Isaka *(lot 2)*. Mkataba wa *lot 1* ulisainiwa tarehe 26 Juni, 2003 kati ya Serikali na Kampuni ya *GRINAKER* kutoka Afrika Kusini kwa thamani ya Sh.28,242,605,750/=.

Mheshimiwa Spika, kazi kwa sehemu hii ya Ilula - Shinyanga - Tinde ilianza mwezi Februari, 2004 na inaendelea vizuri kwa lengo la kukamilisha ujenzi mwezi Februari, 2006. Kazi hii inasimamiwa na Kampuni ya *LOUIS BERGER* kutoka Ufaransa yenye mkataba wenye thamani ya Sh.1,135,020,458/=.

Aidha, mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Isaka - Tinde - Nzega wenye thamani ya Sh.20,163,377,764/= ulisainiwa tarehe 8 Septemba, 2003 kati ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na Kampuni hiyo hiyo ya *GRINAKER* na kazi ya ujenzi imeanza mwezi Mei, 2004 kwa lengo la kukamilisha ujenzi mwezi Mei, 2006. Kazi hii inasimamiwa na Kampuni ya *Hydro arch* kutoka Italia yenye mkataba wa thamani ya Sh.991,276,211/=.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii inapita katikati ya Mji wa Maganzo na kwa maana hiyo Wananchi wana hofu kwamba magari yatapita kwa kasi kubwa na yanaweza kuhatarisha maisha ya binadamu.

Je, Serikali itakuwa tayari kuweka *speed bumps* katika ule Mji wa Maganzo ili kuepusha ajali?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, maendeleo yana matatizo yake na ni lazima tuyakubali. Haya sasa ni maombi juu ya barabara kuu zinazopita Mjini zidhibitiwe. Tunazidhibiti tu kwa alama za barabarani, hii ni barabara kuu na italeta maendeleo katika Mji wa Maganzo. Kwa hiyo, Wananchi wa Maganzo kwanza, wafurahie kupata barabara ya lami. Pili, wajue kwamba sasa kuna barabara ya lami, waheshimu alama za barabarani. Kama sivyo, basi tutaendelea kuweka *speed bumps* nchi nzima na maana ya kujenga barabara hizi kuu haitakuwepo tena. *(Makofi)*

Na. 342

**Tatizo la Mabadiliko ya Hali ya Hewa**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza: -

Kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa ni la kiulimwengu, lakini ni tatizo lenye kuathiri zaidi nchi maskini na Tanzania ikiwepo na kwa kuwa ili kupambana na tatizo hilo la mabadiliko ya hali ya hewa ni lazima kujizatiti kuwa na mipango mizuri itakayotuwezesha kufikia malengo ya kupambana na umaskini: -

(a) Je, Serikali imeshapanga mikakati ya kisekta ya kuwawezesha Wananchi kuwa na mbinu bora za kuoanisha hali halisi ya mabadiliko na hali ya hewa na shughuli za jamii za kila siku za kupambana na umaskini?

(b) Je, kwa kuwa kilimo ni njia ya mwanzo ya Watanzania kukabiliana na tatizo la umaskini na kwa kuwa hali halisi ya kilimo chetu bado ni ya teknolojia hafifu, ni lini juhudi za ziada zitafanyika ili kuboresha teknolojia katika shughuli za kilimo ili kusaidia kuondoa tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba radhi kwa sababu jibu langu leo litakuwa refu kuliko kawaida ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli mabadiliko ya hali ya hewa yanatokea ulimwenguni kote na athari zake huonekana zaidi katika nchi maskini kama Tanzania, ambapo miaka ya hivi karibuni dalili za mabadiliko ya hali ya hewa zimejitokeza kama vile mfululizo wa upungufu wa mvua;, mafuriko ya mara kwa mara, misimu ya mvua kuwa mifupi kuliko miaka ya nyuma na kupungua kwa eneo la theluji juu ya Mlima Kilimanjaro.

Tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa ni la dunia nzima na hadi kufikia wakati huu, hakuna nchi inayojua kwa usahihi kiwango cha mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tatizo hilo na mabadiliko ya hali ya hewa, Serikali imeweka mikakati ya kuboresha utabiri na utoaji wa taarifa za hali ya hewa kama ifuatavyo: -

(i) Upanuzi wa mtandao wa vituo vya kupima hali ya hewa ambapo kwa sasa tunaweza kupata hali halisi ya hewa ya Tanzania;

(ii) Uboreshaji wa uchunguzi na upimaji wa hali ya hewa;

(iii) Kuboresha utafiti, utabiri na matumizi ya taarifa ya hali ya hewa;

(iv) Kuwaelimisha na kuwashauri Wananchi kuhusu hali ya hewa na matumizi yake katika shughuli za kijamii na kiuchumi katika Sekta mbalimbali;

(v) Kuboresha usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari hususan redio, *television* na magazeti; na

(vi) Kubuni mbinu mpya za kutoa utabiri maalum kwa Sekta mbalimbali hususan kilimo, ujenzi, usafiri wa anga na usafiri wa majini, nishati, uratibu wa maafa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya, Sekta inafanya juhudi za kuuelimisha umma juu ya umuhimu na matumizi bora ya utabiri na taarifa za hali ya hewa kwa njia mbalimbali zikiwemo warsha na vipindi maalum katika Vyombo vya Habari. Kwa mfano, taarifa juu ya mwelekeo wa mvua za msimu hutolewa kwa umma mapema kabla ya msingi kuanza kupita kwa kupitia Vyombo vya Habari na kufuatiwa na taarifa za nyongeza za mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa, itaendelea kutoa utabiri na taarifa maalum kwa Sekta ya Kilimo ili kuwezesha Sekta hiyo kuwashauri wakulima kutumia teknolojia ifaayo.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza athari kwenye uzalishaji wa mazao zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa, baadhi ya hatua zinazochukuliwa ni pamoja na: -

(i) Kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo hususan kilimo cha matuta na makingamaji, kilimo mseto, kuvuna maji ya mvua na kutumia mito na maziwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani;

(ii) Kuhakikisha kwamba kilimo katika mabonde yote yenye unyevunyevu na skimu za umwagiliaji zinazingatia matumizi bora ya maji chini ya usimamizi ya wataalam; *(Makofi)*

(iii) Kuendesha kampeni ya kuhifadhi chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya na kutoa mafunzo ya teknolojia ya usindikaji na hifadhi ya mazao; na

(iv) Vituo vya Utafiti vya Kilimo vinaendelea kuzalisha mbegu ambazo zinastahimili ukame. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na pengo kubwa sana ambalo linazidi kuongezeka siku hadi siku kati ya watafiti ambao wamekuwa wakifanya tafiti mbalimbali zinazoweza kusaidia sana kupambana na matatizo haya ya mabadiliko ya hali ya hewa na kusaidia kupunguza tatizo la umaskini, lakini pengo hilo limekuwa kubwa kati yao na watumiaji wa tafiti hizo ambazo zimekamilika.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba pengo hilo kati ya watafiti na watumiaji wa tafiti hizo ambazo zimekamilika hasa wakulima na wanajamii maskini wa Tanzania linapunguzwa ili kuondokana na tatizo hili la uharibifu wa mazingira na hali ya hewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba, kuna *coordination* nzuri baina ya Wizara na Wizara na tafiti mbalimbali zinazofanyika. Tafiti hizo ndiyo zinazotumika kupanga mipango yetu ya maendeleo na mipango mingine ambayo tunaitoa katika Vyombo vya Habari na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kufanya hivyo ili Wananchi waweze kutumia tafiti hizo kwa manufaa yao na jamii kwa ujumla.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa matumizi ya pembejeo hasa mbolea za chumvi chumvi yanazidi kutiliwa mkazo na mbolea hizi zinasaidia sana kuharibu ardhi, je, ni njia zipi zinazotumiwa ili kupunguza uharibifu wa ardhi uletwao na mbolea za chumvi chumvi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli matumizi ya kemikali kama mbolea si mazuri sana na tunasisitiza umuhimu wa kutumia samadi. Lakini kubwa ninaloweza kusema ni kwamba, uharibifu wa ardhi hautokani na hilo tu, lakini ni ufugaji holela, kutaka miti ovyo, kuchoma mkaa, kuchoma mashamba na kadhalika. Tukiweza kudhibiti haya tunaweza kuiacha ardhi yetu ikiwa nzuri na ikiwa *productive.*

Na. 343

**Umeme Bukoba Vijijini**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ilieleza nia yake ya kusambaza umeme Bukoba Vijijini kwenye maeneo ya Katoro, Izimbya, Buyango, Kitobo, Ruzinga, Nsunga, Minziro, Bugandika, Kilimilile, Isanju na Ushozi. Je, ni hatua zipi zimefikiwa katika utekelezaji wa mpango wa kupeleka umeme katika maeneo niliyoyataja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kusambaza umeme Bukoba Vijijini. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali imewasilisha maombi ya kufadhili mradi wa kusambaza umeme katika Vijiji alivyotaja Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala kwenye Shirika la *SIDA,* ili kuweza kupata fedha za kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2003, Wizara ilituma wataalam wa *TANESCO* kutembelea maeneo husika, kuandaa makadirio ya gharama na kufanya maandalizi yote yanayotakiwa kwa ajili ya kuwasilisha kwa wafadhili na Serikali kama nilivyosema awali, imeshafanya hivyo kwa Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na mwezi Juni, 2004 wakati wa mazungumzo rasmi ya kila mwaka kati ya Serikali yetu na Serikali ya Sweden, Serikali iliomba mradi huu ufadhiliwe na *SIDA* iliahidi kufikiria ombi hilo na kurejea kwetu mapema.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Wananchi wa Jimbo la Nkenge, wavute subira wakati Mheshimiwa Mbunge wao, akiendelea kushirikiana na Serikali katika jitihada za kupata fedha kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye maeneo husika.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa inapokuja kwenye suala la petroli Mkoa wa Kagera tunalipa bei kubwa zaidi kuliko sehemu yoyote ile ya Tanzania na hoja ni kwamba, ni kwa sababu tuko mbali na kwa kuwa umeme tunaotumia Kagera unazalishwa kwa gharama ndogo kutoka Uganda.

Je, Serikali haioni kwamba ni busara, kwa busara ile ile inayotumika kwa kulipa petroli bei kubwa, kwa kuwa tunapata umeme kwa bei ndogo basi tulipie umeme huo kwa bei ndogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Sikumsikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hakusikia swali lako. Hebu lirudie na useme pole pole, naona unakwenda kama Mheshimiwa Semindu Pawa. *(Kicheko)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Mkoa wa Kagera bei ya petroli hivi sasa tunalipa zaidi ya Shilingi 1,200/= kwa lita, wakati maeneo mengine wanalipa kidogo na kwa kuwa hoja ya Serikali ni kwamba gharama ya kupeleka petroli Kagera ni kubwa kuliko sehemu nyingine, kwa hiyo, ni lazima walipe kwa gharama kubwa kuliko sehemu yoyote ya Tanzania na kwa kuwa sasa umeme tunaopata Kagera unatoka Uganda na ni wa maji na unazalishwa kwa bei nafuu. Je, busara hiyo hiyo inayotumika kufanya sisi katika Mkoa wa Kagera tulipe bei kubwa ya petroli, ni kwa nini sasa haitumiki ili tulipie umeme kwa bei ya chini kwa sababu umeme huo unapatikana kwa bei ya chini? *(Makofi)*

Kwa kuwa mradi uliopeleka umeme Kanyigo unajulikana kama 'Mradi wa Kanyigo' kuanzia eneo la Bwanja mpaka Kanyigo hawakuweka waya wa *earth* na kwa sababu hiyo unasababisha vyombo mbalimbali vinavyotumia umeme huo kuungua mara kwa mara. Je, Wizara iko tayari kurekebisha tatizo hilo ili Wananchi wa maeneo ya Kanyigo, Kashenye na Bukabuye waondokane na tatizo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze na swali la pili.

Mheshimiwa Spika, nitashangaa sana kama *TANESCO* au wasambazaji wa umeme, watafikisha umeme bila ya kutimiza masharti yanayotakiwa ya kiufundi na ya kiusalama katika kuhakikisha kwamba, umeme huo unakuwa salama kwa watumiaji. Lakini kwa kuwa hoja hii kaitaja Mheshimiwa Mbunge na nisingependa kufikiria kwamba ameitaja tu hivi hivi, ni lazima kutakuwa kuna matukio mahsusi, basi nitapenda nichukue fursa baada ya kipindi cha maswali na majibu, nikutane na Mheshimiwa Mbunge ili tuwasiliane na Shirika la *TANESCO* kuona kama hizo hitilafu ambazo amezizungumzia ni hitilafu ambazo zinaweza kuhakikiwa kwamba zipo na kama zipo zishughulikiwe kwa sababu nia na mipango ya Serikali, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, Wananchi wake wanapata huduma iliyo salama na moja ya huduma hiyo ni umeme ambao unatakiwa upatikane ukiwa salama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya umeme, bei ya umeme inatozwa kinchi, ni *Pan-territorial* kwa lugha ya Kiingereza na ni kwa sababu tu kwamba, kuna maeneo ambayo gharama za kuzalisha umeme ni kubwa zaidi kuliko sehemu nyingine. Kwa mfano, maeneo yote ambayo yanazalisha umeme kwa kupitia mafuta gharama zake ni kubwa sana. Umeme unaozalishwa kwa kutumia *generators* za mafuta unatumia karibu asilimia 35 ya mapato ya *TANESCO* wakati mapato yanayopatikana kwenye vituo hivi ni kama asilimia 7.

Kinchi inabidi bei ziwe sawia kuhakikisha kwamba, Wananchi wetu walio katika maeneo mbalimbali wanapata huduma hii kwa unafuu na kwa bei ile ile na kama ambavyo tumesema mara nyingi hapa, suala la bei kubwa ya umeme kinchi ni suala ambalo linafuatiliwa kwa karibu na Serikali, wakati muafaka ukifika na kutokana na vyanzo mbalimbali vya umeme vinavyoshughulikiwa tunaamini kabisa bei ya umeme inaweza ikashuka.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Napenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara husika kwa juhudi wanazofanya ili kuhakikisha kwamba, Jimbo la Bukoba Vijijini nalo linapata umeme kwa miaka yote tangu tupate uhuru, lakini nina swali moja dogo tu.

Kuna maeneo ambayo yako kando kando ya barabara inayokwenda Muhutwe, maeneo ya Kanazi ambapo yapata miaka mitano iliyopita waliweka nguzo pamoja na kutandaza nyaya, lakini umeme haujaunganishwa kwa sababu katika miaka yote hiyo hawakuweka transfoma. Je, Wizara inasema nini juu ya upatikanaji wa hiyo transfoma ili kwa Wananchi wa Bukoba Vijijini iwe ni ishara tu ya kuwapa matumaini kwamba haya yanayozungumzwa yako njiani yanakuja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ni suala la transfoma moja, kama ambavyo anasema Mheshimiwa Mbunge na eneo lenyewe haliko katika umbali mrefu sana, napenda nimuahidi Mheshimiwa Nazir Karamagi kwamba, tuonane baada ya Bunge ili tuweze kushughulikia. Tumeshafanya hivyo tayari kwa Jimbo la Mheshimiwa Ruth Msafiri kuhusu transfoma vilevile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo mengine, nafahamu kabisa kwamba, kwenye Jimbo la Mheshimiwa Nazir Karamagi, kuna matatizo mahsusi ya usambazaji umeme kwenye maeneo yale ambayo kuna nguzo zimesimamishwa na mradi ule haukukamilika. Niseme kwa ujumla tu kwamba, kuna sehemu mbalimbali nchini ambazo miradi ya umeme haikukamilika kutokana na *TANESCO* kuishiwa fedha wakati wanaendeleza miradi hiyo, lakini ni azma ya Shirika na ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, miradi ambayo imeanzishwa inakamilishwa na Serikali imetoa maelekezo hayo kwa *TANESCO* na miradi hii itashughulikiwa kadri fedha zitakapokuwa zinapatikana. Ninafahamu sana kwamba, kwa upande wa Jimbo la Mheshimiwa Nazir Karamagi, wale watani zetu wa kisiasa wanajaribu kutumia hiyo kama ndiyo njia ya kuweza kupenya. Lakini napenda niwahakikishie kwamba, Serikali inashughulikia suala hili ili kuwashughulikia Wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Nazir Karamagi. *(Makofi)*

Na. 344

**Kuunda *Task Force* kwa ajili ya Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza: -

Kwa kuwa Ugonjwa wa Malaria ni hatari sana na unaongoza kwa kuua watu wengi hapa nchini na kwa kuwa ugonjwa huo haujaundiwa *Task Force* kama ilivyo ugonjwa wa *HIV/AIDS: -*

(a) Je, ni lini Serikali itaunda *Task Force* kwa ajili ya ugonjwa huo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kama itaunda chombo cha kupambana na ugonjwa huo kama *National Malaria Control Program (NMCP),* itafanya kazi kulingana na maelekezo ya *Task Force* hiyo ili kukabiliana na ugonjwa huo?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja kubwa ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupambana na tatizo hilo kama ilivyo kwa *HIV/AIDS?*

**WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Ugonjwa wa Malaria ni hatari sana na unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wanaohudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na ni sababu kuu ya vifo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli huu, Serikali kupitia Wizara yangu iliunda Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Ugonjwa wa Malaria *(National Malaria Advisory Committee)* tangu mwaka 1990. Kamati hii ina Wajumbe toka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya, TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na Utamaduni, pamoja na Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa likiwemo Shirika la Afya Duniani *(WHO).* Kazi kubwa ya Kamati hii ni kutoa miongozo na maelekezo kwa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria. Chini ya Kamati hii kubwa kuna Kamati tatu ndogo ndogo ambazo ni Kamati ya Tiba, Kamati ya Udhibiti wa Mbu na Kamati ya Habari, Elimu na Mawasiliano *(Information, Education and Communication - I. E.C).*

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali hapo awali, Kamati hii ndiyo inayotoa maelekezo kwa Menejimenti ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria juu ya namna ya kuudhibiti ugonjwa huu.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo haja ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu na kwa kweli Wizara yangu ilitenga Shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, licha ya fedha za wahisani tulizopata toka *Global Fund for TB, Malaria and HIV/AIDS,* ambazo ni Shilingi bilioni 12. Mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 6.056 kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa malaria.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ilikuwa inafanya utafiti wa chanjo kwa ugonjwa huu wa malaria, je, sasa Mheshimiwa Waziri analiambia Bunge hili kwamba utafiti unaendelea? Kama utafiti wa dawa ya chanjo unaendelea, je, umefikia wapi hadi sasa?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli malaria ni ugonjwa mgumu kidogo ambao chanjo pekee haiwezi ikauzuia, lakini hasa ni tabia ya usafi wa mazingira na kuzuia mazalio ya mbu ndiyo dawa kamili ya tiba na kuzuia ugonjwa huu wa malaria. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kumwuliza Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa imegundulika kwamba, malaria inaua kuliko UKIMWI na kwa kuwa dawa za UKIMWI hutolewa bure au zinapewa ruzuku ili watu wasife, ni kwa nini sasa dawa za malaria zisitolewe bure ili watu wasiendelee kufa?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka niseme kwamba, tulipoanza huko nyuma dawa za malaria *(chloroquine),* zilikuwa zinatolewa bure na utafiti ukafanywa tukienda kwenye *dispensaries* wakati huo unakuta umepata dawa, nenda huko nje unakuta dawa ile imetupwa. Kwa hiyo, kitu cha bure watu kweli walikuwa hawakithamini. Sasa hivi mtu analipia kidogo sana na wala halipii ile dawa analipia tu kumwona daktari kwa shilingi 200, anapata dawa zote anazozihitaji. Lakini kwa kuwa pia amelipia, anaheshimu ile dawa na anaithamini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Matangazo ya vikao kwa siku ya leo ni kama ifuatavyo: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane chumba namba 133 ghorofa ya kwanza kuanzia saa 8.30 mchana. Kamati mbili, Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Hesabu za Serikali zote kwa pamoja wanakutana leo saa 5.45 chumba Na. 133, kikao hicho ni kwa ajili ya kukutana na Wajumbe wa *CPA* Tawi la Uingereza kwa mazungumzo, Kamati zote mbili. Hali kadhalika Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Jackson Makwetta, anaomba Wajumbe wa *Executive Committee* wa Tawi letu wakutane saa 5.00 asubuhi kwenye chumba namba 133 kwa lengo hilo hilo la kukutana na Ujumbe wa *CPA* kutoka Uingereza.

Halafu Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Wanawake, wanaendelea na maandalizi yao ya Usiku wa Mwanamke Mwafrika. Kwa hiyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba Wabunge wote Wanawake wakutane saa 7.00 mchana kwenye viwanja vya burudani, nyuma ya Jengo la Utawala.

Kuna Kamati Ndogo ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kubwa, anawatangazia Wajumbe hao wa

Kamati Ndogo ya *PAC* kuwa kutakuwepo na kikao saa 4.30 asubuhi kwenye chumba Na. 219, ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005
### Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, inayohusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri hatusikii vizuri, basi nitakuambia *time* ya kuanza.

**MBUNGE FULANI:** *Speed* kubwa!

**SPIKA:** Sasa kumetulia Mheshimiwa Waziri muda wako wa kusoma unahesabiwa kuanzia sasa. Lakini usiende na *speed* kama ya Mheshimiwa Semindu Pawa. Soma pole pole. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda na Waziri wa Fedha, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa Hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Malengo, maelekezo na vigezo vilivyomo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Sophia Simba, iliyojadili makadirio ya matumizi ya Wizara yangu tarehe 25 na 26 Mei, 2004. Ushauri uliotolewa na Kamati utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya, waliochaguliwa katika chaguzi mbalimbali ndogo zilizofanyika nchini kote bila kumsahau Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wa kishindo alioupata kule Bariadi. Aidha, napenda pia kutumia nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa vifo vya Wabunge, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, pamoja na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki na kwa Waheshimiwa

Wabunge wote, ambao walifiwa na wazazi wao au ndugu zao na pia wale walionusurika katika ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu na ahadi zilizotolewa na Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na mipango itakayotekelezwa kwa mwaka 2004/2005.

Wizara yangu kupitia Idara ya Kazi ina majukumu ya kuratibu na kusimamia Sera na Sheria za Kazi ili kuleta amani sehemu za kazi, kwa kulinda haki na wajibu wa wafanyakazi na waajiri, kupunguza na kutatua migogoro ya kikazi, kukuza majadiliano kwa azma ya kuwezesha ukuaji wa uchumi, ajira, tija na wakati huo huo kulinda kazi ya staha *(Decent Work)*. Katika mwaka 2003/2004 Idara ilitekeleza majukumu na ahadi zifuatazo:-

- Ilifanikisha kufikisha Bungeni miswada miwili ya Awamu ya Kwanza ya Marekebisho ya Sheria za Kazi nchini na Sheria hizo zilipitishwa na Bunge lako tukufu mwezi Aprili, 2004 ambazo ni *Employment and Labour Relations Act* na *Labour Institutions Act,* kwa msaada wa *DANIDA.*

- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* na mpango wa uimarishaji Sheria katika nchi za Afrika Mashariki *(SLAREA),* Wizara ilifanikisha mafunzo ya ukufunzi kwa maafisa kazi katika masuala ya kaguzi za kazi na usuluhishi wa migogoro ya kikazi, nao wamesambaza mafunzo hayo kwa maafisa wengine nchi nzima.

- Kwa kushirikiana na *DANIDA,* maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Sheria za Kazi yameanza, yakiwemo kuandaa mafunzo ya Stashahada ya juu ya Maafisa Kazi Wakaguzi ambao kada yao inafutwa ili waweze kupata sifa za kuwa Maafisa Kazi na pia kuandaa mafunzo ya Maafisa Kazi na wengine watakaohusika na masuala ya usuluhishi na uamuzi *(Mediation* na *Arbitration).*

- Ilifanikisha safari ya Mafunzo kwa Viongozi wa juu wa Wizara, Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri huko Afrika ya Kusini katika Taasisi za Utawala wa Kazi zikiwemo zile za Utatu.
- Ilipokea migogoro ya Kikazi 87 na kati ya hiyo migogoro 52 ilipelekwa Mahakama ya Kazi. Jumla ya rufaa mpya za Kikazi 235 zilipokelewa, na jumla ya rufaa 241 zikijumuisha rufaa mpya na za zamani zilishughulikiwa na kutolewa maamuzi. Mikataba ya Hiari 23 ilipokelewa na kati ya hiyo 20 ilishughulikiwa na kupelekwa Mahakama ya Kazi. Jumla ya kaguzi 451 zilifanyika na Mabaraza ya Usuluhishi 521 yaliendeshwa katika Ofisi za Kazi nchini. Jumla ya malalamiko 1,559 yalishughulikiwa na kiasi cha Sh.170, 939,254.70/= zililipwa kwa wadai mbalimbali.

- Madai 324 ya fidia ya kuumia kazini kwa watumishi wa serikali yalishughulikiwa na jumla ya Sh.34,992,000.00/= zililipwa. Pia madai ya fidia ya kuumia kazini kwa wafanyakazi wengine yalishughulikiwa na jumla ya Sh.52,973,166.45/= zililipwa na waajiri.

- Katika kushughulikia migogoro ya kazi ya milipuko, Wizara iliwezesha kufikiwa muafaka wa muda katika migogoro kwenye Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA),* Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)* na Benki ya Taifa ya Amana Ndogo *(NMB).*

- Katika kuendeleza vita dhidi ya utumikishwaji wa watoto na kukomesha ajira mbaya ya watoto, Wizara kupitia kitengo chake kinachohusika na ukomeshaji wa ajira ya mtoto, imeandaa mwongozo wa ukaguzi wa kazi katika kufanya kaguzi za ajira ya mtoto.

- Mikakati ya kukomesha ajira ya mtoto imeandaliwa kwa kuhusisha maoni ya wadau wa mradi huu. Wizara pia imeandaa orodha ya kazi mbaya sana *(Worst forms of Child Labour)* ambazo hazipaswi kufanywa na mtoto chini ya umri wa miaka 18.

- Pikipiki sita zimenunuliwa na kukabidhiwa waratibu wa programu ya ukomeshaji wa ajira ya mtoto katika Wilaya sita kati ya wilaya 11 zinazotekeleza mradi huu. Aidha, pikipiki mbili kati ya nne zimenunuliwa kwa ajili ya waratibu wa Wilaya nne zinazotekeleza programu hii mashambani.

- Jumla ya simu 13 za mkononi *(Cellular Phones)* zilinunuliwa na kukabidhiwa kwa waratibu wa Wilaya na Mikoa inayotekeleza programu ya ukomeshaji ajira ya mtoto.

- Warsha mbili zenye lengo la kutoa elimu kuhusu Programu ya kupambana na ajira ya mtoto ziliendeshwa kwa Waratibu wa Wilaya na moja kwa Waheshimiwa Wabunge.

- Ili kuendeleza Uongozi Bora na demokrasia sehemu za kazi, Wizara kwa kushirikiana na Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi imesimamia uchaguzi wa mabaraza ya wafanyakazi 13 na mafunzo kwa wafanyakazi yaliendeshwa kwenye Taasisi 11.

- Katika kupambana na janga la UKIMWI, shughuli za kupata mbinu bora za utekelezaji mzuri *(Best Practices)* katika vita hii ambazo zinatumika na Taasisi mbalimbali ili kuboresha na kukamilisha Kanuni za Maadili zinaendelea.

- Kwa upande wa mahusiano ya Kimataifa, Tanzania imehudhuria vikao vinavyohusu masuala ya kazi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Umoja wa Afrika *(AU)* na Mkutano wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO).*

- Ili kuongeza na kuboresha utendaji kazi wa Idara, Wizara inatarajia kuajiri maafisa kazi wengi zaidi na wengine kupangiwa vituo vipya vya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kusimamia utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Marekebisho ya Sheria za Kazi kwa kujenga Taasisi husika na kutayarisha nguvukazi ili kuwezesha sheria mpya za kazi kuweza kutumika.

- Kusimamia uundaji wa Bodi za Mishahara kwa sekta mbalimbali nchini kwa lengo la kutayarisha vima vya chini vya mishahara kulingana na uwezo na mapato ya sekta.

- Kuendeleza shughuli za utekelezaji wa sheria za kazi ikiwa ni pamoja na kushughulikia malipo ya fidia, kaguzi za kazi, migogoro, malalamiko, mikataba ya hiari na usimamizi wake nchi nzima.

- Kushughulikia kikamilifu masuala ya kimataifa katika nyanja za kazi kwa ngazi ya *ILO, AU, SADC, EAC* kuhusu majadiliano ya *Free Movement of Persons.*

- Kuendeleza vita dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi kwa kushirikiana na wadau na kukamilisha Kanuni ya Maadili *(Code of Conduct),* kwa kuhusisha mbinu za utekelezaji bora *(Best Practices)* ambazo tayari zinatumika katika Taasisi mbalimbali nchini.

- Kuendelea kuelimisha waratibu wa programu ya kupambana na ajira ya mtoto. Kuendelea na jitihada za kuwapatia vitendea kazi wakaguzi wa kazi na waratibu wa programu ya kupambana na ajira ya mtoto.

- Kuendelea kukuza uwezo wa watumishi kiutendaji na kupambana na rushwa ili kudumisha Uongozi Bora na Utawala wa Sheria.

- Kuendelea kusimamia uundaji na uelimishaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi ili kuwezesha kuwako kwa majadiliano kati ya wafanyakazi na waajiri wao.

- Kuendelea kuimarisha UTATU ili kuwezesha kutatua masuala yatakayojitokeza sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ajira. Idara hii pamoja na majukumu mengine iliendelea kutoa huduma za kuwaunganisha watu wanaotafuta kazi na waajiri wanaotafuta kuajiri wafanyakazi. Katika mwaka 2003/2004 Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliandaa, kuratibu na kushiriki Maonyesho ya Tano ya Sekta isiyo rasmi ambayo yaliyofanyika Mjini Dar es Salaam tarehe 4 - 9 Novemba, 2003 na yaliwashirikisha watu wapatao 436 kutoka Kenya, Uganda na Tanzania. Lengo la Maonyesho hayo ni ukumbusho wa kufufua Jumuiya ya Afrika Mashariki, kubadilishana ujuzi na uzoefu katika utengenezaji bidhaa, kuimarisha na kupanua masoko katika nchi wanajumuiya na kudumisha ushirikiano miongoni mwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Iliandaa Mpango wa kuendesha Mafunzo juu ya utaratibu wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini *(Demand-Driven SkillsTraining Programme).*

- Ilipokea maombi ya vibali vya ajira kwa wataalam wa kigeni 1,637 kati ya haya, maombi 1,347 yalikubaliwa na mengine 290 yanaendelea kushughulikiwa. Sekta za Madini, Biashara, Viwanda, Ujenzi, Utalii na Elimu ndizo zinazoongoza katika kuingiza wataalamu wengi wa kigeni.

- Wizara ilisajili watafuta kazi 1,927, ambao kati yao asilimia 32 walikuwa katika kada ya wataalam, asilimia 37 walikuwa katika kada ya mafundi na makarani, na asilimia 31 waliobaki walikuwa katika kada nyingine mbali mbali.

- Iliwasiliana na waajiri mbalimbali nchini na kufanikiwa kupata nafasi za kazi 708. Aidha, watafuta kazi 1,587 wenye ujuzi mbalimbali waliunganishwa na waajiri kwa ajili ya kufanyiwa usaili na kati yao watafuta kazi 135 au asilimia tisa ya waliounganishwa na waajiri walipata ajira.

- Iliendesha warsha 16 za mafunzo ya namna ya kujitafutia ajira kwa watafuta kazi 271 ili kufanikisha juhudi zao za kutafuta ajira.

- Katika kuwaongezea watafuta kazi uwezo wa kufanya vizuri katika usaili na hivyo kupata ajira, Kituo cha ajira kiliendesha vipindi 38 vya kuwapatia maelekezo maalum wasailiwa 375 kuhusu njia za kufanya vizuri katika usaili.

- Ilitoa ushauri wa kazi *(Vocational Guidance)* kwa watafuta kazi 67 waliohitaji huduma hiyo.

- Katika kuboresha huduma, Kituo cha ajira kilifanya utafiti kuhusu uridhishaji wa waajiri *(Employers Satisfaction Survey)* katika Mkoa wa Dar es Salaam na kugundua kwamba kati ya waajiri waliowahi kutumia huduma za kituo hicho asilimia 89 wanaridhika na huduma za Kituo hiki kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa dhati waajiri wote wanaokiunga mkono Kituo cha Ajira kwa kukitumia katika kuajiri wafanyakazi. Ninawaomba waajiri ambao hawajaanza kukitumia Kituo hiki wafanye hivyo ili wajipatie wafanyakazi wenye sifa zinazolingana na mahitaji yao kwa gharama nafuu. Vilevile ninavishauri Vyuo vya Elimu ya Juu na vyuo vya mafunzo ya ngazi mbali mbali vikitumie Kituo hiki ili kuwaongezea wahitimu wao uwezekano wa kuajiriwa na wakati huo huo kukiwezesha Kituo hiki kupanua hazina yake ya wafanyakazi watarajiwa, wenye elimu na ujuzi katika fani na viwango mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya utafiti wa nafasi za kazi zilizopo katika Jiji la Dar es Salaam *(Job Vacancy Survey),* ambao tayari taarifa ya matokeo yake imekwishachapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Katika kipindi cha utafiti huu ilionyesha kuwa, Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na jumla ya nafasi 12,321 na nyingi

ya nafasi hizi kiasi cha asilimia 62 zilihitaji watu wenye kiwango cha elimu ya stashahada au zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea na hatua ya pili ya marekebisho ya Sera na Sheria za Kazi na Ajira zinazohusu Hifadhi ya Jamii, Fidia, Afya na Usalama Sehemu za Kazi, Ukuaji wa Ajira na kuzihusisha Sheria hizi na zile za awamu ya kwanza.

- Kufanya utafiti wa ukuzaji wa ajira katika sekta mbali mbali ili kupima kasi ya ukuaji ajira nchini.

- Kuimarisha kazi ya ukusanyaji wa takwimu zitokanazo na utoaji wa huduma mbalimbali chini ya Wizara.

- Kuendeleza Mpango wa kuendesha Mafunzo juu ya utaratibu wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umasikini *(Demand-Driven Skills Training Programme).*

- Kutathimini na kutafuta njia ya kuboresha jinsi ya kuwawezesha wananchi kunufaika na nafasi za kazi zinazopatikana katika soko la ajira la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Kuhudhuria mikutano inayohusu masuala ya ajira na umasikini.

- Kushiriki katika maonyesho ya Nguvu Kazi/Jua Kali yatakayofanyika nchini Kenya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii iliendelea kushughulikia Sera mbalimbali, sheria, miongozo na shughuli zinazohusu huduma za Ustawi wa Jamii. Katika mwaka 2003/2004 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ilikamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliendelea kuelimisha jamii na asasi mbalimbali kuhusu Sera ya Taifa ya Wazee.

- Imeandaa Waraka wa kuiwezesha Serikali kuridhia taratibu za Umoja wa Mataifa kuhusu Fursa na Haki sawa kwa Watu wenye Ulemavu.

- Iliendelea kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuwatambua na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Zoezi hili limefanyika katika Wilaya za Temeke, Masasi, Ilala, Singida Mjini, Mtwara, Singida Vijijini, Bunda, Mwanza Mjini, Iringa Mjini. Hadi kufikia sasa zoezi hili limefanyika katika Wilaya 17 hapa nchini na jumla ya watoto 38,014 wametambuliwa.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliendelea kutoa mafunzo ya wawezeshaji haki katika ngazi ya jamii ili kusaidia kulinda haki za watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika Wilaya za Musoma Vijijini, Magu, Kisarawe na Karagwe.

- Mwongozo wa Kitaifa na Mikakati ya Malezi na Matunzo kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu umeandaliwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali.

- Iliendelea kuboresha Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii kwa kufanya mikutano ya kushauriana *(Consultative Meeting)* na wadau mbalimbali wanaohusika na usuluhishi wa ndoa ili kujadili njia na mbinu mbalimbali za kuboresha ushauri nasaha na usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa faida ya ustawi na uimarishaji wa familia.

- Iliendelea kutoa misaada kwa akina mama waliojifungua watoto watatu au zaidi kwa mara moja, watoto waliozaliwa wameungana na akina mama waliopata ulemavu wakati wa kujifungua. Jumla ya akina mama 16 walipata msaada huu.

- Iliendelea kuratibu, kusimamia na kukagua makao ya watoto yatima/wenye shida, makazi ya wazee/watu wenye ulemavu na vituo vya walezi ili kuhakikisha ubora wa huduma zitolewazo katika maeneo hayo.

- Iliendelea kutoa na kuboresha huduma ya matunzo kwa wazee, watu wasiojiweza na watu wenye ulemavu katika makazi na nje ya makazi, watoto yatima na mahabusu walio katika mahabusi za watoto na waadiliwa katika shule ya Maadilisho - Irambo.

- Iliendelea kuwawezesha watoto walio katika makao ya watoto yatima/wenye shida, makazi ya wasiojiweza, Shule ya Maadilisho, mahabusu za watoto na walio katika familia zenye dhiki kupata Elimu ya Msingi, Sekondari na Ufundi.

- Iliendelea kutoa huduma ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia. Jumla ya washitakiwa 8,275 waliokuwa wanakabiliwa na makosa mbalimbali ya jinai walishughulikiwa. Kati ya hao washtakiwa 470 waliamriwa na Mahakama kuwa chini ya uangalizi wa Maafisa Majaribio na Ujenzi wa Tabia. Watoto 2,347 waliokuwa wanakabiliwa na mashitaka mbalimbali ya jinai walihifadhiwa na kutunzwa kwenye mahabusu tano za watoto. Aidha, watoto 79 walipatiwa huduma ya uadilishi katika shule ya Maadilisho Irambo Mbeya.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliendesha semina kwa Maafisa Wafawidhi wa Mahabusu tano na Shule ya Maadilisho, ili kuboresha huduma kwa watoto walio katika mgogoro wa kisheria.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha Mahabusu tano kutoa elimu ya msingi *(COBET)* kwa watoto washtakiwa na wale ambao hawakuweza kuendelea na elimu ya msingi.

- Kwa kupitia mradi mdogo wa majaribio unaotekelezwa katika Mahabusu ya watoto Dar es Salaam iliendelea kuboresha huduma kwa watoto walio katika Mahabusi za Watoto na Shule ya Maadilisho.

- Iliendelea kutoa misaada kwa familia zenye dhiki na zilizoathiriwa na UKIMWI. Misaada hiyo iligharamia masomo kwa watoto yatima pamoja na mitaji kwa kuanzisha miradi midogo midogo ya uzalishaji mali ili kupunguza umaskini ndani ya familia zao.

- Iliendelea kutoa huduma za usuluhishi kwenye ndoa zenye mifarakano pamoja na kusimamia matunzo kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Jumla ya mashauri 7,018 ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa na mashauri 5,524 ya matunzo ya familia zilizo farakana yalishughulikiwa.

- Iliendelea kuratibu huduma za malezi ya kambo na kuasili. Jumla ya watoto watano waliasiliwa na jumla ya watoto tisa walichukuliwa na wazazi kwa malezi ya kambo.

- Iliendelea kutoa mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu 413 katika vyuo vya ufundi vya Yombo, Mirongo, Masiwani, Singida, Masasi, Chang'ombe na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Anatoglou.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanya utafiti kuhusu Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto katika wilaya ya Kibaha.

- Kwa kushirikiana na Mradi wa *Swedish Organisation of Handicapped International Aid Association (SHIA)*, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya lugha ya alama na *Braille* kwa waalimu wa Chuo cha Watu wenye Ulemavu Yombo na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Anatoglou ili waweze kuwasiliana na wanafunzi kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Wizara itaboresha huduma za Ustawi wa Jamii kwa kufanya yafuatayo:-

- Itaendelea kuhamasisha jamii na asasi mbalimbali juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee.

- Itaandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa watu wenye Ulamavu.

- Itaendelea kutoa na kuboresha huduma katika Makazi ya Wazee, Watu Wasiojiweza, watu wenye ulemavu, Makao ya watoto Yatima, Vyuo vya Watu wenye Ulemavu, Mahabusi na Shule ya Maadilisho.

- Itaendelea kutoa matunzo kwa wazee, watu wenye ulemavu katika makazi, makao ya watoto yatima, mahabusi za watoto, Shule ya Maadilisho na vyuo vya watu wenye ulemavu.

- Itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwatambua na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

- Itaendelea kutoa mafunzo kwa wawezeshaji haki katika ngazi ya wilaya na jamii.

- Itaendelea kutoa misaada kwa akina mama waliojifungua watoto watatu au zaidi, waliopata ulemavu wakati wa kujifungua na kwa watoto waliozaliwa wameungana.

- Itaendelea kuratibu uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo vya kutwa na makao ya watoto yatima/wenye shida kuhakikisha ubora wa huduma zitolewazo katika maeneo hayo.

- Itaandaa mwongozo wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Itaendelea kutoa misaada kwa familia zenye dhiki na zilizoathiriwa na Virusi vya Ukimwi.

- Itaendelea kuratibu huduma za malezi ya kambo na kuasili.

- Itaendelea kuboresha Baraza la Usuluhishi na Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

- Itawasilisha Serikalini Waraka wa kuiwezesha Serikali kuridhia taratibu za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Fursa Sawa kwa Watu wenye Ulemavu.

- Itaendelea kutoa huduma ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia.

- Kwa kushirikiana na wadau itaboresha huduma zitolewazo katika Mahabusi za watoto na Shule ya Maadilisho.

- Itaendelea kuelimisha na kutoa ushauri nasaha kwa watoto/vijana kuhusu athari za madawa ya kulevya na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu la kujenga mazingira endelevu yanayowawezesha vijana kujifunza na kuendeleza maadili mema katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ili kuweza kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi Wizara yangu katika mwaka 2003/2004 ilitekeleza yafuatayo:-

- Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani *(UNICEF)* na pia Vijana kutoka kwenye vikundi vya vijana vya uzalishaji mali, *NGOs, CBOs,* shule, vyuo mbalimbali na sehemu za kazi, iliendelea kuboresha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. Warsha sita zenye lengo la kukusanya maoni juu ya sera hii ziliendeshwa katika kanda sita: Kanda ya kwanza ilishirikisha vijana kutoka Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara, Kanda ya pili (Tanga, Kilimanjaro na Arusha), Kanda ya Tatu (Manyara, Singida na Dodoma), Kanda ya Nne (Iringa, Ruvuma, Rukwa na Mbeya),

Kanda ya Tano (Mwanza, Kagera na Mara) na Kanda ya Sita (Shinyanga, Tabora na Kigoma).

- Iliendelea na jukumu lake la kusimamia na kuratibu shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizoanzia Mkoani Tabora tarehe 7 Juni, 2003 na kilele cha Mbio hizi kilifanyika huko Mkoani Mwanza tarehe 14 Oktoba, 2003. Ujumbe kwa Mwenge wa Uhuru mwaka wa 2003 ulikuwa na sehemu kuu mbili ambazo ni Vita Dhidi ya UKIMWI na Haki ya Mtoto. Jumla ya miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. 31,317,398,552/= ilizinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi. Wananchi walichangia jumla ya Sh. 409,669,367/=. Kwa utaratibu uliopo sasa fedha hizo hubakia katika Wilaya kuendeleza shughuli za maendeleo.

- Ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wizara iliendesha warsha ya kutathmini mbio hizo kwa Mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 15 - 18 Desemba, 2003 huko Mkoani Arusha.

- Iliendelea kuratibu shughuli za Wiki ya Vijana. Wiki hii ina lengo la kuwakutanisha vijana na kuwawezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusu maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla. Wiki ya vijana iliadhimishwa huko Mkoani Mwanza kuanzia tarehe 8 - 14 Oktoba, 2003. Vikundi mbalimbali viliweza kuwapa vijana fursa ya kujadili matatizo yanayowakabili, kuonyesha na kuuza mali na vifaa vingine vinavyozalishwa na vikundi hivyo.

- Ilifanya maandalizi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru ambazo zilizinduliwa huko Mkoani Kagera tarehe 7 Juni, 2004, sherehe za kilele chake zinatarajiwa kufanyika Mkoani Lindi tarehe 14 Oktoba, 2004.

- Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* pamoja na wadau wengine, ilifanikisha kuandaa na kuadhimisha siku ya kimataifa ya wanaojitolea iliyofanyika Mkoani Dar es Salaam tarehe 8 Desemba, 2003. Aidha, katika kutekeleza lengo hili mafunzo ya ujasiliamali kwa washiriki 30 wa Mkoa wa Dar es Salaam yaliendeshwa.

- Baada ya kuandaliwa kwa mwongozo mpya wa mfuko wa maendeleo ya vijana, Serikali imeamua kuendelea na utoaji wa fedha za mikopo ambapo jumla ya Shilingi 370,770,780/= ziligawiwa kwa mikoa yote ikiwa ni jumla ya Shilingi 3,089,777/= kwa kila Halmashauri ya Wilaya, Mji na Manispaa.

- Mafunzo ya ujasiliamali yalitolewa kwa vijana 30 kutoka Mikoa ya Singida, Dodoma, Tanga na Morogoro katika Chuo cha Vijana cha Ilonga - Morogoro.

- Maboresho ya Mitaala ya kutoa mafunzo kwa vijana ilifanyika Mkoani Kilimanjaro. Baadhi ya Mitaala hiyo ilifanyiwa mapitio ya kuboreshwa ambayo ni Ujasiri na Masuala ya Jamii, *Physical education* na Stadi za Maisha.

-	Ilifanya utafiti wa kina katika maeneo wanapokaa vijana bila kazi maalumu Vijiwe katika Mikoa ya Ruvuma na Kagera. Taarifa muhimu ambazo zimekusanywa katika mpango huu ni pamoja na jina la kijiwe, mahali kilipo, idadi ya wanakijiwe, shughuli zinazofanywa na kijiwe, matarajio ya kijiwe pamoja na mahitaji ya kijiwe. Lengo la zoezi hili ni kuiwezesha Wizara kupata takwimu ambazo zitaiwezesha kupanga mikakati mbalimbali ya kuvigeuza vijiwe hivyo kuwa ni sehemu ya uzalishaji mali na kuwapatia vijana kipato kwa njia ya kujitegemea. *(Makofi)*

-	Iliendelea kushirikiana na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na programu ya miaka 10 ya kukuza ajira kwa vijana. Mtandao wa Kitaifa wa Ajira ya Vijana Duniani *(YES 2002)* ni mpango shirikishi baina ya vikundi vya vijana, Taasisi za vijana za Kitaifa na kimataifa vyenye lengo la kukuza ajira ya vijana Duniani. Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kuzindua mpango huu katika Afrika na imeendelea kuwa miongoni mwa nchi chache Duniani zinazofanya vizuri katika mpango huu.

-	Imeratibu na kutekeleza mpango wa kubadilishana vijana na nchi za Japan Canada na Sudan. Lengo la mpango huu ni kuimarisha mahusiano kati ya vijana wa Kitanzania na mataifa mengine ulimwenguni. Katika mpango huu vijana hupata fursa ya kujadili masuala mbalimbali kuhusu maendeleo yao, matatizo yanayowakabili na kubadilishana uzoefu katika maeneo mbalimbali yakiwemo masuala ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Katika kutekeleza mpango huu Wizara yangu iliandaa Vijana 12 kwenda nchi ya Japan na vijana wengine tisa kwenda Canada. Vijana 12 wa Kitanzania waliungana na vijana 300 wa mataifa mengine 13 huko Japan katika programu ya Meli. Mwaka huu wa 2004, Bandari ya Dar es Salaam ilichaguliwa kwa mara ya tatu kuwapokea vijana hawa. Bandari nyingine zilikuwa ni Mumbai-India na Victoria-Seychelles. Vijana hawa walikaa nchini kwa siku tatu na kutembelea taasisi mbalimbali zikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kituo cha kulelea watoto yatima Kurasini, Shule ya Kihistoria ya Sekondari ya Pugu na sehemu nyingine kama vile Makumbusho ya Taifa.

-	Chini ya mpango wa kubadilishana vijana wa Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Youth Programme - CYP),* Wizara yangu ilishiriki kwenye mkutano ulifanyika huko Australia kwa lengo la kukuza ushirikiano miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola na hasa masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya vijana.

-	Iliendesha warsha ya uboreshaji mitaala kwa ajili ya chuo cha ujasiri Marangu iliyofanyika katika Chuo cha Ujasiri Marangu Moshi. Lengo la warsha hiyo ilikuwa kuangalia upya baadhi ya mitaala ili ilingane na mabadiliko ya taaluma yaliyopo.

-	Iliendesha mafunzo ya ujasiliamali na stadi za maisha kwa vijana 30 na Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam kwa kushirikiana na Asasi isiyo ya Kiserikali ijulikanayo kama *SEBA TANZANIA.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendelea kuratibu utoaji mikopo kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa kwa lengo la kuviongezea uwezo vikundi vya uzalishaji mali vya vijana.

- Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa vijana katika masuala ya uongozi usimamizi na uendeshaji wa miradi ya uzalishaji mali kwa lengo la kuboresha uzalishaji na kuongeza vipato vya Vijana.

- Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana pamoja na sherehe za kilele ambazo zitafanyika Mkoani Lindi tarehe 14 Oktoba, 2004.

- Kuandaa na kutekeleza programu za elimu na malezi bora kwa vijana.

- Kutekeleza mpango wa kudhibiti UKIMWI *(Multisectoral Aids Project)* mahali pa kazi na kwa vijana utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

- Kushirikiana na viongozi wa Wilaya na Serikali za Mitaa katika kuimarisha, kukuza na kusimamia utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo ya vijana nchini kote.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Michezo, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea na jukumu la kuendeleza michezo hapa nchini kulingana na Sera ya Maendeleo ya Michezo, ambapo yafuatayo yalitekelezwa:-

- Kuendelea kusimamia ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa.

- Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya uongozi, utawala, ukocha na uamuzi, ili kuboresha uwezo wa watendaji katika michezo. Mengi kati ya mafunzo haya yamekuwa yakifanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, Kituo cha Michezo cha Arusha na kituo cha Songea.

- Katika kuboresha utulivu na amani ndani ya vyama vya michezo, Wizara iliendelea kutoa maelekezo ya namna ya kuhuisha na kurekebisha katiba za vyama na vilabu vya michezo ili zifanikishe kuleta utawala bora ndani ya vyama na vilabu. Zoezi la kurekebisha Katiba ya *FAT* linaendelea na tuna matumaini makubwa kwamba baada ya katiba kukamilika hakika uongozi mbovu utaweza kuwa unapata shida kuingia katika nafasi za uongozi. Jumla ya katiba 175 zilishughulikiwa na kusajiliwa. *(Makofi)*

- Huduma ya Kinga na Tiba kwa wanamichezo iliendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuongeza watumishi. Wachezaji wote wa timu za Taifa wamekuwa wakipimwa afya zao. Aidha, Kitengo cha Tiba kwa Wanamichezo kiliwafanyia uchunguzi wa afya zao Makatibu Wakuu wa Wizara zote na Makatibu Tawala wa Mikoa yote huko Bagamoyo walipokuwa katika Warsha iliyandaliwa na Shirikisho la Michezo katika Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI). Viongozi hao walipewa ushauri wa namna ya kuboresha afya zao kwa kufanya mazoezi ya viungo vya mwili.

- Kwa lengo la kuboresha mazoezi na mashindano kwa watu wenye ulemavu, Wizara iliwagharamia kozi za mafunzo nje ya nchi viongozi na walimu wa michezo kwa watu wenye ulemavu Paralimpiki *(Paralympics)*. Jumla ya walimu wawili walipata mafunzo haya.

- Ilifanikisha mashindano ya Taifa ya Paralimpiki yaliyofanyika Dar es Salaam kwa mafaniko makubwa, yaliyowashirikisha jumla ya wanamichezo 250.

- Jumla ya wanamichezo wawili wenye ulemavu na mwalimu mmoja walikuwa ni miongoni mwa walioshiriki katika timu ya Taifa iliyoshiriki Michezo ya Mataifa Huru ya Afrika.

- Katika kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa, Wizara iligharamia ushiriki wa timu za Michezo ya Mataifa Huru ya Afrika yaliyofanyika Abuja Nigeria. Timu ilikuwa na jumla ya wanamichezo 20 walioshiriki michezo ya riadha, ngumi, judo na kunyanyua uzito kwa watu wenye ulemavu. Jumla ya medali mbili, moja ya dhahabu na moja ya shaba zilitwaliwa na Tanzania ilikuwa nchi ya wa 18 kati ya nchi 51 zilizoshiriki.

- Michezo ya *SADC* iliyofanyika Maputo Msumbiji, Tanzania ilipata jumla ya medali 6 zikiwemo tatu za dhahabu na tatu za fedha na kushika nafasi ya sita katika nchi 12 zilizoshiriki. *(Makofi)*

- Katika mapambano dhidi ya rushwa michezoni, Wizara iliandaa warsha kwa wadau 61 wa Kanda ya Mashariki iliyofanyika Morogoro, kujadili sababu na mianya ya rushwa michezoni na kutoa mapendekezo ya namna ya kuyakabili.

- Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA),* Wizara ilifanikiwa kumpata mtaalamu mmoja wa mchezo wa karate kutoka Japan, ambae atakuwa nchini kwa miaka miwili akitoa mafunzo kwa makocha wa mchezo huo na wachezaji pia.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa michezo inaendeshwa kisayansi, Wizara yangu imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa Maendeleo ya Vyama vya Michezo, ukiwa na maeneo 10 ya ufanisi. Muundo huu unaendelea kufundishwa kwa vyama vya michezo. Vyama ambavyo vimeutumia vimeshaonesha kupata mafanikio ya kutia moyo.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa michezo utakaojengwa Mjini Dar es Salaam.
- Kuiwezesha timu ya Taifa kushiriki katika michezo ya Olimpiki itakayofanyika Athens-Ugiriki mwezi Agosti, 2004.

- Kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu kwa viongozi, makocha na waamuzi wa michezo kwa nia ya kuboresha taaluma, hivyo kuinua viwango vya michezo hapa nchini na hatimaye kushinda katika mashindano ya Kimataifa.

- Kuendelea kuvishauri vyama kuhusu marekebisho ya katiba na kuzifuata ili kuleta amani na utulivu. Aidha, kuendelea kudurusu katiba mpya za vyama na vilabu na kuzisajili.

- Kuendelea kuvisajili vyama na vilabu vya michezo nchini.

- Kutoa ushauri wa kitaalamu katika kuboresha na kuimarisha miundombinu ya michezo kwa nia ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kucheza michezo.

- Kusimamia uendeshaji na utoaji wa mafunzo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo - Malya na Vituo vya Kanda vilivyoko Arusha na Songea.

- Kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa kwa kusimamia mashindano ya Taifa ya Olimpiki Maalum yatakayofanyika Mwanza mwezi Desemba, 2004, ikiwa ni maandalizi ya mashindano ya Kimataifa yatakayofanyika China mwaka 2007. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo maalum ya kitaalamu ndani na nje ya nchi kwa wataalamu na walimu wa michezo kwa watu wenye ulemavu.

- Kuendelea kutoa mafunzo ya namna ya kuandaa Mpango wa Maendeleo kwa Vyama vya Michezo.

- Kuendelea kupima afya za wanamichezo na kutoa ushauri wa kuboresha hali zao. Aidha, Wizara itaimarisha Kitengo cha Tiba kwa wanamichezo na kufungua matawi katika Mikoa yote 21 kwa nia ya kuhakikisha huduma hii inawafikia wachezaji wengi zaidi nchini.

- Kufuatilia mikataba yote ya kimataifa ili kubaini maeneo ya ushirikiano na kuzitumia fursa zote zilizoko humo. Pia kutafuta uwezekano wa kuanzishwa mikataba mipya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri iliendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria Na. 10 ya mwaka 1998 ya Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri nchini. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- Imepokea jumla ya maombi matatu ya usajili wa Vyama vya Waajiri na Waajiriwa, moja kati ya haya lilikihusu Chama cha Waajiri na maombi mawili mengine kutoka kwa Wafanyakazi wa sekta ya ulinzi na mawasiliano ya simu. Maombi haya mawili bado yanaendelea kuchambuliwa.

- Chama cha Waajiri *(The Association of Tanzania Employers - ATE),* kimesajiliwa kikiwa ni chama cha kwanza cha Waajiri nchini kusajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, tangu Sheria hiyo ianze kutumika tarehe 1 Julai, 2000. Kusajiliwa kwa umoja huo wa Waajiri nchini kutaimarisha majadiliano baina yao, Serikali na Vyama vya Wafanyakazi pamoja na kuendeleza mahusiano mema mahali pa kazi.

- Serikali inatoa wito kwa Waajiri wote wengine wenye lengo la kuendeleza mahusiano mema kati yao na wafanyakazi kutumia uhuru na haki yao kujisajili kwa mujibu wa Sheria hii.

- Jumla ya Kaguza 43 za Vyama vya Wafanyakazi zilifanyika katika Mikoa saba kama ifuatavyo:-

Morogoro vyama sita, Dodoma kumi, Tanga (vitano, Kilimanjarovinane, Arusha vinane, Pwani viwili na Singida vinne. Katika kaguzi hizi ushauri ulitolewa kwa Watendaji wa Vyama Mikoani kuweka utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu za wanachama yaani (Rejista) ili kuwasaidia kufuatilia michango na ada kwa ufanisi zaidi na kuepukana na tatizo la kunyang'anyana wanachama.

- Iliendelea kuelimisha Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri kwa njia ya Semina. Semina moja iliyojumuisha Makatibu Wakuu wa Vyama vyote vilivyosajiliwa ilifanyika Mwezi Desem, 2003, ambapo mada mbalimbali zilijadiliwa zikiwemo, Mkataba wa Kimataifa wa Kazi Na. 87, unaohusu Uhuru wa kujiunga na kuanzisha Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Wajibu wa Vyama katika ulimwengu wa mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii; Majadiliano ya Mikataba ya Hiari, Vyombo vya Utatu na Mwelekeo Mpya wa Sheria za Kazi.

- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Wizara iliendelea kuuelimisha umma kwa njia ya Redio juu ya uhuru na haki ya kuunda na kujiunga na vyama vya waajiri au wafanyakazi kwa hiari yao.

- Mkutano wa watendaji wakuu wa vyama ulifanyika kwa lengo la kukumbushana juu ya utekelezaji wa masuala yaliyo ndani ya Sheria ambayo yamekuwa hayatekelezwi kwa muda unaotakiwa, hususan uwasilishaji wa taarifa za mapato na matumizi za kila Mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- Itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Aidha, maombi ya vyama vya wafanyakazi yaliyopo na yale yatakayopokelewa yataendelea kushughulikiwa kwa Mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

- Itaendelea kufanya kaguzi za vyama katika Mikoa ambayo haijakaguliwa.

- Itaendelea kuelimisha vyama kwa njia ya mikutano na semina, ili kuviwezesha kujenga umoja na ushirikiano ndani ya vyama vyote, pia kuvisaidia katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

. Mheshimiwa Spika, umuhimu wa usalama na afya na wafanyakazi katika sehemu za kazi uliendelea kupewa uzito na Wizara yangu. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi *(OSHA)* ilitekeleza yafuatayo:-

- Sheria mpya ya Usalama na Afya Mahali pa kazi ilianza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Agosti, 2003. Napenda kuchukua fursa hii, kuwakumbusha waajiri wa Wadau wote kwa ujumla kuwa ni vyema kuzingatia sheria hiyo ili kuboresha afya na usalama sehemu za kazi hatimaye kuongeza tija.

- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* mnamo tarehe 28 Aprili, 2004 ilifanikisha kuadhimisha siku ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi Duniani ikiwa ni Kampeni Maalum ya Kimataifa ya kuwataka wadau wote na umma kwa ujumla kujenga utamaduni katika nyanja ya Usalama na Afya *(Safety and Health Culture),* zoezi hili litakuwa likifanyika kila mwaka.

- Jumla ya kaguzi 4,534 za kawaida *(General Workplace Inspections)* zilifanyika na ushauri stahili kutolewa.

- Kaguzi 2,207 maalum na za kisheria *(Special and Statutory)* ambazo zinajumuisha zana mbalimbali zitumikazo viwandani na sehemu zingine za kazi *(Statutory Plant Inspections),* kaguzi za umeme *(Electrical Inspections),* upimaji wa afya za wafanyakazi *(Medical Examinations),* upimaji wa viwango vya afya sehemu za kazi *(Industrial Hygiene Measurements),* uandikishaji wa viwanda/sehemu za kazi, uchunguzi wa ramani za majengo mapya yanayokusudiwa kuwa Viwanda/sehemu za kazi *(Scrutiny of Industrial Plants)* na uchunguzi wa ajali sehemu za kazi *(Accident investigations)* zilifanyika.

- Ofisi za Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi ilihamia katika jengo la Wizara lililoko Kinondoni ambalo lilikarabatiwa kwa msaada wa *DANIDA.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, *OSHA* itatekeleza yafuatayo:-

- Kufanya kaguzi 2,810 maalum na za kisheria *(Special and Staturtory).*

- Kufanya kaguzi 2,000 za kawaida *(General Workplace Inspections)* katika maeneo mbalimbali ya kazi ili kutambua athari ziwapatazo wafanyakazi na kutoa ushauri unaostahili.

- Kukamilisha ukarabati wa sehemu ya jengo iliyosalia kwa msaada wa *DANIDA* ili kuruhusu kuwepo kwa maabara ndogo, kliniki *(Occupational Health Clinic),* chumba cha mafunzo, mikutano na maktaba.

- Kutoa mafunzo ya afya na usalama mahali pa kazi kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo Redio, Televisheni, Magazeti na vipeperushi ili kuwafikia walengwa wengi zaidi, kwa msaada wa *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Baraza la Michezo (BMT) lilitekeleza yafuatayo:-

- Lilikamilisha Rasimu ya marekebisho ya sheria Na. 12 ya BMT ya mwaka 1967 na kuiwasilisha Serikalini kwa hatua zaidi.

- Lilitoa maelekezo kwa Vyama vya Michezo kuandaa mikakati ya michezo kwa Vijana ambapo Vyama vya *TCA, TABA, TAHA, TAAA, FAT* na *TTTA* vimeanzisha timu za Taifa za Vijana wa rika mbalimbali.

- Kwa kushirikiana na Wadau wengine liliendesha mafunzo mbalimbali ya kuhamasisha Wanawake kushiriki katika michezo. Mafunzo hayo ni pamoja na kuendesha matamasha ya Kitaifa na Kimataifa kwa njia za mashindano kwa timu za wanawake za michezo mbalimbali. Jumla ya matamasha matatu yamefanyika. Aidha, liliwahamasisha wanamichezo wanawake kuunda Chama cha Michezo kwa Wanawake ambacho hivi sasa kinaendelea kukamilisha taratibu za Usajili.

- Idadi ya washiriki kwa watu wenye ulemavu katika michezo imeongezeka na vilabu vya michezo vimeanza kuundwa miongoni mwa washiriki. Jumla ya vilabu saba vimeundwa kwa michezo ya kunyanyua uzito *(Powerlifting),* Viti vya walemavu *(Wheelchairs),* Mpira wa vikapu *(Basketball)* na Riadha. Pia viongozi, walimu na wanamichezo 10 wamepatiwa mafunzo kuhusu michezo kwa watu wenye walemavu katika nchi za Ethiopia na Uholanzi.

- Lilisimamia chaguzi za Vyama vya Michezo vinne. Aidha, lilishughulikia rufaa za michezo mbalimbali zipatazo 10 na kusuluhisha migogoro katika Vyama vitatu vya michezo.

- Kwa kushirikiana na Wadau wengine, liliendesha mafunzo kuhusu fani mbalimbali za michezo huko Zanzibar, Ngara, Temeke na Morogoro. Mafunzo hayo yalihusu Uongozi na Utawala wa Vyama vya Michezo, utatuzi wa migogoro na uundaji wa Vilabu.

- Kwa kushirikiana na Wadau wengine lilishiriki katika kuandaa na kuendesha Kongomano la Kimataifa kuhusu Elimu kwa jamii kuhusu mapambano dhidi ya UKIWMI kwa kutumia michezo.

- Lilisimamia maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika Michezo ya Afrika. Jumla ya wanamichezo wanne wa Tanzania walichaguliwa kuunda Kombaini ya Afrika iliyoshiriki katika mashindano ya Bara la Afrika na *ASIA (AFRO-ASIA)* yaliyofanyika huko India mwezi Oktoba/Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Baraza la Michezo la Taifa litatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha kuratibu Mkakati wa Taifa wa michezo kwa vijana.

- Kuendelea kuendesha mafunzo kwa viongozi wa vyama vya michezo kuhusu utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa katika michezo na namna ya kutumia michezo katika vita ya kupunguza umaskini miongoni mwa jamii.

- Kusimamia na kuendesha uchaguzi wa vyama vitano vya michezo mbalimbali.

- Kuongeza jitihada za kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kutatua matatizo ya vilabu vya vyama vya michezo.

- Kuendesha mafunzo kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo na Utawala Bora kwa viongozi wa Kamati za michezo za Mikoani na Vyama vya Michezo vya Taifa.

- Kushirikiana na Vyama vya Michezo kwa watu wenye ulemavu na Chama cha Michezo kwa Wanawake katika kuhamasisha watu wenye ulemavu na Wanawake ili waunde vilabu na Vyama vya Michezo katika ngazi mbalimbali kwa ajili ya kuongeza idadi ya washiriki.

- Kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya timu za Tanzania zitakazoshiriki mashindano ya Olimpiki na Paralimpiki huko Athens Ugiriki mwezi Agosti na Septemba, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *VETA* inasimamia na kuratibu shughuli za mafunzo ya ufundi stadi nchini, kutoa mafunzo katika stadi mbalimbali zinazochangia kukuza ajira nchini na kusajili vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, *VETA* imetekeleza yafuatayo:-

- Ukarabati na upanuzi wa vyuo vya ufundi stadi vya Oljoro (Arusha), Musoma, Kagera, Mikumi na Songea umendelea kutekelezwa. Utekelezaji umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Ukarabati umekamilika katika vyuo vya Oljoro (Arusha), Musoma, Kagera na Mikumi. Samani na vifaa vya kufundishia vinasubiriwa. Mafunzo kwa Mameneja na Walimu yataanza mwezi wa nane mwaka huu. Aidha, kwa upande wa Songea utekelezaji umesimama kwa ajili ya kumpata mkandarasi mpya.

- Taratibu za ukarabati na upanuzi kwa vyuo vya ufundi stadi vya Shinyanga, Singida, Mpanda, Tabora, Ulyankulu na Ujenzi wa Chuo kipya na Hoteli na Utalii Njiro (Arusha) zimeanza. Ujenzi huo unagharamiwa na *African Development Bank (ADB),* kwa mkopo wa masharti nafuu na msaada kutoka *African Development Fund (ADF).*

- Ujenzi wa Chuo kipya cha ufundi stadi Kigoma uliendelea kutekelezwa na tarehe 14 Mei, 2004, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi. Ujenzi wa chuo umezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwenye maeneo mbalimbali vikiwemo vyoo na vyumba vya kulala. Chuo kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 wa kozi ndefu katika fani 18 kila mwaka. Wanafunzi 200 kati yao ni wa bweni. Aidha, kozi fupi fupi kwa ajili ya washiriki zaidi ya 2000 kutoka sekta isiyo rasmi nazo zitatolewa kila mwaka. Serikali ya Korea ya Kusini imekubali kimsingi kutoa mkopo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo na samani kwa ajili ya chuo hiki.

- Mkazo uliendelea kuwekwa katika utoaji wa kozi fupi fupi ili kupanua nafasi za mafunzo na kupiga vita umasikini kupitia mafunzo maalum kwa vikundi katika sekta isiyo rasmi. Mafunzo ya kozi fupi fupi yalitolewa katika vyuo vyote vya *VETA* kwa jumla ya washiriki 10,400 kutoka sekta isiyo rasmi. Hii ni ongezeko la asilimia 16 kulinganisha na idadi ya walishiriki katika kozi za aina hii zilizotolewa mwaka 2002/2003.

- *VETA* imeratibu Vyuo vinavyomilikiwa na Taasisi na Asasi zisizo za kiserikali, watu binafsi na mashirika ya kidini vilivyoanza kutoa mafunzo ya kozi fupi fupi ambazo zimewanufaisha jumla ya washiriki 25,405.

- Mafunzo ya ufundi stadi ya kozi ndefu yameendelea kutolewa katika vyuo vya *VETA* kwa jumla ya vijana 7,920 hili ni ongezeko la asilimia 9 kulinganisha na idadi ya vijana waliojiunga na mafunzo hayo mwaka 2002/2003. Vyuo vya taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya dini na watu binafsi vilitoa mafunzo ya muda mrefu kwa jumla ya vijana 22,193. Hili ni ongezeko la asilimia 11 kulinganisha na idadi ya washiriki kwa mwaka 2002/2003.

- Mafunzo ya ufundi stadi kwa wasichana katika kozi ndefu na fupi katika fani za ushonaji, ufundi uashi, magari, umeme, useremala, urembo, uchapishaji, kilimo na usindikaji chakula yameendelea kutolewa. Jumla ya wasichana 18,126 walihudhuria mafunzo haya.

- Utoaji wa mafunzo umeendelea kuboreshwa kwa kuendeleza mafunzo ya walimu wa ufundi stadi, vielelezo vya kufundishia *(Learning Materials),* pamoja na taratibu za usajili na ithibati *(accreditation)* ya vyuo vya ufundi stadi. Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi Morogoro kimepanua wigo wa utoaji wa mafunzo nje ya chuo *(Off-Campus)* katika vituo vya Dar es Salaam, Moshi, Tanga, Iringa, Mbeya na Morogoro. Lengo ni kuwa na kituo katika kila Mkoa ili kukidhi mahitaji makubwa ya mafunzo kwa walimu waliopo kazini *(In-service Training).*

- Mfumo mpya wa mafunzo ya ufundi stadi (*Competence Based Education and Training)* unaolenga sekta rasmi na isiyo rasmi umeendelea kuimarishwa. Aidha, washiriki kutoka vyuo 80 vya ufundi stadi hapa nchini walihudhuria warsha ya kitaifa

ambapo walipata fursa ya kujadili na kukubaliana juu ya mkakati wa kipindi cha miaka minne ijayo (2005 - 2008).

- Kitengo maalum cha Mafunzo katika sekta ya nyama *(Meat Industry)* kimeanzishwa katika Chuo cha *VETA* Dodoma kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Tayari majengo na ufungaji mitambo umekamilika na mitaala imeandaliwa. Kwa kuanzia walimu watatoka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na mafunzo yanategemewa kuanza mwezi Septemba 2004.

- Utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa ushirikiano na *DANIDA* unaolenga kuboresha mbinu za ukusanyaji na utoaji wa tafsiri za mahitaji ya stadi katika soko la ajira *(Labour Markert Demands for Skills)* umeanza kwa kufanyiwa majaribio *(piloting)* katika Mkoa wa Morogoro.

- Mpango wa kupanua na kuboresha mpango wa mafunzo ya kupambana na janga la UKIMWI kwenye vyuo vyote vya ufundi stadi nchini unaendelea kutekelezwa.

- *VETA* imeendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa mitihani ya ufundi stadi na biashara *(Trade Test and NABE)* hapa nchini. Jumla ya wanafunzi 21,997 walifanya mitihani hii katika madaraja mbalimbali na kati yao 15,459 au 70.28% walifaulu. Idadi ya watahiniwa imeongezeka kwa 16% ikilinganishwa na waliofanya mitihani katika mwaka 2002/2003. Mitihani katika mfumo mpya *(Competence Based Assessment)* ilitolewa kwa vijana 5,074 katika vyuo vya *VETA* hadi kufikia Novemba 2003 na kati yao vijana 4,214 au 83% walifaulu. Idadi ya watahiniwa imeongezeka kwa asilimia 39. Katika mitihani ya *NABE,* jumla ya washiriki 1,812 walifaulu.

- Katika kipindi hiki, *VETA* kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* inatekeleza mradi wa *IPEC* ambao unalenga kuwaondoa na kuwazuia watoto walio chini ya umri wa miaka 18 kwenye ajira mbaya kwa kuwapatia mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri. Mradi huu unalenga watoto 7,500 na familia 2,000. Katika mradi mzima *VETA* ni waratibu wa mafunzo ya ufundi na mafunzo yanayotolewa na vyuo vya ufundi ambavyo vimesajiliwa na *VETA* katika Wilaya 11 ambako mradi huo unafanya kazi.

- *VETA* imeendelea kushirikiana na Zanzibar katika suala la utoaji wa mitihani ya ufundi stadi na *NABE.* Jumla ya watahiniwa 430 wa Zanzibar walifanya mitihani hii, na kati yao 301 ambao ni sawa na (70%) walifaulu.

- Chuo cha *VETA* Kihonda, kimeendelea kushirikiana na shirika la kuhudumia wasioona *(Tanzania Society for the Blind)* kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana. Vijana sita wanajifunza ushonaji, utengenezaji wa *batik* na *tie and dye* na watakaofaulu watapewa vifaa vya kutendea kazi *(Tools and Materials)* ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, *VETA* imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kukamilisha ukarabati na upanuzi wa Chuo cha Ufundi cha *VETA* Songea chini ya mradi unaofadhiliwa na *OPEC Fund.*

- Kuendelea na taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya vifaa vya mafunzo kwa vile vyuo vilivyokarabatiwa chini ya ufadhili wa *OPEC Fund,* yaani Oljoro (Arusha), Mara, Kagera, Mikumi na Songea.

- Kuendelea na utekelezaji wa ukarabati na upanuzi wa vyuo vya ufundi stadi Shinyanga, Singida, Mpanda, Tabora, Ulyankulu na Ujenzi wa Chuo cha Utalii Njiro (Arusha) chini ya mradi unaofadhiliwa na *ADB.*

- Kuendelea na ukamilishaji wa Mradi wa Chuo cha *VETA* Kigoma. Kwa upande wa vifaa vya kufundishia pamoja na kuanza mafunzo katika kozi fupi fupi.
- Kuendelea kuweka mkazo katika utoaji wa kozi fupi fupi ili kupiga vita umaskini.

- Kuendelea kuweka mkazo katika kuimarisha na kupanua mafunzo ya ufundi stadi kwa wasichana.

- Kuendelea na uboreshaji wa utoaji wa mafunzo kwa kuendesha mafunzo kwa waalimu wa ufundi stadi, kuchapisha vielelezo vya kufundishia na kuimarisha usajili na ithibati ya vyuo vya ufundi stadi.

- Kuendelea kuimarisha na kuendeleza mfumo mpya wa mafunzo, hususani katika vyuo vya taasisi za kidini, watu binafsi na taasisi zisizo za kiserikali.

- Kuendeleza uimarishaji wa kitengo cha mafunzo kwa ajili ya sekta ya nyama *(Meat Industry)* kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

- Kuendelea kupanua elimu ya maisha *(Life Skills)* katika vyuo vyote vya ufundi stadi nchini inayojumuisha elimu ya kujikinga na janga la UKIMWI.

- Kuendelea kutekeleza mkakati wa kubadili mfumo wa sasa wa utoaji mitihani ya ufundi na biashara *(Trade Tests* na *NABE)* kuelekea mfumo mpya wa *(Competence Assessment)*.

- Kuenedelea kushirikiana na Zanzibar katika suala la utoaji wa mitihani ya ufundi stadi za biashara.

- Kuendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kuhamasisha na kuongeza idadi ya wanafunzi wenye ulemavu watakaopewa mafunzo ya ufundi stadi na biashara.

- Kuendelea na taratibu za kupata hati miliki kwa kiwanja cha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Lindi pamoja na kumpata mshauri kwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004.

- Kuendelea kujadiliana na serikali ya Korea ya kusini kuhusu mkopo wa ujenzi wa vyuo vya ufundi vya Pwani, Manyara na Lindi.

- *VETA* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(BICCO),* watatoa mafunzo kwa waalimu wa ufundi stadi 200 na Mameneja 50 kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* ambalo ni moja ya Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu liliendelea na majukumu yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao kwa wanachama. Aidha, liliboresha mafao ya wanachama, Shirika liliendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile Dhamana za Serikali na mabenki, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)* na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha na kuuza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004 Shirika lilitekeleza yafuatayo:-

- Lilikusanya kiasi cha shilingi milioni 159,734.2/= kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali. Kiasi hiki ni asilimia 102.3 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 156,656.4/= katika kipindi hicho.

- Liliboresha mafao ya wanachama, shirika liliendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali na mabenki, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Stock Exchange)* na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha na kuuza.

- Limelipa mafao ya wanachama jumla ya shilingi milioni 18,486.9 kufikia kipindi cha mwezi Juni, 2004. Hii ni sawa na asilimia 125.0 ya lengo lililokusudiwa katika kipindi hicho.

- Lilikamilisha ukarabati na upanuzi wa jengo la *Water Front House* lililopo Mkoani Dar es Salaam.

- Lilikamilisha ujenzi wa nyumba 104 za gharama nafuu katika kiwanja cha Kinyerezi.

- Liliendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni Mjini Dar es Salaam.

- Liliendelea kuendesha semina mbalimbali na mafunzo ili kuwawezesha Wananchi kuuelewa mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii. Semina na mafunzo hayo yalitolewa kwa waajiri na wanachama wa *NSSF.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Shirika litatekeleza yafuatayo:-

- Litakusanya mapato yanayofikia shilingi bilioni 172.7 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na kutumia kiasi hicho hicho cha fedha.

- Litaendelea kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii.

- Litaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya nyumba 91 za gharama nafuu eneo la Kinyerezi na maeneo mengine yaliyotengwa kwa kazi hiyo.

- Litatoa Fao la Matibabu kwa Wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuanzia mwezi Oktoba, 2004.

- Litaweka kompyuta katika ofisi zake zote na kuziunganisha.

- Litaendelea kuboresha uwekezaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama.

- Litajenga jengo la ofisi katika Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

- Litakamilisha ujenzi wa Jengo la *Mafuta House* ambalo Shirika limekabidhiwa na Serikali mwezi Juni, 2004.

- Litaendelea kufanya utafiti wa kina zaidi juu ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ni Chuo cha Elimu ya Juu kilicho chini ya Wizara yangu, kiliendelea na shughuli zake kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 26 ya 1973. Katika mwaka 2003/2004 Taasisi ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliongeza idadi ya wakurufunzi kutoka 320 hadi 450 na kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili ya kisasa ambayo tayari yameanza kutumika.
- Iliendesha mafunzo kwa wadau (Wafanyakazi na Wajumbe wa Bodi) kuhusu Mkakati wa Maendeleo *(Strategic Plan)* wa Taasisi ili waupokee kuwa ni wao.

- Ilikamilisha maandiko *(Project Write-ups)* matano yatakayotumika kuombea misaada ya utekelezaji malengo yaliyowekwa ya upanuzi miundo mbinu na maendeleo ya wafanyakazi.

- Iliongeza muda wa mafunzo ya vitendo kwa wakurufunzi wake wanaochukua mafunzo ya cheti na kuboresha usimamizi wa mafunzo hayo.

- Kwa kupitia mitaala yake Taasisi imekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji ilani ya uchaguzi kuhusu masuala ya Watoto, jinsia, UKIMWI, Walemavu, Wazee, dhana ya Uongozi Bora na Vyama huru vya Wafanyakazi kwa kutoa mafunzo kwa wakurufunzi wake na kufanya tafiti mbalimbali hapa nchini.

- Imeunda Kamati ya kupambana na UKIMWI na kuendesha mafunzo maalum ya malezi na nasaha *(Guidance and Counselling)* kwa wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi na wafanyakazi.

- Imeongeza kipengere katika kanuni za Utumishi *(Service Regulations)* kuhusu udhibiti wa vitendo vya utoaji na upokeaji rushwa.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo iliyojiwekea, Taasisi katika mwaka 2004/2005 inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendeleza upanuzi na uboreshaji miundo mbinu (madarasa, maktaba na ofisi za waalimu) ili kuongeza uwezo wa kuanzisha kozi na programu mpya.

- Kuanzisha Stashahada ya Uzamili ya Sheria ya Usuluhishi na Uamuzi *(Post Gradute Diploma in Mediation and Arbitration)* katika fani ya Uongozi Kazi ili kuwawezesha wahitimu kuyamudu mazingira ya utekelezaji wa Sheria Mpya za Kazi na Ajira kwa kuwapa mbinu mpya na za kisasa za kushughulikia masuala ya kazi.

- Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali yakiwamo ya kompyuta, malezi, nasaha na kadhalika.

- Kuimarisha usalama na mandhari ya eneo la Chuo kwa kujenga uzio imara kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia na kuratibu shughuli za kuboresha tija kupitia Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Shirika lilitekeleza yafuatayo:-

- Liliendesha mafunzo yote 60 yaliyopangwa kuendeshwa ambayo yalihudhuriwa na washiriki 710 kati ya 900 waliotegemewa.

- Lilitoa huduma ya ushauri katika fani za miundo ya shirika, mifumo ya utumishi, mifumo ya mishahara, kanuni za utumishi, usaili na miundo ya mashirika kwa wateja watano kati ya sita waliotegemewa.

- Lilitoa huduma ya utafiti kwa Taasisi moja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Shirika la Tija la Taifa litatekeleza yafuatayo:-

- Litaendesha mafunzo 80 ya mbinu za maarifa ya kuboresha tija mahala pa kazi ambayo yanategemewa kuhudhuriwa na washiriki 960.

- Litaendelea kuwaelimisha washiriki juu ya mbinu za kupambana na janga la Ukimwi.

- Linategemea kutoa huduma za uelekezi kwa wateja 10.

- Linategemea kuanza kuimarisha shughuli za utafiti wa tija kwa kutekeleza Mpango wa Taifa wa kuboresha na kusimamia Tija katika sekta za viwanda, huduma, kilimo na huduma ya umma kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato wakati likisubiri kupata msaada kutoka Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*.

- Litaendelea kufanya utafiti kuhusiana na madhara ya janga la Ukimwi kwenye tija, sehemu za kazi na athari za rushwa kwenye utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi iliendelea kupunguza migogoro ya miaka ya nyuma kwa kuongeza kasi ya utoaji wa maamuzi ya migogoro inayowasilishwa Mahakamani. Msukumo mkubwa unalenga kumaliza migogoro kati ya miezi sita na ndani ya mwaka mmoja pindi migogoro inapofunguliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Mahakama ya Kazi ilitekeleza yafutayo:-

- Ilitolea maamuzi Migogoro ya Kikazi 144 kama ifuatavyo: Migogoro ya kikazi nane kati ya 21 iliyokuwepo, migogoro ya Uchunguzi 68 kati ya 142 , Mikataba ya Hiari 35 ilisajiliwa kati ya 55 iliyokuwepo, maombi ya Marejeo 32 yalitolewa Uamuzi kati ya 60 iliyokuwepo na ombi la Ushauri moja lililetwa na Ushauri ulitolewa.

- Ilisogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kuongeza idadi ya Vikao vya Mikoani kama ifuatavyo: Mbeya vikao vinne, Morogoro vikao vitatu, Mwanza vikao vitatu, Dodoma kikao kimoja na Tanga kikao kimoja, na kwa sasa Kanda ya Arusha imepata Naibu Mwenyekiti Mkazi. Pia juhudu zimefanyika kupata jengo la Mahakama katika Mkoa wa Mwanza.

- Iliandaa Semina kwa ajili ya kuelimisha wafanyakazi kuhusu Sheria mpya ya Utumishi wa Umma *(Public Service Act)* na mabadiliko mbalimbali yanayoambatana nayo ikiwemo upimaji na utendaji kazi kwa utumishi kwa uwazi *(Open Performance Review Appraisal System - OPRAS),* Maadili ya Kazi *(ethics)* na mapambano dhidi ya maambukizi ya Ukimwi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2004/2005 Mahakama ya Kazi itatekeleza yafuatayo:-

- Itaimarisha utendaji utakozingatia muda na ubora katika maamuzi ya Mahakama katika kutoa haki kwa lengo la kuboresha na kukuza tija sehemu za kazi.

- Itawaelimisha wadau wa Mahakama misingi na umuhimu wa mahusiano ya kisheria na haki katika uzalishaji wenye tija sehemu za kazi.

- Itajenga uwezo wa mahakama ili ifanye kazi zake kwa ufanisi.

- Itaimarisha, kuendeleza na kulinda mahusiano na haki sehemu za kazi kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazofanana za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Sheria za kazi zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu hivi karibuni, Mahakama hii sasa itafanya kazi chini ya Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi ina majukumu mbalimbali yakiwemo majukumu makubwa ya kuajiri, kusimamia utendaji kazi, kutoa mafunzo ya utendaji kazi, kupambana na rushwa na ugonjwa hatari wa Ukimwi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na Kitengo cha Utawala Bora Ofisi ya Rais - Ikulu iliandaa Warsha ya kukusanya maoni ya vyama mbalimbali vya michezo nchini ili kuboresha maadili, kupambana rushwa na kusisitiza Utawala bora katika vyama vya michezo. Maoni ya Wadau yamepatikana na sasa yanafanyiwa kazi na Serikali.

- Ilikamilisha programu ya mafunzo kwa watumishi wake 1,220 na sasa inatafuta fedha ili kuweza kukidhi gharama za mafunzo hayo.

- Iliajiri Watumishi wapya 20 wa Idara ya kazi ili kupunguza mlundikano wa kesi nyingi za masuala ya kazi, Watumishi watatu kwa Idara ya Michezo na wengine watatu kwa Idara ya Maendeleo ya Vijana.

- Imeanza zoezi la kuandaa mikataba ya kazi kwa watumishi wake 1,220 na kuanzishwa kwa Kamati ya Ajira ndani ya Wizara, hii ni katika kutekeleza programu ya kuboresha Utumishi wa Umma inayolenga katika kuongeza ufanisi katika kazi kwa Watumishi wa Serikali.

- Ilitoa elimu ya mbinu za maisha kuhusu Ukimwi kwa watumishi 915 wa Wizara na kazi bado inaendelea kwa watumishi wengine.

- Kwa kushirikiana na Chuo cha *Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI)* Watumishi wapatao 235 wa Wizara wamepata mafunzo ya *(Open Performance Review Appraisal System - OPRAS).*

- Iliandaa na kuendesha Vikao vya Baraza la Wafanyakazi.
-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuboresha utendaji kazi, kutoa mafunzo mbalimbali, kudumisha maadili ya utumishi na kuboresha mfumo wa menejimenti na utoaji huduma bora. Katika mwaka 2004/2005 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Itaandaa utekelezaji wa kuanzishwa kwa kamati za ajira za Wizara zitakazohusika na ajira, kuthibitishwa kazini, upandishwaji vyeo na nidhamu ndani ya Wizara.

- Kupitia, kurekebisha na kuboresha mikakati ya utekelezaji wa kazi za Wizara *(Strategic Plan)* ili kuboresha utendaji na usimamizi wa kazi ndani ya Wizara.

- Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu ya mabadiliko ya utendaji kazi ndani ya Wizara na *Open Performance Review Appraisal System,* kwa watumishi ambao bado hawajapata mafunzo haya.

- Kuandaa na kusimamia vikao vya Baraza la Wafanyakazi.

- Kuandaa na kusimamia shughuli za kupambana na ugonjwa hatari wa Ukimwi kwa watumishi na vile vile itaendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na rushwa.

- Wizara ipo katika mchakato wa kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma kwa umma.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotolewa na Wizara yangu zinamgusa kila mwananchi kwa njia moja au nyingine. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa michango yao mbalimbali ya mawazo na ushauri walioutoa ndani na nje ya Bunge hili kwa Wizara yangu kwa nia ya kuboresha huduma tunazotoa. Wizara iko tayari kuyapokea na kuyafanyia kazi mapendekezo, ushauri na maoni watakayoendelea kuyatoa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusaidiana katika kuboresha huduma hizi muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda pia nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Naibu wa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa msaada na ushauri wake wa karibu. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bwana Abubakar M. Rajabu, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Bodi zao, ambao wameshirikina na Wizara katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru washiriki wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa njia ya pekee naomba niitaje Kamati Maalumu ya kurekebisha Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Jaji John Mrosso, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya ya kurekebisha Sheria za Kazi na Ajira, Bodi ya Ushauri wa Kazi *(Labour*

*Advisory Board),* Bodi ya Ushauri ya Wizara *(Ministerial Advisory Board)*, Shirikisho la Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA),* kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kutambua michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yetu. Kwa kuwa siwezi kuwataja wahisani wote, kwa uchache naomba Shukrani za dhati ziende kwa Serikali za nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, Japan, China, Sweden, Canada, Ujerumani, Finland na Korea ya Kusini, *ILO, UNDP, UNICEF, FES, SHIA, ADB, ADF, OPEC. ABBORT Phamacetical and Laboratories, AXIOS, SIDE by SIDE, JICA* na Mashirika na makampuni ya hapa nyumbani ambayo ni *EOTF, TACAIDS, TTCL, TBL, OILCOM, VODACOM,* Mpango wa Taifa wa kuthibiti Ukimwi *(NACP), African Youth Alliance (AYA), Kahama Mines* na *Kagera Sugar. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2004/2005/= naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.61,113,986,200/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo chini ya Fungu 65.

Aidha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha Sh.765,305,900/= chini ya Fungu 60 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wasemaji wa mwanzo mwanzo katika hoja hii atakuwa ni Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Aziza Ali, wajiandae. Sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, atoe taarifa ya Kamati hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Na.60 na 65 ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka 2003/2004, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2004/2005 ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu, kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Wabunge wafuatao kwa kufiwa na wapendwa wao: Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi. Vilevile Mheshimiwa Omar Juma Omar, kwa kufiwa na baba yake mzazi. Mheshimiwa Parmukh Sigh Hoogan na Mheshimiwa Dr. Laurence Gama, kwa kufiwa na watoto wao.

Naomba kutoa salamu za rambirambi za dhati kabisa kwa familia za Marehemu waliokuwa Waheshimiwa Wabunge, ambao kwa ghafla wametutoka katika kipindi hiki kifupi cha Mkutano huu wa Bunge la Bajeti linaloendelea. Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, aliyefariki tarehe 24 Juni, 2004 hapa Dodoma na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, aliyefariki tarehe 22 Julai, 2004 naye hapa hapa Dodoma. Vifo vyao ni msiba mkubwa kwa Bunge letu Tukufu na kwa Wananchi wa Majimbo waliyokuwa wakiyawakilisha. Mungu aziweke pema roho za Marehemu hawa mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2003/2004, pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao katika kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Janeth Mashelle, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ramadhan Nyonje Pandu, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Bakari M. Mbonde na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea maelezo ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2003/2004, pamoja na Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo tarehe 25 - 26 Mei, 2004, Mjini Dar es Salaam. Mambo yaliyojadiliwa katika taarifa hiyo ni pamoja na Dira ya Wizara, Majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, mapato na matumizi kwa kipindi kilichopita 2003/2004, mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji, kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2004/2005 na maombi ya fedha kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2003/2004, Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji uliofanywa na Wizara. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado kuna matatizo katika kumaliza kwa haraka kesi za watoto watukutu waliopo Mahabusu na hii inatokana na kutokuwepo kwa Mahakama za watoto pamoja na upungufu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la Watumishi, Kamati imeona kuwa bado kuna tatizo la upungufu wa Watumishi hasa katika Mahakama ya Kazi na Walimu katika vyuo vya watu wenye ulemavu na upungufu huu unasababisha Watumishi waliopo kutokufanya kazi kwa ufanisi unaostahili.

Pamoja na Serikali kutenga maeneo kwa ajili ya michezo, bado kuna tatizo la viwanja hivi kuvamiwa na wakaaji wa maeneo husika.

Kuhusu migogoro ndani ya Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania *(FAT),* Kamati imeona kuwa bado lipo tatizo kubwa kwani baada ya Wajumbe wa Kamati ya Utendaji kusimamishwa, baadaye wamerudishwa Viongozi wale wale bila kuwepo na badiliko lolote.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati yangu kupata maelezo na kupitia mapendekezo ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara. Lakini hata hivyo, Kamati imesikitishwa sana tena sana na kiasi cha Sh.204,568,100/= kilichotengwa kwa ajili ya kugharamia chakula cha makazi 17 ya wazee na wagonjwa wa ukoma yenye watu 3,650. Kiasi hicho hicho kinategemewa kitumike kuwahudumia watoto yatima 120 kutoka Makao ya Watoto Yatima Kurasini, Mahabusu 435, kutoka Mahabusu tano za watoto na watoto 230 kutoka Shule ya Maadilisho ya Irambo. Kamati inashauri kiasi hicho cha fedha kiongezwe ili kiweze kuwakimu, kwani bajeti hiyo kila mtu mmoja katika makundi haya ametengewa kiasi cha Sh.126 tu kwa siku, kiasi ambacho kinasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza Shule ya Mafunzo na Mahabusu ya Watoto ili Watoto wasichanganywe na watu wazima Gerezani, kwani kwa sasa kuna Shule ya Mafunzo moja tu ya wavulana pekee na kuna Mahabusu za Watoto tano kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mlundikano wa kesi za watoto watukutu walioko Mahabusu, ambazo zimekuwa zikichukua muda mrefu hadi kumalizika, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha Mahakama ya Watoto itakayoshughulikia kesi hizo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuvihudumia Vyuo vya watu wenye ulemavu ni kubwa na inahitaji kuwepo na vifaa vya kutosha na Walimu wenye taaluma maalum katika kuwahudumia watu wenye ulemavu. Hata hivyo, juhudi za kuvihudumia Vyuo

hivi zinakwamishwa na upungufu wa vitendea kazi na ukosefu wa Walimu wenye taaluma hii. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: Kununua vifaa muhimu na vya kutosha kwa ajili ya kuwahudumia wanafunzi katika Vyuo hivi, kuona uwezekano wa kuwaajiri Walimu na Watumishi wengine wenye taaluma maalum katika kuhudumia watu wenye ulemavu na kutokana na ugumu wa kazi inayofanywa na Watumishi wanaowahudumia watu wenye ulemavu, Serikali ione uwezekano wa kuwalipa watumishi hawa malipo maalum *(Special Payments). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa juhudi zake, lakini vilevile tunatoa wito waendelee na juhusi zaidi ili wasigeuke mgema akisifiwa, tembo hulitia maji. Halikadhalika, Kamati inalipongeza Shirika hili kwa kuwa mshindi wa kwanza katika Maonesho ya Saba Saba ya mwaka huu wa 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini mafanikio yafuatayo katika Shirika hili la Hifadhi ya Jamii:-

(i) Thamani ya Mfuko imeongezeka kutoka Shilingi milioni 239.37 hadi kufikia Juni, 2002 na kufikia Shilingi bilioni 287.88 hapo Juni, 2003. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 20.24.

(ii) Shirika limefanikiwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa eneo la Kinyerezi Dar es Salaam.

(iii) Jengo la *NSSF Water Front* limekamilika na kukabidhiwa rasmi kwa Shirika hilo kutoka kwa Kandarasi.

(iv) Mahesabu ya Shirika yanakamilishwa kila mwaka bila kuchelewa. Mahesabu ya mwisho ambayo yamekwisha kaguliwa ni ya mwaka 2002/2003 na yana hati safi ya ukaguzi.

(v) Shirika limeendelea kutoa mafao kwa wanachama wanaostahili chini ya Sheria na taratibu zilizowekwa na Sheria. Mafao ya matibabu yanatarajiwa kuanza kutolewa ifikapo mwezi Oktoba, 2004

Mheshimiwa Spika, penye mafanikio hapakosi matatizo, yafuatayo yamejitokeza:-

(i) Ulipaji wa kodi ya mapato ambayo hupunguza uwezo wa Shirika kulipa mafao bora zaidi kwa Wanachama, nchi nyingi duniani hazitozi kodi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuipa uwezo wa kutimiza jukumu la kutoa mafao bora zaidi hasa kwa wastaafu ambao idadi yao inaongezeka mwaka hadi mwaka.

(ii) Baadhi ya Waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa wakati au kwa viwango vinavyostahili.

(iii) Upatikanaji wa hati za kumiliki ardhi kwa viwanja vya vitenga uchumi na Maofisi unaendelea kuwa mgumu. Aidha, ubadilishaji wa majina kwenye hati za viwanja vilivyonunuliwa na Shirika hilo bado una matatizo.

(iv) Kutokuwepo kwa ushindani ulio sawa kati ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* kwani *PPF* wanaruhusiwa kuandikisha wanachama kwenye Sekta Binafsi wakati *NSSF* hawaruhusiwi kuandikisha wanachama kutoka Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA).* Hata hivyo, kutokana na utaratibu wenye mlolongo mrefu katika kununua mali ghafi kwa ajili ya kutengenezea Bidhaa, *VETA* inalazimika kuuza vitu kwa bei za juu sana na hivyo kutokupata wateja wa kutosha. Kamati inaishauri Serikali kuziruhusu Taasisi za Umma ndogondogo kama *VETA* kununua vitu (malighafi) kutoka *sources* kama walivyoruhusiwa Wakuu wa Shule za Sekondari ili kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kupunguza bei za bidhaa zinazotengenezwa. Kamati inaipongeza *VETA,* kwa kujenga Chuo Mkoani Kigoma kwa kuzingatia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Vijana, Ilonga - Kilosa, kwa muda mrefu sasa hakina wanafunzi pamoja na kwamba wapo Walimu ambao wanalipwa mishahara bila kufanya kazi yoyote, kutokana na kutokufanya kazi kwa Chuo hiki, majengo yake yameendelea kuchakaa siku hadi siku. Ili kukinusuru Chuo na fedha ya Serikali inayolipwa kwa walimu ambao hawafanyi kazi yoyote. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kufanya juhudi za makusudi kukamilisha ukarabati wa Chuo ili kianze kuchukua wanafunzi mara moja. Aidha, kama Wizara ya Kazi imeshindwa kukiendesha basi, iridhie kichukuliwe na Halmashauri ili kitumike kama Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imesikitishwa sana tena sana na baadhi ya watu kuvamia maeneo yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya michezo. Hivyo, inapenda kushauri kuwa, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, wawe mstari wa mbele katika kuona kwamba, viwanja hivyo havivamiwi. Wabunge kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya, wawachukulie hatua za kisheria wavamizi wa viwanja hivi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu Uongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT).* Kutokana na ushauri wa Kamati hii, Kamati ya Utendaji ya *FAT* ilisimamishwa na kuchagua Viongozi wa muda. Kinachosikitisha ni kwamba, baada ya uchaguzi kufanyika, wamerudishwa Viongozi wale wale na hivyo kuzidi kuwakatisha tamaa Wananchi juu ya matumaini yao kuhusu mpira wa miguu Tanzania. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kuona kuwa Katiba mpya ya *FAT* inakidhi matarajio mema ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Dr. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa kujenga uwanja wa kisasa wa michezo ambao kwa hakika utachochea ari ya michezo

kwa Watanzania wote wapenda michezo na kurudisha heshima ya michezo kwa Taifa letu. Aidha, Kamati inawasiwasi na mchakato mzima wa ujenzi ambao unaenda taratibu sana na huenda ahadi ya kuukamilisha ujenzi huu kabla ya Mheshimiwa Rais kumaliza muda wake wa kuwepo madarakani, isitekelezeke.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni na mapendekezo ya Kamati, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, inayakubali mapendekezo ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Fungu Na. 60 na 65 kama ifuatavyo:-

Fungu 60: Matumizi ya kawaida Sh.513,490,900/=, Miradi ya Maendeleo Sh. 251,815,000/=, Jumla Sh. 765,305,900/=.

Fungu 65: Matumizi ya Kawaida Sh. 5,795,175,200/=, Miradi ya Maendeleo Sh. 55,338,811,000/=, Jumla Sh. 61,113,986,200/=.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru wewe tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Napenda nimshukuru Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu wa Wizara, Bw. Abubakar Rajabu, pamoja na Maafisa wote wa Wizara na Wakurugenzi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano wao katika kuiandaa Bajeti yao na kutoa maelezo mbele ya Kamati pale walipohitajika kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao katika kuichambua bajeti ya Wizara na kutoa maoni yao. Aidha, napenda nimshukuru Katibu wa Bunge Bw. Kipenka Mussa, kwa ushirikiano alioutoa kwenye Kamati hii kila tulipohitaji ushauri wake. *(Makofi)*

Mwisho, napenda nimshukuru Katibu wetu wa Kamati, Bibi Angelina L. Sanga, kwa kuihudumia Kamati hii kwa makini pamoja na kuandaa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nawashukuru Wabunge wote, kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nina kikao kingine cha Tume ya Kurekebisha Sheria, kwa hiyo, kabla hajaitwa Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, anipokee Kiti na ataendelea mpaka jioni.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia kukutana hapa ndani ya Bunge hili Tukufu na kufanya wajibu wetu tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa mwaka wa 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b) na (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa niaba ya Wapigakura wa Jimbo la Mtambwe, napenda kutoa pole kwa familia na Wapigakura wote wa Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu, awalaze mahala pema. Kadhalika Mwenyezi Mungu awape ustahamilivu Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote, waliofiwa na wapendwa wazazi wao na watoto zao hivi karibuni.

Sio vyema kuwasahau pia Waheshimiwa Wabunge, ambao wamewahi kupata misukosuko mbalimbali kama ya kupata ajali njiani wakija hapa Dodoma kwenye Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba, sitawatendea haki kama sitawataja na kuwashukuru, Mheshiniwa Alhaj Prof. Juma Athumani Kapuya, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Naibu wake, Mheshimiwa Mudhihiri Mudhihir, Katibu Mkuu wao, Bwana Abubakar Rajab, kwa ushirikiano mkubwa ambao mara kwa mara hunipatia katika kutekeleza wajibu wangu. Nawaomba wasichoke kuniwekea wazi milango ya Ofisi zao ili isiwe tabu kwangu, kuingia kwa mashauriano kwa maslahi ya Taifa letu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, pamoja shughuli nyingine, ina majukumu makubwa matatu. Inashughulika na mambo ya kazi, maendeleo ya vijana ambao ni wengi na Wadau muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa hili. Kadhalika Michezo ambayo ina nafasi kubwa katika maisha na furaha za Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa Nchini hasa kwa Vijana wanaohitimu Elimu ya Msingi, Sekondari, vyuo mbalimbali hata Chuo Kikuu. Inakadiriwa kuwa zaidi ya Watanzania 700,000 huingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Wakati Sekta Rasmi huajiri takriban Watanzania 30,000 kwa mwaka. Hali hii imepelekea Watanzania wengi kutegemea sekta isiyo rasmi ambayo pia iko katika hali mbaya. Miongoni mwa matatizo yanayoikabili sekta hii ni ukosefu wa mitaji, elimu duni ya ujasiriamali, miundombinu hafifu hasa Vijijini, ufinyu wa soko la ndani na kadhalika. Aidha, masharti magumu na riba kubwa ni kikwazo kwa Wananchi kujipatia mikopo katika benki nyingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha ukosefu wa ajira kimekuwa kikiongezeka miaka hadi miaka licha ya ubinafsishaji kudaiwa kuwa umeongeza nafasi za ajira. *Overall unemployment rate* Tanzania inakisiwa kufikia wastani 13%. Hata hivyo, hali ni mbaya zaidi Mijini ambako *unemployment rate* ni 31.6% kama ilivyobainika kwenye *Labour Force Survey 2000/2001* na hakuna dalili za kupungua kwa hali hii.

Aidha, hali ya ukosefu wa ajira inachangiwa na ukosefu wa sera madhubuti na Mikakati ya Kitaifa inayolenga kuanzisha ajira *(Clear National Policies and Programme on Employment Creation).* Hivyo basi, ipo haja ya kuwawezesha Watanzania kujiajiri kwa kuhakikisha wanapata mikopo inayokidhi mahitaji ya biashara kwa masharti na riba nafuu. Aidha, miundombinu iboreshwe hadi Vijijini. Elimu ya ujasiriamali sharti sasa iingizwe kwenye mitaala ya elimu kuanzia Shule ya Msingi hadi Chuo Kikuu kama ilivyoainishwa kwenye *National Policy on Small and Medium Enterprises.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji, maslahi ya Wafanyakazi wa kawaida yamedhulumiwa. Miongoni mwa uvunjaji wa haki za Wafanyakazi ni pamoja na kufanya kazi muda mrefu, kufanya kazi kwa lazima muda wa ziada na kuzuiliwa kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi. Mahali pengine tafiti zimeonyesha kuwa, Waajiri binafsi huwalazimisha wafanyakazi kufanya kazi saa 14 bila malipo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, aidha, kumekuwa na tabia ya wawekezaji kutoka nje ya nchi kubagua Wafanyakazi katika malipo kati ya Watanzania na Wageni, hata pale wanapokuwa na kiwango sawa cha elimu na wanashikilia *Post* inayofanana. Utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ulibaini kuwa, Mfanyakazi kutoka Afrika ya Kusini anayefanya kazi katika Makampuni ya Afrika ya Kusini yaliyopo Tanzania, analipwa Dola tano hadi saba za Marekani kwa saa wakati Mtanzania analipwa chini ya Dola mbili za Marekani.

Ipo haja ya kutoa Elimu ya Sheria za Haki za Wafanyakazi kwa Waajiri na Waajiriwa. Vilevile kuboresha utendaji wa Mahakama ya Kazi ikiwa ni pamoja na Watumishi wa kutosha na kusogeza huduma za Mahakama hii kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makubwa ya *NSSF* ni pamoja na kuandikisha Wanachama kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, kukusanya michango ya Wanachama na kulipa mafao kwa Wanachama; kuwekeza mafao ya Wanachama kwenye vitega uchumi mbalimbali ili kuboresha mafao ya Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji Wakuu wa *NSSF* ni Wafanyakazi wa kawaida, ikiwa ni pamoja na kundi kubwa la Wafanyakazi wa ngazi za chini. Pamoja na mafanikio hayo makubwa ya Shirika hili, lakini Shirika limewasahau sana wachangiaji wake sahihi na matokeo yake wanaofaidi zaidi huduma zake sio wale wanaolibeba kikwelikweli Shirika hili kupitia michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado *NSSF* haijaweza kuwa Shirika lenye manufaa makubwa kwa Watanzania wa daraja la chini. Vitega Uchumi vyake kama ujenzi wa nyumba za kuishi, umewapa manufaa zaidi watu wa daraja la juu na daraja la kati. Hakuna mlalahoi wa kikwelikweli anayeweza akanununua kile kinachodaiwa kuwa ni nyumba za bei nafuu, kwa mfano, zile za eneo la Kinyerezi kule Dar es Salaam. Nyumba hizo kimsingi zina bei kubwa sana na Mfanyakazi wa kawaida wa ngazi ya chini wala hawezi kuota kuzipata! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri *NSSF* ilinde na kuboresha maslahi ya Wanachama wake kwanza kupitia vitega uchumi vyake. *NSSF* ni Shirika la Wananchi kwa manufaa yao na ni lazima lisaidie kuondoa umaskini, hasa kwa kuhakikisha watu maskini wanapata makazi bora na kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la umaskini, kuna kundi kubwa la vijana ambalo halina ajira ya uhakika na limejiingiza katika matumizi mabaya ya madawa ya kulevya, ujambazi, ukibaka, utapeli na ukahaba. Vijana wasio na ajira daima wana njaa na kila mwenye njaa anao uwezekano wa kuwa na hasira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lisipuuze matatizo ya vijana kwa sababu hatari yake kwa Taifa ni kubwa sana. Matatizo ya vijana yashughulikiwe kisayansi na siyo kijazba. Taarifa za Viongozi wengi za kuendesha operesheni za kufukuzana na Vijana mitaani na mabarabarani, hasa wale wanaoitwa "Wamachinga", Jijini Dar es Salaam, hazina msaada wowote wa maana katika kumaliza tatizo, zaidi ya kuahirisha na kukuza zaidi tatizo. Serikali itafiti kujua vyanzo sahihi vya matatizo ya vijana badala ya kutumia misuli na maguvu kuwakamata vijana mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya *VETA* vinaendelea kuleta ukombozi mkubwa miongoni mwa vijana wetu, pamoja na majukumu yake mengi, pia kuratibu, kusimamia na kutoa mafunzo ya ufundi stadi nchini, kutoa mafunzo katika stadi mbalimbali yanayochangia kuleta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* ni mdau muhimu katika kufanikisha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. Kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha *VETA* na ni jambo la msingi kupunguza utegemezi wake kwa Wafadhili wa nje. Serikali iiunge mkono *VETA* kwa ruzuku na kadhalika, lakini *VETA* nayo iendelee kujenga uwezo wa kujitegemea. Jukumu la kuwaendeleza vijana wa Tanzania ni la Watanzania wenyewe na Serikali isikwepe kwa namna yoyote ile jukumu hilo. Mtandao wa Kitaasisi unaohusisha *SIDO, VETA, CAMARTEC, DIT, Prospective College of Engineering, TIRDO, TEMDO* na *TATC* chini ya mwamvuli wa *COSTECH* umebeba siri ya mafanikio ya kisayansi na kiteknolojia ya Tanzania. Ushirikiano wa Taasisi hizo za utafiti na uendelezaji bidhaa ni mwanzo mzuri kabisa wa kuwa na maendeleo ya kiviwanda. Viwanda vinavyozalisha kwa ufanisi ni chanzo cha ajira kwa Wananchi na hasa vijana, mapato kwa Serikali na upatikanaji wa bidhaa bora na huduma bora kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kudaiwa mbio za mwenge ni kwa ajli ya kuhamasisha miradi ya maendeleo na kusambaza ujumbe wa kapambana na Ukimwi,

bado Wananchi wengi hasa vijijini hawatofautishi "Mwenge wa Serikali" chini ya mfumo wa Vyama Vingi na "Mwenge wa CCM " chini ya Mfumo wa Chama Kimoja, pia kuna mawazo ya Watanzania wengi ambayo hayapaswi kupuuzwa kwamba, mwenge umeficha ajenda ya kisiasa ambayo ina manufaa makubwa na CCM. Mwenge bado ni kifaa cha kuendeshea propaganda za kisiasa, kufanyaia kampeni za kisiasa na wakati fulani kuhujumu demokrasia kwa kuukejeli Upinzani kupitia vijembe vinavyoambatana na mbio za mwenge. Umuhimu mzima wa mbio za mwenge ni lazima uangaliwe upya kupitia mjadala wa Kitaifa. Wananchi waamue kama kweli wanaona bado Tanzania inahitaji kuwa na mbio za mwenge au laa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa lolote ulimwenguni. Mchango huu huonekana pale michezo inapoendelezwa na kutazamwa kama taaluma au ajira na chanzo cha mapato kwa Taifa. Kwa mfano, wachezaji maarufu wamekuwa wakiwekeza katika nyanja mbalimbali za jamii na uchumi. Tunayo mifano hai hata kwa wenzetu wa Nigeria, Mchezaji wa Kimataifa wa Nigeria Nwanko Kanu, amejenga hospitali kadhaa za magonjwa ya moyo nchini Nigeria, Dekembe Mutombo, raia wa *DRC,* anayecheza mpira wa kikapu nchini Marekani, ameanzisha Shirika la kusaidia afya na elimu na amejenga Hospitali kubwa nchini humo iitwayo *Mutombo Hospital.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ikifanya vibaya katika baadhi ya michezo mbalimbali hasa soka katika medani ya Kimataifa. Hali hii imepelekea Watanzania kupoteza matumaini katika michezo na ni dhahiri Watanzania wanapenda kushabikia Timu za Nje ya Nchi kuliko Timu zao, hii ni hatari. Timu ya Taifa ni sawa na haipo na klabu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na zile kubwa na zenye historia ndefu kama Yanga na Simba, zimeendelea kuonyesha kandanda ya hali ya chini sana. Klabu zimeendelea kuboronga kwenye mechi za Kimataifa. Migogoro imeendelea kutamba katika klabu mbalimbali na timu kama Yanga sasa hakuna tena shughuli za mpira isipokuwa mizozo na migogoro na malumbano yasiyoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali nayo imeonekana kuwa na maamuzi ya kuyumbayumba na kubabaika, hasa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na hata kauli na maamuzi ya Waziri mhusika. Sote tulishuhudia namna suala dogo la wachezaji wa klabu za Yanga na Simba kukiuka sheria za usajili lilivyomyumbisha Mheshimiwa Waziri na kumpotezea muda mwingi. Ni lazima maamuzi ya Mheshimiwa Waziri, yatokane na taarifa za kutosha na sahihi ili aepuke tatizo la leo anaamua hivi, kesho vile na keshokutwa analeta lingine na mtondogoo anarudi kwa alilolikataa juzi. Katika mambo haya ya kusimamia haki katika utatuzi wa migogoro michezoni, ni vizuri mtu kama Mheshimiwa Waziri, akaepuka kabisa kuonekana anayo maslahi fulani na upande fulani *(partisanism).* Yeye ni lazima awe huru kabisa *(neutrality or impartiality)* ili aaminike na aheshimike na pande zote husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuinua michezo Tanzania, tunahitaji kutambua matatizo yanayoikabili sekta hiyo:-

(i) Ukosefu wa mikakati endelevu inayotekelezeka na kuboresha michezo licha ya kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Michezo. Kwa mfano, hakuna vyombo madhubuti vinavyowaandaa vijana kuwa wachezaji wazuri tangu wakiwa na umri mdogo *(Sports Academy)*.

(ii) Ufinyu wa bajeti na matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya michezo.

(iii) Migogoro ya mara kwa mara ndani ya Vyama vya Michezo nchini kama vile *FAT,* migogoro ndani ya vilabu na kadhalika. Migogoro hii inatokana na ubinafsi wa Viongozi wenye nia ya kujinufaisha na siyo kuendeleza michezo kwa manufaa ya Watanzania. Mfano mzuri ni migogoro ya kudumu ndani ya *FAT*.

Aidha, migogoro ya *FAT* inachangiwa pia na tatizo la Kikatiba. Ipo haja ya kuhakikisha Katiba mpya ya *FAT* ambayo rasimu yake iliyo katika lugha ya Kiingereza, itakayojadiliwa tarehe 13 Agosti, 2004, ishirikishe wadau mbalimbali. Aidha, ni vyema rasimu hiyo iandikwe pia kwa lugha ya Kiswahili na kutolewa kabla ya tarehe 13 Agosti, 2004, ili wadau wa michezo waweze kushiriki kikamilifu katika kupata Katiba mpya ya *FAT* inayotoa mwelekeo wa kuendeleza soka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila sababu ya kuendesha klabu zetu kisayansi zaidi. Wizara na Chama cha Mpira *(FAT)* wafanye juhudi kutengeneza mazingira ya kuwepo kwa soka ya kulipwa katika Tanzania. Kila inapowezekana klabu ziwe makampuni, ziuze hisa na zikae mkao wa kibiashara zaidi. Wachezaji wauzwe na kununuliwa katika soko huru la soka, matajiri washawishiwe kuwekeza katika soka na ikiwezekana wamiliki klabu zao kibiashara. Klabu zijenge viwanja vya kisasa na viwanja hivyo viendeshwe kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni mbalimbali yameanza kujitokeza kudhamini klabu fulani fulani na hata kudhamini ligi kuu. Tatizo linaloonekana wazi ni udhamini wa kubangaiza na usiosaidia sana ustawi wa wachezaji na maendeleo ya klabu na soko kwa ujumla. Ni ajabu kuona timu kubwa yenye wadhamini wanne wenye majina makubwa haiwezi ikamudu kumpa kila mchezaji angalau mshahara wa shilingi za Kitanzania laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wadhamini wanatamba kuzidhamini klabu fulani kwa mamilioni lakini wachezaji njaa inazidi kuwa kali na wanaishi kwa vijiposho vya kubabaisha na hisani za watu fulani fulani. Anayedhamini basi na adhamini kikwelikweli na siyo kufurahia tu kutangaziwa bidhaa zake na jezi za wachezaji halafu timu inasafiri kwa basi bovu kutoka Dar es Salaam hadi Kigali-Rwanda na inatoka tena Kigali hadi Dodoma kwa usafiri wa barabara na kwa shida nyingi sana! Matajiri wasifaidi tu katika biashara zao kwa kutumia majina ya klabu kubwa kama Yanga na Simba na halafu wachezaji wa timu hizo wanapiga miayo kwa njaa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), kutakiwa kukabidhi viwanja kadhaa vya michezo Serikalini. CCM

imeng'anga'ania kwamba, viwanja kama Kirumba kule Mwanza, Jamhuri Mjini Dodoma, Sokoine kule Mbeya, Majimaji kule Songea na kadhalika, eti ni vya kwake! Viwanja vyote hivyo ni vya Watanzania wote na walivijenga kwa kodi zao na hata nguvu zao za moja kwa moja, pia fedha zao kupitia michango yao mbalimbali enzi zile za Chama kimoja. Viwanja hivyo havina matunzo wala uangalizi wa uhakika na vimechakaa vikiwa vinahitaji matengenezo makubwa. CCM ione busara ya kuvirudisha Serikalini viwanja hivyo ili angalau vifanyiwe matengenezo na viwe na menejimenti ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuhusu ujenzi wa uwanja mpya na wa kisasa wa Taifa, Watanzania wanataka uanze kujengwa na si lazima sana uwanja huo eti umalizike kabla ya Mheshimiwa Rais Mkapa, kutoka madarakani na si lazima kila kitu sasa kiitegemee Serikali ya China kama vile nchi hii haikusanyi mabilioni ya fedha za kodi kila mwezi. Kutokana na kuchelewa sana kuanza kujenga uwanja huo na wakati huo huo kuwepo kwa shinikizo la uwanja kuzinduliwa kabla ya Mheshimiwa Rais Mkapa, kumaliza muda wake, ipo hatari ya uwanja huo kujengwa mbiombio na kwa uchapuchapu wa aina yake na kwa hali hiyo ubora wa kiujenzi kukosekana. Ujenzi mzima wa uwanja mpya wa Taifa uongozwe na busara za kiuchumi na utulivu wa kimaamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo wa Netiboli unaendelea kuzorota na zinahitajika juhudi kubwa kuurudisha kwenye chati mchezo huo. Pamoja na akina dada kuanza kuvutiwa na soka na sote tunafurahishwa na akina dada wa Timu ya Taifa ya Wanawake *(Twiga Stars),* akina mama wote nchini, ikiwa ni pamoja na Wabunge Wanawake, wawe mstari wa mbele kurejesha mvuto wa mchezo wa netiboli lakini hawazuiwi kuunga mkono soka inayochezwa na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzorota sana na hata kufa kwa mashindano ya michezo mbalimbali katika shule za sekondari na zile za msingi, kumetibua sana maendeleo ya michezo katika Taifa letu. Mwanzo wa klabu imara na timu imara za Taifa ni malezi mazuri ya kimichezo miongoni mwa watoto tangu shule za awali, shule za msingi shule za sekondari na hata vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni uchumi katika nchi nyingi duniani na ni muhimu Taifa letu liwekeze katika michezo kabla ya kuwazia kuvuna. Suala lisiwe sisi na viongozi wetu kushindana tu kuipongeza Afrika Kusini kwa kushinda kinyang'anyiro cha kuandaa kombe la dunia mwaka 2010, ila tujiulize ni kwa vipi sisi kama Taifa, kweli tumekamia kuendeleza michezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la lazima kwa Taifa letu kulinda haki za kibinadamu za watoto kwa kuepusha kuwachanganya na watu wazima katika Magereza na Mahabusu. Mahabusu na Magereza kwa ajili ya watoto ni muhimu yawe katika hali nzuri na lengo liwe kuwafunza watoto ili waachane na utukutu badala ya kuwakomoa. Malezi ya watoto katika familia zetu na pia katika shule zetu yawe katika hali ya umakini zaidi ili kupunguza kesi zinazowahusu watoto. Taifa lipambane na tabia za kutelekeza

familia na watoto ambazo kwa kiasi kikubwa huwajengea watoto chuki dhidi ya jamii na kuzaa uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa linaloathiri maendeleo ya watoto na kuhatarisha nguvukazi au rasilimali watu *(Human Resources)* ya miaka ijayo. Hii inatokana na ukweli kwamba, mbali na kuhatarisha afya za watoto, wengi wao huathirika kimasomo na wengine hukosa kabisa haki ya kupata Elimu. Aidha, mikakati ya kukomesha ajira ya Watoto inakwamishwa na kiwango kikubwa cha umaskini miongoni mwa Watanzania mijini na vijijini. Hivyo, jitihada za dhati zinatakiwa kuelekezwa katika kuondoa umaskini. Umefikia wakati sasa maendeleo ya Tanzania yapimwe kwa *mtazamo wa hali ya maisha ya Watanzania* (People Centred Development) na sio tu ongezeko la mapato ya Taifa ambayo yananufaisha wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii inalo jukumu la kuwapatia makazi, chakula, mavazi na huduma nyingine, wazee ambao kwa sababu moja au nyingine, hawana namna ya kujikimu na watu wa kuwapatia msaada ili waendelee kuishi. Mara nyingi wazee wenye ulemavu unaowakwamisha kabisa kujipatia riziki kwa nguvu zao, hufikiriwa kwanza katika kusaidiwa na Idara. Kwa sababu si rahisi kuwahudumia Wazee wote wasiojiweza na kwa mara moja, inashauriwa kwamba, jamii ya Watanzania ihamasishwe na kuelimishwa zaidi kuhusu umuhimu wa kuwatunza wazee wetu majumbani mwetu, mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali nayo itenge fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kujenga makazi mapya na mengi zaidi kwa ajili ya Wazee wetu wasiojiweza. Makazi yaliyopo sasa yamechoka sana na ni chakavu mno kimajengo. Ukarabati mkubwa na vifaa muhimu kama vitanda na magodoro, mashuka, mablanketi, madawa na hata mavazi ni muhimu vinunuliwe haraka na Idara hii. Wazee wetu ni Vijana wa zamani na baada ya kutulea na kutusomesha wanayo haki kutunzwa na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo yenye jukumu la kusimamia uandaaji wa vijana kwa ajili ya Tanzania ya leo na kesho. Vijana waliopikwa vizuri kielimu na kimafunzo ndiyo mhimili wa Tanzania katika karne hii ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya leo michezo ni ajira, michezo ni biashara, michezo ni uchumi, michezo ni siasa, michezo ni afya na michezo ni diplomasia. Taifa letu liwekeze katika maendeleo ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wasio na ajira kwa kukosa elimu na mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi ni kama bomu linalosubiri kulipuka. Taifa lione umuhimu wa kuijali Wizara hii kwa kuitengea fedha za kutosha katika Bajeti. Vijana ni nguvukazi na uhai wa Taifa leo na kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ingawa sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushirikiano wetu wa pamoja wakati wote wa vikao na ziara za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena wewe binafsi, kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hotuba yangu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JINA KHATIB HAJI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kuniweka mtu wa mwanzo ni dalili nzuri pengine 2005 nitakuwa hivi hivi mshindi wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, sina budi kutoa pole au rambi rambi kwa wafiwa wa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Vilevile natoa pole kwa sisi Wabunge kufiwa na Wabunge wenzetu ghafla, kwa hiyo, tujipe pole. Tusiwe tunanung'unika na kulia lia ni rehema ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya ngonjera nyingi nitatoa mazungumzo yangu, kwanza, kuna hili suala la Wazee wa Kigamboni. Mchango wangu utakuwa ni wa Wazee wa Kigamboni na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya kwa kweli ni maeneo sugu au manyonge au dhalili au vipi. Wizara hii naipongeza kwanza kwa kazi zao nzuri, hasa kwa wale watendaji wake, kuanzia Mheshimiwa Waziri, ingawa si mtendaji kama watendaji wengine, yeye ni Kiongozi Mkuu, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, nawapongeza kwa utendaji wao mzuri vilevile au kwa uhimizaji wao mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ni kubwa lakini ina unyonge wa kutosha. Unyonge wake imepewa majukumu, lakini haya majukumu kadri wanavyoyatekeleza, naona watafikia pahala watadunda kama mpira waende kule warudi huku, wajigonge warudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazee wanaolelewa Kigamboni, wazee wasiojiweza. Kwa kweli wale watu wanasikitisha kutokana na hali ilivyo. Lakini Wizara haifanyi makusudi ndivyo inavyopangiwa na Serikali. Mipango inayopangiwa na Serikali si mibaya ni mizuri, lakini inaleta taathira kubwa, kwa wasiojua tunawalaumu Watendaji pamoja na Viongozi wanaoiongoza Wizara hii, kumbe vile wakulaumiwa ni wale wanaowapangia vifungu vya matumizi. Kifungu kinachopewa Wizara hii kwa kweli hakitoshi kwa watu hawa kuwa wagawane watu wawili, wazee na watoto hakitoshi, hakitoshi kabisa, hakitoshi kukorogea wala kupakulia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii inayopewa Wizara hii kwa wale wanaojua mahesabu wanajaribu kuipanga haifiki hata shilingi 150 kwa mtu mmoja. Itatumikaje kwa kila siku kwa watu hawa fedha hiyo? Kwa hiyo, kama kuna uwezekano, tunaiomba Serikali iwazidishie chochote au kifungu chochote ili angalau na wale wazee wajisikie. Tulipokwenda kwenye ziara kutazama makazi ya wale watu wananung'unika, wanasononeka, wanasikitika, wana kilio. Mwisho walisema hata Mheshimiwa Waziri

hatujamwona, Waziri ananiambia kwani yale mablanketi waliyopewa, yameshachanika? Wamegeuza lugha. Yote tunajua ni ukosefu na kupangiwa bajeti nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiongee na ngonjera za wazee. Niingie kwenye watoto. Kwa kweli sisi humu ndani sote ni wazazi, walioko mitaani na wanaokuja kusikiliza Bunge wote ni wazazi, tunaujua uzazi ukoje. Lakini lazima tukubaliane wazazi wa leo tuna uchungu mkali sana, tunawapenda watoto wetu mno na wazee wanasema mno ikizidi hatari inakuwa nyingi. Ndiyo mara nyingi tunasema kizazi kinachozaliwa hakistahiki. Mwenendo unaokwenda haustahiki, malezi hatujazungumza. Kumbe kutokana na pendo tulilowaachia watoto wetu ndiyo tukafikia hatua hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi tunavyowapenda watoto wetu tunafikia hadi sisi wazazi, baadhi ya wazazi siyo mimi. Sisi wazazi tunawapenda watoto bila ya kiasi. Tunawaogopa bila ya mfano. Sijui malezi hayo watoto watakuwaje na mtoto akisha kujibaini ninapendwa na mzee wangu, ndiyo yule mama nipe kila wakati. Hebu tujaribu kukaa tutafute mikakati ya kuwalea watoto wetu. Kwa sababu ninasema hivyo kwa kkuwa watoto wametuharibikia na mwisho ndiyo tunakuta watoto wanazaa watoto wenzao, wanatiwa kwenye mifuko ya lambo badala ya mtoto kuwekwa kwenye paja la mama au kwenye ubavu wa mama, leo mfuko wa rambo unakuwa ndiyo mlezi. Tujitahidi, tutafute mikakati, tukae tuzungumzie malezi ya watoto, tusiwe tunajiuliza watoto wanatupwa kwa sababu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefikia hadi sisi wazazi tunawapa rushwa watoto watufanyie kazi majumbani mwetu. Watoto wetu tuliowazaa wenyewe. Rushwa yenyewe unamwambia mtoto wako mwanangu nenda kapike chai. Mama siwezi. Nenda nitakupa pesa. Kweli ulezi huu ndiyo tutafika pahala? Hatufiki popote. Mtoto hawezi kupika mwenyewe na yeye mnyime, lakini huwezi kumnyima unasema utakufa na njaa. Kweli njaa ya siku moja itamuua? Haiwezekani njaa ya siku moja kumuua mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ujumbe kwa watoto umefika. Sasa naingia kwenye michezo, ingawa si mwanamichezo siku hizi. Nilikuwa mwanamichezo zamani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ulikuwa unaweza? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JINA KHATIB HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiweza baadhi. Natoa salamu zangu kwa Mheshimiwa Rais, ikiwa wewe utazipeleka au ikiwa Waziri mwenyewe atazipeleka, kwa kupita na kuhangaika kututafutia fungu la kujengewa kiwanja. *(Makofi)*

Kiwanja cha michezo, ingawa wengi wanakata tamaa na kusema hakitajengwa. Lakini kwa vile Mwenyezi Mungu, siyo Athumani, kiwanja huenda kitajengwa na upeleke salamu, useme kwamba, tunawashukuru na Wabunge wanasema ahsante, isipokuwa ujenzi uendelee haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba nikae. Naunga mkono hoja mia kwa mia au kwa zote. *(Makofi)*

**MHE. ASHA A. NGEDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, napenda kuungana na wenzangu kutoa pole za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge waliopoteza maisha yao, Mungu azilaze mahali pema peponi roho zao. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kujipongeza mimi mwenyewe, kwa nafasi niliyopata ya Ukamishna, pamoja na mikwala yote ya Wapinzani, lakini nimeweza kushinda, ila napenda kuwaambia Wapinzani wenzangu, hizi habari za kupeleka mambo ya Bunge katika Balozi au Umoja wa Mataifa, hivi vitu vimepitishwa na wakati na ninajua hizi ni habari za chama changu cha *CUF,* ndiyo wanaopenda kukimbilia kimbilia nje. Lakini vitu hivi walitusikiliza mwaka 1995 mpaka 2000, wakatuambia tumechoka mambo ya ndani ya nchi hayawezi kuingiliwa. Kwa hiyo, napenda Wapinzani wenzangu, msipende kupoteza poteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa najielekeza katika mchango wangu. Napenda kuzungumzia suala la michezo, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri na Wataalam. Ni kweli mmetuandalia hotuba nzuri, lakini kwa upande wa michezo, michezo upande wa watoto mmesahau. Mwisho, najiuliza kaka yangu, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, hana watoto, hana wajukuu au yeye anamwona Ndolanga tu na *FAT* basi? Ukiangalia hasa kubwa ni viwanja vya michezo. *(Makofi)*

Viwanja vya michezo hakuna kabisa na kama vipo basi vya kupachika pachika tu. Lakini viwanja hasa vimetengwa ndiyo katika Wizara ya Ardhi lakini havifanyi kazi na mimi siwezi kuilaumu Wizara ya Ardhi, kama imeshatenga kinachotakiwa ni Wizara ya Michezo ifuatilie. Ukiangalia nakumbuka nilipokuwa mdogo tulikuwa wakati wa sikukuu za Iddi tunavishwa na mama zetu tunaenda kucheza mabembeya katika viwanja hivyo, lakini sasa hivi hakuna. Ndiyo unakuta watoto wanatoka kwa mfano, kama Dar es Salaam wanaenda labda *Beach,* akifika kule mtoto hawezi kuogelea. Mtoto anaweza mambo ya mabembea. Lakini sasa anajikuta ameshafika baharini matokeo wengine wanazama, wengine wanapotea. Hilo ndiyo nilikuwa napenda kulizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hilo hilo la michezo, linatufanya sisi akina mama hata kama tunafanya shughuli zetu za nyumbani, tunakuwa na wasiwasi watoto hawana sehemu ya kwenda kuchezea. Kwa hiyo, huku wewe huku unapika au unafua, unamwangalia na mtoto tena barabarani unaenda kuchungulia chungulia. Mtoto ndiko anakocheza, hamna viwanja vya michezo. Pia ukitaka kitu kizuri anza mwanzo. Sasa watoto hao hao wanapotengewa viwanja vya michezo wanakuwa wachezaji wazuri wa *netball, football,* aina zote za michezo. Lakini nyie mnakuja tu mnaangalia huku juu juu, basi mnapata wachezaji sio wazuri, viongozi si wazuri, mwisho tena inakuwa habari ya Ndolanga ndiyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa napenda kuzungumzia ajira kwa watoto. Ni kweli wanawake wenzangu wa kipato cha chini hawatanielewa, lakini nitafanya nini,

inabidi tulizungumzie. Ni kweli watoto wengi wanaoajiriwa inatokana na wanawake wengi wenye kipato cha chini na kwa ujumla hasa ni umaskini wetu. Umaskini wa kipato, uyatima, watoto wanafiwa na wazazi wao, inabidi sisi ndugu wengine ambao bado tunaendelea kuishi duniani, tuwachukue wale watoto tuwalee. Sasa ndiyo unakuta mtu anampa ndoo ya plastiki akauze apate kuleta senti kidogo zipate kusaidia katika familia. Lakini ndiyo nasema, wanawake wenzangu mnivumilie na samahani sana. Ni kweli bora kupata tabu ya miaka mitano, lakini ukapata raha miaka 40. Tukubali tutafute njia zingine tubuni za kuongeza kipato ili wale watoto wetu waende shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na pia kwa upande wa watoto wa kike ambao wanafanyishwa kazi majumbani, wale watoto wa kike ndiyo wanapata madhara mara mbili. Kwanza, wanakosa masomo, pili, wanafanya shughuli ambazo bado hawajafikia umri, wanapokuwa katika zile kazi za ndani, wengine wanabakwa. Unakuta pengine baba mwenye nyumba ni mpenda kunywa au mlevi, anarudi usiku yule mtoto ndiye anamfungulia na mle kichwani ndio kuna pombe, basi anaanza kumshika matiti na nini, ndio mambo yanavyoenda tena. Kwa hiyo, mtoto anapata matatizo mara mbili, kwanza, anakuwa hana elimu, pili, kama hivi tunavyojua sasa hivi, kuna ugonjwa wa UKIMWI halafu pia anaweza kupata mimba na baadaye akafukuzwa yule baba anamwogopa mkewe, hawezi kumuoa na hawezi kumchukua pia sheria itambana mtoto mdogo kwa hiyo mtoto anarudishwa kwao, watoto wa mitaani wanazidi kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema kwa Mheshimiwa Waziri, sheria iko wazi lakini sijui kwa nini haitekelezwi kwa vitendo inatekelezwa tu kwa maneno? Sasa hivi unakuta kwa mfano, kama Dar es Salaam kwenye *traffic lights* zile, watoto wadogo wadogo wanauza maji, *juice,* hivi kinasubiriwa nini pale sheria kuchukua mkondo wake? Ukiwachukua wale watoto watakueleza nani kawatuma ile kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, ni kweli umaskini wetu lakini tufanye nini, tubuni vitu vingine na tukubali tabu ya miaka mitano lakini Taifa liwe na watu wasomi. Cha ajabu wote tunapita Mawaziri, Wabunge, wafanyakazi wa kawaida, wafanyabiashara kwenye *traffic lights* zile, tunawakuta watoto wanakimbizana lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Ukiangalia kwa mfano, kama majumbani humu, wako watoto wanafanya kazi na Wajumbe wa nyumba kumi kumi wanayaona, Wenyeviti wa Mitaa wanayaona, Wenyeviti wa Vijiji wanayaona lakini tukija hapa kwenye sheria basi ndio sheria ndio inashia hapo hapo! Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri, hili jambo la ajira kwa watoto sasa hivi imefikia wakati wake wa kufanya vitendo sio tena hadithi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila hotuba na pia leo umezungumzia mambo ya UKIMWI, lakini bila kuwakomboa watoto wa kike kwenye ajira hizi za majumbani, UKIMWI haupungui. Hiyo tusijidanganye kabisa.

Mtu mzima atakapokuwa ameajiriwa kufanya kazi za ndani anajua kwanza ana hiari yake amkubali yule baba au anaweza atumie kinga, lakini mtoto mdogo kwanza anaogopa, baba mwenyewe anatisha halafu la pili anaogopa labda atafukuzwa kazi, kwa

hiyo, inabidi akubali na UKIMWI unazidi. Hilo napenda uliangalie na napenda pia unipe majibu pamoja na kuwa naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michezo, kuna zile *open spaces,* huwa najiuliza sawa Wizara ya Ardhi wameshagawa viwanja, kuna maeneo haya ya michezo, Halmashauri za Wilaya zinakuja ndio kama vile wakati ule tena wanauziana, wanagawana, lakini mimi bado nalaumu Wizara ya Michezo hii yale maeneo yapo ninyi mnayashughulikia vipi? Inabaki hadhithi tu. Kwa mfano, kama Wilaya ya Temeke katika maeneo ya Tandika Mwisho katika Shule ya Tandika, nyumba zimeshajengwa kila siku ukiuliza, tena mimi huwa napita nawaambia wale wenye nyumba jamani watoto wetu wanagongwa na magari nyumba ndio mmeshajenga watacheza wapi?

Aah hili suala unajua liko Serikalini! Naomba Mheshimiwa Waziri, *open spaces* zote zile zilizojengwa, ufuatilie tuone viwanja vya watoto vya michezo hata kama Taifa letu ni maskini, halina vifaa vya kuwapa lakini watoto wale wachukue mpira wa makaratasi wacheze kwenye viwanja vile sio wacheze barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sina mengi, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, ninasimama kwa lengo la kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake leo kwa *speed* nzuri, sio ile ya cherehani aliyoanza nayo na akatupatia nafasi ya kuweza kuielewa vizuri hoja ambayo aliiweka Mezani asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe salamu za pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, kwa kifo chake cha ghafla kilichotokea tukiwa hapa Bungeni. Namwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi na familia yake yote, wapewe moyo wa ujasiri katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nizungumzie suala la vijana chini ya Wizara inayohusika. Vijana wanatafsiriwa kwa maana mbalimbali, lakini ninavyofahamu, vijana ni wale wenye umri unaogota kati ya miaka 14 - 35. Kwa hiyo, kwa umri wao huo, vijana wengine ni Taifa la leo na wengine ni Taifa la kesho. Wale wenye umri wa miaka 14 -2 5 lazima wawe ni Taifa la kesho kwa sababu ni kipindi cha kujiandaa, kupata elimu na kujiandaa kwa ajili ya kulitumikia Taifa, jamii na familia zao. Wale wenye miaka inayozidi hapo kufikia 35 hao ni vijana wa Taifa la leo kwa sababu tayari wamekwisha wezeshwa wanaweza kulitumikia Taifa na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni nguvu kubwa ya Taifa na ni nguvukazi ambayo kwa sehemu kubwa sana Taifa letu limeiachilia pembeni ile nguvukazi ya vijana ambao wengi wao hawakuweza kupata elimu rasmi, kwa hiyo, hawakupata ajira katika sekta rasmi. Kwa msingi huo, nguvu kubwa ya vijana imeachiliwa kuendesha maisha yao peke yake, ambayo hayana mwelekeo unaoelekea kulijenga Taifa wala nguvu hii ya pamoja bado haijaweza kuwekewa nguvu ya mwelekeo wa Kitaifa unaoweza kulifadisha Taifa ipasavyo kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na hata kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira rasmi ambayo inachukua watu wachache inao utaratibu unaeoleweka lakini ile ajira ambayo sio rasmi inayochukua vijana wengi, jambo hili halieleweki sawasawa. Hatufahamu vijana hawa wako wapi, wachache wameonekana sehemu za vijiwe na Mkoa wa Kagera, Mkoa ninaotoka uliingizwa katika utafiti ikaonekana vijana wako katika vijiwe, vijiwe hivyo vinakusudiwa kugeuzwa kuwa ni sehemu pengine ya kuwapa kazi rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, sio wazazi wote wanaoruhusu watoto wao kwenda katika vijiwe. Kwa hiyo, takwimu za vijiwe zikichukuliwa kama ndio takwimu rasmi za kuwachukua vijana kuwaingiza katika sekta rasmi, tutakuwa tumeacha idadi nyingine nzuri, kubwa ambayo inadhibitiwa vizuri na wazazi, yenye nidhamu ambayo haiendi kwenye vijiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, ninashauri kwamba, Serikali ifanye utaratibu wa kufanya sensa upya, ichukue takwimu rasmi za vijana hawa kutoka katika ngazi ya kaya, ifahamu kuna vijana wa miaka 14 - 35 wangapi, wanafanya nini na wana mawazo gani. Vijiwe ni sehemu nyingine ya nyongeza ya kutaka kuona wale vijana ambao tayari wameshazichomoka familia kwa sababu kwa mujibu wa taratibu za vijijini, vijana walioanzisha vijiwe ni wale ambao hawazisikii familia. Kunapokucha asubuhi badala ya kwenda katika kazi za kujenga Taifa, kushirikiana na wazazi wao kwenda katika mashamba, hawa huenda kukakaa katika vijiwe lakini vijana wazuri utakuta wako katika kazi mbalimbali za kujitegemea. Kwa mfano, utakuta wako katika bustani zao, uvuvi, ufundi seremala na shughuli nyingine ndogo ndogo wanazoziendesha wenyewe. Sasa inawezekana tukachukua wale vijana walioko katika vijiwe lakini wale ambao wako katika sehemu zao mbalimbali za kujitegemea, wakawa wameachwa bila kujulikana wako wapi na wanafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna pesa za mfuko wa kusaidia mikopo, naipongeza Serikali kwa pesa kiasi ambazo imekuwa inapata na inazipeleka katika ngazi zote za Halmashauri za Wilaya nchi nzima kwa kutumiwa na Wilaya zote kwa ajili ya kusaidia kazi mbalimbali za vijana kama mikopo. Pesa hizi zimeonyeshwa kwamba, ni kiasi cha milioni tatu na kuzidi kidogo kwa kila Wilaya. Ukweli wenyewe ukizingatia kwamba, Wilaya nyingine zina mpaka Majimbo matatu na idadi kubwa ya vijana, utaona kwamba, mgao wa pesa hizi unaweza ukaenda kwa kiasi cha wastani wa shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni moja na nusu ama kwa Jimbo au kila Jimbo shilingi milioni moja. Kiasi hiki ni kidogo sana. Nashauri kwamba, taratibu nyingine za kuongeza pesa hizi kwa ajili ya kuwasaidia vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa, ziongezwe ili ziweze kusaidia kuimarisha nguvu ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine linalojitokeza katika ile 10% ya Halmashauri ya Wilaya, ni kwa maendeleo ya wanawake na vijana lakini utakuta kila zinapopatikana 10% wakati mwingine vijana huwa hawaambulii kupata pesa yoyote. Sababu kubwa inayotolewa na watoa pesa hizi wanasema kwamba, vijana hawako katika maeneo yanayojulikana. Kwa hiyo, wachache waliowahi kupewa mikopo basi waligawana pesa wakaishia mbungani, wakatafutwa hawakuweza kupatikana na kwa hiyo, wakaharibia vijana wengine ambao wameweza kuwa katika shughuli za kujitegemea wasiweze kupata tena pesa za kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku. Ninaomba suala hili liangaliwe upya nalo litatatuliwa kama tutaweza kupata takwimu za vijana kujua wako wapi na wanafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nizungumzie hoja nyingine inayohusu walemavu na wasiojiweza. Tukitazama hawa walemavu na wasiojiweza, tutakuta kwamba, limekuwa ni tatizo la kifamilia na sio tatizo la kijamii. Kwa hiyo, familia ndio yenye uamuzi juu ya huyu ambaye ni mlemavu. Kama inaona haja ya kumpeleka shule akapate elimu ya msingi na hata kumwendeleza kufika elimu ya juu, basi inategemea familia yenyewe. Kwa msingi huo, unakuta walemavu wengi hawakusoma, hawakwenda shule kabisa na hata wengine wanafichwa mpaka kipindi hiki, hawakuweza kupata elimu yoyote na kwa hiyo, wengi hata sasa wanadai kama wangeweza kupata angalau elimu ya watu wazima ikaweza kuwasaidia kusoma na kuandika na kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walemavu wanapokuwa ni watu wazima, wanapata tabu sana kwa sababu ni wakati ambapo sasa wanajikuta hawana elimu, wanapenda kuendesha maisha lakini hawajui hata elimu ya ufundi, hawana elimu ya biashara, hawawezi kwenda katika ajira yoyote kwa sababu hawawezi kumudu ajira rasmi kwa sababu hawana elimu, ujuzi na hata ajira isiyo rasmi inakuwa ni ngumu kwao kwa sababu ambazo nimezitaja. Lakini vilevile madhara ya dunia hayawaachi nao wanashambuliwa na matatizo makubwa ya UKIMWI. Ni kwa kiwango gani walemavu wanawekwa katika taratibu za maisha kama wengine ambao hawana ulemavu ili na wao waweze kumudu maisha ambayo wenzao wanayaendesha?

Nashauri sana Serikali iangalie suala zima la Sera ya Walemavu, ambayo wamekuwa wakiidai kwa muda mrefu. Kama hakutakuwa na Sera ya Walemavu, ambacho kitakuwa ni kitu cha Taifa kuelekeza ni kwa kiwango gani walemavu waweze kupata haki zao na Taifa kuzifuata, hawa walemavu wataendelea kuonekana kwamba, si sehemu ya haki zote za Taifa kwa sababu haki zao za msingi hawapewi na hawana nguvu ya kuzidai kisheria wala hawana hata wahisani wanaoweza kuwasaidia kwa ule moyo wa kweli. Wengi wamekuwa wakipenda kuwatumia kama vile ni mali yao binafsi ili waweze kujiongezea kipato chao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiojiweza wako katika maeneo mbalimbali na kwa kweli hawajulikani. Nao vilevile jamii imebaki kuona ni mzigo ambao hauna mwenyewe, unatupwa huku na kule. Ukiangalia hapa katika orodha ya makazi ya watu wasiojiweza utaona kwamba, idadi iliyotajwa hapa ni watu 2,705 tu lakini ukweli ni kwamba,

wasiojiweza na wazee ni wengi sana kuliko idadi hii. Ni idadi ndogo sana ambapo watu binafsi na mashirika ya hiari wameweza kuwachukua na kuwapa huduma wao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda niwatambue hata wale ambao ni watu binafsi waliojitolea kukaa na hawa watu wasiojiweza na yatima ambao hawatambuliki. Ninaomba katika orodha ya Wizara, aongezwe Mama Adivela. Mama huyu tangu mwaka 2003, nilieleza katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kwamba, aangaliwe. Huyu mama anaishi katika Kata ya Ngenge katika Wilaya ya Muleba. Mama huyu anatunza watu wasiopungua 40 wakiwemo yatima 30 na wazee wasiopungua 10, lakini mama huyu amekuwa akitunza watu hawa kwa nguvu zake mwenyewe. Ni *sister* aliyestaafu lakini maisha yake sasa waliokuwa wakimsaidia *(White Fathers),* baada ya kuondoka amebaki akiwa akijihudumia yeye peke yake na hili kundi la watu. Kwa sababu anasaidia Taifa, ninashauri kwamba, huyu mama naye awekwe katika orodha na awe akisaidiwa ama atambulike ili itakapotokea namna yoyote ya kumsaidia, ajulikane yuko wapi na yuko na akina nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kuhusu Sera ya Wazee. Nianze kutoa pongezi nyingi sana kwa Wizara hii kwa kuitoa Sera ya Taifa ya Wazee. Nimeisoma kwa haraka haraka katika huu muda mfupi, nikakuta yale yote ambayo nilikuwa nimepanga kuyazungumza, kwa kweli yameonyeshwa katika sera hii, nami napenda niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kubwa ninazowapa, napenda nizungumze machache. Dhana nzima ya uzee imetafsiriwa katika kitabu hiki kuanzia ukurasa wa pili ambao inaonyesha kwamba, ni hatua ya mwisho ya ukuzi wa mwanadamu kutokea utoto kuelekea utu uzima. Kwa Tanzania tumechukulia kwamba, ni ya watu wenye umri unaoanzia miaka 60 na kuendelea. Kwa hiyo, tunakiri huyu mtu mzima ambaye ni mzee, ni hazina kubwa ya Taifa, ni dawa kwa sababu anayo elimu ya kutosha ama aliyoipata rasmi au siyo rasmi, pia ana ujuzi na uzoefu. Kwa hiyo, mtu huyu ni mtu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote mazuri yaliyoelezewa katika Sera hii ya Taifa, tunaona watu wazima wanashambuliwa na magonjwa na hata mazingira magumu katika uzee. Wanashambuliwa na magonjwa ya migongo, macho, misuli, maungo, hata kupungua nguvu zao za kufanya kazi za kujitafutia kipato. Wazee hawa walioangaliwa sana ni wale waliokuwa katika ajira rasmi lakini wale ambao walikuwa katika ajira isiyo rasmi, ambao ni wakulima, wavuvi na wafugaji, hawamo katika sera hii kwa msingi kwamba, mipango yao haijawa rasmi, wanatajwa tu kuonyesha kwamba, ni kwa kiwango gani wanaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika waathirika wakubwa ambapo sera hii ninaomba iwape nguvu zaidi ni wale akina mama wazee ambapo licha ya umri wao na mazingira magumu, pia wanashambuliwa na mila na desturi ambazo nazo huwafanya wanapozeeka hawana mahali pa kukaa kwa sababu hawana ardhi, watoto wamekwishahama, watoto wengi wamekufa kwa UKIMWI, hawana Wasaidizi, umaskini

unawaandama. Kwa hiyo, wakati wa utekelezaji wa sera hii, ninaomba suala hilo lizingatiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuomba katika sera hii ni utekelezaji. Nimejaribu kuangalia kwa haraka haraka, nikawa najaribu kutazama pengine nitaweza kuona ni muda gani sera hii imepangwa kuanza kutekelezwa, pengine ni kwa sababu nimekuwa na haraka ya kuisoma lakini sijaona itaanza kutumika wakati gani. Taratibu zake za kutumika, mkakati wake unaandaliwa vipi? Naomba utekelezaji wake uwe ni wa haraka isiendelee tena kuja kwa habari kwamba tutafanya, tutafanya bali bajeti ijayo Mwenyezi Mungu akitujalia kukutana tena mahali hapa, basi tuje kuelezwa utekelezeji wa sera hiyo ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii kama itatekelezwa ipasavyo, ninaamini kabisa kwamba, itakwenda kupunguza matatizo mbalimbali, huduma za afya kwa wazee, hata wale wa vijijini ambao kwa sababu ya kazi ngumu, huonekana bado ni vijana kumbe wamezeeka sana wapewe vitambulisho ili waweze kupata huduma za afya ambazo tayari ziko kwa ajili ya wazee. Vilevile hawa wazee ambao maisha yao yamekuwa ni magumu yaweze pia kuwekwa sawasawa, washirikishwe katika kupanga mipango ya Taifa na wapewe mikopo ya kuendesha maisha yao. Vilevile hii habari yule anayezeeka katika sekta rasmi anapewa Sh. 20,000/= kwa mwezi kama *pension* yake, hali halisi ni ngumu sana kwa Sh. 20,000/= mtu kuweza kuendesha maisha. Hali ya maisha imepanda. Ni vizuri sana ikatazamwa ili walau apate malipo yasiyopungua kima cha chini kwa kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kutoa rambirambi kwa ndugu, jamaa na Wapiga Kura wote wa Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na Wabunge wengine wote nawapa pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kwanza, kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nachangia katika suala la ajira kwa vijana. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ni Wizara inayoshughulika na suala la vijana. Lakini suala la vijana limesahaulika kwa kiasi kikubwa na hatimaye Wizara hii imejikita zaidi kwenye michezo. Lakini tunaopata shida ni vijana au vijana wenzangu ambao wanapata shida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu ambao Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imejiwekea ili Wananchi wake waweze kupata elimu kuanzia msingi na sekondari na wanajiendeleza kwa kiwango kikubwa zaidi. Vijana wengi wanajiendeleza kwa kupata vyeti vya Chuo Kikuu na kuendelea lakini baada ya kupata vyeti hivyo, vijana hawa wanakosa ajira. Ajira hizo wanazikosa kutokana na vigezo ambavyo Wizara au maofisi wameviweka. Wanaweka kigezo kuwa kijana ambaye anahitajika kuajiriwa lazima awe na uzoefu wa miaka mitano au kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo hiki ni kigezo ambacho kinamnyima kijana yule aliyepoteza muda wake kwenye elimu au aliyepata elimu, kuwa mkazi wa nyumbani sio mfanyakazi katika ofisi. Kama unaweka kigezo cha kuwa na uzoefu wa miaka kumi au mitano, tunaomba basi Wizara iweze kutenga rasmi shule au chuo cha uzoefu huo kusudi vijana hawa waweze kupata huo uzoefu mnaotaka katika vyuo hivyo. Sasa inakuwaje unaweka kigezo hicho wakati hakuna chuo wala shule zozote zinazotoa hicho kigezo cha ujuzi, kijana huyu akitoka shule lazima apitie kwenye chuo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba suala hili kwa kweli mliangalie zaidi au kwa undani kwa sababu wazazi wengi wanapenda vijana wao wasome waweze kupata ajira na kuwasaidia. Wengine wanapoteza pesa zao nyingi kuwasomesha shule za *private* baada ya kumaliza katika shule hizo hawana ajira, mnategemea vijana hawa waende wapi, matokeo yake vijana hawa wanakuwa na mawazo kwamba, watakuwa wazamiaji. Kwa maana hiyo, wanapoteza mwelekeo wa elimu yote kwa muda wote walioutumia. Mnawanyima haki zao za elimu waliyoipata na bado mnawanyima haki zao za kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili naomba nichangie kwa vijana ambao wanaitwa ni vijana wazururaji au vijana wanaojiajiri wenyewe. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kuwa, uko uwezekano na lipo shinikizo zaidi la Halmashauri kuweza kutoa mikopo. Nadhani Mheshimiwa Waziri, hajaelewa kuwa Halmashauri hizo hazitoi mikopo kwa vijana na kama zinatoa ni Halmashauri chache tu. Kwa maana hiyo, mikopo kwa vijana bado ni tatizo kwa sababu hawapati. Kwenye hotuba yake nina imani mpaka ameiweka humu atakuwa na mikakati zaidi au rasmi ya kuweza kushughulikia mikopo hiyo ili vijana waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana ambao wanaitwa Wamachinga, wale wanaobeba mizigo mikononi lakini wako Wamachinga wanaobeba mizigo mikononi na wako Wanyamwezi wanaobeba mizigo kichwani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunategemea Wizara yako kwa kushirikiana na ninyi Mawaziri wawili, mtakuwa warefu wale Wanyamwezi wa mizigo kichwani na wale Wamachinga wa mizigo ya mikononi, mtawatua mizigo hiyo kwa kuwawekea sehemu maalum ya kufanya shughuli zao bila kusumbuliwa sehemu hii au ile. Vijana hawa wanapata shida sana, Mheshimiwa Waziri nashukuru kwa kuniangalia, nina imani kuwa unanisikiliza kwa makini. Vijana hawa wanapata shida sana. Kwa hiyo, tunaomba sehemu zote au Wizara iweke utaratibu Halmashauri zetu ziweze kuwa na sehemu zitakazowatengea vijana sehemu watakazofanyia biashara zao bila kusumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara hii kwa kuandaa utaratibu wa *VETA*. *VETA* ni sehemu nzuri ambayo inaandaa vijana wetu waweze kupata elimu au kujiendeleza kielimu. *VETA* ni sehemu ambayo sisi vijana au vijana au Wizara tunatakiwa kuiangalia kwa macho mawili. Kuna sheria ambayo tumeipitisha sisi wenyewe Wabunge mwaka 2001 hapa hapa Bungeni ya *Public Procurement Act*, ni sheria ambayo hawawezi kununua vitu mpaka wapitie kwenye *tender*. Kwa maana hiyo, watu wa *VETA* wanapata shida sana kuandaa utaratibu wao au kutengeneza vitu na kuuza kwa bei rahisi bila kupitia kwenye *tender*. Mheshimiwa Waziri, naomba sana Wizara yako iangalie sheria hii ya mwaka 2001 kusudi *VETA* iweze kupewa nafasi ya kununua vitu bila kupitia katika *tender*. Wakipitia huko wana maana ya kwamba, lazima watanunua vitu kwa bei ya juu na wao watatengeneza vitu vile kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshangaa zaidi maofisi yetu mengi ya Serikali yanashindwa kununua vitu vya *VETA,* ambapo ni vitu vyetu sisi wenyewe Watanzania. Matokeo yake wanaagiza vitu vya bei ya juu kuliko hata vile vilivyokuwepo *VETA* kwa maana ya kwamba, wao wenyewe hawakubaliani na kuendeleza nchi yao, wanakubaliana na kuendeleza vifaa vya nje kwa maana hiyo hawataki maendeleo ya Wizara hii au kitengo cha *VETA*. Naomba Mheshimiwa Waziri, sheria hiyo iangaliwe ili vijana wa *VETA* waweze kuendelea na kujiendeleza, kujielimisha kwa maana ya kwamba, sisi wenyewe tunapowasaidia *VETA,* ndipo tunapoisaidia nchi yetu na vijana na kitengo cha *VETA* kiweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia *NSSF*. Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake hiki ambacho amekiandaa vizuri na kwa mapambo mazuri, kinaonyesha ni *VETA* na *NSSF*. Lakini *VETA* pia inashughulika na mambo ya ujenzi na nyumba za *NSSF* zimejengwa hapa na zimepambwa vizuri lakini sio kwa kutumia wajenzi wa *VETA*. Kama hoja lazima kuwe na kampuni, basi *VETA* na wao muwaandalie kampuni au wafungue kampuni ya ujenzi. Kinachonishangaza zaidi *VETA* na *NSSF* wote wako maendeleo ya jamii, kwa nini wasiweze kusaidiana wao wenyewe kwa wenyewe? Kwa maana hiyo, mnaweza kujifunika shuka moja mkaona halitoshi mkalikata katikati halafu sehemu nyingine ndio zikabaki hivyo hivyo. Ninachoomba ninyi wenyewe, mshirikiane na kusaidiana kwa sababu mko katika Wizara moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia kwenye mambo ya michezo, nampongeza sana kaka yangu, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, kwa kuwa kwenye Timu ya Simba na nampongeza sana kaka yangu, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwa kuwa Timu ya Yanga. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni ya wote na michezo ni furaha, lakini maana nzima ya michezo inakuwepo kutokana na maendeleo. Kama tutakuwa na maendeleo katika michezo lazima kila mmoja atapenda michezo na atakuwa na furaha ya michezo. Kikifika kipindi cha jioni kila mmoja atakuwa anapenda kuangalia michezo, kama muda uliopita tulikuwa tukikaa muda wote tunaangalia michezo ya mechi za wenzetu majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuongelea kidogo kuhusu vilabu vyetu. Kama hatutaweza kuimarisha vilabu vyetu basi ina maana michezo kwa ujumla

haitaweza kuendelea au kuboreka au kuwa na maendeleo. Kinachotakiwa zaidi tuweze kuvisaidia vilabu vyetu ili viweze kuendelea kufanya vizuri. Tukiwa na kelele tu za kupigia *FAT* bila vilabu kuendelea vizuri, itakuwa hakuna maana nzima ya michezo. Kwanza vilabu viweze kuangaliwa na viweze kusaidiwa. Kwa mfano kama Simba ikiweza kusaidiwa kupatiwa pesa nina imani kuwa itacheza vizuri zaidi na zaidi na kuwa ni kiongozi. Kwa maana hiyo kama Serikali itatenga mafungu ya kuweza kusaidia vilabu itaendelea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri mdogo ambao kwa mwono wangu si kama nasisitiza lakini ni mwono wangu kutokana na matatizo ya *FAT,* inatakiwa lazima tuyaangalie kwa undani zaidi. Mapendekezo yangu yanazungumzia kwamba kama Mwenyekiti tunampata kwa kuchaguliwa basi Katibu Mkuu tuweze kumpata kwa kuteuliwa ambaye atawajibika. Kwa maana hiyo kwa sababu Katibu Mkuu akiwajibika nina imani hakuna Mwenyekiti atakayeleta tatizo wala Katibu Mkuu mwenyewe hataleta tatizo, michezo itaweza kwenda vizuri na kwa utaratibu na kama *FIFA* watatuletea pesa nina imani pia hata Serikali kwa kupitia Katibu Mkuu yule aliyekuwepo pale wataweza kupitia mahesabu yake kwa muda wote. Lakini tutakapoacha Katiba hiyo iendelee Mwenyekiti awe ni wa kuchaguliwa na Katibu awe ni wa kuchaguliwa, mimi naona hapa tatizo litazaa tatizo. Leo atatoka Ndolanga na Wambura atakuja Aziza na Kipole na tatizo litaendelea kuwa pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu wazee wa *East Africa Community,* wale ambao walikuwa wakifanya kazi bandarini. Pale Dar es Salaam kuna wazee wale ambao wanahangaika kila siku kudai pesa zao, lakini je, Serikali inawasaidiaje wale wazee? Jamani wazee ni dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kidogo kuhusu hoja ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Kwanza napenda kabisa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kapuya, Waziri pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mudhihir na Katibu Mkuu, Bwana Abubakar pamoja na watendaji wa Wizara hiyo na Mashirika yake kwa kutekeleza majukumu yao vizuri. Wizara hii mimi kwa muono wangu naona imepewa majukumu mazito na yenye matatizo kemkem. Kwa hiyo, tunapoizungumzia tuizungumzie katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache lakini kabla ya hapo napenda kusema kwamba naunga mkono hoja yao hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyoona ni kwamba hii michezo imeachiwa Wizara hiyo peke yake na Vyama vya Michezo. Kuna Taasisi na Idara za Serikali ambazo zimekabidhiwa majukumu ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika maeneo mbalimbali, mfano, Halmashauri za Miji, Wilaya na kadhalika. Hivi ni mara ngapi tumepewa taarifa kuhusu michezo katika vyombo hivyo? Ni kwamba hii kazi imeachwa tu inakwenda yenyewe. Mimi nadhani ni vema tuwakumbushe na pengine

tumkumbushe Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba angetoa maelekezo tena mapema sana kwamba michezo ni sawasawa na kilimo, elimu au afya. Kwa hiyo unapopanga mipango ya kuendeleza sekta hizi, basi ni pamoja na michezo, vinginevyo tutakuwa Taifa la ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta katika baadhi ya maeneo, maeneo yalikuwa yameachwa wazi kama viwanja vya michezo na burudani yamegeuzwa kuwa viwanja au maeneo ya biashara. Hivi kweli tuangalie hili liendelee tu? Kwa hiyo katika haya maagizo ni pamoja na kutogawa maeneo ya michezo na burudani kwa shughuli nyingine. Yaachwe wazi hayo maeneo. Tutakuta watoto wote wapo barabarani, wanacheza chandimu katika barabara na ajali zitakuwa nyingi, ndiyo hali ilivyo. Kwa hiyo, hili tunasema ni agizo kwa kweli litolewe kwa sababu ni kazi za Serikali hii.

Wizara hii kazi yake ni kusimamia sera na kusaidia kusimamia eneo hilo, wala sio kuendesha vilabu. Kwa hiyo ni vizuri pale katika Kijiji vile vile maeneo yaanze kutengwa sasa hivi. Huko tunakokwenda kama hayatatengwa maeneo ya burudani na michezo hakutakuwa na kitu. Kwa hiyo, tunaanzia kwenye Kijiji tunakuja kwenye Wilaya na Miji na haya maeneo yatangazwe japokuwa Serikali haiwezi kuwa na hati lakini haya tunadhani yangekuwa na hati. Mbona Serikali imezuia Gymkana pale, haivurugwi vurugwi.

Wale wanaocheza pale Ghymkana si watu wa kawaida, ni watu wenye uwezo, hivyo watu wasio na uwezo wa kule Temeke awe na uhakika akichoka na kutoka nyumbani kwake, atakwenda kukaa mahali gani apunge upepo? Tusipoangalia kwa kweli tutakuwa na maeneo ya ajabu ajabu ambayo watu wengine hawatatuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la michezo mimi nina ushauri wangu, mimi nadhani kama Wabunge tuzungumzie masuala ya michezo *(issues),* hii habari ya kuzungumzia watu humu ndani mimi inanipa tabu sana na tutaeleweka vibaya. Ni afadhali watajwe katika utekelezaji wa majukumu kwa sababu hawamo humu ndani. Sio kwamba nasema waache kusema, lakini mimi maoni yangu kwamba imefika mahali tuzungumzie issues za michezo kama vile kutopatikana viwanja, vifaa vya michezo, walimu wa michezo, bajeti ya michezo, halafu ndio twende kwenye hao waliokabidhiwa majukumu; kama kuna mwenye matatizo, twende kwenye kanuni na Katiba washughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu ni hilo kwa sababu na mimi kwenye Jimbo langu naulizwa, hivi huyu Ndolanga ni Mbunge wa wapi maana kila siku mnamtaja huko Bungeni? Nikawaambia ni Mbunge wa Michezo. Sasa tumpe nafasi yake kama ni hiyo ili naye aje hapa aweze kuzungumza hapa na kujitetea. Mimi namwelewa sana Ndolanga, nimefanya naye kazi, nilikuwa Mkurugenzi wake wa Mkoa, yeye akiwa wa Wilaya. Ni mtu ambaye anasimamia haki yake vizuri na ukiwa na hoja uende vizuri kwa Ndolanga, vinginevyo atakutoa na anasoma sana sheria. Kwa hiyo ni vizuri mkajua mnashughulika na mtu gani, mimi alikuwa kijana wangu yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasaini Mikataba na Makubaliano mbalimbali ya Kimataifa. Kwenye Wizara hii kuna Mkataba ule wa Ajira ya Watoto. Mkataba wa Ajira ya Watoto inabidi tuutekeleze kwa makini sana kwa sababu katika jamii ya Tanzania kuna taratibu za malezi ya watoto pale kwenye familia na kwenye jamii. Sasa tusipoangalia tunaweza kukurupuka na haya ambayo zaidi yanatatua matatizo ya Mijini kuliko kule Vijijini. Kwa mfano, tukizungumza ajira ya mtoto ni ajira ya namna gani, ni ajira ya kulipwa mshahara au ni vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu juzi juzi kuna utafiti umefanywa katika Jimbo langu wakaenda mpaka kwenye mashamba ya chai. Wakakuta watoto siku ya Jumamosi wanachuma chai. Napenda kukumbusha hapa kwamba wale watu wa Vijijini wana akili sana, wanampangia mtoto kazi kufuatana na rika lake. Sasa waliuliza wewe mtoto umeajiriwa, akasema ndiyo kwa sababu kulikuwa na fedha nadhani zinatolewa, akasema ndio. Nani kakuajiri, akasema baba yangu. Ahaa, baba yako kakuajiri, akasema ndio. Anakupa mshahara, akasema ananinunulia *uniform* za shule na ninakula chakula. Hayo ni mazingira kwamba kila mtu anachangia kwenye shughuli za familia na anapangiwa ile kazi ambayo ipo katika uwezo wake. Wale watu sio wajinga kiasi kwamba mtu amtese mtoto wake kwa kumbebesha jiwe wakati anajua huyo ni mtoto mdogo. Haiwezekani. Kwa hiyo, twende na taratibu zetu na kanuni zetu tusijiendee tu hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna fikra ambazo sasa hivi katika *globalization.* Watu wanaanza kujiuliza kwa mfano, nimemsoma mwandishi wa makala ya uchumi anaitwa Robert Samuelson. Nadhani Mheshimiwa Masilingi huyu anamtambua na ni mwandishi wa makala za uchumi katika gazeti la *News Week.* Sasa katika article yake ambayo ameandika Sharing the Wealth ambapo amewanukuu wachumi wa Kimataifa wawili ambao wasomi wanawajua, nao ni Jagdish Bhagwati na Martin Wolf. Hawa wameandika vitabu. Kitabu cha huyu Bhagwati kinaitwa *In Defence of Globalization* na huyu Wolf ameandika *Why Globalization Works.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatoa hoja zifuatazo, ningeomba nizisome kwa lugha hii ya Kiingereza wanasema hivi: *"Child labour predates globalization and is preferable to child starvation.* Mmeipata hiyo? Halafu wameendelea wanasema katika utafiti wao *Wolf reports that, about 250 million children between five years and fourteen work; seventy percent in traditional agriculture, only about ten million to fifteen work in export industries. But as incomes raise families are less likely to resort to child labour. Therefore, outlawing it simply doesn't work. Families need money too much".* Halafu akaendelea akasema, *"It will only drive poor parents to send their children to work by stealth* (kwa mbinu mbinu) *and often into even worse occupations such as prostitution".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema hivi, hivi wale watoto wadogo ambao wamemaliza shule za msingi tuseme wasiajiriwe. Kwa hiyo, wakimbilie Mjini wakafanye ukahaba, ndio wanavyo-*argue* hawa. Kwa hiyo, *child labour* tuitafsiri vizuri sana. Mtoto apewe kazi ambazo ana uwezo nazo, sio za kumtesa. Mimi ndio *interpretation* yangu ya hizi sheria katika mazingira yetu. Naomba nizungumzie kuhusu Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi. Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara

tulitembelea Viwanda Jijini Dar es Salaam pamoja na Kiwanda kimoja cha Nguo, tukauliza masuala ya usalama na afya kiwandani. Tukakuta pale wenye kiwanda wameweka vifaa vya kutumia wafanyakazi wakati wanapofanya kazi, lakini wakatwambia baadhi ya wafanyakazi hawataki kutumia vitu hivyo. Mimi niliwaambia kwa nini msiwafukuze kazi ijapokuwa mwingine atashangaa. Nikawaambia, huyu kesho kutwa akipata athari zozote itabidi umlipe wewe, sasa ni vizuri umwondoe mtu mjinga. Watu wengi wanatafuta kazi, yeye kama hataki kuvaa *gloves* au mask wakati anafanya kazi hizi atakuletea matatizo, itabidi umwuguze na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba hii Wakala wa shughuli hii ya usalama na afya mahali pa kazi iongezewe nguvu zaidi kwa maana ya *staffing.* Hiyo Idara bahati nzuri naielewa, ya siku nyingi sana. Nadhani ni ile *Factory Inspection Department,* ilikuwa na watu wachache sana tena adimu. Sasa ipewe nguvu kwa sababu sasa hivi tume-*privatize* Mashirika na kwenye *private sector* kuna mambo huko yanaweza kufanyika yakaathiri sana wafanyakazi. Tuwasaidie huko. Nitashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni hili la migogoro kazini. Mahakama ya Kazi iongezewe nguvu ya kushughulika na migogoro hii kwa sababu kuna baadhi ya migogoro inachukua muda mrefu sana mpaka watu wengine wanaodai wanakufa na wanakufa kwa ajili ya kihoro na kutokuwa na kitu cha kuweza kukidhi mahitaji yao ya maisha. Kwa hiyo napenda kushauri kabisa kwamba, Mahakama ya Kazi kwa kweli ipewe nyenzo za kutosha ili tufanye hii kazi sasa, maana yake tume-*privatize* Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna Sheria hii ya Udhibiti wa Afya za Wafanyakazi. Basi isimamiwe vizuri, tukiacha hivi kwa kweli tunaweza kupoteza nguvu kazi ambayo pengine imefundishwa lakini kwa kuwa mazingira wanayofanyia kazi hayafai wataumia. Kwa hiyo mimi naomba hili liwahusu wote, wale wenye viwanda na hawa ambao ni wafanyakazi. Kama wafanyakazi wanakataa kuvaa vifaa vinavyohitajika, basi wachukuliwe hatua hata kwa kushtakiwa kuliko kuwaacha tu na hizi nadhani ni *weak managements.* Nadhani ni vizuri Wizara hizi ambazo zinashirikiana na *private sector* ziwasaidie, wachukue mafunzo ya *corporate management,* wasiende tu hivi hivi kwa sababu mtu kutotekeleza masharti ya namna hiyo ni kwenda kinyume na shughuli za shirika na inaathiri hata heshima ya kampuni ambayo inahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni huo tu mdogo ila nasema naunga mkono hoja yao kabisa kabisa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa siku ya leo. Lakini nilikuwa napanga sehemu tatu za kuzizungumzia leo hii nazo ni *VETA* na ajira kwa vijana pamoja na michezo. Maeneo mawili haya au yote matatu kwa ujumla yamekwishazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wameshanitangulia. Lakini sasa zaidi nitazungumzia suala la michezo kwa sababu michezo ninaielewa vizuri kwani hata hii leo bado ni

mchezaji wa timu ya *Bunge Sports Club* nikiongozwa na kocha wangu Mheshimiwa Joel Bendera na msaidizi wake Mheshimiwa Mudhihir wa Mudhihir Sheikh Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba sina pingamizi sana na hotuba hii kwa sababu nimeisoma binafsi badala ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri kwa spidi aliyokuwa akienda, basi niliipitia mwenyewe nikaisoma na nikaifahamu na kidogo nimeifanyia uhakiki. Kitu ambacho nilikiona humu yeye ameomba fedha jumla ya Sh. 61,113,986,200/= ukiacha zile fedha za fungu 60. Nasema kwamba kwa mujibu wa hotuba yake na aliyoyapanga humu fedha hii ni ndogo sana. Pamoja na kwamba yeye ameomba na ametoa hoja, sasa mimi nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu tumpe hizi fedha Mheshimiwa Waziri ili atuonyeshe maajabu yake kwa fedha hizi kwa miradi hii aliyoipanga. Mimi nasema ni fedha ndogo kwa miradi iliyomo humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba leo Wizara yake itapita kiulaini kwa sababu sote tumekufahamu. Ila nataka nizungumzie kama nilivyosema kwamba nataka nizungumzie suala la michezo. Lakini kabla sijaanza hapo, nina misemo miwili ambayo nimeikuta ulimwengu huu na mimi inanipa shida sana na siielewi maana yake. Sasa naomba mwenye kuelewa si lazima anijibu sasa hivi humu Bungeni, lakini anaweza kuniona popote akanieleza kwamba misemo yako maana yake ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna ule msemo unaosema pumbavu likipumbaa pumbaa nalo na likiingia msituni liachie, huu msemo unanisumbua. Msemo wa pili ni ule unaosema na unaimbwa na wasanii wa vikundi hasa katika Kisiwa cha Pemba wanasema, siharibu kisu changu kwa mnyama asiyeliwa. Sasa misemo miwili hii inanipa shida sana, naomba jibu kwa anayefahamu, anielimishe maana ya misemo hii miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze na suala la michezo kwa sababu misemo hii ilikuwa ikinikereketa sana, sasa niendelee na michezo. Ni juzi tu Jumatatu nilishuhudia sakata hapa hapa Dodoma la suala la michezo ya *football* na *netball*.

Michezo hii imeandaliwa na kanda ya Chamwino, lakini timu moja ya netball siku ya Jumatatu kwa majina siwezi kuzifahamu hizi timu, lakini timu moja ilituhumiwa kwamba eti wachezaji wake ni wanachama wa Chama cha *CUF* au Chama cha Upinzani. Sasa timu hii ikakataliwa kabisa kuendelea na michezo pale, nao wameshaingia katika usajili. Timu zote mbili zilifika uwanjani, lakini ile moja ikaambiwa hakuna ruhusa ya kucheza na *CUF,* mzozo ulitokea, tena likaanza sokomoko kali sana kiasi cha jamii kutokuelewana kwa sababu gani vijana wao wamekatazwa kuingia katika mashindano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa baadhi ya wachezaji wa *netball* wa timu hiyo waliotuhumiwa kwamba ni *CUF* mimi sina ushahidi kwa sababu walikuwa

wamevaa nguo za michezo na sio sare ya Chama. Nina wasiwasi kwamba watoto wale watakuja kuzuiliwa masomo yao kwa sababu ya kisiasa.

Bahati nzuri au mbaya uwanja ambao ungefanyiwa mashindano haya ni uwanja wa shule ya Chamwino. Sasa hoja inaweza ikaja hii shule ya Chamwino je, ni ya Chama cha Mapinduzi? Inaweza kuja hiyo hisia. Sasa kwa hili namwomba Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na suala hili aliingilie kati.

Leo asubuhi nimeonana na kiongozi wa timu hiyo iliyozuiliwa kucheza kwa sababu ni ya *CUF,* akaniambia kwamba wameambiwa ili waweze kucheza mashindano haya lazima wajaze fomu maalum ya kwamba wao ni wana CCM damu. Ikiwa Mheshimiwa Waziri unamhitaji kiongozi huyo, nitakuletea na msemaji wa neno hilo ni Diwani wa Kata hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge unam-*address* Mwenyekiti.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijakuelewa.

**MWENYEKITI:** Unaposema unam-address Mwenyekiti.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** *Oooh okay, okay.* Hata hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuelekeza, lakini nikasema namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye kushughulikia suala hili aliingilie kati. Kwa hiyo hili jambo ni suala zito sana na kwa sababu Chamwino ni hapa hapa Dodoma ningeomba leo au kesho lifuatiliwe suala hili ili liondoe utata mzima wa masuala ya michezo. Tukiingiza ushabiki wa Vyama basi linalotokea ni hivyo vilabu vikubwa vinavyoanza kufanya mizengwe yake na tutaona mbele nitazungumzia kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la michezo ya netball Chamwino naomba niishie hapo. Sasa naomba nizungumzie migogoro ya *FAT,* Chama cha Michezo. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Aziza kwa kunijulisha kwamba Waziri Kapuya ni mwanasimba damu na Mheshimiwa Mudhihir akiwa ni Naibu wake ni mwanayanga damu. Sasa nisieleweke kwamba labda na mimi ni mshabiki ama wa Yanga au Simba.

**MBUNGE FULANI:** Wewe wa Yanga, wewe wa *CUF.*

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba nilikuwa na hoja ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri lakini sasa hoja yangu imefifia kwa sababu nimeshamjua kwamba Waziri ni Simba ndio ile hotuba ya Wasemaji wa Kambi ya Upinzani au Kambi ya Upinzani ilivyoeleza kwamba Waziri leo anasema suala hili, kesho hili na keshokutwa lile kumbe ni sababu ya kwamba yeye ni Simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na sakata la mchezaji. Mchezaji huyu kwa kweli alitupa tabu sana kila siku tukinunua magazeti ni mchezaji huyu, mchezaji alikuwa ni wa Simba halali, akatoka kwa ridhaa yake akaingia Yanga na Yanga wakampokea, wakampeleka hadi Zanzibar, lakini matokeo yake mchezaji huyo huyo alisema leo mimi

ni Simba na nitapachika daluga zangu juu iwapo sitaruhusiwa kuichezea Klabu yangu ya Simba, eti tishio lilikuwa ni hilo la kupachika daluga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza cha kufanya ni kujiamini katika suala la michezo. Hata ingekuwa Diago Maradona Watanzania kwa mchezaji huyu basi bado tungemwambia ahsante pachika daluga. Kwa hiyo mtoto umleavyo ndivyo akuavyo na ndiyo maana kwa sababu *FAT* mpaka viongozi wakuu wa Serikali wanayumba ndio na wachezaji wakatufanyia vituko kama hivi. Leo tulisikia wachezaji kadhaa wa nje ya nchi walivyoikiza mambo mazuri katika nchi zao. Lakini sisi tunaanza kuzaa wingu la balaa. Sasa tunasubiri nini, mafuriko.

Baada ya maeneo hayo ya Chamwino na migogoro ya *FAT* nilisema kwa sababu ni nyota njema imechomoza kwa hotuba hii, nilikuwa sina mengi zaidi ya hayo kwa sababu wasemaji waliopita waliweza kuzungumzia maeneo mawili ambayo nilikuwa niyazungumze, lakini nahofia kurudia maneno yale yale ambapo kanuni zinatukataza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitamke wazi na kwa roho safi kabisa kwamba naunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Naomba nami niungane na wenzangu kwanza kwa kutoa salaam zangu za rambirambi kwa wafiwa na Ndugu wa Marehemu Comrade Kasapira na Mheshimiwa Yete Mwalyego. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza kwanza Waziri kwa hotuba yake nzuri na pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wenzao katika Wizara yao kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya japo wakiwa na ukwasi mkubwa wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizipongeze taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii ambayo inasimamiwa kwa umahiri sana na Waziri Profesa Alhaj Kapuya. Naipongeza sana *NSSF* kwa kazi kubwa ambayo inaifanya, wote tumeona kwa jinsi inavyobadilisha sura ya Miji mingi hapa nchini na pia katika kutoa huduma bora kwa wanachama wake na kuwajali pia wananchi raia ambao wana hali duni kwa kujenga nyumba za bei nafuu. Mimi nawashauri waendelee hivyo hivyo. Pia naipongeza *VETA* kwa kazi nzuri ambayo inafanya, imeenea katika sehemu nyingi na inatoa huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisisahau Taasisi nyingine kama *OSHA,* Ustawi wa Jamii na nyinginezo ambazo kwa kweli zinafanya kazi kwa hali ngumu kama Mahakama ya Kazi. Hapa kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumza kwamba kesi zinachukua muda mrefu, kwa kweli hali kule siyo nzuri na hizi Mahakama ziko chache sana na wafanyakazi ni wengi. Kwa hiyo tunaomba Serikali iangalie jinsi gani ya kuboresha huduma hizi kwa vile Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kuzungumzia Idara moja nyeti moja sana nayo ni ya Ustawi wa Jamii. Katika Taifa lolote ambalo limestaarabika linajali sana Ustawi wa Jamii yake na hivyo Idara za Ustawi wa Jamii katika Mataifa makubwa ni Idara kubwa sana. Idara ya Ustawi wa Jamii inahudumia walemavu, inahudumia watoto yatima, inahudumia wajane, inahudumia wazee na ina kazi nyingi sana. Lakini ukienda Mikoani hata Dar es Salaam penyewe ukifika katika Idara inayoitwa Ustawi wa Jamii utashangaa hata wazee wenyewe hawaoni sababu ya kwenda Ustawi wa Jamii kwa sababu haitiliwi maanani katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali iangalie upya mtazamo wake. Kwa sababu wazee hawa ndiyo waliotulea mpaka tumefika hapa tulipo. Walemavu ni wetu, yatima ni wetu, hii Idara ya Ustawi wa Jamii inahitaji kuwa na Maofisa wa Ustawi wa Jamii katika kila kata na siyo katika Wilaya tu. Katika kila Kata ili wao wafanye kazi kubwa ya kujua jinsi jamii inavyohudumiwa hasa katika wakati huu mgumu wa magonjwa. Tuna Maofisa Maendeleo katika kila Kata wale hawajui jinsi gani ya kuwahudumia au kuwafuatilia wagonjwa wa UKIMWI na hawajui jinsi gani ya kushughulikia wazee. Lakini hao wa Ustawi wa Jamii wanajua hayo. Naiomba Serikali ifikirie kupanua Idara hii na ipewe nyenzo ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie watoto yatima ambao wako chini ya Wizara hii. Watoto yatima ni dhahiri wote tunajua sasa wamepita kwa tafiti za *UNICEF* inaonyesha watoto takriban milioni 2.5 ni yatima na tumekuwa tukiona kwenye televisheni na tunasikia radio jinsi watoto yatima wanavyojilea wenyewe, jinsi wanavyolea wazee na jinsi wanavyopata taabu kwa kukosa huduma za muhimu. Jukumu hili Waheshimiwa Wabunge ni letu, sisi kama tukiwa ni wawakilishi wa wananchi na ni sisi ambao ndiyo tunaingia katika Halmshauri zetu, sisi wote hapa ni Madiwani tuhakikishe hao watoto yatima wanaingia katika bajeti zetu. Fedha zipo Waheshimiwa Wabunge *TACAIDS* ina fedha, Mashirika ya nje ya fedha na nyingine hawajui wazipeleke wapi kwa sababu hakuna mfumo mzuri wa kujua wampelekee nani? Hata hizi *NGOs* ni sisi Madiwani tunatakiwa tufanye kazi nao in *partnership* ili tuwafikie wenzetu wale ambao wanahitaji msaada wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile suala la yatima kwa Mheshimiwa Jackson Makwetta kule ni kitu kidogo tu. Mimi ninadhani kuna sehemu nyingine pengine wamezidi wa kule Makete. Kwa hiyo ile ni dalili kwamba tunahitajika tutoe huduma zetu na tuwaangalie wale watoto wameathirika kisekolojia. Mtoto anahitaji malezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo mimi naamini Wizara hii inalifanyia kazi na mikakati ipo mizuri isipokuwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zetu zinatakiwa zitoe msukumo wa jinsi ya kuwasaidia suala hili. Sasa hivi tena ule utaratibu wetu au mila zetu nzuri za kulea watoto yatima zimeshindikana kwa kuwa watoto yatima wenyewe ni wengi na hali ya kiuchumi hairuhusu, kwa hiyo lazima Serikali iliingie kati suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa nizungumzie suala la ajira ya vijana. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, amelizungumzia vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge

wengi wamelizungumzia. Vijana wengi wanazurura wako Mijini hawana kazi ya kufanya, lakini tukubali yale ni matokeo ya sisi wenyewe wale watoto hawakuweza kuendelea kusoma kwa sababu wazazi wao hawana uwezo. Kwa hiyo, sasa tuwasaidie tujue tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* inajitahidi inavyoweza kuwaelimisha katika kutoa mafunzo ya fani mbalimbali. Tunachokifanya sisi kama Serikali kinatofautiana na kidogo. Mimi ningependa niulize hawa vijana wa *VETA* wakimaliza wataajiriwa na viwanda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda vingine vimefungwa au vina-*produce under the capacity* kwa sababu *products* zake hazinunuliwi na Serikali na hazinunuliwa na sisi. Sasa hivi tumeingia ulimbukeni wa kununua vitu vya kutoka nje. Tulikuwa na viwanda vikubwa tu vikiajiri watu, vya *tiles* tumeacha kununua *tiles* za Tanzania tunanunua *Havey Tiles* sasa hata kwa nyumba za Serikali, kwa nini tusi-*suppor*t viwanda vyetu hivi. Kule katika Wilaya ya Ilala tuna kiwanda kikubwa cha matofali ya kuchoma *Kisarawe bricks* kitafanyaje kazi wakati wanunuzi hakuna? Lakini kwa kweli Serikali hata hizi nyumba inazozijenga sasa hivi ingekuwa inataka kuzijenga kwa kutumia matofali ya kuchoma vijana wetu wangeajiriwa. Kile kiwanda kina *capacity* ya kuajiri watu 4,000 hakiwezi kutengeneza matofali ya kuchoma kitamuuzia nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona afadhali tubadilishe utaratibu tukumbuke tunavyofanya mambo yetu kwamba kuna vijana wanaajiriwa. Uzalendo tumeupeleka wapi au ameondoka nao Marehemu Baba wa Taifa tu. Wale vijana mafundi seremala wametoka *VETA* wako mitaani wanatengeneza samani zao tunanunua akina sisi, Serikali inanunua *furniture* za *South African, furniture* za nje, za *Italy* na wapi hawa vijana wakauze wapi *furniture* zao. Juzi hapa tumelalamika magogo yanaenda nje, Serikali nunueni hizi *furniture* za vijana wetu ili muwa-*encourage* wafanye kazi. *(Makofi)*

Vijana hao hao mimi nashauri pia *Fish Industry* ikuzwe wasiishie kupaa tu wale samaki. Hakuna lolote linalofanyika kuwa-*support* hawa vijana, tunavyo vitu vya kufanya katika nchi hii, ardhi tunayo, bahari tunayo, Maziwa tunayo vijana kweli ni wa kuzurura hawa! Ni sisi tunatakiwa tufanye hii kazi sera nzuri za CCM zipo wenzetu zifanyieni kazi na sisi kama Wabunge wenu tutawa-*support* na tutawaonyesheni wako wapi hawa vijana ambao wanataka kufanya hizo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweza kutoa Sera ya Taifa ya Wazee. Kuna majukumu ambayo yametolewa mazito. Majukumu hayo yako katika ukurasa wa 14 yanazungumzia Serikali ina jukumu, Serikali za Mitaa ina majukumu yake na familia na vijiji vina majukumu yake. Jamani tutekeleze. Sasa hivi vijana tunakufa tunaacha wazee ule utaratibu wa zamani wa kusema atalelewa mtu na mwanaye umepita na wakati kwa sababu watoto wote wamekufa wamebaki vikongwe na vijukuu huko Vijijini na Mijini na hii tabia ya kufikiria ni Vijijini tu na Miji kuna vikongwe ambao wanapata taabu sana. Sisi uwezo hatuna, lakini kwa kweli ipo haja ya kutafuta Mfuko wa Wazee

na kwa kutumia Maofisa wa Ustawi wa Jamii waweze kuwa-*identify* hao wazee wanaopata matatizo wako wapi ili Mifuko hiyo iwasaidie wazee. Mimi siamini kama mzee wa miaka 70 bado anategemewa afanye kazi tunatakiwa tuwasaidie hao wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia kuhusu michezo. Naomba sisi kama Wabunge huko tunakokwenda kwenye Majimbo yetu ndiyo michezo inakoanzia michezo siyo Simba na Yanga tu. Michezo ipo inatakiwa ianze huko ambako tunaanzia na michezo siyo Ndolaga peke yake, Ndolaga amepewa jukumu la kuendesha michezo, na kama tunamwona ameshindwa ni watu wa huko huko wa vilabu ndiyo wanaomchagua. Sasa sisi ni wapiga kura wetu tunashindwa nini kuwambia ili wafanye vile ambavyo sisi tunataka. Hivi kweli tunashindwa kuongea na hivi vilabu ili watusaidie.

**MBUNGE FULANI:** Ipo rushwa ndani ya vilabu.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Rushwa kwenye michezo sidhani kama inasababisha tushindwe hata kuchagua wale ambao tunataka kuwachagua. Lakini mimi naamini hii Katiba mpya ambayo inataka kutolewa itatusaidia na nadhani katika gazeti leo mmeona kwamba rasimu imekwenda na *FIFA* nao wameleta maoni yao. Mimi naamini tunakokwenda kutakuwa kuzuri tusubiri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza nataka kuzungumzia kuhusu mishahara ya wafanyakazi. Wafanyakazi mishahara yao ni midogo sana hawawezi kumudu *basic needs.* Kwa hiyo, ipo haja ya kufikiria kuwaongezea mishahara. Mimi najua kima cha chini shilingi 50,000/= hakisaidii, akiumwa tu huyu mfanyakazi familia nzima inakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati inayohusiana na Wizara hii nimeletewa barua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho mchana wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo kutokana na pengine ufinyu wa muda sitapenda kuutawanya sana na nitauelekeza zaidi kwenye upande wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pengine niungane na Mheshimiwa William Shellukindo kwamba tunapojadili mustakabali wa michezo katika nchi yetu pengine ni muhimu tuka-*address issue* kuliko ku-*address personalities.* Ninaungana naye kwa msingi kwamba yapo mambo ya msingi ya kuzungumza kuhusu michezo na ya

kuzungumzia michezo kama chombo ama kama Idara nyeti ambayo inaweza ikasaidia sana katika maeneo mbalimbali ya kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulizungumza hili la michezo pengine mimi nijaribu zaidi kujikita upande wa misingi yenyewe ya michezo. Kwamba kama Taifa tuna umuhimu sasa wa kuanza ku-*address* tatizo la michezo kuanzia ngazi za Vijiji badala ya kuzungumzia michezo katika *level* ya juu kama Simba na Yanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini na nina imani watu wote ambao wanaitakia nchi yetu mema wanaamini kwamba chimbuko la michezo ni lazima lianze angali vijana wetu wakiwa na umri wa mdogo. Sasa kuwatayarisha vijana wetu kama wanamichezo wa kesho pamoja na kuboresha afya zao na miili yao katika hatua zao za maisha za awali zinawezekana zikafanyika kama Wizara zinazohusika zitashirikiana katika kuweka mkakati na programu ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili na ninashaukuru Mheshimiwa Joseph Mungai Waziri wetu wa Elimu na Utamaduni yuko hapa, nina hakika atalitilia maanani. Mimi nina imani kabisa kwamba kuna umuhimu wa kipekee kuanza mkakati maalum wa kuimarisha michezo katika shule zetu na hasa kuanzia shule za msingi. Pamoja na kwamba michezo au yale mashindano baina ya shule na shule yalisimamishwa kwa sababu ya kupunguza muda wa watoto kusoma. Lakini bado nina imani kabisa kwamba mitaala ya michezo inaweza ikaimarishwa kwenye shule za msingi sambamba na mfumo mzima wa kuboresha elimu katika taaluma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze vilevile kwamba ili michezo sasa basi iweze kuimarika kuna ulazima wa kuimarisha miundombinu ya michezo, na miundombinu ya michezo tunavyoizungumza hatuizungumzii katika upande mmoja wa kujenga uwanja mpya wa kisasa Dar es Salaam. Tanzania ni nchi kubwa na ni nchi ina Mikoa 26 na tuna viwanja vingi vya michezo ambavyo tayari vilijengwa miaka mingi ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakumbuka kwamba katika miaka ya sabini na miaka ya themanini kulikuwepo na wimbi kubwa la Watanzania kujenga viwanja mbalimbali vya michezo. Viwanja mbalimbali vya michezo vilijengwa katika nchi yetu nzima kwa kushirikisha nguvu za wananchi, nguvu ya Serikali na hata Mashirika kadhaa yaliyokuwa ya umma. Kuna kiwanja cha Kirumba ambacho ni kizuri kikiboreshwa kina hadhi ya Kimataifa, kuna kiwanja cha Maji Maji Songea, kuna kiwanja cha Amri Abeid Arusha, uwanja wa Jamhuri wa Dodoma, kiwanja cha Mkwawani Tanga, uwanja wa Ali Hassan Mwinyi Tabora, uwanja wa Samora Iringa, uwanja wa Sokoine Mbeya, uwanja wa Ilulu Lindi, uwanja wa Umoja Mtwara, uwanja wa Kambarage Shinyanga na viwanja vingine vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi leo tukajidanganya kama Taifa kwa kujenga uwanja moja wa Dar es Salaam tukawa hatuna mkakati wa kujenga miundombinu ya michezo katika Mikoa yote ya nchi yetu. Kwa sababu uwanja wa Kimataifa wa Dar es Salaam unaokusudiwa kujengwa utatumika kwa ajili ya michezo ya Kimataifa zaidi. Lakini bado hatutakuwa na watu wa kucheza katika uwanja huu wa Dar es Salaam kama

tutakuwa hatujaimarisha viwanja vingine kwenye *peripheries* ambavyo vitachangia sasa basi wachezaji wa kucheza kwenye uwanja huo wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vyote ambavyo nimevitaja hapa ni viwanja ambavyo kwa njia zisizoeleweka baada ya kuanza Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa vilisemekana ni viwanja vya Chama cha Mapinduzi. Sasa mimi nasema siyo vya Chama cha Mapinduzi ni viwanja vya Taifa kwa sababu vinatumika kwa Watanzania wote, kwa vijana wote wa Kitanzania na vinahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi la kuwa viwanja vya Chama cha Mapinduzi halinisumbui sana. Linalonisumbua zaidi ni namna Chama cha Mapinduzi kimeweza kuendeleza viwanja hivyo baada ya kuvichukua. Wote ni mashahidi na tukiweka mambo ya ushabiki wa kisiasa pembeni hali ya viwanja hivi vyote ni mbaya. Labda nitumie lugha ya kutaifishwa. Tangu baada ya hivi viwanja kutaifishwa mwaka 1992 na Chama cha Mapinduzi viwanja hivi havikuendelea tena kujengwa vile ambavyo vilikuwa havijakamilika hakuna tofali moja lililoweza kujengwa. Sasa hili suala ni kwa hasara ya nchi yetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa uhakika kabisa kwa sababu nimetembelea viwanja vingi katika viwanja hivi, kwa kweli hatujui wenzetu wana programu gani ya kuendeleza viwanja hivi, na sioni ni sababu gani itakayozuia wasibebe lawama kwa kudumaza michezo kwa kuua miundombinu ambayo ilijengwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni katika ngazi ya Mkoa. Mimi ninahoji Serikali ina mpango gani na masuala ya michezo katika ngazi za Wilaya. Katika Halmashauri nyingi nchini hakuna kabisa mikakati yoyote wala mipango yoyote ya michezo. Kwa hiyo, vijana wengi mara kwa mara wamekuwa katika maeneo ya kujihusisha na mambo ya ulevi, mambo ya ufusika na hatimaye mambo ya ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu kwa kweli wako *idle* na vijana wako *idle* kwa sababu hawajawekewa mkakati wowote wa Kiserikali au wa kijamii ambao utawafanya washiriki katika michezo, na hivyo kujiimarisha kiafya na hatimaye vilevile kutumia muda wao wa ziada kufanya mambo ambayo pengine siyo uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba sasa ni vyema Serikali kwa kupitia Wizara zote zinazohusika uwe kama mkakati wa Kitaifa. Ninaishukuru Serikali na Idara mbalimbali za Serikali zimeona ugonjwa wa UKIMWI kama suala linalohitaji mkakati wa Kitaifa na Idara nyingi za Serikali zimeshirikishwa katika kupiga vita UKIMWI. Lakini suala la michezo bado nafikiri tumeliona kama ni *secondary issue,* siamini kabisa kweli kama nchi na sisemi kama Chama ama kama Idara au kama Wizara kama nchi sijaona kama kweli tumeona michezo kama ni *economy force* kama ni kitu ambacho kinaweza kikatumika kwa ajili ya kuboresha uchumi, kuongeza mapato ya Taifa, kuongeza mahusiano mazuri ya ki-*diplomacy* na nchi mbalimbali na hata kujenga utalii na jina la nchi. Tunaona wenzetu kwa mfano Kenya, maana yake pengine nchi yetu

tunafikiri michezo ni mpira wa miguu peke yake. Asilimia 90 ya mazungumzo ya michezo katika nchi yetu yanazungumzia mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Kenya imeweza kujitangaza dunia nzima kwa ajili ya riadha peke yake. Nchi kama Ethiopia na Morocco zimeweza kujitangaza dunia nzima kwa ajili ya michezo tena hususan mbio za kati mita 5,000 na mita 10,000. Sasa vitu kama hivi ni vitu vya msingi. Nchi kama Cuba imeweza kujiendeleza kimichezo dunia nzima kwa nyanja moja ya ngumi za ridhaa not professional boxer ni hizi ngumi za *amateur* . Lakini tunajiuliza sisi kama Taifa *priority* yetu iko wapi? Mimi naomba kabisa Serikali ikae ilizungumzie hili suala tusione suala la michezo kama suala ambalo labda halina msingi wala halina maana kwa Taifa letu. Halmashauri za Wilaya zinastahili kuwa na programu zake za michezo kwa sababu hata ukisoma taarifa za Wizara hakuna taarifa yoyote inayoongelea programu za michezo ya aina mbalimbali katika ngazi ya Wilaya au katika ngazi ya Mkoa. Sasa mimi nasema huu ni upungufu mkubwa kwa sababu kule ndipo hasa penye vyanzo vya wachezaji na misingi ya wachezaji katika ujumla wake. Sitakuwa nimemtendea haki Mheshimiwa Rais kama sitampongeza kwa juhudi basi angalau za kujenga huo uwanja mmoja wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni vyema vilevile nikumbushe kwamba Mheshimiwa Rais pamoja na majukumu mengi makubwa aliyonayo anabidi kulea Watanzania katika michezo kwamba uwanja mmoja ameufanyia kazi kwa nguvu kubwa sana, lakini Tanzania ni kubwa anamaliza miaka yake 10 sasa Mheshimiwa Rais wetu. Lakini vilevile ajaribu kwenda kwenye michezo kuwaongezea nguvu akina Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na Mudhihir Mudhihir kwa sababu mara kwa mara Mheshimiwa Rais amekuwa kidogo ametingwa na shughuli na anakosa muda wa kutosha kwenda michezoni.

Kwa hiyo, ni vyema akawasaidia wachezaji kwa kutia motisha angalau kwa mara moja kabla hajamaliza muda wake aende uwanja wa Taifa akawatia vijana wake moyo hasa Timu za Taifa zinavyocheza kama Marais wa nchi nyingine wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu tena kusisitiza kuhusu suala la viwanja vya michezo. Mimi nashauri kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi kutoka pande zote wamelizungumza hili na hata Serikali imelizungumza kwa muda mrefu. Mimi nilikuwa nashauri jambo moja la msingi sana kwamba viwanja vya michezo siyo vile viwanja tu vya kuchezea mpira miguu ni hata yale maeneo ya wazi ambayo Watanzania na watoto wetu wanacheza ama wanajipumzisha. Wizara hii ina majukumu makubwa kwa sababu Wizara hii inashughulika na mambo ya kazi na mambo haya yana utata na migogoro mingi, inajihusisha na masuala ya Maendeleo ya Vijana na Michezo. Sasa kama vile ambavyo Serikali imechukua hatua mbalimbali ya kuimarisha baadhi ya Idara ambazo inafikiria ni nyetu kwa kuunda *Agency* ama Wakala Huru. Mimi ningeshauri kabisa Serikali iangalie uwezekano wa kuunda Wakala Huru wa kushughulikia viwanja vya michezo na maeneo ya wazi. Baada ya *Agency* hii kuundwa iweze mara moja kupima maeneo yote ama kutathmini maeneo yote ambayo yalikuwa yamepimwa kwa ajili ya shughuli za michezo na ambayo bado yapo ama ambayo yamevamiwa. Kwa yale

maeneo ambayo yamevamiwa ningeshauri kabisa *Agency* hiyo kwa kushirikiana na Serikali ifanye yale yale ambayo Mheshimiwa John Magufuli amekuwa anayafanya ya kubomoabomoa vitu vyote na vitega uchumi vyote vilivyojengwa katika maeneo ya wazi na hapo litakuwa funzo kwa watu kutovamia maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambayo yalikuwa yametengwa kwa ajili ya michezo ya watu yamevamiwa na wafanyabiashara, mengine yamevamiwa na viongozi ama washirika wao na ndiyo sababu kunakuwa na utata mkubwa katika Serikali kwenye kufuatilia suala hili. Mimi ninashauri kabisa kama tunataka kuwa *serious* na kuondoa uozo ama upungufu huu katika siku za usoni basi kwa kweli Agency hii ishughulikie kwa kuangalia zile *Master Plan* za Miji yetu ambazo zilikuwa zimetenga maeneo ya wazi ili maeneo hayo yaweze kuchukuliwa tena kama nyumba zimejengwa zibomolewe yaachwe maeneo ya wazi kwa ajili ya huduma za michezo kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kumalizia niishukuru Wilaya ya Hai. Kule kwenye Jimbo langu la Uchaguzi nilianza mkakati wa michezo baada ya kugundua vijana wengi kwa kweli wanakaa bila michezo na tuliweza kuanza mpango wa michezo ambao ulihusisha vijiji vyote katika Wilaya na hatimaye katika Kata na sasa hivi tuko katika ngazi ya Wilaya. Tulipoanza mpango ule wengi walifikiria labda ni mpango wa kisiasa wakitegemea pengine Mheshimiwa Freeman Mbowe anataka umashuhuri wa kisiasa kwa michezo. Lakini ukweli lengo lilikuwa ni kuwasaidia vijana wale ambao wengi wao walikuwa hawana cha kufanya.

Kumekuwa na mafanikio makubwa na michezo ile imesimamiwa na Chama cha Mpira cha Wilaya ya Hai kwa kushirikiana na hata Halmashauri ya Wilaya. Ninaomba niwashukuru hata Mkuu wa Wilaya naye alishiriki hata kufungua michezo hiyo. Mimi ninaomba niwashukuru na nishauri Halmashauri nyingine zote nchini zijaribu kuangalia uwezekano wa kutumia Chama cha Mpira kule katika ngazi ya Wilaya badala ya ngazi ya Wilaya ya Chama cha Mpira kutumika tu wakati wa kwenda kufanya uchaguzi Mkuu wa *FAT* na kuwachagua viongozi. Kwa sababu tuna viongozi wengi katika ngazi ya Wilaya ambao hawafanyi kazi yoyote wanachofikiria wao ni kwenda kuwachagua viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kutokuunga mkono hoja hii. Naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Joseph Mungai lakini tuna dakika mbili.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi nimeona kwa ninalotaka kulisema nitumie tu dakika hizi zilizobaki kwa sababu ni kwa kifupi kabisa kukumbusha kifungu 49(8) ukurasa wa 34 wa kanuni, kinasomeka kama ifuatavyo:- “Katika mjadala wowote Mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya

nyadhifa zao, Wabunge wengine wote watatajwa kwa kutumia neno Mheshimiwa kabla ya majina yao."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kanuni inazidi kukiukwa mara nyingi sana hata Mheshimiwa Freeman Mbowe sasa hivi amesema nafurahi na Mheshimiwa Joseph Mungai Waziri wa Elimu na Utamaduni yupo hapa. Hata katika hotuba zetu nyingine Mawaziri tumeandika tunatajana kwa majina. Sasa nilikuwa napenda kuchukua nafasi hii kukumbusha kwamba kifungu hicho ndivyo kinavyosema. Nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ni kweli kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wako hapa kwa nyadhifa zilizowaweka na sisi Waheshimiwa wengine basi ndiyo tunatajwa kwa majina yetu. Kwa hiyo, nadhani tutazingatia hilo.

Waheshimiwa Wabunge kwa jioni itakapofika saa 12.00 itabidi Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika waanze kujibu hoja zao. Kwa hiyo, wataozungumza jioni ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Stephen Kahumbi na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. Kwa hiyo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tulipoahirisha Bunge mchana tulibakiwa na wenzetu wanne. Tunaanza na Mheshimiwa Venance Mwamoto atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia kidogo.

Kwanza nianze kwa kutoa pole nyingi kwa wenzetu ambao wametutoka katika kipindi hiki cha Bunge hili. Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Comrade Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, "Haijapata Kutokea". Wote wawili wametutoka katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kutoa pongezi kwa Wizara hii na hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na wataalamu wake. Hotuba imeandikiwa vizuri sana kama kawaida. Lakini kama jina la Wizara lilivyo kifupi chake *KVM* maana yake "Kapuya Vumilia Matatizo". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara ambayo inawagusa vijana, walemavu, inagusa sheria na migogoro mingi. Kwa hiyo ni Wizara ambayo ina ugumu wake. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mpaka leo Waziri wetu hajapata kipigo kwa sababu Mawaziri wenziwe walionja joto la jiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuamua kujenga kiwanja kizuri ambacho kwa kweli kimeonyesha kwamba kitageuza sura na dira ya nchi yetu kwenye nyanja ya michezo. Uwanja ule maana yake ametuelekeza kwamba anatutengenezea ajira kwa vijana. Wabunge wengi wamelalamika kwamba vijana wengi wanamaliza masomo lakini wamekosa ajira. Sasa mimi nilikuwa nataka kutoa pendekezo kwamba sasa zawadi hiyo ambayo Rais wetu ametuachia na sisi tumpe zawadi, zawadi ambayo sisi tunapaswa kumpa ni kuanzisha soka ya kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kazi ya kuanzisha soka ya kulipwa ina utaratibu wake. Kwa sababu soka ya kulipwa haitaanza mkiwa na Viongozi wababaishaji. Kwa sababu watu wengi watawekeza kwenye michezo. Sasa anapowekeza mtu anatoa fedha hategemei kuona kwamba kuna ubabaishaji kwa upande wa Viongozi na waamuzi na wachezaji. Kwa hivyo ikabidi vilabu vyote vitakavyokubali visajiliwe kisheria na kuwe na vyama huru ambavyo vitasajiliwa kisheria ambapo vitaungana na wenzetu shirikishi *FA*T na *FIFA* vyama itabidi viwe na Wanasheria wake ambao watawasaidia kuangalia mambo yanavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niwaombe Wabunge wenzangu kwamba suala la kujadili watu ni kuwapa umaarufu wa bure. Sasa hivi kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbowe pamoja na Mheshimiwa Mbunge wetu wa vijana hapa ni kwamba twende kwenye rasimu ya Katiba tuirekebishe ile. Kwa sababu sasa hivi vyama vyetu vinakuwa vinababaisha kwa sababu hatuna rasimu ya Katiba nzuri. Cha kushangaza tu ni kwamba Katiba yetu ambayo imekuwa ikitengenezwa mpya imepelekwa kuonwa na watu wa *FIFA* wakati sisi wadau wa Tanzania tumekosa nafasi ya kuijadili na kuiangalia.

Sasa ningeshauri Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na kuwa rasimu hiyo ya Katiba imeshapelekwa *FIFA* na wenzetu wa *FIFA* na wameifanyia marekebisho basi na sisi tupewe nafasi kama wadau tuweze kuwasaidia kuiboresha. Kwa sababu kelele zote ambazo zinakuwepo ni kwa sababu ya watu wana mapenzi katika michezo. Kwa hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri ufanye jitihada za lazima ili hata sisi Wabunge kupitia *Bunge Sports Club* tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu BMT. Kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Iringa nimshukuru sana Waziri Kapuya pamoja na Baraza kwa uamuzi mzuri wa kuamua kuufungulia Mkoa wa Iringa kuendelea na michezo. Mambo ambayo yalipelekea kuufungia Mkoa wa Iringa katika michezo ukisikia na kuelewa ni vitu vya aibu. Kwa sababu Viongozi walitoa maamuzi kutokana na matatizo na ugomvi wa binafsi. Sasa kwenye michezo hii tukiingiza ugomvi binafsi hatutafika. Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba bado Bunge la mwaka jana nilitoa mapendekezo kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza apewe meno. Lakini mpaka leo Mheshimiwa Bendera bado ni kibogoyo. Meno yake hayafanyi kazi ni ya *plastic* kwa sababu hajapewa uwezo wa kuamua kwa sababu kwenye Baraza ndiko kuna wataalamu. Lakini mambo mengi yamekuwa ya kubabaisha kidogo. Wale ambao hawana

nia nzuri na Mheshimiwa Waziri Kapuya ndiyo wanamletea mambo ya kubabaisha aonekane hafai. Mimi naamini kabisa Mheshimiwa Kapuya anafaa vizuri tu. Mheshimiwa Naibu wake anamshauri vizuri tu na ukijua kama kweli wao sio wao wanaofanya hivyo ila kwa shinikizo unaangalia yale maamuzi ambayo yanapelekea wenzetu wa vyama vingine kukata rufaa BMT wanapeleka rufaa ambazo hazina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kuna vitu ambavyo niliviomba Wizara hii ivifanyie marekebisho. Mojawapo ni kuomba Wizara yake iongeze ruzuku kwa BMT kwamba waongezewe asilimia 30 lakini kitu hicho hakikufanyika. Pia nilimuomba Mheshimiwa Waziri afanye marekebisho ili kanuni zao zirekebishwe kitu ambacho nafikiri hakijafanyika. Pia niliomba ofisi zile za BMT ziweze kutengenezwa upya lakini ukienda pale utashangaa kama kweli wanaishi binadamu. Mimi nilivyofika kwa mara ya kwanza nilifikiri ndiyo Iraq kwa kweli. Kwa sababu utafikiri wamepigwa na mabomu jana. Wakati Wizara hii ina watu ambao wanajua kufanya kazi kwa mfano hata *NSSF* tukiwapa pale wafanye ile kazi itafanyika vizuri. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri baadaye utakapokuwa unatujibu basi itabidi utupe maelezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningeomba kifanyike ni kwamba unapoingiza vyakula kutoka nje ya nchi mara nyingi tunavipeleka *TBS* kwanza vinakaguliwa ili tuone ubora wake kama vinafaa kuliwa na binadamu. Lakini kitu cha ajabu makocha wameingizwa nchi hii bila ya kwenda kupimwa kwamba kweli ni makocha au watu wameokotwa. Mfano mzuri tumeona kocha wa Yanga kwa taarifa ambazo tumezipata inaonekana yule kocha sio kocha. Sasa hii ni ubabaishaji wa soka. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri uwape meno pia BMT ili waweze kukufanyia kazi yako kwa sababu wao ni wataalamu.

Pia naungana kabisa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwamba ili soka ubabaishaji uishe nafasi ya Katibu Mkuu wa *FAT* iwe ni ya kuajiriwa, kwa sababu yule ndiyo mtendaji. Yeye ni mtendaji na ni mtaalamu wa soka. Kwa hiyo, ni vizuri tukatoa nafasi ikawa ajira kama zamani. Walikuwepo marehemu Katibu Gwivaha, aliwahi kushika nafasi hiyo na wengine na kadhalika. Kwa hiyo, tungerudisha iwe rahisi kwa Serikali ku-*control* chombo hicho. Kwa sababu sasa hivi ukiangalia Mheshimiwa Kapuya hana uwezo nacho kwa sababu mwenye maamuzi yote ni *FIFA* yeye hawezi kufanya chochote. Kwa hiyo, ili kukipa nguvu basi tuongeze hicho kipengele kwamba Katibu Mtendaji Mkuu awe wa kuajiriwa na Serikali iwajibike mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niwapongeze sana wenzetu wa *NSSF* mambo ambayo yamefanyika sio siri kila mmoja ameona, wana mipango mizuri, wanafanya kazi nzuri na sasa hivi wanategemea kujenga daraja la Kigamboni. Lakini kikubwa ningependekeza kwamba Serikali ishirikiane na watu wa *NSSF* na waweke makubaliano ya kibiashara na *NSSF* ili chombo hicho kiweze kuchangia maendeleo.

Lakini bado Serikali inakuwa na kigugumizi. Kwa mfano hata uwanja ambao unajengwa na wenzetu wa kutoka China wangepewa *NSSF* tungekuwa tumemaliza. *NSSF* hawana mkopo benki yoyote ni chombo cha Serikali na kinachangiwa na wananchi. Kwa hiyo nafikiri muangalie vitu kama hivyo kwa maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukumbi wetu wa Bunge mpya *NSSF* wapewe waujenge ili wajenge kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. Nichukue nafasi hii pia niwashukuru sana na kuwapa pongezi wenzetu wa *VETA*. *VETA* wamefanya kazi nzuri nchi nzima na pendekezo langu ni kwamba wale vijana wanaomaliza *VETA* wanapotoka Serikali iwagharamie wapewe *tools* kama ni fundi magari basi anatoka na *tool box* yake akitoka pale anakwenda kujiajiri badala ya kusubiri ajira ambazo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la UKIMWI linateketeza sana katika Wizara yetu hii ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo sababu ndiko kwenye wadau wa kwanza. Kwa hiyo, mimi ningependekeza kwamba tuanzie kuyaondoa matangazo ambayo yanaonekana hayafai mfano yale maneno usione soo mengi yanachangia zaidi kuhamasisha UKIMWI. Badala ya kuleta yale matangazo ya kupapasana basi tuweke matangazo ya wagonjwa au makaburi ya watu ambao wameathirika ili watu kidogo waogope. Kwa sababu yale yanaashiria kwamba kitu hiki kinachofanyika kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la walemavu naomba liangaliwe vizuri kwa sababu sisi sote hapa ndani ni walemavu watarajiwa. Kwa hiyo unapozungumza suala la walemavu tuliangalie kwa makini. Wanatakiwa wasaidiwe wawekewe sera yao vizuri. Mheshimiwa Margareth Mkanga peke yake hawezi, lakini amejitahidi kupiga kelele sana na nichukue nafasi hii niwaambie kabisa walemavu wengine kwamba mama yetu Mheshimiwa Margareth Mkanga anawatetea kwa nguvu zote. Kwa hivyo ni mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya wazee niipongeze kwa jinsi ambavyo mmeiweka kwa sababu sisi sote ni wazee watarajiwa. Tuiweke vizuri kitu ambacho baadaye kitatusaidia wenyewe huko tunakokwenda. Leo hii uko kwenye madaraka na lina nafasi kutengeneza mambo vizuri ili baadaye utakavyotoka mambo yale yakusaidie. Uwekezaji wa mpira au michezo kama nilivyosema unahitaji gharama. Kwa hiyo lazima tukubali kugharamia pamoja na kukiweka vizuri chuo chetu cha Malya cha Michezo ambacho Mheshimiwa Richard Ndassa kwa kweli amekuwa msitari wa mbele kuhakikisha kwamba michezo inakwenda vizuri. Kwa hiyo kile chuo basi kijengwe na kingine kama vile pale Kilolo na sehemu nyingine ili kile cha Malya kiwe Chuo Kikuu.

Nichukue nafasi hii niwashukuru sana wenzetu wa *NSSF* ambao kwa kweli walitoa ahadi yao nategemea itatekelezwa pale Ilula na tukimaliza hapa nafikiri baada ya miaka mitatu mtakuwa na soko zuri la Kimataifa pale Ilula. Wenzetu wa Dodoma, Mbeya na Iringa watanufaika nalo. Nakuhakikishia hiyo itakuwa ni lengo zuri na faida kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia niwashauri wenzetu wa Wizara hii kwamba bado wanatakiwa washirikiane na Wizara ya Serikali za Mitaa ili wawekewe fungu la fedha kuhamasisha michezo katika nyanja mbalimbali. Kitu kingine cha kushangaza ukiangalia fedha zimepangwa kwa ajili ya maendeleo ya michezo utashangaa hakuna hata senti tano. Kama fedha haikupangwa kwa ajili ya michezo tunategemea

kwenda kushiriki kwenye *Olympic,* tuna Timu ya Taifa hivi tutasikia kiini macho. Kama tutafanya vizuri kwa hiyo baadaye Mheshimiwa Waziri usiponieleza vizuri tutabanana. Naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu hotuba ya Waziri wa Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo. Naanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii pamoja na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya tukizingatia kwamba kama walivyosema waliotangulia Wizara hii ni Wizara ngumu ambayo inafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kuzungumzia suala la ajira mbaya kwa watoto. Napenda niishukuru sana na kuipongeza Wizara kwa kazi inayofanya ya kuhamasisha jamii kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wananchi kwa ujumla kuweza kuhakikisha kwamba watoto wanatolewa kwenye ajira mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa sana na nikizungumza hilo nazungumzia Mkoa wa Iringa ambao watoto wengi na hasa watoto wa kike wanachukuliwa kwenda kufanya kazi katika miji mikubwa na hata nje ya nchi. Napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili tatizo kwa undani naelewa kwamba kuna programu ya Serikali inashirikiana na Shirika la *ILO* chini ya mpango wa *IPEC*. Lakini mradi huu unajumuisha Wilaya tatu tu na sio kila Kijiji. Sasa mimi namwomba Mheshimiwa Waziri kwa upendeleo maalum na wa makusudi kabisa Mkoa wa Iringa uingizwe kila Wilaya au zitafutwe juhudi zingine za kuhakikisha kwamba kila Wilaya, Wilaya zote saba yaani Ludewa, Makete, Njombe, Mufindi, Kilolo, Iringa Vijijini na Mjini zote zifikiwe kwa sababu tatizo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumza mwezi wa Septemba watoto wakishamaliza darasa la saba, watoto wote wanaondoka Vijijini na kuna watu ambao wameanzisha Makampuni ya kuja kuwachukua hawa watoto kuwakusanya kuwapeleka huko Dar es Salaam na maeneo mengine. Serikali inawajua hivi inafanya nini kuwafungia hawa watu. Wanakuja wanawadanganya wazazi huko watoto wenu wanakwenda kupewa ajira za maana, kumbe watoto wanapelekwa kwenye ajira mbaya na kupelekwa pia kwenye madanguro. Mimi naomba Wizara Mheshimiwa Kapuya wewe ni mtani wa Wahehe naomba usaidie hiki kitu kabisa. Tunaomba utusaidie tatizo ni kubwa kiasi kwamba mkoa hauwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapofanya ziara zangu ninapoongea na wanawake, wanawake wanasononeka. Kuna mahali walifika wakaniambia hata sasa watoto wa kiume hawana hata wasichana wa kuoa huko Vijijini. Watoto wote wa kike wameondoka na wanarudi wakiwa wagonjwa. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie mikakati maalum ambayo inaweza kusaidia lakini iwe kila Kijiji na mikakati hii iendane na kuwapa shughuli za kufanya. Sio kuwakataza tu kutokwenda Dar es salaam au kutokwenda mahali pengine hawana shughuli za kufanya. Tuhakikishe

kwamba hawa watoto tunawatayarisha wapate shughuli za kufanya ikiwa ni pamoja na miradi midogo midogo, waweze kufanya hivyo wabaki Vijijini. Wakati mwingine inashindikana kubaki Kijijini kwa sababu hawana shughuli za kufanya na umaskini unawafanya waondoke wengine wakiwa mayatima pia. Kwa hiyo, naomba Wizara ilitazame hili tatizo kwa jicho la aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo naomba nizungumzie suala la yatima. Tatizo la yatima ni kubwa kama walivyozungumza wenzangu sasa hivi watoto wanazidi milioni mbili. Sasa naomba niiombe Wizara sasa hivi tuangalie kuanzisha mfuko maalum wa kuhudumia hawa watoto na kila mtu achangie kama tunavyochangia Mfuko wa Elimu. Uwekwe mfuko ambao utaweza kusaidia kwa sababu tukifikiria tu hii miradi tunayofanya na shughuli tunazofanya itafika mahali Serikali itashindwa.

Lakini kama kutakuwa na mfuko maalum ambao utakuwa kila mtu atachangia tunaweza tukahakikisha kwamba watoto hawa wanapata huduma bora. Kwa sababu hawana malazi, nyumba wengine hawapati elimu hata fedha tunazopanga hapa hazitoshi kuweza kuwasomesha watoto wote hawa. Kwa hiyo mimi nilikuwa naiomba Wizara iangalie sasa utaratibu mpya. Mheshimiwa Waziri aje na utaratibu wa kuweza kuanzisha mfuko maalum wa kuweza kusaidia watoto hawa na nina uhakika akileta humu Bungeni Waheshimiwa Wabunge tutaunga mkono kwa sababu wote tunakabiliwa na tatizo hili katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie hili suala la wazee. Suala la wazee ni tatizo kubwa sana na naipongeza Wizara kwa kuweza kutayarisha sera ya wazee. Kwa kweli hii ni hatua moja kubwa sana kuweza kuwa na sera ya wazee. Naomba niwapongeze sana. Sera hii inatakiwa itolewe elimu huko Vijijini kuweza kuitafsiri hii sera ili wazee waelewe na wananchi wote waweze kuelewa hii sera ina maana gani na pia tuweze kuitekeleza. Nichukue kwa mfano wa matibabu iko wazi kabisa kwamba wazee wanatakiwa wapate matibabu bure.

Lakini watakapokwenda zahanati au hospitali mara nyingine hizo dawa anazohitaji hazipo na hawana mahali pa kuzipata. Sasa kutokana na hii sera nzuri kabisa niliyoiona, Wizara iangalie utaratibu wa kuwa na sehemu ambazo wazee wakienda kupata huduma kama hizi waweze kuzipata na kama ni madawa waweze kuyapata.

Lakini pia namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hata sisi Iringa kupata kituo cha wazee. Nimeona mikoa mingine ina vituo. Hawa wazee wanaokuwa hawana mtu wa kumtunza hata ndugu hayupo tupeleke wapi Mheshimiwa Waziri tupeleke mikoa mingine? Mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni jambo la muhimu angalau kila mkoa ukiwa na kituo kwamba wale wanaoshindikana kabisa kuwa na ndugu wa kuweza kuwatunza basi wahudumiwe kwenye kituo.

Sasa sehemu nyingine kuna vituo vya Serikali kwingine hakuna, vigezo gani vilivyotumika kuweka vituo kwingine viwili na kwingine havipo. Mheshimiwa Waziri aangalie sehemu ambazo hazina vituo kama Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala la walemavu. Suala la walemavu ni tatizo na walemavu wana ulemavu wa aina mbalimbali na tunao huko kwenye jamii, lakini huko kwenye jamii hakuna mpango wowote wa kuweza kuwasaidia. Kama alivyosema Mheshimiwa Mkanga anafanya kazi nzuri sana, lakini kwa vile yuko peke yake sio rahisi kuweza hata kuwafikia walemavu wote. Sasa mimi naiomba Wizara hii iweze kuhakikisha kwamba walemavu, elimu ya kuelimisha jamii kuhusiana na suala la ulemavu litiliwe umuhimu. Pia kuhamasisha jamii kujali walemavu huko tuliko kwenye maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na sisi Wabunge tutashiriki lakini pia Serikali ihakikishe kwamba suala la walemavu linatiliwa umuhimu. Walemavu wapo Vijijini hawajui hata mahali pa kwenda. Hajui aende wapi kutoka katika Kijiji chake.

Hata yule mzazi ambaye ana ulemavu hajui ampeleke wapi. Hakuna mahali kwenye Wilaya kulikoandikwa kwamba ukiwa na mlemavu labda anaweza kupata huduma mahali fulani matokeo yake anakaa naye tu nyumbani, labda wakati nyingine ulemavu ule ungeweza hata kutibiwa kutokana na aina ya ulemavu lakini hana pahali pa kwenda. Mwongozo gani ulioko mpaka kwenye ngazi ya Kijiji kuweza kuhudumia hawa walemavu.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba Wizara kwa mipango mizuri iliyonayo na kama nilivyoona kwenye kitabu cha bajeti kilichoandikiwa vizuri sana, hotuba ya Mheshimiwa Waziri hili suala sasa liangaliwe ili angalau kila Kijiji kiulizwe kina mpango gani wa kuhudumia walemavu. Iwe ni *agenda* ya kujua mna walemavu wangapi hapa na mna huduma gani mnayoipata. Hata maelekezo pia ukijua kwamba una walemavu wa aina hii kuna huduma za aina fulani ambazo zinaweza kusaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukipongeza Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Taasisi hii inafanya kazi kubwa na ni Taasisi pekee ambayo inatoa wataalamu wa Ustawi wa Jamii ambao wako huko kwenye jamii huko Vijijini na kwenye Kata na hata kwenye Serikali. Mimi nilikuwa naomba Taasisi hii iongezewe fedha ili programu zingine zipangwe ili ihakikishe kwamba inatoa wataalamu wengi wa Ustawi wa Jamii ambao wanahitajika sasa mpaka kwenye ngazi ya Vijiji na Kata. Uandaliwe mpango mahsusi kama tulivyoweka mpango wa kufundisha Walimu. Basi na wataalamu wa Ustawi wa Jamii wafundishwe wengi ili kuweza kukidhi mahitaji makubwa ambayo yako kwa sasa. Ninaomba hilo pia Mheshimiwa Waziri aliangalie.

Naomba niwashukuru na kuwapongeza Shirika la *NSSF* kwa kazi nzuri inazofanya kuhakikisha kwamba huduma zimeboreshwa na hata huko mikoani tuliko majengo mengi tunayoyaona mazuri na majengo ya *NSSF* na yangeweza pia kusaidia vyama mbalimbali na maofisi mengine kuweza kuwa kwenye ofisi za *NSSF* na huduma mbalimbali wanazotoa. Sasa ninawaomba kwa huduma walizonazo za kuhudumia wastaafu basi na wenyewe waanze programu ya kuhudumia watoto yatima ya wale wanachama wao. Pale wanapofariki basi waangalie utaratibu pia wa kuweza kuwapa elimu watoto yatima hao ni watoto wa wanachama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba niipongeze *VETA* kwa kazi nzuri inayofanya kuweza kufundisha vijana wengi Vijijini. Kama isingekuwa *VETA* nina uhakika vijana wengi wangekuwa wapo mitaani. Lakini imetoa vijana wengi wanapata elimu kwa taaluma mbalimbali wanazozihitaji. Ninaomba waendelee na wasaidie vyuo vya binafsi na vya Taasisi zisizokuwa za Serikali ili kuweza kuwafundisha vijana wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga hoja hii mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii nami nizungumze machache sana. Nitazungumzia mambo mawili tu ili ndugu yangu, mwenzangu, Mheshimiwa Kapuya na timu yake waweze kuyatafakari na kuyachambua. Nitaanza kuzungumzia kwanza Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia yanajikita katika chuo hiki. Wanazungumzia kuhusu walemavu, wazee, yatima, vikongwe wote mahali ambapo kazi yao inaweza kufanyika inatengenezwa katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Hapa ndipo tutakapopata wataalamu wa kutunza vikongwe, walemavu, yatima, UKIMWI wote wanafundishwa pale.

Mimi zamani nilikuwa sijui, nilikuwa najua Wizara ya Kazi basi ni Bwana *Labour* kumbe si kweli. Kuna mambo mengi cha kushangaza au kusikitisha tu ni kwamba Taasisi hii mwaka jana ilikuwa na wanafunzi 450 huko nyuma ilikuwa 300 ni wachache sana.

Sasa hivi nawapongeza uongozi wa Taasisi wamepanua wanajenga, madarasa, maktaba nimeyaona kwa macho yangu. Ni nia nzuri ya kupanua hiki chuo. Lakini ingekuwa vizuri zaidi Wizara ikawaunga mkono ili chuo hicho kikapanuliwa zaidi.

Naishukuru Serikali moja ya vikwazo vilivyokuwa vinasababisha wanachuo kuwa wachache katika Taasisi hii ni ada. Kwa sababu ni wachache tu ambao walipata msaada wa ada. Kwa sheria tuliyoipitisha hapa mwaka huu kuhusu kukopesha wanafunzi nafikiri uwezo wa kupata wanafunzi zaidi katika Taasisi hii utakuwepo.

Tunategemea mwakani liwe tatizo la upungufu wa miundombinu lakini tunaamini kabisa Wizara itatusaidia kuweza kukipanua chuo hiki maana ni cha muhimu sana. Ukitazama Wabunge waliozungumza, wamezungumzia kimazingira pale pale tu ukiacha wale wanazungumzia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kazi ya Wizara ya Kazi. Wizara ya Kazi inatazama welfare ya wafanyakazi. Tuna wafanyakazi wa aina mbalimbali, wapo wafanyakazi wazuri, wanaotenda kazi zao kwa mujibu wa sheria na kanuni, lakini wapo na watendaji kazi wakorofi. Vile vile, wapo waajiri wakorofi na wapo waajiri wazuri. Wote hawa wanategemea miongozo ya Wizara hii. Mfanyakazi mkorofi akikorofisha kazini mwenye kazi yaani mwajiri anamuadhibu na

hukimbilia Wizara ya Kazi kwenda kulalamika kwamba nimeonewa. Pia, mwajiri anaweza akaonewa na mfanyakazi akakimbilia Wizara ya Kazi: "Ooh Kahumbi mbaya, nimeona nimfukuze."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Waziri au Wizara ina sheria zake za kusuluhisha mambo haya, lakini kilichonitia wasiwasi na kuomba nichangie hapa ni kwamba nina mfano mmoja. Yuko mtumishi mmoja wa *TRA* kule Mbeya, huyu alionekana ana makosa akafukuzwa kazi. Mtumishi huyu akapeleka malalamiko kwenye Baraza la Usuluhishi la Mkoani Mbeya, Baraza la Usuluhishi likasuluhisha likaona kwamba huyu mtu hakuwa na hatia ya kufukuzwa kazi, likaamuru arudishwe kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Usuluhishi lilipoamuru huyu mtu arudishwe kazini, mwajiri ambaye ni *TRA* akaomba rufaa, hakuridhika na usuluhishi uliotolewa na Baraza la Usuluhishi la Wafanyakazi. Alipoomba rufaa, rufaa hii ikasikilizwa na Mheshimiwa Waziri wa Kazi. Mheshimiwa Waziri wa Kazi naye alipopitia maneno haya ya mtumishi huyu, akaona kwamba huyu mtu hakuwa na hatia, akaamuru mfanyakazi huyu arudishwe kazini miaka mitatu iliyopita, mwaka 2001, lakini mpaka leo hajarudishwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti nilizungumza na Waziri wa Fedha kwa sababu *TRA* iko chini ya Waziri wa Fedha na nikazungumza vile vile na Kamishna Mkuu kuhusu suala hili. Ilielekea kama anaelewa, lakini zaidi alionekana kama haelewi, ukichunguza unaona ni kama chuki binafsi. Waziri wa Fedha akaandika barua, akanipa nakala mimi, alimwandikia huyu bwana mkubwa kwa nini hakutekeleza agizo la Waziri wa Kazi. Barua iliyoandikwa ninayo hapa, inadai kwamba wao baada ya rufaa yao kushindwa walirudi ofisini na mrufani mkubwa wa *VAT* katika *TRA* akatoa ushauri kwamba afukuzwe tu na Kamishna Mkuu akaona ushauri wa Mkurugenzi wa *VAT* ni wa muhimu zaidi kuliko amri aliyopewa na Waziri wa Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitu hiki kinanitia wasiwasi, kama wafanyakazi watakuwa wanatendewa hivi kwanza itakuwa unajiuliza; je, kama hawakuona umuhimu wa Waziri wa Kazi kwa nini waliomba rufaa kwenda huko? Hilo ni swali la kwanza.

Lakini swali la pili unajiuliza, hivi kweli mtu aliyekata rufaa, rufaa yake ikishindwa akirudi nyumbani ana haki ya kuwa Hakimu anamhukumu tena huyo mtu?

Nasema hivyo kwa sababu huyu Mkuu wa *VAT* katika *TRA* ndiye alirufaa kwa Waziri, Waziri akaona rufaa yake haina miguu, yule mtu hana kosa arudi kazini. Aliporudi anamshauri mkubwa wake kwamba: "Hapana, afukuzwe tu." Sijui kwa vifungu gani! Je, vifungu hivi anavijua yeye kuliko Waziri wa Kazi? Unashindwa kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hayo tunauliza, huyu Kamishna wa *TRA* anachojua yeye maagizo ya Waziri ya Kazi yalikuwa ni ya hekima zaidi au ni yale ya Mkuu wake wa Kitengo cha *VAT?* Ninavyofahamu ni kwamba, Waziri akisema jambo ni agizo, sasa agizo la Kapuya kupuuzwa kiasi hiki ni sawa?

Ninaomba kidogo tu kwamba, Mheshimiwa Kapuya atakapokuwa anahitimisha anieleweshe; je, amri yake kutotiliwa maanani anaona ni halali au yeye ana unyonge kiasi gani? Au anieleze; je, huyu mtu atarudi kazini? Vinginevyo basi, Waswahili husema: "Ukitaka kuchinja kuku bila matatizo chinja kuku wako." Sasa mimi nitachinja kuku wangu Kapuya, nitashindwa kumuunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, asubuhi tumekumbushwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwamba, kifungu 49 (8) Waheshimiwa Mawaziri watatamkwa kwa vyeo vyao.

Kwa mfano, mfano aliosema Mzee Kahumbi sasa hivi, kama ni Kapuya akiondoka ile amri yake haina maana, lakini kama ni Waziri wa Kazi hata akiondoka amri yake bado ina maana. Ndiyo maana itabidi mtaje vyeo vyao. Tunaendelea.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ifuatayo. Awali ya yote naomba kutoa rambirambi zangu za dhati kwa familia ya Marehemu Captain Comrade Kasapira, kwa wapigakura wake wa Jimbo la Ulanga Mashariki na vile vile kwa Chama alichokuwa ameingilia ambacho ni CCM, Chama ambacho ni cha jadi katika utani na sisi. Poleni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa huruma yake Mwenyezi Mungu, Marehemu Captain Kasapira apate rehema zake na apumzike kwa amani. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niingie katika suala lenyewe lililo mbele yetu. Kabla ya hapo kweli nimesahau, nataka kuwapongeza Timu ya Soka ya Wanawake yaani *Twiga Stars* kwa ajili ya kutuletea sifa sisi kama akina mama na Taifa kwa ujumla. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kwamba na mimi nilipokuwa msichana nikisoma *Tabora Girls* nilikuwa nacheza soka. Kwa hiyo, nawapongeza kama mchezaji wa zamani wa soka ya wakati huo. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile, napenda kutoa *challenge* kwa Chama cha *Netball* (CHANETA) kwa kuwa hawajatufikisha mahali pazuri mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, kama akina mama wanaocheza *Twiga Stars* wametufikisha hapo sisi kama akina mama kutupa sifa na Taifa kwa ujumla, basi ni *challenge* kwa CHANETA kufanya hivyo ili tuweze kuringa nao na kujidai nao katika *challenge* zinazofuata katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na watoto watukutu. Ukitazama haraka haraka huwezi kujua kwa nini watoto hawa watukutu wanawekewa magereza au shule zao. Ni sababu gani inayofanya hawa watoto wawe watukutu na wadokozi wa vitu vidogo vidogo? Ukijikita sana utakuta ni umaskini. Umaskini huu ambao unatokana na familia zao yaani baba na mama wamekua katika mazingira ya umaskini uliokithiri

unafanya watoto hawa waende wakatafute chochote nje na wanatafuta chochote kwa njia iliyo halali na wakati mwingine kwa njia isiyo halali. Kwa hiyo, kwa sababu msemo wa Kiswahili unasema: "Samaki mkunje angali mbichi" ninomba Serikali iongeze shule za aina hiyo za watoto watukutu ili wapate elimu ambayo ni haki yao kama watoto na vile vile tuwatengeneze na kuwajenga katika maadili yanayokubalika kitaifa wawe ni raia wema hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule hizi au magereza haya watoto wasichanganywe na watu wazima kwa sababu watu wazima wana mambo yao na watoto nao wana mambo yao. Kwa hiyo, tuangalie rika zao. Watoto hawa watukutu kama ni wizi wao wanadokoa dokoa tu, lakini watu wazima wanaiba haswa. Tutofautishe matatizo yao hata na adhabu zao.

Kwa hiyo, ningeomba sana na kushauri sana shule za watoto watukutu ziwekwe mbalimbali, zisichangangwe na za watu wazima na wala zisichanganywe za wasichana na wavulana ili kuhakikisha watoto hawa watukutu kesho wanakuwa ni akina baba wa Taifa hili walio wazuri na akina mama wa Taifa hili walio wazuri na wa maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye watoto yatima na watoto walio katika mazingira magumu. Sasa hivi tuna mfuko kwa ajili ya watoto yatima, lakini tunaangalia hasa watoto yatima katika kujikita zaidi kwenye UKIMWI, kwamba wazazi wamekufa kwa sababu ya UKIMWI. Lakini ukiangalia kwa undani zaidi unakuta ni umaskini kwa watoto walio katika mazingira magumu na hasa hasa katika kuvunjika ndoa za baba na mama.

Baba anakwenda kivyake, anakwenda kuoa mwanamke mwingine ambaye ni mama wa kambo na mama naye anakwenda kivyake anakwenda kuolewa na tunapata baba wa kufikia. Mazingira haya yanafanya hawa watoto washindwe kupata haki yao ya matunzo kama watoto kutoka kwa wazazi wao.

Kwa hiyo, ninaamini ili kupunguza watoto wa mitaani na ili kupunguza umaskini wazazi wanaozaa watoto wao wawajibike wakati ndoa zinavunjika ili kuhakikisha watoto hawa hawapati tatizo au kero kutokana na makosa ya wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, mila na desturi zinachangia katika hili hasa katika mirathi. Kwa mfano baba akifariki, mama anabaki pale na ndugu wote wa mwanaume. Ndugu hao wanakwenda kumtoa kwenye ile nyumba, wanamnyang'anya kila kitu, hata mwiko wakati mwingine wanachukua! Kwa hiyo, unakuta huyu mama anapoondoka pale hana chochote. Kwa mfano, sisi mila ya kwetu kule unaondoka peke yako kama ulivyokwenda, watoto unawaacha kwa ndugu zake mwanaume.

Lakini ndugu hao wakichukua mali hawashughuliki kutunza watoto wako. Kwa hiyo, pesa ile inachukuliwa na ndugu wa mwanaume na wala hawasaidii chochote, wanajitajirisha wenyewe. Kwa misingi hiyo, ninaamini kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuleta Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi ili kuhakikisha kwamba kila mtu anapata haki yake na watoto hawa wanatunzwa ipasavyo na wazazi wao.

Pia, ninaamini tutapunguza watoto walio katika mazingira magumu na vile vile tutapunguza yatima wasio wa lazima wa kujengewa nyumba za yatima na mifuko ya yatima kwa sababu Serikali itaendelea kujenga nyumba hizi ngapi na mifuko hii tutachangia mingapi! Ninaamini tukitekeleza haya tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa sana matatizo ya yatima na watoto walio katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wengine wanaozunguka mitaani ni kwa sababu baba zao wamekataa kuwatunza, wamewakataa kabisa na wengine wamewakubali, lakini hawatunzi. Wakati mwingine, lakini siyo mara nyingi, akina mama vile vile huwa wanachanganya mpaka inashindikana kujulikana baba wa mtoto yule ni nani.

Kwa hiyo, ku-*solve* hii *problem* ninaamini matunzo ya Sh.100/= hadi leo yaliyopo pale katika sheria hayafai. Ni lazima tukubaliane tulete sheria hapa tuweke matunzo ya watoto yalingane na wakati na vile vile yatolewe kufuatana na wakati.

Kwa hiyo, akina baba wanaozaa ovyo ovyo Serikali ihakikishe inawabana ili watunze watoto wanaowaleta duniani bila mipangilio na kuhakikisha akina baba na mama wanatunza mtoto waliyemleta na kuhakikisha wote wanazaa kwa wakati waliokubaliana, siyo ovyo ovyo tu. Suala lingine ni kwamba, ninaamini kama elimu ya kuandika wosia itawekwa vizuri na kila mzazi akaandika wosia kabla hajafa kwa ajili ya watoto wake tutakuwa tume-*solve* hii *problem,* kwa sababu ile *document* ya wosia itasaidia katika mirathi na vitu vingine.

Kwa hiyo, hapa mtu utahakikisha kwamba unachuma kwa ajili ya watoto wako na unahakikisha watoto wako ndiyo watapata mali uliyoiacha na siyo mwingine yeyote. Kama unataka kuongeza ndugu ni hiari yako, lakini kwa kweli sisi wote tunachuma kwa ajili ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii itolewe pamoja na *family planning.* Unapokwenda kukutana na mwanaume au unakutana na mwanamke siyo lazima kuzaa.

Kwa hiyo, elimu ya *family planning i*wekwe wazi ili ujue kwamba unataka watoto wako wawili au watatu, basi uwazae wakati unapokubaliana na mtu unayetaka kuzaa naye. Hata katika ndoa pia mkubaliane kwamba tunataka watoto wawili au watoto watatu ambao tunaweza kuwatunza na vile vile tunaweza kuwaachia urithi wa kutosha, siyo kuacha watoto wanazurura hapa na unawaongezea kuwa maskini.

Sisi tuliozaliwa wengi tumelundikana, tumeshapata *experience* hiyo na tunatakiwa kujifunza, watoto wetu sasa ni lazima waende katika *planning* ili walete mabadiliko makubwa na kuwatoa Watanzania katika hali ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie katika makazi ya wazee. Mimi niko katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii, tuliweza kutembelea makazi ya wazee au wakoma kule Nunge Kigamboni.

Nilichojifunza katika safari hiyo na kuona wale wazee, kwanza hatimiliki ya kiwanja hicho haipo na hiyo nimeiona katika Wizara nyingi tu, hata Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Tengeru na wapi huko kote hakuna hati. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Wizara hii na Wizara zingine zote ni kwamba, kwanza kabisa hatimiliki zipatikane ili watu wengine wasivamie viwanja hivyo.

Vile vile nimejifunza kwamba, watoto wa wazee hao wanataka kufanya kwamba hapo ni nyumbani kwao, wanataka kurithi. Elimu ya kuwaeleza watoto kuwa ni wajibu wao kutunza wazazi wao itolewe kufuatana na mila na desturi. Hata amri 10 za Mungu na amri nyingine katika dini zote tunaamini kwamba ni wajibu wa watoto kutunza wazazi wao.

Kwa hiyo, Serikali isaidie inapobidi, pale ambapo mtoto hajawa tayari kuwachukua wazazi wake. Lakini ukishafikia, basi watoto hawa wachukue wazazi wao na wawatunze, ni wajibu wao. Pia, wale wachache ambao wanabaki basi waendelee kutunzwa na Serikali na hivyo tutakuwa tumepunguza mzigo mkubwa kwa Serikali badala ya kuongeza mzigo. Wazee wote tukianza kupelekwa kwenye makazi ya namna hiyo itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie walemavu. Wazazi wanaozaa walemavu mara nyingi wanawaficha. Naomba basi wawapokee hawa watoto kama walivyopewa na Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiyo ametaka akupe hivyo pengine kwa majaribu na mapenzi yake. Kwa hiyo, wawapokee watoto hawa, wawasomeshe kwani wengine wanaweza kusoma mpaka wanakuwa na degree. Hawa watoto walemavu wanaweza kufanya kazi kufuatana na utaalam wanaosoma, wasijali hiyo.

Vile vile, ni lazima tukumbushane kwamba sisi wote hatujafa, hatujaumbika, kwa hiyo tunaweza kuwa walemavu kutokana na accident zinazotokea hapa na pale. Hivyo, ni lazima tuwaheshimu na kuwathamini na kuwapa heshima yao walemavu wote.

Pia, shule zinazofundisha walimu yaani Vyuo vya Ualimu viongeze wataalam wa kufundisha watoto walemavu kama vile vipofu, viziwi na kadhalika na wakianza kufundisha pale shuleni akipatikana mtu mmoja au wawili basi wapewe mshahara maalum. Vile vile, tunapogawa urithi basi tusiwanyime watoto hawa walemavu, tuwape urithi wao na tuwamilikishe mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kidogo kuhusu *NSSF* hasa nyumba za Kinyerezi. Kusema kweli nyumba hizo zilitengenezwa ili ziwasaidie walalahoi na kwa bei rahisi. Cha kushangaza ni kwamba nyumba hizi zimekuwa za bei ya juu sana ambapo mtu wa kawaida hawezi ku-*afford* kununua! Kwa misingi hiyo, naomba watafakari tena ili kupunguza gharama ilingane na mahitaji ya watu wa kawaida na hivyo kutengeneza nyumba bora kwa familia za kawaida.

Vile vile, *NSSF* ni Shirika ambalo wenye hisa zake ni wafanyakazi ambao wanapeleka makato ya mishahara yao kila mwezi, kwa hiyo, inapopatikana faida basi wapewe na wenyewe faida ya hisa hizo kama tunavyopewa sasa hivi tukiingia kwenye hisa ya *Tanga Cement* na kadhalika. Kwa hiyo, na wenyewe wagawiwe ili waweze kujisikia kwa sababu pesa zile ni zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kuzungumzia mambo ya vijana. Vijana hawa mara nyingi tunawaita wazururaji, wengine tunawaita machangudoa na wengine wanaishia kula dawa za kulevya. Lakini ni kwa nini hawa wanafika hapo? Sisi wote tunajua kwamba Katiba yetu inasema nchi hii ni ya ujamaa na kujitegemea. Mpaka sasa hivi haijabadilika pamoja na kwamba tumeshakwenda kwenye ubepari. Lakini Katiba bado inazungumzia ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujamaa huu wala siyo ujamaa hatujafika hata hapo kwenye ujamaa, tupo kwenye ujima. Tukiwa tunazungumzia ujima tulionao watoto hawa ambao wanatokea kule vijijini, ambao wanakuja kuwa vijana baadaye wengine wana vipaji vyao na wengine wanaweza kufanya kazi kama za kilimo na vitu kama hivyo, basi Serikali iweke maadili au utaratibu mzuri kuhakikisha watoto hawa wanapotoka shuleni, Shule za Sekondari au *Primary Schools* basi watayarishwe ili kuondokana na umaskini kwa sababu wanatakiwa kujitegemea. Watajitegemea vipi watoto waliomaliza Shule ya Msingi, Sekondari na hata *University?*

Uwekwe mkakati unaoeleweka ili kuhakikisha kwamba hata wanapata mikopo kwa ajili ya elimu na baadaye hawa waweze kuwafundisha wenzao kwa miaka mitatu kama vile Cuba. Hivyo, wanakuwa wamepata ajira na kupata *experience* vile vile kutokana na ajira hiyo na pia wanajikomboa kiuchumi kuliko kuwaweka huko mitaani wanazunguka tu.

Vile vile, vitu vyote vipelekwe vijijini kama *television,* umeme na vitu vingine ili waweze kukaa huko huko na kama wanalima basi walime mazao yao kama wale vijana wanaolima vitunguu pale Puge, watafutiwe masoko ili waweze kupeleka Burundi kwa utaratibu unaoeleweka na waweze kupata pesa ili waweze kuondokana na umaskini. Au wale wanaolima nyanya pale Karitu basi wapelekewe hata kwenye ile Kampuni ya Madini pale Nzega, inunue nyanya zao ili kuhakikisha kwamba na wenyewe wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliopita katika chaguzi za Ubunge wa Afrika na pia nampongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kugombea kiti cha CCM na akaweza kupata ushindi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Sina budi pia kuwapa pole wananchi wa Mbeya Vijijini pamoja na wananchi Jimbo la Ulanga Mashariki, Morogoro pamoja na familia ya Marehemu kwa vifo vilivyotokea tukiwa hapa Bungeni Dodoma. Naomba Mola aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuipongeza hotuba hii kwa dhati kabisa. Mchango wangu ni kuhusu vijana na majukumu ya kujenga mazingira endelevu yanayowawezesha na kuendeleza maadili mema katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Naomba Idara ya Maendeleo ya Vijana katika kutekeleza majukumu haya mliyoeleza katika hotuba hii na ingawa hamkuelezea kilimo, lakini mimi nimewakuta vijana katika eneo la Kirungu, Mkoa wa Kigoma, ambao nilipangwa na viongozi wa Mkoa huo tulikwenda kwenye sherehe ya familia, ili nikaone kazi ya kilimo cha bustani kama mahindi, nyanya, matango, pilipili, mihogo, viazi vitamu na mpunga ambao vijana hao wanapata maji nya kumwagilia kwenye bwawa lenye maji ya chamchemi la Rukanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya umwagiliaji wao unaotumika, ni wa kutumia ndoo na ukubwa wa konde lao ni hekta nne. Vijana hao wanaifanya kazi hiyo katika mazingira magumu sana, wala hawana mtaji na hawana pembejeo za kilimo. Wameniomba niwafikishie salamu zao katika Serikali, iwawezeshe wapatiwe mtaji. Pembejeo za kilimo zipunguzwe bei. Pia wanaomba mkopo wako Mheshimiwa Waziri, wakopeshwe mashine ya kumwagilia maji *(Super Money Maker Pump).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo anipe majibu au akubali kuonana na mimi kwa maelezo zaidi pindi kama hakunifahamu Kiswahili changu, kwa sababu nilikubali jukumu la kuwafikishia ombi lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri na Naibu Waziri, pia Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa taarifa yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya haya sina, mimi napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuiunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini, ni kero kubwa. Wapo wengi hawajalipwa maslahi yao. Wizara inachukua hatua gani kubwa ili wote walipwe? *Workmen's*

*Compensation* bado iko chini. Ni lini fidia hii italingana na mahitaji halisi ya wanaoathirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya milipuko sehemu za kazi ni tatizo la Wizara kupuuza umuhimu wa kitengo cha Elimu ushirikishwaji na usuluhishi sehemu za kazi. Wizara haikuonyesha ni vipi vitengo hivi vitaimarishwa ili kupunguza migogoro ya mlipuko au mnataka mfanye kazi kama *fire brigade.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa wafanyakazi katika Idara na vitengo vya Wizara ni kero ya muda mrefu. Wizara inafanya nini kupata wataalam wanaotakiwa na vitengo vyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *OSHA* ni taasisi muhimu kwa usalama wa wafanyakazi. Wanayo matatizo ya kifedha ili waweze kutekeleza majukumu yao ya msingi. Je, Wizara imetenga fedha kiasi gani kusaidia kitengo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara isilete Muswada hapa Bungeni ili kila mwajiri alipe angalau 2% ya bajeti ya mshahara wa wafanyakazi ili wapate fedha za kutekeleza kazi hii muhimu kwa afya ya wafanyakazi, ili iwe sawa na *VETA* inavyopata michango toka kwa waajiri? Bila kupata fedha hiyo, sheria mpya ya usalama na afya mahali pa kazi itatekelezwa vipi? Naomba maelezo.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri aliyoifanya kwa mwaka uliopita na pia kwa hotuba yake nzuri na sina budi kumpongeza kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na kwa unyenyekevu, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kulipatia Jimbo la Kikwajuni shilingi 500,000/=. Fedha hizi ni katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri, aliyoitoa wakati alipokuja kuweka jiwe la msingi kwenye uwanja wa *Basket Ball* hapo Mnazi Mmoja. Hii inaonyesha dhahiri jinsi Mheshimiwa Waziri alivyo muungwana na sisi wananchi wa Kikwajuni tumeshamkabidhi ufunguo wa Jimbo letu na tunamkaribisha wakati wowote ule afike Jimboni na hasa tukitilia maanani kwamba yeye ni mwana wa *Simba Sports Club* na 95% ya wakazi wa Jimboni kwetu ni washabiki wa Simba.

Mheshiumiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano mzuri baina yake na Wizara husika kule Zanzibar katika masuala ya *VETA* na hatimaye wakaweza kuwaelimisha vijana wetu wa Zanzibar kwa masuala ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi naomba kutoa kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na pongezi za pekee zimwendee Ndugu R. Dau. Nilipokuwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nilibahatika kukutana naye mara nyingi katika vikao vyetu na nimeona jinsi alivyokuwa na upeo, ufanisi na uwezo mkubwa hasa katika masuala ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu Jengo la Baraza la Michezo *(BMT).* Kwa kweli hali ya jengo hilo ni mbaya sana na halina hadhi kabisa ya *BMT.* Ningeshauri Wizara ikalishughulikia jengo hilo kwa kulikarabati haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wizara kwa ujumla kwa mwaka huu wa bajeti. Asante sana.

**MHE. MOHAMED ABDULY ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini *FAT* ipo na *FIFA* tayari wamesema ivunjwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu Alhaj Muhidin Ndolanga ana kesi ya kujibu. Mbona anaendelea na kazi? Mheshimiwa Waziri unamwogopa Ndugu Alhaj Muhidin Ndolanga?

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya na napenda kusema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo.

Kituo cha Ajira kiongeze bidii ili kijitangaze na kieleweke kwa wananchi wengi kama inavyowezekana na hasa vijana waliohitimu fani mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani. Sasa hivi ajira zinakwenda na utaalam na uzoefu na zinapatikana sehemu mbalimbali duniani. Hivyo, vijana wetu waelimishwe kutafuta kazi/ajira kupitia katika tovuti mbalimbali ndani ya *Internet.* Sasa hivi ukitembea huko duniani, utaona vijana wengi wa Kenya, Uganda na kadhalika, wakifanya kazi katika Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa, ambazo wamepata kupitia *Internet.*

Kuhusu utafiti katika vijiwe. Nashauri utafiti huu uliofanywa katika Mikoa ya Ruvuma na Rukwa, usambae Tanzania nzima (Bara na Visiwani) ili tuweze kupata takwimu ambazo zitaiwezesha Wizara kupanga mikakati mbalimbali ya kuvigeuza vijiwe hivyo kuwa sehemu ya uzalishaji mali na kuwapatia vijana kipato kwa njia ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya miaka 10 ya kukuza ajira kwa vijana, unaofanywa na Mtandao wa Kitaifa wa Ajira ya Vijana Duniani *(YES 2002),* napendekeza usambae nchi yote, usiishie Dar es Salaam tu, ufike mpaka Zanzibar. Sasa hivi tatizo la ajira ni kubwa sana, hivyo jitihada zozote za kuidhibiti hali hii ni lazima ziimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo iendelee kuimarishwa. Lakini kuna haja ya kuwa na Chuo Kikuu cha Kuendeleza Michezo na hasa vijana wenye vipaji katika fani mbalimbali, ili waweze kuipeperusha vizuri bendera ya Tanzania, Kimataifa.

**MHE. OMARI MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji na Watumishi wote wa Wizara hii. Naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa sehemu kubwa inagusa maisha ya watu pamoja na shughuli zao za kimaendeleo, burudani na michezo ambayo ni moja kati ya vitu muhimu ambavyo vinaunganisha jamii yote ya Watanzania na hata watu wengine wa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maendeleo ya vijana, naiomba Wizara hii kusimamia kama ambavyo imelielezea kupitia Idara yake hii ambayo inasema kuwa Idara hii ina jukumu la kujenga mazingira endelevu yanayowawezesha vijana kujifunza na kuendeleza maadili mema katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa kweli naipongeza Wizara hii na Idara yake hii ya Maendeleo ya Vijana kwa kuelezea jukumu lake hili la ikuwa wao ndio wajenzi wa mazingira endelevu yanayowawezesha vijana kujifunza na kuendeleza maadili mema katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara hii kuyasimamia haya kama ilivyoelezwa katika hotuba hii kwa vitendo na wala siyo kwa maneno au kuwekwa katika vitabu hivi au katika mafaili ya Wizara na Idara husika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa nchi hii katika karne hii tuliyo nayo hivi sasa, wanahitaji haya masuala ya kujifunza na kuendeleza maadili mema kwao na familia zao, kujifunza shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mambo yote haya yaliyoelezwa hapa ni muhimu sana na ni msingi sahihi kwa maendeleo ya vijana wote hapa nchini na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni, iwe inaangalia mienendo na maendeleo ya vijana wetu hapa nchini hasa katika maeneo ya elimu, siasa na uchumi, ili waweze kujijengea misingi imara ya maendeleo yao ya baadaye kwa ajili wenyewe, familia zao, maeneo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, inatueleza kuwa katika mwaka 2003/2004, Wizara hii iliendelea na jukumu la kuendeleza michezo hapa nchini kulingana na sera ya maendeleo ya michezo, ambapo ametuelezea mambo kumi ambayo yalitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo haya kumi, naomba ninukuu mawili au matatu tu. Kwanza, "Kuendelea kusimamia maandalizi na ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Kisasa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii kwa kulielezea suala la ujenzi huu wa kiwanja cha kisasa cha michezo hapa nchini katika hotuba yake hii ya

mwaka 2004/2005. Naitakia kazi njema katika kufanikisha ujenzi huu wa kiwanja hiki kitakachojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, "Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya uongozi, utawala, ukocha na uamuzi, ili kuboresha uwezo wa watendaji katika michezo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuamua kutoa mafunzo haya katika maeneo haya iliyoyataja. Lakini naiomba iendelee kusimamia kumaliza matatizo na migogoro ambayo inatokea mara kwa mara katika maeneo haya, jambo ambalo limesababisha kuwa kiwango cha michezo nchini kuwa cha chini sana na kisichokuwa na maendeleo yoyote yale, ukilinganisha na nchi nyingine za Kiafrika na za Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, "Katika kuboresha utulivu na amani ndani ya vyama vya michezo, Wizara iliendelea kutoa maelekezo ya namna ya kuhuisha na kuboresha Katiba za Vyama na vilabu vya michezo ili zifanikishe kuleta utawala bora ndani ya vyama na vibabu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara katika kazi hii muhimu kwa maendeleo ya vilabu na vyama vyetu hapa nchini. Ninawatakia kazi njema na usimamizi wa mafanikio katika majukumu yake haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 29, Wizara inatueleza kuwa ili kuhakikisha kuwa michezo inaendeshwa kisayansi, Wizara imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa maendeleo ya Vyama vya Michezo, ukiwa na maeneo kumi ya ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kuwa imetueleza ili kuhakikisha michezo inaendeshwa kisayansi. Wizara imeandaa muundo na kutengeneza mpango wa maendeleo ya Vyama vya Michezo, ukiwa katika maeneo kumi. Ni matumaini yangu kuwa mpango huu utafanikishwa kama ambavyo umeandaliwa ili katika nchi yetu tuweze kuendesha michezo yetu hapa nchini kisayansi, ili kuleta ufanisi na maendeleo zaidi katika suala zima la michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* ni moja ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii na katika hotuba
yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao kwa wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu haya ya *NSSF,* naliomba Shirika hili kulipa mafao ya wanachama wao pale inapofikia kulipwa na zaidi iwe kwa haraka sana na kwa kuwarahisisishia katika maeneo ya karibu na wanachama bila ya kulazimika kufuata Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono 100%. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu

pamoja na Wakurugenzi wote wa Idara zilizo chini ya Wizara kwa kutekeleza vyema majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mkurugenzi wa *VETA* kwa kuvisimamia vyema vyuo vyote vya *VETA* kwani vimekuwa chachu ya vijana wetu kujitegemea kutokana na mafunzo ikiwa ni njia ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, Wizara kwa kushirikiana vyema na vyama vya wafanyakazi ili kuondoa migogoro ya kikazi, hasa nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuuzima mgogoro ulioanza kufuka wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* naiomba Wizara iendelee kuwashirikisha wafanyakazi pamoja na vyama vyao (utatu) ili kuondokana na migogoro ya kikazi ambayo haina tija kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie michezo, kwanza nami naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa ujenzi wa kiwanja cha mpira, uwanja wa kisasa. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uwanja huo utumike vizuri ni lazima kuwe na watumiaji ambao ni wanamichezo wenyewe, sasa bado najiuliza je, wanamichezo (wadau) wako wapi? Kwani vyama vyote vya michezo vina migogoro, nashauri Katiba zao zibadilishwe ili ziendane na mazingira tuliyonayo. Katika kitabu cha Mheshimwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Mchezo, sikuona sehemu chuo cha Malya kimetengewa fedha kwa ajili ya maendeleo. Ukizungumzia michezo ni lazima pia uimarishe vyuo vinavyozalisha watalaam. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera Profesa Simba, Waziri na Mheshimiwa Yanga, Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini migogoro inazidi ndani ya vilabu vya michezo ya vilabu vya michezo nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni Idara ya michezo ihamie Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili wadhibitiwe.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika Wizara hii ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia watumishi wote hususan Katibu Mkuu, Ndugu Abubakar Rajab, kwa kazi nzuri katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukumbushia tatizo la wazee ambao walipigana katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1939 hadi 1945. Tatizo la uongozi

katika *Tanzania Legion Club* kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri tarehe 28 Julai, 2004 kwenye swali langu ni tatizo ambalo naamini kuwa wadau wote tukishirikiana linaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa akina Mzee Elirehema Ngowo na wenzake wanateseka kwani hali zao za maisha inazidi kuwa ngumu siku hadi siku. Naamini Serikali yetu ambayo inawajibika kwa wananchi mara kwa mara, haitaacha kuingilia kati ili ufumbuzi wa kudumu uweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa wale wanaotaabika nipo tayari kushirikiana na Wizara ili tatizo hili liweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja hii.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa ruhusa yako nitoe mchango wa maandishi, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 15 Waziri amesema kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii iliendelea kuratibu, kusimamia na kukagua Makao ya watoto yatima na wenye shida na makazi ya wazee wakiwemo walemavu kuwa wataboresha Makao hayo ni vyema Waziri akanieleza ameboresha nini katika kambi ya Wazee ya Bukumbi Wilayani Misungwi, Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anafahamu kuwa kati ya Kambi zenye watu wengi ni Bukumbi, jedwali katika ukurasa wa 68 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, linaonyesha idadi ya wakazi 515. Idadi hiyo ni kubwa, inahitaji matunzo ya hali ya juu ikiwemo makao yao, chakula chao na kuwahudumia watoto wao katika swala zima la elimu ni vyema nikapata ufafanuzi wa hayo yote. Walemavu hao ni wazee, walemavu ukiwemo upofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamekuwa na upungufu wa waganga wa kuwatibu wakiwa kambini kwao badala yake huhitaji waende *Bukumbi Hospital* ambayo iko mbali ukilinganisha na uzee, je, hilo kwa bajeti hii limepatiwa ufumbuzi upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi hiyo inayo majengo yaliyojengwa siku nyingi, hayajafanyiwa ukarabati, je, bajeti hii inasemaje? Kambi hiyo ina matatizo ya maji, bajeti inasemaje kwa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi hiyo imesahaulika, haijatembelewa na viongozi wa Kitaifa kama Waziri, wazee wanaomba awatembelee, Waziri anasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kazi njema na naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa hotuba yake nzuri ambayo naiunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tatizo la ajira inasikitisha sana kuona kwamba kwa Mkoa wa Dar es Salaam kati ya nafasi 12,321 ni 30% waliopata nafasi wakati 62% walikaa kwa ajili ya kutokuwa na ujuzi wa juu au kukosa sifa zilizohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana hasa ukiangalia kwamba kila mwaka vijana wanaoingia kwenye *labour market* wanazidi kuongezeka *(chasing few places)* kuliko nafasi zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Serikali ikitafuta ufumbuzi wa tatizo hili, vijana wetu wengi sana wanakuwa *frustrated* kwa kukosa kazi na hivyo uwezekano wa wao kujiingiza kwenye madawa ya kulevya, uhuni na hivyo kuendeleza umaskini na hatimaye kwenye gonjwa la Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iendelee kutafuta njia nyingine zaidi za kuwapatia vijana wetu kazi, kwa mfano, kupeleka vivutio mikoani kwenye mikoa yote ya kilimo ili vijana hawa wajiajiri kwenye kilimo. Vivutio hivyo viwe ni pamoja na nafasi za kujiendeleza ki masomo *(evening classes),* michezo, sinema na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ustawi wa Jamii inasikitisha sana kwa Serikali imegoma kabisa kutamka ni lini mfuko wa wazee utaanza, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anakuwa na kigugumizi na anakuwa *hazy* na *nebulous* juu ya mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kwenye toleo la Sera ya Taifa ya Wazee katika ukurasa wa tisa wa hotuba yake inasema: "... Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ... itaunda mfuko wa Wazee *(Revolving Loan Fund)* kuwawezesha kukopa ili waendeshe miradi yao."

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa nne tangu Serikali ianzishe mradi huu ambao ningetegemea uanzishwe *during the life time of this Parliament* lakini inaonekana sera hii na mfuko huu hautafanikiwa mpaka labda awamu ya nne?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali itamke kwamba pamoja na kuwajali wazee kinadharia, lakini pia inawajali kiutekelezaji na iseme sasa lini mfuko huu utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wengi sana walikuwa na imani kwamba mfuko huu ungeanza hapo mwaka wa fedha 2001/2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mwenyezi Mungu kuniwezesha kukamata kalamu na kuandika machache kuhusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, namkushukuru hasa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya leo pamoja na Naibu wake, pia nampa pole sana kwa kusafiria chombo kidogo chenye kuyumbishwa na mawimbi ya upepo mkali wa Chama cha Soka Nchini *(FAT).* Aidha, maoni yangu zaidi yatalenga juu ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi kwa Mheshimiwa Waziri, juu ya suala zima la Pasaka. Kwa nini limepungua kasi kimichezo? Tamasha hili limewekwa sasa kama ni nguvu za kichama kuliko kimichezo. Vilabu vikubwa vyote vimejitoa katika Tamasha hili na upo uwezekano likafa au kupunguza dhamira ya mwanzo, uhusiano sasa uliopo baina ya vyama vya soka vya *FAT* na *ZFA* ni mbovu, unavunja hamasa na utendaji kwa Muungano wetu, ipo haja viongozi wa vyama hivi waunganishwe na kupewa ushauri juu ya uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo yetu inakosa motisha na huduma kwa wachezaji wetu hasa timu za Taifa, ahadi zinakuja mwisho kuliko maandalizi mfano, *Twiga Star,* iliahidiwa shilingi 300,000/= kwa kila mchezaji wakishinda Zimbabwe. Kama tungeiandaa timu, ingefanikiwa zaidi kuliko ahadi za kujua uwezekano ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa timu ya Taifa, kamati ya ufundi na makocha wetu wana ubinafsi, wanakosa muda wa kuteua wachezaji, tuliangalie na tulichunguze zaidi suala la uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za michezo Tanzania zina mapungufu, kwa Katiba hii nafikiri sheria zitakuwa ni bora na zinakidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri apunguze ushabiki katika maamuzi ya michezo. Awe kama hana timu ili uamuzi uwe wa heshima na unaojali kanuni na sheria. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa mpango wa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuleta ufanisi kwa Idara zote ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, kabla sijaanza kutoa ushauri na mapendekezo kwa maeneo kadhaa nitamke rasmi kuwa naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwani imekuwa karibu na vijana katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Pamoja na pongezi hizi, napenda niishauri Serikali kwamba, kwa kuwa vijana walianzishiwa mfuko pamoja na akinamama kwa kila Halmashauri nchini, mfuko ambao umekuwa ukiungwa mkono na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa kuchangia shilingi milioni nne kwa kila

Halmashauri na kila mwaka, basi na Wizara hii iige tabia hii nzuri na ione umuhimu wa kuchangia mfuko huu wa vijana ambao ni sehemu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba wakitumia ushauri wangu itasaidia sana kuboresha mfuko wa vijana ambao lengo lake kuu ni kuwasaidia kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitumie nafasi hii kuzungumzia juu ya Idara ya Kazi, nashukuru Serikali kwa kuiweka Idara hii kuwa chombo cha awali cha kutatua migogoro kati ya vibarua, wafanyakazi na waajiri wao pindi inapobainika kuwa kuna mgogoro kati ya mtumishi na mwajiri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na azma hii nzuri ya Serikali, kumejitokeza mara nyingi watumishi ama vibarua kutokutendewa haki na haki mara nyingi kumwegemea tajiri kwa sababu ya kutoa chochote kwa maafisa wengi wanaosuluhisha migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe inawachukulia hatua za kinidhamu ama za kisheria watendaji wa Idara hii mara wanapobainika kumgandamiza mtumishi na kumpotezea haki yake kwa sababu ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa nikitoa mfano kwamba mtoto hudoea kwa jirani anapokuwa na njaa. Hivyo basi inawezekana mapungufu haya hujitokeza kwa sababu ya watendaji wetu kuwa na kipato kidogo, naiomba Serikali iangalie pia uwezekano wa kuboresha maslahi ya watendaji wetu ili kuwapunguzia tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuridhia mkataba wa Kimataifa wenye kupiga vita ajira mbaya kwa watoto, ambao mkataba huu umesaidia kwa kiasi fulani wimbi kubwa la watoto ambao walikuwa kwenye ajira hizi mbaya ambazo zilikuwa zinawadhalilisha na kuwanyanyasa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati hii mizuri ya Serikali bado tatizo hili lipo ambalo linapinga haki ya watoto, naiomba Serikali ifuatilie tatizo hili kwa karibu kwa kutumia Mabaraza ya Mitaa, vijiji, kata na kadhalika ambayo ndiyo yako karibu na wakazi wenye tabia hizi, kwa kufanya hivi nina hakika tutakuwa tumekomesha tabia hii mbaya ambayo inaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayapongeza Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kwa kuanzisha au kufungua vituo vya kulelea watoto waliokuwa wanaishi kwenye mazingira magumu kwa kukosa wazazi kwa kufiwa ama wazazi kutelekeza watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Serikali kwani imekuwa ikishirikiana na Mashirika haya kwa suala zima la malezi, chakula taaluma na kadhalika. Lakini bado Serikali haijajikita vizuri katika suala zima la kusaidia wahisani ili kuboresha huduma itolewayo na kupanua vituo hivi, kwani jukumu kubwa bado imewaachia wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifike mahali sasa ifanye kazi sambamba na Mashirika haya ikiwa ni pamoja na kutenga fungu la kusaidia Mashirika haya kwa kuboresha shughuli mbalimbali za vituo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala zima la michezo, naipongeza Serikali kwani imekuwa ikishiriki kwa namna moja ama nyingine katika suala zima la michezo kwa kutambua umuhimu wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ihakikishe inashiriki kikamilifu katika fani mbali mbali za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mpira wa miguu kwa jinsia zote, mpira wa kikapu kwa jinsia zote, mpira wa wavu kwa jinsia zote, mpira wa pete kwa wanawake, riadha na kadhalika. Nina hakika Serikali ikijituma kikamilifu tutakuza fani ya michezo nchini kwa lengo la kuongezea Taifa kipato wachezaji kujiajiri, kulipatia Taifa sifa na kulitangaza Taifa, Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niendelee kuishauri Serikali kwani imekuwa ikitambua michezo kwa ngazi ya Taifa tu, ikisahau kuwa wachezaji wazuri wanatoka chini. Hivyo basi, naiomba Serikali, pamoja na kuunda vyama vya michezo kwa ngazi ya Wilaya na Mikoa, ikumbuke pia kutenga mafungu ili kuwawezesha vijana kushiriki kwa wingi na kuwapa moyo wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujihusisha kuunda uongozi wa Baraza la Michezo la Taifa na kadhalika, lakini bado kuna malalamiko kwamba uchaguzi mara nyingi unakuwa sio wa huru na haki kwa kung'ang'ania viongozi wachache ambao tayari wamekwisha kuwa kero kwa wanamichezo na washabiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kusimamia kwa karibu suala zima la michezo ili kupunguza ama kuondoa migogoro ndani ya vyama vya michezo mfano, *FAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wanawake kwani sasa wameamka na wametambua umuhimu na faida ya michezo. Hivyo basi, naishauri Serikali ihakikishe inasimamia suala zima la michezo kwa kuunda uongozi imara na kutenga fungu kwa ajili ya kuboresha fani hii ya michezo kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kutoa pongezi na kuunga mkono bajeti hii asilimia mia moja.

**MHE. DR. LUCY NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na wataalam wote kwa kazi nzuri na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, huduma kwa watoto yatima, nashauri watoto yatima watunzwe na ndugu za wazazi wao ili waweze kupata upendo wa karibu na pia waweze kupata fursa ya kujisikia kwamba wanao ndugu na kile kinachoitwa *the roots of a family.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na asasi nyingine ziwawezeshe hawa *care takers/guardians* au walezi ili waweze kumtunza mtoto wa ziada katika familia zao. Wanaweza kupewa mikopo kwa ajili ya mtaji, msaada wa *uniform, school fees* na vitabu kwa ajili ya watoto yatima wanaowatunza. Mkakati wa aina hii unatumiwa na Shirika la *Faraja Trust* la Morogoro. Limeweza kuwasaidia watoto wasiopungua 3,500 wakiwa katika uangalizi wa ndugu na *fostering parents.*

Pili, watoto wa mtaani, Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha mpango kamambe wa kuwapatia ushauri nasaha na mafunzo ya ufundi stadi ili waweze kujitegemea. Hawa wasiposaidiwa kwa wakati muafaka ni kwamba watakuja kuwa tishio kwa usalama wa raia na mali zao. Wizara ishirikiane kwa karibu zaidi na risasi *(NGOs)* zinazojitahidi kuwasaidia watoto wa mtaani kupata elimu na stadi za maisha.

Tatu, ukosefu wa ajira, ushauri ni kuwa Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha *Community Based Vocational Training* kwa mfano vyuo vya ufundi stadi vijijini vizingatie mahitaji ya vijijini kama ufundi seremala, *mansory.* Hii ni hatua muhimu sana katika kupunguza ukosefu wa ajira pamoja na kupunguza wimbi la vijana kuhama kutoka vijijini kwenda mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana walio na utaalam wahamasishwe kuunda vikundi vya kitaaluma *(professional groups)* halafu wasaidiwe kupata mtaji ili wajiajiri wenyewe kwa kutumia utaalam walio nao, ningeshauri ajira ya majumbani itambulike kama ajira rasmi na mwongozo wa ajira utolewe Kitaifa. Utambuzi huu utawashawishi vijana wengine kuingia katika ajira hii ili waweze kujikimu kimaisha.

Nne ni kuhusu walemavu. Ili kupunguza wimbi la ombaomba, Serikali ikishirikiana na *NGOs* ianze mkakati wa kuwahamasisha walemavu kuacha kuwa ombaomba na badala yake wapewe mafunzo ya namna ya kusaidiana wao kwa wao na namna ya kuanzisha na kuendesha miradi midogo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *approach* hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika Shirika la *Faraja Trust,* Morogoro. Hvi sasa Shirika linaendesha mafunzo ya Ukimwi kwa walemavu wa Mkoa wa Morogoro. Pamoja na elimu ya Ukimwi hawa walemavu wanapata elimu ya namna ya kuanzisha miradi midogo midogo na namna ya kutunza mahesabu. Pia wale ambao wameonyesha mwelekeo wa kufanya mradi wanapewa mikopo ya masharti nafuu. Gharama za hii elimu zimegharamiwa na Mheshimiwa Reginald Mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Shirika la Faraja ni kuwasaidia walemavu wa makundi yote kuunda vikundi vya kiuchumi na hatimaye waweze kuanzisha chama cha akuweka na kukopa *SACCOS.*

Tano ni kuhusu michezo, Shirika la *Faraja Trust* limeanzisha mradi wa vijana wasio mashuleni *(OSYP).* Mradi huu unatumia michezo kama njia muhimu ya kuwafikia vijana hasa wale wenye matatizo ya tabia na ukosefu wa ajira. Mtindo huu umeonyesha mafanikio makubwa kwa mfano, tuna timu zaidi ya 20 za mpira wa miguu, wanne kati ya hawa vijana wamechukuliwa na timu kubwa. Wasichana wawili sasa wamo katika timu ya *Twiga Stars.* Pia timu ya *Volleyball* imetoa vijana ambao wamejiunga na Jeshi la Magereza, timu moja sasa imeshika nafasi ya kwanza katika ligi ya daraja la nne mkoa na wachezaji wengi wamejiunga katika vikundi na wamepewa mikopo. Wanafanya vizuri sana.

Naomba Wizara itambue juhudi ya Shirika la Faraja na iwasaidie kwa hali na mali. Mradi huu wa *OSYP* unaweza kuwa kielelezo kwa mikoa mingine. Mheshimiwa Waziri unakaribishwa sana kuuona mradi huu.

Sita na mwisho, naomba kusisitiza kwamba ujana ni mtaji hivyo Taifa liwekeze kwa vijana kwani Taifa la kesho linawategemea sana vijana walio na uwezo wa kujitegemea wao wenyewe pamoja na kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia afya njema na naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Kazi, Maendeleo na Vijana na Michezo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kazi nzuri wanaofanya kuliendeleza gurudumu la kazi, vijana, michezo, watu wenye ulemavu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kukamilisha sera ya Taifa ya Wazee. Nashauri Sera ya watu wenye ulemavu, pia ikamilishwe.
Mimi ni mdhamini wa *CHAVITA* ngazi ya Taifa na kilio chao kikubwa ni sera yao. Nashauri basi mtoe maelezo ya kina juu ya hatua mliyofikia kuikamilisha sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya mafunzo na mahabusu ya watoto tukizingatia suala la jinsia na pia tukizingatia kwamba hata watoto wa kike watukutu wapo, basi nashauri kuwe na shule yao pia. Hivi sasa kwa sababu ya utandawazi, kuna mmomonyoko wa hali ya juu wa maadili. Matokeo yake wavulana kwa wasichana ni wepesi kuiga tabia zisizoendana na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama ya watoto ina umuhimu wake. Kesi za watoto ziko nyingi na zinacheleweshwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali zinavutia, nashauri kuwe na *disaggregated data* nyingi tu yaani michanganuo ya wanawake na wanaume kama vielelezo D, E, H, huwa inatusaidia tunapohudhuria mikutano ya ndani na nje ya nchi. Nashukuru mpo *gender sensitive.*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itapeleka Maofisa wa Kazi kila Wilaya na kuwapatia vitendea kazi ukiwemo usafiri? Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha za mikopo kwa vijana ili kusaidia vijana kujiajiri wenyewe au kuanzisha miradi midogo midogo ya kuboresha maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watoto yatima wapo kila Wilaya na kwa kuwa watoto hao wanahitaji kupata elimu, je, kwa nini Serikali isitenge fedha za kutosha kusomesha watoto yatima badala ya kuziachia Halmashauri za Wilaya ambazo mapato yake ni kidogo baada ya kufutwa vyanzo vingi vya mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sera ya Wazee imekwishaandaliwa, je, ni lini Wazee nao wataanza kupata mikopo kama ilivyo kwa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Michezo, kwanza napenda kuipongeza timu ya Mji Mpwapwa kwa kufanya vizuri katika Ligi kuu ya *Vodacom 2004* na kubaki Ligi Kuu ya *Vodacom* katika timu 16 za Tanzania Bara pamoja na kwamba haikufanikiwa kucheza Nane Bora. Pia niwapongeze wananchi wa Mpwapwa akiwemo Mbunge wao kwa kuichangia timu yao kwa kipindi cha miaka sita inashiriki Ligi Kuu ya *Vodacom.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe vyama vya michezo na kujitahidi kutatua matatizo yanayohusu migogoro ndani ya vyama vya michezo ili kuendeleza michezo na hasa mpira wa miguu ambao unapendwa na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itakubaliana nami kwamba migogoro ndiyo chanzo cha kushuka kwa mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuvikarabati viwanja vya mpira wa miguu hapa nchini? Hata hivyo nawapongeza viongozi wa michezo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya kwa mafanikio makubwa. Aidha, nawapa pole kwa matatizo na usumbufu mkubwa wanaoupata kutokana na hali halisi ya chama chetu cha michezo nchini *(FAT).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya vijana katika Taifa lolote ndiyo mstakabari wa maendeleo ya Taifa kwa ujumla, kwani vijana wakiendelezwa kiasi cha kutosha *reflection* ya maendeleo hayo itaonekana kwa Taifa zima katika *sector* zote katika uchumi, michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na bidii na mazuri yote wanayopendelea kufanya, nawashauri waongeze kasi zaidi katika kubuni namna mbalimbali za kuliokoa hili genge la vijana linalokabiliwa na vikwazo vingi ukiwemo Ukimwi, madawa ya kulevya, uhaba wa ajira pamoja na athari za utandawazi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali kwa sasa lazima ibuni mikakati ya kuwatayarisha vijana wetu katika kuingia kwenye dunia ya utandawazi iliyojaa vikwazo kwa nchi zetu zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

Aidha, napenda pia kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu vijana na ajira. Tunao vijana wengi ambao Serikali kwa namna moja au nyingine imeshiriki katika kuwasomesha hadi baadhi yao kufikia vyuo vikuu nchini au nje ya nchi. Matokeo yake wanaachwa hivi hivi baada ya kumaliza masomo yao bila kupangiwa sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana kama huyo aliyejipinda mgongo kwa muda wa zaidi ya miaka 20 hadi 30 akiwa darasani, nikiwa na maana kuwa kijana huyu kaanza shule ya msingi hadi vyuo vikuu, kisha Serikali inamwacha kijiweni, tegemeo lake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifike mahali iwafikirie vijana hawa waliosomeshwa na Serikali kulingana na ujuzi wao ili wapatiwe nafasi za kazi, ili kuepuka vijana hao kutoroka nchi yao na kwenda kufanya kazi ugenini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inadiriki kuajiri wataalam kutoka nje, ambapo vijana wetu utaalam kama huo ambao wanaleta hao watu kutoka nje nao wamesomea. Je,

huo ni uungwana? Vijana kama hawa wasomi Tanzania hii ikiwa Bara na Visiwani tunao wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye makusudi mazima ili iwakusanye vijana hawa kwa kuwatafutia nafasi za kazi kulingana na ujuzi wao. Tuwe na tabia ya kuthamini chetu kuliko cha wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuwapongeza na kuwashauri viongozi wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ni vema nikasema ukweli kwamba hali ya michezo nchini katika fani zote, mpira wa miguu, *netball,* riadha (mbio), ngumi na kadhalika inazidi kudidimia kutokana na udhaifu wa uongozi, motisha ndogo kwa wachezaji, uhaba wa wadhamini na upatikanaji wa vifaa vya michezo kwa wanamichezo wasiokuwa na uwezo wa kuvipatia, uhaba na ubovu wa viwanja vya michezo udhibiti hafifu wa mapato yatokanayo na viingilio na hata misaada kwa klabu na wanamichezo na mwelekeo duni wa Serikali na vyombo au taasisi za Serikali katika kutambua, kusimamia na kusaidia michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Katiba ya *FAT.* Pamoja na *FAT* kuwa chama huru chenye Katiba yake, katika hali ya udhaifu niliotangulia kuutaja hapo juu ipo haja ya Wizara kutueleza juu ya wajibu wa Wizara husika katika ushauri wa Muundo wa chama cha Mpira Tanzania *(FAT).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu na mwanya mkubwa wa migogoro kuwa na upeo mdogo wa washiriki katika uongozi wa *FAT* na hivyo nafasi za uongozi kubaki mikononi mwa wachache walioko madarakani kwa sasa ambao wanamudu kuweka udhibiti wa kuhakikisha wanabaki madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia ya *FAT* sasa katika mapendekezo ya muundo mpya inajaribu kuongeza wigo huo, Chama cha Mpira Duniani wiki hii kimeleta mapendekezo tofauti yenye nia ya kutaka kuendelea kupunguza wigo huo. Je, Baraza la Michezo *(BMT)* litaweza kuisaidia vipi *FAT* kipindi hicho kinacholenga kuleta mabadiliko ya Muundo wa *FAT?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti finyu ya *FAT* haiwezeshi chama kuchukua majukumu ya kimichezo Kitaifa. Hivyo ni wajibu wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kupitia Baraza la Michezo la Taifa *(BMT)* kuwa na mpango na mkakati wa Bajeti kamilifu kwa kuwezesha kugharamia maandalizi na ushiriki wa wanamichezo katika ngazi ya uwakilishi wa Kitaifa, katika fani zote za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, klabu zetu zina matatizo ya uongozi na usimamizi wa mapato na matumizi ya klabu zao. Hivyo katika mashindano yanayofanyika kama klabu katika ngazi ya Taifa, Serikali ichukue majukumu hayo kama Taifa kwa manufaa ya wanamichezo na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo, pamoja na pongezi kwa Serikali kuwa na nia ya kutekeleza mpango huo ni vizuri wananchi wakajua yafuatayo:-

Kwanza, nani atakuwa mmiliki wa uwanja huo mpya? Ni *BMT, FAT* au chombo gani?

Pili, je, vyama vingine vya michezo vitakavyokuwa na sehemu za michezo yao ndani ya uwanja huo watakuwa na nafasi gani katika usimamizi na uendeshaji wa uwanja huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa na uwanja mzuri na wa kisasa Dar es Salaam, napendekeza Wizara au Taasisi husika *(BMT)* irejee kuhamasisha kuboresha viwanja vya michezo vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi huko mikoani. Tangu vijengwe, viwanja vingi havipati ukarabati mzuri na hivyo hadhi za viwanja hivyo kushuka mwaka hadi mwaka na pengine mwelekeo ni kuharibika na kushindwa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya njia za kusaidia ni Wizara kuwa na fungu la kusaidia kuendeleza na hata kujenga viwanja vipya kwa kuwasaidia kwa kiwango fulani (%) wadai wa Mikoa na Wilaya zitakazo jitokeza kukarabati na au kujenga viwanja vya michezo. Bila Serikali kukubali na kuthamini kuwa na mpango wa aina hii kwa mfumo uliopo sasa kamwe michezo haitakuwa. Shamra shamra za ushiriki wa wananchi zilizokuwepo miaka iliyopita sasa zimepungua na hasa kutokana na matokeo duni katika ushiriki wa timu zetu mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilaya ya Muheza mwaka 2001 niliiandikia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kuona umuhimu wa kujenga Chuo cha *VETA* makao makuu ya Wilaya ya Muheza. Inaonekana barua hiyo haijajibiwa na hakuna mpango wa *VETA* kuwepo Muheza. Umuhimu wake unakuja kutokana na kuwepo vijana wengi wanaokosa nafasi za kujiendeleza na kushindwa kujiunga na Chuo cha Bweni cha Kiwanda. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na uongozi wa Wilaya upo tayari kutoa eneo la ujenzi wa Chuo hicho, Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mwelekeo wa Wizara juu ya ombi hili la Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi wa Idara ya Kazi Wilaya ya Muheza na Mkoa wa Tanga katika hotuba ya Wizara hii mwaka 2003/2004, niliomba Wizara ipeleke Afisa wa Kazi Wilaya ya Muheza ambayo inaongozwa kwa miaka mingi na Maofisa wa ngazi ya chini baada ya kifo cha Afisa wa Wilaya zaidi ya miaka minne iliyopita. Kabla ya

ombi hilo kutekelezwa, Afisa wa Kazi Mkoa wa Tanga pia akafariki mwaka 2003 na hivyo migogoro ya Wilaya ya Muheza ikakosa pia msimamizi Mkoani. Ipo migogoro mingi ya wafanyakazi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inayoelekezwa kwa Mbunge badala ya Ofisi ya Kazi, tunaomba Mheshimiwa Waziri asaidie Wilaya na Mkoa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kila mara nilipopata nafasi ya kuchangia Wizara hii, nimeonyesha matatizo makubwa ya kituo cha wazee wasiojiweza cha Magugu, Wilayani Babati. Aidha, nimewahi kushauri kuwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe atembelee kituo hiki na kujionea mwenyewe, lakini ahadi hii haijatimizwa. Kupitia mchango huu naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo na anatarajia kufika Magugu lini?

Tatu, naomba kufahamu hatua iliyofikiwa na Serikali katika kujadiliana na Serikali ya Korea ya Kusini kuhusu ujenzi wa Chuo cha Ufundi Mkoa wa Manyara. Kwa kuwa huu ni Mkoa mpya na msukumo wa haraka unahitajika katika eneo la ufundi, ni mazingira yapi sasa Serikali inajenga mkoani Manyara hasa Makao Makuu ya babati kabla ya kujengwa Chuo cha Ufundi cha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kazi njema ikiwa ni pamoja na kupata maelezo ya hoja hizi chache sana.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kuongoza Wizara hii ngumu. Wizara yenye vyama vingi kuliko Wizara yoyote nyingine, lakini kwa umahiri na umakini mkubwa wamefanya kazi nzuri katika kukabiliana na migogoro ndani ya vilabu vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na Chuo cha Ufundi Lindi. Nashauri Wizara itoe kipaumbele katika ujenzi na Chuo cha Ufundi kwa kuanzia Mkoa wa Lindi. Mkoa wa Lindi una shule chache za Sekondari kuliko mkoa wowote mwingine. Aidha, mkoa wa Manyara ni mpya na mkoa wa Pwani upo jirani na mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga ambayo ina vyuo vingi vya ufundi na shule za sekondari nyingi. Naamini busara zitatumika katika maamuzi endapo fedha zitakazopatikana zitatosha kujenga chuo kimoja au viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Lindi, *NSSF* wanacho kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi ni zaidi ya miaka kumi sasa, hakuna chochote kilichofanyika kuendeleza kiwanja hicho. Napenda kupata maelezo nini mipango ya kweli ya kuendeleza kiwanja hicho? Je, bado *NSSF* ina nia ya kujenga hizo nyumba? Au bado mtazamo wa kupuuza mikoa ya Kusini hasa Lindi bado unaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo yanayoeleweka.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuchangia hoja. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watumishi wa Wizara. Baada ya kuwapongeza, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii kuwa na maendeleo ya mazuri ya elimu ya ufundi na ukarabati wa vyuo vya *VETA,* mpaka sasa Chuo cha *VETA* Singida bado hakijaanza kufanyiwa ukarabati licha ya hali mbaya ya Chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu bajeti mwaka 2003/2004 ukarabati wa Chuo hiki ulikuwa umepangiwa kuanza. Naomba kujua ni tatizo gani linaloendelea kufanya ukarabati usianze, je, ni kukosekana kwa Mkandarasi au ndiyo taratibu za sheria ya manunuzi inachelewesha? Naomba kujua hasa ukarabati huu utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mkoa wa Singida aliahidi na kutupa matumaini ya kujengewa *VETA* kwa mfano Chuo cha *VETA* kipya kikubwa. Pia katutaka kutenga eneo kwa ajili ya shughuli hii. Tayari eneo kubwa tumetenga lakini tangu wakati huo sasa ni karibu miaka miwili, naomba kujua Serikali imefikia wapi katika kuandaa ujenzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kujulishwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo hiki katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakutaja ujenzi wa Chuo kipya Singida katika kazi zinazotarajiwa kutekelezwa mwaka wa bajeti 2004/2005. Je, kinategemewa kujengwa lini? Naomba jibu. Ahsante.

**MHE. JANETH E. MASHELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Alhaj Profesa Juma Kapuya na Naibu wake, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo mzuri kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuzungumzia suala la michezo. Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT)* kimekuwa na migogoro muda mrefu sana kutokana na tatizo kubwa la viongozi wa *FAT* kutoelewana. Viongozi hao walisimamishwa lakini cha kusikitisha sana Kamati hiyo hiyo iliwarudisha bila badiliko lolote na ni imani yangu kwamba matatizo yamerudi pale pale na vile vile na inawezekana yameongezeka zaidi. Hivyo napenda kuishauri Wizara iangalie swala hilo kwa makini zaidi kwani migogoro ndani ya vyama ndiyo inazorotesha maendeleo ya mpira badala ya kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile swala la viwanja vya michezo vimekuwa vichache na viwanja hivi huvamiwa na wakaaji na maeneo husika. Sasa kwa kweli viwanja bado hatuna na bila kupatikana viwanja michezo itakuwa vigumu kuendelea. Hivyo naiomba Wizara iangalie hilo suala kwa makini kwani imekuwa miaka inakatika Wizara inaimba wimbo wa kuweka viwanja lakini hakuna lolote. Lakini nina imani sasa umefika wakati wa kuandaa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na swala la vijana kuwa wengi mijini ambao hawana ajira kutaleta hatari kubwa kwa Taifa. Matatizo yamekuwa mengi ya vijana yashughulikiwe vizuri kwani mara nyingi yamechukuliwa kijazba, mara nyingi vijana wanaofanya biashara ndogo ndogo huitwa Wamachinga wamekuwa wakifukuzwa kinyama wakati wanapojitafutia riziki yao bila kujua wale ni binadamu na wana familia zinazowategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ingekuwa vizuri zaidi Wizara ingeandaa mkakati kamambe na mzuri zaidi katika kumaliza tatizo hilo kuliko kukuza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililotaka kuzungumzia ni mbio za Mwenge. Swala la Mwenge nashauri liangaliwe upya kwani ni vizuri swala hili Wizara ingewashirikisha wananchi waamue kama kweli suala la Mwenge bado linahitajika na kama bado kuna umuhimu wa kuwa na mbio za Mwenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la upungufu wa watumishi hasa wa Mahakama ya Kazi, upungufu huo umetokana na watumishi waliopo kutofanya kazi kwa ufanisi unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya watoto imekuwa ni tatizo kubwa linaloathiri maendeleo ya watoto na kuhatarisha nguvu kazi au rasilimali. Watoto wengi huathirika afya zao kimasomo na wengine kukosa haki zao za kupata elimu. Vile vile Serikali ingeweka mikakati kabambe ya kukomesha ajira ya watoto kwani inaongeza kiwango kikubwa cha umaskini vijijini na mijini. Hivyo jitihada za dhati zinatakiwa kuelekezwa katika kuondoa umaskini.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pole kwa familia na wananchi wa jimbo la Ulanga Mashariki kwa kufiwa na mzazi na mwakilishi wao Marehemu Mheshimiwa Capt. James Kasapira na naomba Mungu ailaze pema roho ya Marehemu, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu, wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kueleweka na kutoa matumaini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kupata taarifa ndani ya hotuba kwamba sera ya huduma kwa watu wenye ulemavu tayari imekwishapitishwa na Baraza la Mawaziri. Haya ni mwanzo wa mafanikio na dalili njema ya maisha bora kwa jamii ya watu wenye ulemavu nchini. Nashukuru kwa miaka mitatu iliyopita nimekuwa nikiihimiza Serikali kukamilisha sera hii na hatimaye sasa utetezi na ushauri wangu umetekelezwa na kwa upande mwingine ndiyo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kuhusu jamii ya watu wenye ulemavu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, sera hii ieleweke kwa wananchi kupitia semina na kadhalika. Licha ya elimu, naomba sana Wizara iharakishwe kuleta Sheria hapa Bungeni ili sera (dira) hii iweze kutekelezwa kwa vitendo hivyo kupunguza manung'uniko na umaskini wa kipato kwa watu wenye ulemavu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kukamilisha waraka wa kuridhia taratibu za Umoja wa Mataifa kuhusu fursa na haki sawa kwa watu wenye ulemavu. La msingi ni *speed* ya utekelezaji wa kuridhiwa huko angalau iwe ndani ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inafahamu sana suala la muongo wa watu wenye ulemavu Barani Afrika ulianza 1999 hadi 2009. Kwa vile Tanzania ni moja ya nchi iliyoridhia Azimio hilo, la kusikitisha ni kwamba Serikali wala haijatoa mwelekeo, mipango wala miongozo ya utekelezaji wa yale yaliyomo kwenye tamko hilo angalau kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka inapita hakuna kinachofanyika na nachelea Serikali inapeleka taarifa gani kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Afrika kuhusu utekelezaji wa muongo wa Afrika kwa watu wenye ulemavu ambayo Serikali inapaswa kupeleka mara mbili kwa mwaka. Naomba kufafanuliwa ni mara ngapi taarifa hizo zimepelekwa kwa Katibu Mkuu? Ninaloliona ni kwamba muongo utakwisha na watu wenye ulemavu hawatakuwa wamefaidika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Serikali ina mfuko wa vijana wa kuwakopesha, lakini kwa masikitiko makubwa, vikundi vya vijana wenye ulemavu havipati mikopo hiyo, pamoja na kwamba wao ndiyo maskini wa kipato wa kutupwa. Rai kwa Serikali na Wizara kuwa maafisa vijana wahusika katika kusimamia vema ugawaji wa mikopo hiyo wakiwa wameelimishwa kuhusu uendeshaji wa miradi yao hiyo la sivyo vijana hawa huishia kuzagaa mitaani na kuwa omba omba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana na jitihada za Serikali katika kuendeleza michezo kwa watu wenye ulemavu kwa kuandaa walimu wa michezo hiyo na kusimamia mashindano mbalimbali yanayowahusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kutoa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu. Lakini la kusikitisha ni kwamba kiasi kinachotolea kwa kila Chama ni kidogo sana tena kwa kuchelewa na bila vigezo vilivyo wazi. Naiomba Wizara itoe ufafanuzi wa suala hili kwa viongozi wa *DPOs* kwani manung'uniko ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *VETA* kwa kuwezesha watu wenye ulemavu kuweza kusoma bila vikwazo vingi na hasa kwa azma ya kuwapatia nyenzo za kuanzia kujitegemea baada ya mafunzo.

Nakubaliana na maoni ya Kamati kuhusu umuhimu wa kuendelea kuboresha kwa dhati kabisa utoaji huduma katika makazi ya wazee, watu wasiojiweza na watu wenye ulemavu kwani baadhi ya makazi yanakosa hata chakula na kusababisha walengwa

kuondoka makambini na kwenda kuzagaa mitaani na kuombaomba. Hivyo ni wajibu wa Wizara kujaribu kushirikiana na wadau kwengine katika kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu naomba kuunga mkono hoja na nategemea ufafanuzi sahihi nitapewa katika sehemu nilizoulizia.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Alhaj Juma Kapuya, Mheshimiwa Ustadh Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wataalam wao wote kwa kuwasilisha hotuba yao mble yetu, inayoonyesha matumaini na muelekeo wa kuanza sura mpya ya maendeleo ndani ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu kwa kuchukua uamuzi wa busara kwa kuamua kujengwa kiwanja cha kisasa katika nchi hii haraka iwezekanavyo kabla ya kumaliza muda wake wa uongozi mwaka 2005, hii ni kuikomboa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uwanja huu ni sawa na kutuondoa gizani na kutuweka kwenye mwanga, kwani nchi hii ni miongoni mwa nchi zilizopata uhuru mapema sana katika Afrika kwani hivi sasa tumeshatimiza miaka 43 ya Uhuru wetu, lakini hatuna maendeleo mazuri ya michezo ukilinganisha na wenzetu ambao hawatufikii kiukombozi, wamepiga hatua kubwa kuliko sisi tuliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali pamoja na jitihada zake inazozichukua za kuwaangalia ndugu zetu wenye ulemavu, bado izidishe nguvu zaidi kwani kila siku walemavu wanaongezeka kutokana na maajabu mengi yanayotukabili kwani sisi sote ni walemavu watarajiwa kwani bado tuko hai na mahangaiko mengi tunayo ya kutafuta maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwa na vijana wengi katika Taifa hili ambao ndiyo viongozi wetu wa baadaye tunaowategemea kuliongoza Taifa hili ni vizuri tukawaangalia katika mtazamo wa matumaini ya maisha yao kwa kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa wazi kuwa si rahisi Serikali yetu ikiwapatia kazi vijana wote waliomo ndani ya nchi hii, lakini kama tutaandaa mpango mzuri wakati wanapokuwa shuleni waweze pia kujifunza kazi za mikono na ufundi wa aina mbalimbali wangeweza kumaliza masomo yao na wakaanza wao wenyewe kujitegemea na wasingesubiri wamalize shule ndio sasa waende katika vyuo vya *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya soka hivi na uongozi mbaya ulioko katika *FAT.* Hii ni kutokana na Wizara kuiogopa *FAT* kwa kuhofia kufungiwa na *FIFA,* Namwomba Mheshimiwa Waziri afikirie zaidi katika hili kwani hivi sasa *FIFA* kwa Tanzania iko njiani hata kumchagua Waziri wa Michezo awe ni yule ambaye wanamtaka wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kama Mheshimiwa Waziri, *FIFA* hawatamtaka atakwenda wapi au atakwenda kuwabembeleza wamchague yeye?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema usipowatetea Watanzania walio wengi katika nchi hii utamtetea nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Bajeti yake nzuri sana, ameisoma kwa makini, yenye mwelekeo mkubwa wa kuleta maendeleo katika Taifa letu, nampongeza sana. Aidha, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia suala la kazi. Kazi kwetu Tanzania ni kero kubwa na inaonyesha kuwa kufanya kazi zisizo za Serikali na ajira ni dhambi. Mimi nasema kazi ni uhai, kazi ndiyo maisha. Usipofanya kazi utakufa au utaiba, vinginevyo utatakiwa kufanya kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaongozwa kwa mujibu wa sheria, Katiba, kanuni, taratibu na Kauli za Serikali. Hivyo basi, Tanzania kuifuta Sheria ya nguvu kazi ni kosa kubwa mno. Kufuata taratibu za Mataifa yaliyoendelea sisi tukiwa nchi maskini ni kuididimiza nchi yetu. Tanzania ina idadi ya watu milioni 35, wanaofanya kazi ni robo yao. Huu ni mzigo mzito kwa Serikali na kwa Taifa zima. Tanzania huongozwa kwa mujibu wa Sheria na ni halali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uhakikishe kuwa watu wote wenye uwezo wa kufanyakazi wanafanyakazi, sharti uwe na sheria, Kanuni na taratibu za kudhibiti mianya ya watu kutokufanya kazi. Tanzania ni nchi maskini duniani. Ili iweze kuondokana na umaskini huo ni sisi Watanzania kufanyakazi kwa juhudi na maarifa, kinyume chake ni kuwa maskini wa kutupwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ombaomba duniani. Ili iondokane na umaskini wa kuombaomba, Watanzania hawana budi kufanya kazi kwa kujituma, kwa juhudi na maarifa, ndipo watakapoondokana na aibu hii mbaya ya ombaomba. Watu wengi ukiwatumia vizuri ndiyo nguvu yako, lakini ukiwatumia vibaya ni mzigo kwako. Watanzania kwa sasa hawazalishi kama ilivyo, yaani kwa kila mtu amezalisha vipi leo, kwa mwezi na hata kwa mwaka. Kinacholiwa ni kingi maradufu kuliko kinachozalishwa. Hatima yake ni kufilisika mkala hata mbegu, mbegu ambazo mlikuwa mmeweka kwa ajili ya kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu tunamwaibisha sana kuwa Rais wa Taifa la ombaomba. Anatembeza bakuli la kuombea chakula na misaada mingine ya maendeleo. Tanzania tunapopewa misaada na wenzetu walioendelea, basi na sisi tujitahidi kufanyakazi kushirikiana na waliotupa misaada hiyo. Kuondoa umaskini Tanzania ni

kupata elimu ya kupambana nao na kisha Watanzania wote wenye nguvu wafanyakazi kwa juhudi na maarifa. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma dibaji ya sera mpya ya wazee nikaona kitu kipya kabisa na nanukuu: "...tunatambua kwamba wazee ni rasilimali na nguvu mpya katika maendeleo ya nchi yetu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetafakari nadharia hii nimeshindwa kuielewa katika nadharia za kawaida za *biology* na *growth and development of organisms.* Wote tungefaidika kwa kuelewa nadharia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Ndugu Muhidin Ndolanga leo yupo? Nadhani atapata vibwagizo leo. Nawatakia kila la kheri na Bajeti yenu.

**MHE. ALHAJI SHWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii inahusu rasimu ya Katiba Mpya ya *FAT.* Naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumo wa uwakilishi katika Mikutano Mikuu ya *FAT* kwa ngazi zote katika mfumo wa sasa, uwakilishi katika mikutano mikuu ya *FAT* kuanzia ngazi ya Kijiji, Mtaa, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, wajumbe wake wanapatikana kwa kuchaguliwa kwa ngazi inayohusika. Mfumo huu inabidi ubadilishwe. Napendekeza nafasi ya uwakilishi katika kila ngazi kuanzia Vijiji, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, itolewe kwa wadau ambao watatokana na *Club* za Mipira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya *FAT* iwe wazi kwamba uwakilishi katika mikutano mikuu ya *FAT* kuanzia ngazi ya Kijiji, Mtaa, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, upatikane kutoka katika *Club* za mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa sasa, Katiba ya *FAT* haitoi nafasi kwa vilabu vya mipira kuteua wawakilishi wao katika mikutano mikuu ya ngazi yoyote ile ya *FAT,* badala yake inatoa nafasi kwa mtu yeyote yule asiyehusika na *Club* yoyote ya mpira kugombea nafasi yoyote katika ngazi yoyote ya *FAT.* Mfumo wa sasa kwa maoni yangu, hautoi haki kwa wadau kushiriki katika vikao vinavyotoa maamuzi ya mchezo wa mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo wa mpira ni mchezo maarufu sana duniani. Nchi yetu katika mchezo wa mpira, haipo Kisiwani. Kwa ajili hii, ni muhimu sana kujifunza kutokana na namna ya mchezo huu unavyoendeshwa kwa ufanisi katika nchi nyingine duniani. Nchi yetu haiwezi kuongoza Chama cha Mpira Tanzania kwa mfumo wa kuwaacha nje viongozi wenye *Club* za mipira. Viongozi hawa wakipewa haki ya Kikatiba, watakuwa nguzo kubwa sana ya kujenga mchezo wa mpira Tanzania.

Kwa hiyo, napendekeza mfumo wa kupata viongozi wa mikutano mikuu ya Chama cha Mpira Tanzania, wapatikane kwa kuteuliwa na *Club* za mpira. Katiba

ionyeshe mikutano mikuu ya ngazi yoyote. Wajumbe wa mkutano mkuu wateuliwe na *Club* zilizopo katika ngazi hiyo. Pengine ingekuwa bora kila *Club* iteue viongozi watatu wa kuhudhuria mikutano mikuu ya ngazi yoyote husika ya Chama cha Mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo utaondoa kiwingu cha rushwa kwa kiwango kikubwa katika kuchagua viongozi kwa sababu wote wenye vilabu ndiyo wadau. Aidha, Katiba itamke watakaoomba kutaka nafasi za kugombea uongozi kwa ngazi yoyote ya Chama cha Mpira, wapeleke majina na maombi yao katika Baraza la Michezo la ngazi husika ya Chama hicho cha Mpira. Baada ya kuchujwa na Baraza la Michezo la ngazi husika, Baraza la Michezo la ngazi husika litapendekeza majina ya waombaji waliopitishwa na Baraza la Michezo la ngazi husika. Watayatangaza majina ya wagombea hao ili yapigiwe kura na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mpira wa ngazi husika. Utaratibu huu nionavyo mimi utaondoa kabisa kiwingu cha rushwa katika kuchagua viongozi wa Chama cha Mpira kwa ngazi yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili inahusu mfumo wa uendeshaji wa ligi. Mfumo wa sasa hautoi nafasi kwa Taifa kujua vijana wake wenye vipaji vya mchezo wa mpira. Napendekeza mfumo wa sasa ubadilishwe, badala yake, uwepo mfumo wa ligi kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Ligi za timu za vijijini ziendeshwe ili kupata timu moja.
(ii) Kila Kijiji katika Kata, kitatoa timu moja kushiriki katika Ligi ya Kata.
(iii) Kila Kata itatoa timu mbili katika Ligi ya Tarafa.
(iv) Kila Tarafa itatoa timu tatu katika Ligi ya Wilaya.
(v) Kila Wilaya itatoa timu tatu katika Ligi ya Mkoa.
(vi) Kila Mkoa utatoa timu moja katika Ligi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya tatu, ili mchezo wa mpira wa miguu uwe na hadhi ya *agenda* ya Kimataifa, Serikali lazima ishiriki katika uendeshaji wa mchezo huu. Haitoshi na wala haipendezi kwa Serikali kujitoa kwa hoja kuwa sasa Serikali haihusiki au inajitoa na uendeshaji wa mchezo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza rasimu ya Katiba mpya itamke kabla ya Chama cha Mpira *(FAT),* kwa ngazi zote kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, ziandae *Business Plan* itakayoonyesha namna watakavyoendesha shughuli za mchezo wa mpira kiuchumi. Napendekeza kama Chama cha Mpira kitashindwa kuandaa *Business Plan,* Katiba itamke Chama cha Mpira hicho hakitosajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napendekeza *Club* zote za Mpira, nazo zionyeshe *Business Plan* itakayoonyesha jinsi *Club* zitakavyoendesha shughuli za Mchezo wa Mpira. Kama *Club* itashindwa kuandaa *Business Plan* ya kuendeshea mchezo wa mpira, isipewe usajili. Hii ni pamoja na *FAT* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya nne, inahusu upatikanaji wa Mwenyekiti wa *FAT* na Katibu wa *FAT* wa ngazi yoyote. Napendekeza Katiba itamke Mwenyekiti

wa Chama cha Mpira wa ngazi yoyote kuanzia Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa apatikane baada ya jina lake kuchujwa na Baraza la Michezo la ngazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mwombaji wa nafasi ya Mwenyekiti au Mjumbe wa ngazi yoyote baada ya kuthibitishwa kugombea na ngazi ya Chama cha Mpira husika, anaweza kuwa mtu yeyote yule, lakini wapigaji kura wa nafasi ya Mwenyekiti au Mjumbe kwa ngazi anayotaka, Katiba itamke Wajumbe wa kupiga kura hizo watokane na *Club* zilizosajiliwa na kwamba Katiba itamke ni idadi ya Wajumbe wangapi watakaoatoka katika vilabu kwenda Baraza la kuchagua viongozi wa ngazi husika. Nashauri Katiba itamke Wajumbe watatu wa kila *Club* iliyosajiliwa ndiyo watakaofanya Wajumbe wa kumchagua Mwenyekiti na Wajumbe wa Chama cha Mpira kwa ngazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nafasi ya Katibu Mkuu, napendekeza *very seriously,* Katiba itamke atateuliwa na Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na hii ni pamoja na uteuzi wa Makatibu wa Mkoa na Wilaya baada ya kupelekewa mapendekezo na Baraza la Michezo la Taifa. Kwa hiyo, atakuwa mwajiriwa wa Wizara, lakini Katiba itamke atakuwa na mkataba wa miaka mitatu. Katiba itamke anaweza kufukuzwa bila malipo endapo utendaji wake utakuwa mbovu kiasi cha kusababisha timu zetu katika mashindano makubwa tuwe wasindikizaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine, nashauri Katiba itamke waziwazi nafasi ya wachezaji maarufu wa zamani walioacha kucheza, ama kwa uzee au ugonjwa. Wachezaji wa aina hii tuwe nao kwa ngazi zote kuanzia Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa. Nimegundua mara nyingi baadhi ya viongozi wa *FAT* kwa ngazi yoyote ile, kujiona kuwa wao ndio rejea kubwa ya mambo yanayohusu mchezo wa mpira. Kwa ajili hii, huwa hawatoi nafasi kwa wachezaji wa zamani kutoa maoni na ushauri wao. Hilo ni kosa.

Napendekeza Katiba ya Chama cha Mpira Tanzania *(FAT)* itamake nafasi ya wachezaji wa zamani katika vikao vya ngazi husika za Chama cha Mpira Tanzania. Pengine ingekuwa vizuri zaidi kama Baraza la Michezo la ngazi husika ya Chama cha Mpira ndiyo inayoteua majina ya wachezaji wa zamaji katika vikao vya ngazi husika ya Chama cha Mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kuwa mfumo wa sasa wa Ligi ubadilishwe. Kwa maoni yangu, hautoi nafasi kubwa ya kuendeleza mchezo wa Mpira Vijijini, Katani, Tarafani, Wilayani, Mkoani na Taifani. Vijana wanadhani wakichezea timu za Dar es Salaam, watakuwa wameongeza kipaji cha ufundi wa mchezo wao. Aidha, wakicheza timu za Dar es Salaam watakuwa wanapata malipo ya fedha nzuri. Hoja hiyo inazungumzika, lakini haitaendeleza mchezo wa mpira katika nchi yetu hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri kubwa ya kuendeleza mchezo wa mpira ipo katika maandalizi ya uendeshaji wa ligi ya mchezo wa mpira. Nchi inapata wawakilishi wazuri kama itakuwa na michezo ya ligi inayowakilisha timu zilizoshiriki kuanzia Vijijini.

Chama cha Mpira kionyeshe kukubali kwake na kionyeshe kushiriki kwake katika kusimamia ligi za ngazi zote, isiishie kwenye ligi ya Taifa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa na Chama cha Mpira cha Taifa, nashauri ikubali wajenge mfumo mpya wa kuweka nguvu katika ngazi za ligi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa. Utaratibu huu ukiwemo ndani ya Katiba, utatuwezesha kila Mkoa utoe timu mbili kwa Ligi Kuu ya Taifa. Zamani tulipokuwa na mashindano ya Mpira ya *Sunlight,* kila Mkoa ulikuwa unaleta timu moja ambayo kupatikana kwake huundwa na wachezaji wa kutoka kila Wilaya za Mkoa husika. Kwa wakati ule mikoa ilikuwa inatoa wachezaji wazuri sana na kuifanya nchi yetu kuwa tishio kubwa sana katika mashindano na *Gossage Cup* hapa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tuliokuwa tunautumia sisi ndiyo utaratibu unaotumiwa na nchi ya Brazil. Wenzetu kila *State* inajua timu moja katika ligi ya Taifa. Timu inayoingia mashindano ya Ligi ya Taifa, mara nyingi huongeza nguvu kwa kuongeza wachezaji wengine wazuri wa timu nyingine zilizomo ndaniya *State* hiyo. Mfumo huu unasitisha kuhamahama kwa wachezaji kutoka *State* moja kwenda *State* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu napendekeza sasa turudie mfumo uliokuwa unaendesha mashindano ya *Sunlight Cup* katika kupata bingwa wa Ligi Kuu. Katiba itamke kila Mkoa uwe na ligi yake. Hatimaye timu itakayoshinda katika ligi ya mkoa, iruhusiwe kuongeza nguvu ya wachezaji wengine wa kutoka katika timu zilizoshiriki ligi ya ndani ya Mkoa husika. Hali hiyo pia ianze kwenye Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa.

Kwa maoni yangu, mfumo huu ukiwemo ndani ya Katiba, utaboresha namna nzuri ya kupata wachezaji wazuri wa mpira na kupunguza mlundikano wa wachezaji wa kutoka Mikoani kuja Dar es Salaam. Aidha, mfumo huu utakuza vipaji vya mchezo wa mpira kwa vijana wetu kuanzia Vijijini, Katani, Tarafani, Wilayani, Mkoani na Taifani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri michango ya wadau wa mchezo wa mpira inaweza isiwe na umuhimu wowote kwa sababu Chama cha Mpira Tanzania *(FAT)* tayari kimekwisha peleka rasimu ya Katiba mpya ya *FIFA* kabla ya kupata michango ya mawazo ya wadau wa mchezo wa mpira Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, hili ni kosa kubwa lililofanywa na uongozi wa *FAT.* Kwa kuwa Katiba ya *FAT* inahusisha Taifa zima, nakushauri uwasiliane na *FIFA* kwa kuwaeleza wasizingatie kabisa mapendekezo yaliyokuwemo katika rasimu waliyopelekewa na *FAT,* wasubiri mpaka rasimu itakapozingatia maoni na mapendekezo ya wadau wa mchezo huu wa mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa Katiba ya *FAT* lazima ipate usajili, napendekeza Baraza la Michezo la Taifa lisitambue usajili wa Katiba hiyo mpaka hapo rasimu ya Katiba hiyo itakapojadiliwa na wadau wa mchezo wa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nakushauri uongozi wa *FAT* wa sasa wawajibishwe kwa kudanganya wadau wa mchezo wa mpira kwa kuwataka watoe michango yao katika rasimu ambayo wao *FAT* tayari wamepeleka rasimu ya Katiba hiyo *FIFA*. Serikali lazima ikemee uamuzi huo wa *FAT* na iwaagize waufute kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu mchezo za mpira ni sawasawa na askari wa Jeshi la Wananchi linapopigana vita. Hata siku moja katika jeshi haitawezekana liongozwe vitani na Afisa wa Jeshi aliyekosa mafunzo ya kijeshi. Mchezo wa Mpira ni kielelezo muhimu sana cha kulitangaza Taifa letu Kimataifa. Hivyo, kukiachia chombo hiki kuendeshwa au kuongozwa na watu ambao hata mchezo wa Chandimu hawakucheza, ni kulidhoofisha Taifa letu duniani katika mchezo huu maarufu wa mpira duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa kwa nini Serikali yetu inashindwa kuona na kuelewa upungufu huu wa viongozi wa *FAT*. Nimesoma katika gazeti la Uhuru la hivi majuzi kuwa Mwenyekiti wa *FAT* anawalaumu Waheshimiwa Wabunge kuzungumzia udhaifu wa *FAT* na amewataka Wabunge kama wanautaka uongozi wa Uenyekiti wa *FAT,* wachukue fomu za kuomba kugombea. Huu ni udhaifu wa kiongozi huyu wa *FAT,* kwa sababu anadhani Wabunge wana mipaka ya kuzungumzia masuala ya Kitaifa ndani ya Bunge.

Namshauri asome Katiba ya Tanzania ili apate kujua majukumu ya Wabunge ndani ya Bunge. Mchezo wa mpira ni kielelezo cha Taifa letu Kimataifa, ndiyo maana kila timu zetu zinapotoka nje au zikicheza hapa hapa nchini, Bendera ya Taifa letu inapandishwa na wimbo wa Taifa letu unapigwa. Mambo haya yote ni kielelezo cha Taifa letu, hivyo kuwabana Waheshimiwa Wabunge wasikemee udhaifu ulio dhahiri ndani ya utendaji wa *FAT,* ni utovu wa nidhamu na inastahili Serikali ikemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepata heshima kubwa sana duniani wakati Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipopinga mapendekezo ya Uingereza katika *Commonwealth* kuhusiana na uanachama wa Afrika Kusini. Huo ni mfano mmoja tu wa namna Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alivyoweza kutoa maamuzi yaliyoipatia heshima kubwa sana Taifa letu Kimataifa. Nashangaa sana kwa sasa Serikali yetu inakaa kimya kwa suala zito kama hili la Katiba ya *FAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia katika vyombo vya habari kuwa ipo Mikoa kwa sababu ya kukosa kufanya uchaguzi wa uongozi wa *FAT* ya mikoa hiyo na kwa sababu mikoa hiyo haikupeleka maoni yao juu ya rasimu ya Katiba ya *FAT,* haitaruhusiwa kuhudhuria mkutano utakaofanyika Mwanza wa kupitisha Katiba ya *FAT*. Baadhi ya mikoa hiyo Mkoa wa Morogoro ni mmoja wapo. Huu ni uamuzi dhaifu sana. Napendekeza Serikali irudishe mfumo wa zamani wa kuwapata viongozi wa *FAT*. Mchezo wa mpira si lelemama, unahitaji viongozi waliopevuka na masuala ya mchezo wa mpira. Haipendezi hata kidogo kwa Serikali kuwaonea haya viongozi wenye mwelekeo wa kudhoofisha mchezo huu maarufu wa mpira.

Katika nchi yetu, Mkoa wa Morogoro ni mkoa mmojawapo ulitoa wachezaji wazuri sana katika Taifa letu. Kwa hatua hii ya *FAT* ya kuwanyima viongozi wa mpira kutoka Mkoa wa Morogoro kuhudhuria mikutano wa Katiba mpya ya Mchezo wa Mpira wa Miguu utakaofanyika Mwanza, ni sawa na kutaka kuigawa nchi yetu katika mchezo wa mpira na mtu akitaka kufuatilia historia ya mchezo wa mpira hata akianzia wakati bado hatujapata Uhuru, atagundua Mkoa wa Morogoro wakati huo ukiitwa *Eastern Province,* atakubali wachezaji wazuri walitoka mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi leo viongozi wa *FAT* kwa udhaifu wao na upungufu wao wa utoaji wa Taarifa kwa wakati muafaka, wanautenge Mkoa wa Morogoro? *FIFA* si Mungu. Haiwezi kutuamulia mambo yetu. Je, *FIFA* inafanya hivyo kwa nchi za *Latin America* na nchi za Ulaya? Au tuseme viongozi wetu wa *FAT* wanatumia kivuli cha *FIFA* ili kupitisha mambo wanayotaka wao. Nashauri kwa jambo hili, Serikali isiwe na kigugumizi. Serikali iingilie kati suala la hoja hii. Serikali inahitaji iendeshe mambo yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, inapotokea sheria, kanuni na utaratibu hazifuatwi, Serikali inahitajika lazima ichukue hatua kali dhidi ya viongozi wa vyombo vinavyofanya kazi nje ya sheria, kanuni na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayofanya kazi yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu, lazima itatazamiwa kuchukua hatua kali dhidi ya viongozi wanaokwenda kutekeleza kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Inawezekana hatua hii si jambo jepesi kuchukuliwa na Serikali, lakini halina budi litekelezwe na Serikali kwa shabaha ya kujenga nidhamu na uwajibikaji kwa watendaji wanaokiuka sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda Serikali haina sheria, au kanuni na utaratibu wa kuendesha *FAT.* Kama sheria, kanuni na taratibu hazipo, hili ni kosa ambalo lazima lirekebishwe kwa kutungiwa sheria, kanuni na taratibu. Ikiwa kweli sheria, kanuni na taratibu za kusimamia uendeshaji wa *FAT* hazipo, ninavyofahamu mimi Serikali imeunda Baraza la Michezo la Taifa ambalo muundo wake, Wajumbe wake wote wa Baraza hilo la Michezo la Taifa wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya michezo. Mwenyekiti wa Baraza hilo la Michezo pia anateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia michezo, ikiwemo pamoja na mchezo wa mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza hili la Michezo la Taifa ni *Regulatory Board* ya Wizara katika masuala ya michezo. Kwa maana hii, Wizara ya Serikali yenye dhamana ya michezo inaweza kabisa kupitia Baraza lake la michezo la Taifa kumwadhibu kiongozi yeyote yule anayekiuka kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za mchezo wa mpira kama ilivyokwisha toa adhabu kwa baadhi ya wachezaji wa mpira. Kwa maana hii, madai ya hoja kwamba Serikali yenye dhamana ya Michezo haina uwezo wa kuingilia shughuli za *FAT,* hayana msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa na Katibu Mkuu wa *FAT* kuwa *FIFA* imekataa kuwepo kwa Halmashauri Kuu ya *FAT.* Ninavyofahamu mimi, Makatibu wa *FAT* wa Mikoa ni sehemu ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya *FAT.* Kama rasimu hii kabla ya kupelekwa *FIFA,* nina hakika mapendekezo ya rasimu ya Katiba mpya ya *FAT,*

isingefuta Halmashauri Kuu ya *FAT.* Kwa sababu Halmashauri Kuu ya *FAT* inawakilisha mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika hali hii, mchezo wa mpira utaendelezwaje wakati mikoa haina wawakilishi katika vikao vinavyotoa maamuzi ya shughuli za uendelezaji wa mchezo huu wa mpira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naleta maombi kwako kwa mchango wangu unaohusisha sana rasimu ambayo naomba wakati Katiba mpya ya Chama cha Mpira cha Tanzania *(FAT)* itakapokuwa inapitishwa, maoni yangu haya yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukujulisha kuwa, mimi mpira nimecheza, naomba ukubali kuwa naujua. Asante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, hoja ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwaomba wote waliofiwa tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. James Kasapira, kuwa na subira. Mwenyezi Mungu, azipumzishe mahali pema roho za wapendwa wetu. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika ufafanuzi kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizogusa maeneo ya *VETA,* vijana, ustawi wa jamii na michezo. Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutupa maoni na hoja nzito nzito ambazo ni nyenzo katika utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, wametoa maoni yao kwa kutoa ushauri kwamba Serikali iruhusu Taasisi za Umma ndogo ndogo kama *VETA* kununua vitu au malighafi kutoka kwenye *source* moja kwa moja kama walivyoruhusiwa Wakuu wa Shule za Sekondari ili kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kupunguza bei za bidhaa zinazotengenezwa.

Tunashukuru kwa ushauri huo, Wizara itawasiliana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu ili kujua taratibu zilizotumika kuruhusu Shule za Sekondari kununua malighafi kutoka kwenye *source* na hivyo kuona uwezekano wa kutumia taratibu hizo kwa *VETA.* Naamini uamuzi huo kama utakubalika utapunguza sana gharama za vifaa vinavyotengenezwa *VETA.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameitaka Serikali iunge mkono *VETA* kwa kuongeza ruzuku. Mpaka sasa Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa *VETA* kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama vile kupitia misaada na mikopo kutoka Mashirika mbalimbali ya Kimataifa mfano, *ADB, OPEC Fund, JICA, DANIDA* na *GTZ.* Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Korea ya Kusini kwa

ajili ya kupata mkopo kwa masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, yeye anataka kujua hatua ya Serikali ilipofikia kuhusiana na majadiliano na Serikali ya Korea ya Kusini kuhusu ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Korea imekwishakubali kimsingi kutoa mkopo kwa ajili ya chuo hicho, pamoja na kile cha Pwani na Manyara. Tayari uongozi wa Mkoa wa Manyara umekwishatoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi huo na taratibu za kusajili kiwanja hicho sasa zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Margareth Mkanga, anaipongeza *VETA* kwa kuwawezesha watu wenye ulemavu kuweza kusoma bila vikwazo vingi na hasa azma ya kuwapatia nyenzo za kuanzia kujitegemea baada ya mafunzo. Tunamshukuru Mheshimiwa Margareth Mkanga, kwa pongezi hizo na tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, *VETA* itaendelea na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, ameitaka Wizara kutoa kipaumbele katika ujenzi wa Chuo cha *VETA,* Lindi kutokana na uhaba wa Vyuo vya Ufundi na Shule za Sekondari Mkoani humo ikilinganishwa na Mkoa mwingine wowote. Tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Chuo cha Ufundi Lindi kitajengwa kama tulivyoahidi. Mimi binafsi, Mwenyekiti wa Bodi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu tulishafika Lindi, tumeongea na viongozi wa Mkoa wa Lindi na wa Halmashauri ya Mji wa Lindi, tumeonyeshwa eneo la chuo pale Mitwero na tumelikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, yeye anazungumzia ucheleweshwaji wa ukarabati wa Chuo cha Singida na ujenzi wa chuo kipya Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Singida hakikarabatiwi, ila kitajengwa chuo kipya. Ujenzi wa chuo kipya utaanza mwaka huu wa fedha. Ucheleweshaji ulitokana na taratibu za kutiwa sahihi kwa mikataba kati ya *ADB* na Serikali ya Tanzania ndiyo maana ukaona tumesita kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge wapangaji wote pale hoteli ya *VETA,* ametoa njia bora ya kuboresha hoteli yetu ya *VETA,* huduma, pamoja na ustawi wa wafanyakazi katika hoteli ile. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefarijika sana na ushauri wake na mimi mara kwa mara amekuwa akiniita kila panapotokea tatizo na tumeanza leo. Maadam Mwenyekiti wa Bodi yuko hapa na Kaimu Mkurugenzi, baadhi ya hatua zimeanza kuchukuliwa leo na nafikiri mkirudi usiku mtaona kuna mabadiliko. Ninakuthibitishia kwamba tutaendelea kufuata maoni yako mpaka tuhakikishe kwamba kila kitu kimekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, wameipongeza *VETA* kwa kazi nzuri inayoonekana nchini kote iendelee kutoa mafunzo kwa vijana wengi zaidi. Pia, wametaka *VETA* na Serikali tutafute namna ya kuwapatia vijana wanaomaliza mafunzo vifaa yaani tools, ili waweze kujiajiri. Tunazipokea pongezi zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishieni kwamba, tumeanza kushirikiana na baadhi ya wazazi katika vyuo, lakini hatua kwa hatua tunaongeza wigo wa vyuo ili katika muda mfupi ujao kila chuo kihakikishe kwamba mwanafunzi anapoondoka awe anaondoka na vifaa vya kwenda kuanzia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Margareth Mkanga alizungumzia suala la vijana wenye ulemavu huwa hawapati mikopo toka Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni kukopesha vijana wote bila kujali jinsia yao au hali yao ilivyo kama ni watu wazima kabisa au walemavu. Vijana hawa wawe kati ya miaka 15 na miaka 35. Kama kuna Halmashauri inaacha kwa makusudi kukopesha vijana wenye ulemavu kwa sababu ya ulemavu wao, wanafanya makosa na kwa kweli si ubinadamu na tunaamini kwamba kwa mujibu wa maelezo haya basi watajirekebisha ili mikopo hiyo itoke bila ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kuandika kwa Halmashauri kwamba vijana wenye ulemavu wangepewa kipaumbele mikopo hii inapofika. Nazungumzia juu ya Maafisa Vijana, waelimishwe kuhusu kusimamia mikopo kwa vijana na kusimamia uendeshaji wa miradi ya vijana. Wizara hii kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya itaendelea kuendesha mafunzo kwa vijana na maofisa vijana kuhusu namna ya kusimamia fedha za mikopo na usimamiaji na uendeshaji wa miradi ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya amezungumzia juu ya vijana na mitaji kwamba, vijana ni mtaji wa leo, hivyo Taifa liwekeze kwa vijana, tunakubaliana naye na tunamuunga mkono kwa hilo. Wizara kwa kupitia Sera ya Maendeleo ya Vijana, imeandaa mikakati mbalimbali ya kuwajengea vijana uwezo, mkakati ambao umepewa jina la *Youth Empowerment Programme. (Makofi)*

Halafu, Mheshimiwa Sophia Simba, amesema vijana wengi ni wazururaji kutokana na malezi duni. Vijana wanaomaliza *VETA* wanaajiriwa na nani? Kulingana na rasilimali tulizonazo ardhi, mito, maziwa na misitu kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo ama *Fish Industries* vitakavyoweza kusaidia vijana wetu kujiajiri.

Katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Vijana, suala la malezi na makuzi ya watoto na vijana limepewa kipaumbele sana. Wengi wa vijana wanaomaliza *VETA* wanashauriwa kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali ili kurahisisha jinsi ya

kuwapatia mikopo na maeneo ya kufanyia kazi na ndiyo maana *VETA* mafunzo yake huchukuana sana na mazingira ya mahali hapo. Kama chuo kipo ziwani au kando kando ya Bahari ya Hindi, tunahakikisha vile vile tunaingiza na mambo kama vile kutengeneza boti ili kijana akimaliza asiwe na sababu ya kuhama tena kwenda kutafuta kazi, pale alipo mazingira yake aweze kuyamudu. *(Makofi)*

Lakini suala hili la uzururaji kuna baadhi ya Mikoa na mimi ningependa sana kuwapongeza viongozi wa Mkoa wa Lindi na Halmashauri zote za Wilaya ya Lindi, ambao baada ya kuona kwamba vijana wao wanafurika sana kuja Dar es Salaam, wameamua katika kila kijiji kuanzisha vijiji walivyoviita  Vijiji Mtoto kwamba, vijana kila mmoja anapangiwa eka kumi na misitu tunayo mingi, anaanza kulima kwa eka mbili, tatu, anapewa mbegu bure za mazao ya kudumu kama mikorosho ili baadaye akishafikia eka tatu anaona mambo yake yanakwenda vizuri kwa vyovyote vijana wale watahama wakae kwenye vijiji vyao vingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili nalo linasaidia kupunguza matatizo ya vijana kusafiri kutoka Mikoa yao na kukimbilia Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Miji mingine mikubwa. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, anauliza Serikali ina mpango gani kuongeza fedha za mikopo kwa vijana ili kusaidia vijana kujiajiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha zinazotolewa kwa ajili ya mikopo hazitoshi, ni kidogo na wakati mwingine inakuwa ni masihara kundi la watu watano wanapewa shilingi 100,000. Ni kama masihara ndiyo, kwa hiyo, sisi tunalifahamu na tunaendelea kuongeza ile idadi kila hali ya uchumi inaporuhusu. Mwaka huu wa fedha uliokwisha hali ilikuwa mbaya sana kama mnavyofahamu tulilazimika kuweka kipaumbele zaidi katika matatizo ya njaa ili kutunusuru na ndiyo maana mnaona hali ilishuka kidogo.

Halafu Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji, anataka Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni, tuangalie mwenendo wa vijana wetu katika nyanja za elimu, siasa na uchumi ili waweze kujijengea misingi imara ya maendeleo yao. Tunakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Wizara kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali inahakikisha na itaendelea kufanya hivyo ili vijana wetu wapate huduma na elimu bora. *(Makofi)*

Swahibu yangu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alipata matatizo sana juu ya kutaka kuweka dhana mpya ya Mwenge wa Uhuru. Anaona kama Mwenge wa Uhuru unatumika kukejeli Wapinzania na akashauri ufanyike utafiti kwa wananchi kuona hivi kweli bado wana haja na Mwenge huu.

Mimi nafikiri Mwenge huu unakubalika na ukipita Mikoani ukaona watu wanavyokusanyika kuusubiri Mwenge huu huwezi kuamini. Kwa sababu swahibu wangu atakuwepo hapa Ijumaa aende pale Jamhuri akaone umati wa watu wakiusubiri Mwenge huu, lakini siyo tu, Mwenge huu umekuwa ni chimbuko la shughuli za uchumi na maendeleo. Mwaka 1993 tu jumla ya shilingi 2,855,324,088/=, zilichangwa katika

kushughulikia miradi ya wananchi, ikiwemo elimu, afya na kadhalika. Lakini mpaka kufikia mwaka 2002, kiwango kimepanda mpaka kufikia shilingi 29,186,386,981/=. Kwa mwaka wa 2003 fedha za michango ya wananchi zimefikia shilingi 31,317,398,552/=. Kwa bahati nzuri fedha zinapochangwa zinabaki kwenye Wilaya ile ile haziendi kokote. *(Makofi)*

Lakini Mwenge ni dalili ya kujenga umoja wa namna fulani. Waheshimiwa Wabunge, tumegawa karatasi hii hapa humu ndani, *Olympic* wanautangaza Mwenge wa mbio za kukimbia tu na wanasema, *pass the flame, unite the world,* wakiamini kwamba Mwenge huu unaunganisha dunia. Lakini si *Olympic* tu hata *Commonwealth Games* nao wana Mwenge wao. Katika dunia Mwenge huu wa Uhuru ndiyo wa tatu ninaoufahamu mimi. Sasa badala ya kujivunia tunataka tuondoe, mimi nafikiri hebu tuangalie, *positively* nina uhakika tutakuja kuupenda, wasiwasi mwingine tuuondoe. *(Makofi)*

Kwanza kama ni kejeli hizi za utani wa kisiasa, swahibu yangu si lazima ziwe kwenye Mwenge, humu humu ndani tunaambizana, nje tunaambizana ni jambo la kawaida tu. Mimi nafahamu kwa sababu ndugu yangu ni muelewa sana, hili halitampa tabu. Kwa hiyo, hatuna haja ya kufanya sensa maana watu wanaupenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mwenyekiti wa Kamati ametoa ushauri juu ya Chuo cha Ilonga, kwamba hebu kinyanyuliwe kidogo. Hadi sasa kwa kushirikiana na *Tanzania Commission for Science and Technology* (Tume ya Sayansi na Teknolojia) hivi sasa tunaendelea na mpango wa kufungua Tovuti pale Ilonga katika kituo hiki, tunatarajia kwamba shughuli za mawasiliano kwa njia za kisasa zitaanza mwaka huu wa fedha wa 2004/2005. Tunafikiri hiyo ni hatua mojawapo ya kufufua na kukiendeleza chuo chetu cha Ilonga. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Emmanuel Kipole, ameshauri kwamba maendeleo ya vijana katika Taifa lolote ndiyo nguzo ya Taifa. Kwa hiyo, Wizara iongeze kasi ya kubuni mikakati ya kutafuta matatizo na kupata ufumbuzi wake yanayohusu vijana hasa kwenye UKIMWI, madawa ya kulevya na uhaba wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaamini kwamba Vijana ni moja ya nyenzo muhimu ya maendeleo ya Taifa lolote. Tayari Wizara imeanza kuandaa mkakati wa kutatua matatizo ya vijana ambapo vijana wenyewe watashirikishwa kikamilifu maana huwezi ukapata ufumbuzi wa kweli bila vijana wenyewe kushiriki, wao ndiyo wanaojua matatizo yao. Lakini vijana wanaishi katika mazingira tofauti, matatizo ya kijana wa Dar es Salaam, hayawezi kufanana na matatizo ya kijana wa Kibaha, wala hayafanani na matatizo ya kijana wa Mchinga. Kwa hiyo, siyo suala la kukaa mahali pamoja tu mkapanga utatuzi ukawa ni *uniform,* lazima uendane na maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Moja ya utekelezaji wa Wizara ni kuwasaidia vijana kuingia kwenye dunia ya utandawazi, ndiyo maana hivi sasa kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi ya Teknolojia, tumeamua kufunga mtandao kwa kuanzia na kituo hiki cha Ilonga na baadaye twende katika vituo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lile suala la vijana kuwawekea mahali maalum pa kufanya biashara zao, napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kuwapongeza sana *NSSF* ambao wameamua kutengeneza *Industrial Parks,* Dar es salaam ili kuwapatia vijana maeneo ya kufanyia biashara zao. Lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Venance Mwamoto, ambaye baada ya kupeleka maombi yake na makaratasi yake *NSSF* kama wanavyosema wenyewe sasa mazungumzo hayo yameshaanza kati ya *NSSF* na Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Venance Mwamoto, kwa ajili ya ujenzi wa soko kwa wafanyabiashara wadogo wadogo pale Ilula. *(Makofi)*

Suala ajira kwa vijana Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, amesema linakera, mtu anakwenda kuomba kazi anaambiwa uzoefu wako wa huko nyuma upi? Wakati huyu kijana ndiyo anatoka shule au anatoka chuoni basi anasema kujengwe chuo cha uzoefu wa kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira ya vijana linahitaji sera, lakini wakati sasa umefika kwa vijana wetu kujifunza kazi pamoja na elimu wanayoichukua kwa sababu sasa kwa elimu tu peke yake basi hata kama kompyuta hujui anaweza akachukuliwa mwenzako uliyemaliza naye mwaka mmoja, lakini amemzidi kwa kompyuta tu. Kwa hiyo, lazima sasa tubadilike na wakati wenyewe, ndiyo maana kupitia *VETA* na kupitia vyuo vya watu binafsi na taasisi, tumetilia mkazo suala la ujasiriamali ili vijana wanapotoka hapo wawe na uzoefu kuanzia chuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri, amezungumzia takwimu za vijiwe zisichukuliwe kama ndiyo chanzo pekee cha vijana wasio na ajira. Tulipita vijiweni kutokana na agizo la Bunge hili mwaka 2001/2002 wakati wa bajeti, kwamba kuna vijana wanakaa vijiweni tu badala ya kuwa-*harass,* hebu tukazungumze nao tuone matatizo yao ni nini, ndiyo maana tukafanya *survey* hii na tulianzia Dar es Salaam kwa sababu ndiyo kwenye vijiwe vingi. Lakini suala la takwimu la vijana kwa kila Wilaya, Mkoa, bado linaendelea pale pale, ila hili la vijiwe ilikuwa ni shughuli maalum tu kufuatia maagizo tuliyopewa wakati wa bajeti humu Bungeni mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya vijana kutokupata asilimia 10 inayotengwa na Halmashauri ya Mji, mimi nafikiri lazima tukubaliane linakera hili tunaposema jamani na sisi Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani, lakini ndiyo ukweli wenyewe. Kama tatizo labda ni mapato ndani ya Halmashauri, husika basi tulione hilo tatizo litafutiwe ufumbuzi. Lakini tukija tukisema huku wakati mwingine mimi nahisi kama tunawashitaki Madiwani wenzetu vile kwamba hawalipi, hebu tulimalize kule kwanza tukishindwa ni vema hata kumfuata Waziri wa TAMISEMI, tushirikiane kwa pamoja kuliko kuja kuliibua hapa. Wakati mwingine tunaweza tukawa tunajenga hisia mbaya kwa wenzetu na uchaguzi ndiyo unakaribia mwakani tutaumizana. Kweli unaweza kurudi unakuta Mwenyekiti wako wa Halmashauri kavimba mashavu ndiyo nini? Sasa ni vema tukaangaliana vizuri katika kutatua hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Halmashauri ambazo kwa kweli zimeamua kufungua akaunti kabisa na tungeziunga mkono hizo. Mimi napenda sana kutumia nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Tumewapa fedha wamerudisha asilimia

100 na kama Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ananisikia hivi sasa tunamuomba akamuone Mkurugenzi wa Vijana, hata kesho tunawapa mara mbili ya kiasi kile walichorudisha, pengine itawavutia na Halmashauri nyingine kuwasimamia vijana ili waweze kurudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshiwa Alhaj Shaweji Abdallah, amechangia kwenye michezo na ameleta mapendekezo yake na maoni mengi juu ya mfumo wa uendeshaji wa ligi, maoni yake kuhusu Katiba, mapendekezo ya mfumo ya uwakilishi katika mikutano mikuu ya *FAT,* mapendekezo na ushauri tumepokea na tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutayafanyia kazi na tayari tulikuwa na Mwenyekiti wa *BMT,* Mheshimiwa Joel Bendera, tumemkabidhi aanzie kazi yeye mwenyewe akipenda aanze hapa hapa au baada ya kurudi Dar  es Saalam.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, naye amezungumza kweli kweli kuhusu michezo. Amesema michezo ni duni katika fani zote na yeye anahisi kwamba hii ni kutokana na udhaifu wa viongozi na mwelekeo duni wa Serikali. *BMT* itasaidia vipi *FAT* katika kuleta mabadiliko ya muundo wa *FAT* na Wizara kupitia *BMT* iweke basi mkakati wa kuwa na bajeti na kusimamia mapato.

Sisi tumeamua kuzungumzia matatizo ya *FAT* kwa kutafuta chanzo badala ya kushughulika na matokeo. Tumeona huko nyuma tumeshughulika na matokeo yakatuchelewesha sana. Sasa tukaamua kwenda kwenye chanzo, chanzo tumegundua ni Katiba siyo ya *FAT* tu na Vyama vya Mikoa na Wilaya, kwa sababu hivi ndiyo vinavyozaa viongozi wa *FAT* Taifa. Tumeona kuna mabadiliko, wananchi wameanza kuelewa sasa, chaguzi za Mikoa zinazoendelea unakuta kuna mabadiliko hapa na pale, naamini ikichanganywa na tatizo la msingi la katiba yenyewe ya *FAT* tutafikia mahali tuwe na viongozi watakaofikiria soka zaidi, kuliko matatizo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *BMT* ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi na Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Venance Mwamoto, kwamba basi ifikiriwe kupewe meno ipewe na fedha. *BMT* kwa sheria ambayo tuliipitisha sisi hapa ya michezo ya kubahatisha mimi naamini mara itakapoanza kufanya kazi zake, *BMT* itakuwa na uwezo wa kifedha kusaidia kufufua michezo na kwa uongozi tulionao sasa ndani ya *BMT* nina uhakika tutasonga mbele vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya sheria imeanza kubadilisha na ikikamilika naamini Waheshimiwa Wabunge, mtatuunga mkono hapa Bungeni ili *BMT* iweze kupata meno.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, ameuliza juu ya viwanja. Mpaka hivi ninavyosema Mameneja na wamiliki wa viwanja vyote vinavyotumiwa wakati wa ligi wameshapata mafunzo kutoka Wizara hii, kwa mwaka huu wa fedha ambao umemalizikia juzi, Juni 30 na tunaendelea hivyo kila mwaka. Lakini tatizo la viwanja kuwa vibovu siyo kwa sababu vinamilikiwa na CCM, tatizo ni kwamba viwanja vingi haviingizi mapato ya kutosha kuweza kuviendeleza. Hapa Jumamosi tu ukichezwa mpira ninyi nendani pale, watu wanaokuwa Mnadani  wengi zaidi kuliko wanaobakia pale

uwanjani. Utapata wapi fedha ya kuendeleza viwanja? Lakini kuongoza mchezo jamani kunahitaji vile vile na dhamira, ukiuacha ubinafsi pembeni.

Mimi Wilaya kama ya Mpwapwa, Wilaya ambayo timu yake ya Mji Mpwapwa kwa mwaka wa sita mfululizo iko katika *Vodacom League* na haijashuka. Lakini kuna baadhi ya mikoa hata Makao Makuu ya Mkoa hakuna ile timu na ukiona viongozi wake ni *DED,* Mheshimiwa Mbunge George Lubeleje anaongoza pale, wanakuja kila mechi hapo hata Wabunge wakisikia mnacheza na timu *Veteran* ya Mjini unakuta wako pale. Sasa viongozi wa namna hii ndiyo wanaweza kutuvusha kisoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si pesa peke yake, mimi nitashangaa sana kama atatokea mtu wa kubeza juhudi za Mheshimiwa George Lubeleje, katika michezo. Lakini si ajabu kwa sababu wapo watu wanaoezua bati wakaezeka makuti. *(Makofi/Kicheko)*

Hata mchango wa Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud na yeye ni mfano mzuri, tumechukua ushauri wako wote lakini yeye ni mfano. Jang'ombe kule Wazanzibar wanaita Ng'ambo, lakini timu ya Taifa inayotoka kule ndiyo mkombozi wa Ng'ambo, lakini siyo timu ya Taifa na wachezaji wazuri wa timu nyingi za Zanzibar wanatoka Ng'ambo, kama alivyo mwenyewe amewahi kuwa mpaka *captain* wa timu ya Taifa ya nchi hii. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, tunashukuru pongezi zako na mimi nilikuwa nakwambia kwamba ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya shilingi 500,000 ingefika kwenye jimbo lako na mimi nashukuru kwamba umetambua kwenye mchango wako kwamba umeshapokea, naamini zitatumika kama zilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Eeeh! Muda umekwisha! Halafu Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, tumepokea maoni yako, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali tena, kwenye michezo jamani wote waliochangia Mheshimiwa Freeman Mbowe, tumepokea yote na Mheshimiwa Sophia Simba. Mheshimiwa Philip Magani, tumepokea vizuri, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Dada Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Diana Chilolo, tumepokea hatuwezi kujibu yote lakini tutawahakikishieni tunawafikishieni kwa njia ya maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mwanne Mchemba, ameuliza juu ya sheria ya mirathi, tumepokea maoni yako na Mkurugenzi anayehusika atalishughulikia. Ningeomba wale wote akina dada Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa George Lubeleje tena, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Omar Kwaangw', yote mliyochangia kwenye ustawi wa jamii, majibu tunayo tutawaandikieni vizuri, tutawafikishieni. Kama mlivyoona kengele imeshanililia, ikilia na nyingine itakuwa balaa kubwa hapa. Ndiyo maana nimeamua niwataje majina kabisa. Kwa hiyo, ni

pamoja na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Venance Mwamoto katika eneo hilo, Mheshimiwa Stephen Kahumbi na Profesa Daimon Mwaga. *(Makofi/Kicheko)*

Nataka niwathibitishieni kwamba mchango huu kwetu ni nyenzo za kufanyia kazi. Waliosikiliza kipindi cha michezo jana redio moja ilikuwa inanihoji vipi kesho kutakuwaje, nikawaambia hapana kitu Waheshimiwa Wabunge, watakuwa wawazi katika kutusaidia michango yao na leo wameshuhudia na bila shaka leo watatoa tena kwamba kweli Wabunge walikuwa wazi katika kuchangia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kufafanua kwamba, jana jioni wakati Ofisi ya Makamu wa Rais, Waziri wake mtoa hoja alipomaliza kujibu mimi niliwahoji, wengine walistuka kidogo na mimi nikasema ndiyo nitamwita Katibu.

Sasa naomba kusahihisha kosa nililofanya jana kwamba zamani kabla hatujabadilisha Kanuni, Waziri alikuwa anapowasilisha Makadirio yake alikuwa anasema naomba kutoa hoja kwamba Bunge likae kama Kamati ya Matumizi. Lakini sasa mkiangalia vitabu vya Mawaziri wote wanapoanza wanasema sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, sasa likubali kujadili na kupitisha Mapitio ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara kama hii ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, hasa tunaelezwa kwamba hotuba zao tunakuwa tumepata kabla. Kwa hiyo, sipaswi kumhoji Waziri, baada ya kutoa majibu yake kabla, tunakwenda moja kwa moja kwenye Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, naomba marekebisho haya myazingatie tafadhali. Mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kujibu au kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao madhubuti ambayo inazidi kutuimarisha katika utendaji wetu kazi katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwanza nipongeze sana Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii ambayo leo waliwasilishwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud ambaye ni Makamu Mwenyekiti kwa michango ambayo ilikuwa imeenea katika maeneo yote ya utendaji kazi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini pili, ningeomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake ambayo ilikuwa ya kina inayoonyesha kukomaa kwa sababu kwa kweli aliyoyachangia leo ni mambo ambayo tunapaswa kuyafanyia kazi, ukiacha lile la Mwenge ambalo alidhani lina ushabiki wa kisiasa kutokana na vyama ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri, amelifafanua, lakini mengine yote sisi tutayafanyia kazi na ni mazuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani utakubaliana nami kwamba michango ilikuwa ni mingi sana na ya kina na kwa kweli kwa muda uliopo tunachoweza kwa sisi wawili kama alivyoanza Mheshimiwa Naibu Waziri hapa, ni kufafanua maeneo machache tu yale yote ambayo waliyotushauri Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwahakikishieni kwamba tutayafanyia kazi na kama alivyoahidi mwenzangu kwamba baada ya hapo kwa wale ambao watakuwa wamechangia itabidi kwa kweli tuchukue dhima ya kuwaandikia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza katika Wizara yangu.

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Jina Khatib Haji , Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge wa Mchinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo vile vile Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Hamis Nguli, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte na Mheshimiwa Philip Magani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kujibu na kufafanua baadhi ya maeneo ambayo muda utaniruhusu na nitajitahidi kwenda eneo kwa eneo. Naanza na eneo la utawala. Kilichojitokeza Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi katika idara na vitengo vya Wizara ambayo inakuwa ni kero kwa muda mrefu. Wizara ina mpango gani wa kupata watalaam wanaotakiwa na vitengo vyote. Hii hasa imechangiwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua tatizo la upungufu wa watumishi, watalaam katika idara zake na inalifanyia kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Matokeo ya hatua zilizochukuliwa za kuongeza watalaam hao zimefanikiwa kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara iliweza kuajiri Maafisa Kazi 20, Maafisa Michezo wawili na maafisa vijana watatu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara imeidhinishiwa nafasi za watalaam kama ifuatavyo, Maafisa Kazi 27, Maafisa Ustawi wa Jamii 21, walimu katika vyuo vya walemavu, 20, Maafisa Michezo wawili, walimu wa michezo watatu, wachumi watano, wa takwimu watatu, wataalam wa kompyuta wanne. Vile vile katika kuimarisha wakala wa usalama sehemu za kazi *OSHA,* Wizara imeidhinishiwa nafasi zifuatazo, wakaguzi wa viwanda wanne, madaktari wawili, maafisa afya wawili, wahandisi 5, Mwanasheria mmoja. Kwa vile Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeruhusu Wizara kuunda kama za ajira, zoezi la kuajiri kwa mujibu wa nafasi tulizoidhinishiwa litachukua muda mfupi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Kwa hiyo, mapengo haya mengi sasa tutayaziba. Hata hivyo Wizara itaendelea kuomba nyongeza ya watumishi hadi itakapokidhi mahitaji halisi ya watumishi katika idara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Kazi, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Waziri wa Kivuli Kambi ya Upinzani amesema kulazimisha kufanya kazi kwa saa ya ziada. Hili nataka nimhakikishie kwamba tunalitambua, lakini hata sheria za zamani, zinalikataza jambo hili katika *Employment Ordinance* na ... *terms of employment* ambazo ziko katika *Cap. 300* na *Cap. 366.* Wanaopatikana wanachukuliwa hatua za kisheria kwa kuadhibiwa. Wizara inayo taarifa baadhi ya waajiri kutolipa masaa ya ziada. Malalamiko yaliyopokelewa Serikali imeyafanyia kazi na waliopatikana wameadhibiwa. Lakini vile vile kuna haja ya kuimarisha sana kaguzi ili ziendelee kufanyiwa kubaini matatizo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaguzi katika ulipaji wa mishahara kati ya wafanyakazi Watanzania na wageni, hili tunalifahamu lakini vile vile sheria zetu ambazo zinatokana na kuridhia mikataba mbalimbali imeimarishwa sana kujaribu kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji ni ushirikiano kati ya Vyama vya Wafanyakazi na Serikali kujaribu kupambanua haya ili kuweza kuyafanyia kazi. Ni lazima tutambue kwamba baadhi ya Waajiri hawa wanatoka nje na baadhi yao ndio wenye mali. Kwa hiyo, hizo tofauti zitakuwepo, lakini sio tofauti ambazo misingi yake ni ubaguzi wa rangi. Vile vile Mikataba hii inatiliwa mkazo chini ya sheria mpya kwamba kufanya ubaguzi wa aina yoyote ni haramu na ni kosa la jinai na wametakiwa kila Kampuni au kila Shirika lilete Mkataba kwa Kamishna wa Kazi utakavyoonyesha jinsi ambavyo yeye mwenyewe amejiandaa kupambana na ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ajira ya mtoto ni matokeo ya umaskini na jitihada za dhati zinahitajika. Ni hoja ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa Asha Ngede na nadhani Mheshimiwa William Shellukindo, naye aligusia hili. Serikali inaelewa uhusiano uliopo kati ya ajira ya mtoto na umasikini, ndio maana katika mkakati wa Taifa wa kupambana na ajira mbaya ya mtoto, watoto wanaoondolewa katika ajira mbaya wanapewa shughuli mbadala yakiwemo mafunzo ya ufundi stadi na baadhi ya watoto hao nao wanawezeshwa kufanya shughuli za maendeleo. Tunaangalia tunachoweza kukifanya na kwa kusaidiana na wadau na Mashirika mbalimbali hasa Shirika la Kazi la Dunia *(ILO),* tunajaribu kuwapa wazazi hawa mitaji midogo midogo ambayo inaweza ikawasaidia kuona kwamba sio lazima mtoto wake afanye kazi hizi ambazo ni mbaya ili aweze kuishi.

Mheshimiwa William Shellukindo, anasema kuna haja ya kutofautisha kati ya ajira ya mtoto inayokatazwa na kazi nyingine. Anasema kuna watoto wanachuma chai kule Lushoto. Sasa anasema hawa ukiwakaripia maana yake si umewaambia waende wakafe njaa? Hasa hasa huwa wanachuma siku za Jumapili na alipoulizwa nani mwajiri wako? Akasema baba yangu. Baba yako kakuajiri? Anasema, ndiyo. Anakupa mshahara? Anasema ananipa *uniform,* viatu vya shule na madaftari.

Tunaomba Mheshimiwa William Shellukindo, atofautishe kati ya utumikishwaji wa watoto na kitu kinachoitwa *child work* ambayo inahusiana na makuzi, hii haikatazwi. *Child work* au kazi ya mtoto ya makuzi haikatazwi, kwa sababu inachukuliwa kama ni mafunzo ili mtoto wakati anapokua awe anajua namna ya kuanza kujitegemea tangu akiwa nyumbani kwao. Vinginevyo hata wale watoto ambao wanaanza kulima na wazazi wao itabidi tupeleke Polisi wawakamate hao wazazi wawatie ndani kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo, hata *ILO* inajua hili, tumejaribu kuwaeleza na wamelikubali kwamba kweli kwa child work hapana. Lakini kwa *child labour* ambayo ni utumikishwaji wa watoto, hiyo inakatazwa.

Vile vile, Mheshimiwa Ludovick Mwanzila, alizungumzia kuhusu kuchelewesha malipo ya madai ya fidia. Ulipwaji wa madai ya fidia inategemea vile vile upatikanaji wa fedha na kama mnavyofahamu sasa hivi tunaishi kwa utaratibu wa *cash budget.* Ni mpaka Hazina ikusanye, ikishagawa mgao wake na sisi tupate na wanagawa kwa awamu halafu baadaye ndio tunaweza kutekeleza matatizo haya. Kwa hiyo, sio kwa sababu ya uzembe wa Wizara, hapana.

Kuhusu viwango vya fidia kuwa chini, napenda kumjibu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwamba tunafahamu viwango vya fidia bado ni chini, lakini akumbuke kwamba wakati kilipobuniwa miaka ya 1960 kilikuwa ni kiasi kikubwa sana shilingi 108,000/= kwa wakati ule ungeweza kujenga jumba kama hili au hata zaidi ya hili. Kwa sasa hivi iko haja ya ku-*review.* Lakini haya ni mambo ambayo yatashughulikiwa katika awamu ya pili ya urekebishaji wa sheria za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya milipuko kazini inatokana na Wizara kupuuza umuhimu wa kitengo cha ushirikishwaji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwamba hali anayoielewa sio hivyo. Hivi sasa tunavyoona sisi

mambo haya ya ushirikishwaji ndiyo yamesisitizwa zaidi, kwa sababu zamani ilikuwa ni kwenye Serikali tu wakati hivi sasa iko kwenye *social dialogue* na sheria mpya inatambua kama hii ni mbinu muhimu katika kuzuia migogoro ya kazi yaani hii *social dialogue* inakuwa ni kitu maalum ambacho mwajiri na mfanyakazi wanakaa wanajadiliana, wakishindana Serikali inaingia katika utatu wetu ule, kitu ambacho kimezingatiwa kabisa na sheria iliyopo sasa, sio hiari tena. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ushirikishwaji sasa hivi umeimarika zaidi kuliko ilivyokuwa hapo zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa wafanyakazi katika Idara ya Kazi hoja iliyoungwa mkono na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, nadhani hili nimeshalieleza kwamba juhudi zinafanywa katika Wizara yetu kwa kujaribu kupunguza mapengo ya wafanyakazi ili kuweka ikama inayotosheleza.

Eneo la tatu ni Ajira. Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, amesema Watanzania wengi wanategemea sekta isiyo rasmi. Matatizo yanayowakabili ni ukosefu wa mitaji, elimu duni ya ujasiriamali, miundombinu hafifu, ufinyu wa soko la ndani na kadhalika. Masharti magumu na riba kubwa ni kikwazo kwa wananchi kupata mikopo. Nakubaliana na hoja alizotoa Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, kwamba haya ni matatizo ambayo Serikali inayafahamu kwa muda mrefu na ndio maana imekuwa inatumia mbinu mbalimbali za kutatua tatizo hilo. Baada ya hatua hii ni kama vile kuruhusu uanzishwaji wa Taasisi zisizokuwa za Kiserikali kukopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu baadhi ya Taasisi hizi riba zake ni kubwa na bahati nzuri baadhi ya Wakurugenzi wa Taasisi hizo ni Waheshimiwa Wabunge wenzetu. Kwa hiyo, tutaendelea kuwashauri Waheshimiwa Wabunge hawa wakumbuke kwamba wanaowakopesha ni maskini sana, wajaribu kupunguza riba kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwahusisha washiriki na sekta isiyo rasmi katika maonyesho ya nguvukazi. Hivi juzi juzi mwezi Novemba, 2003, tulikuwa na maonyesho ya nguvukazi ya Afrika Mashariki. Kwa bahati mbaya watu wetu, Watanzania wengi ni waoga kwenda kujumuika na wenzao. Kwa hiyo, unaweza ukakuta hata maonyesho yalipokuwa yanafanyika Tanzania, *majority* walikuwa wanatoka Kenya na Uganda na wakati maonyesho yamefanyika hapa Tanzania. Lakini tutaendelea kujenga moyo wa kujitokeza kwa sababu unapokwenda kule unafanya mambo mawili. Kwanza unaangalia vitu vya wenzako, unaangalia vitu vyako vilivyo hafifu au vilivyo bora zaidi, napo unaweza ukajirekebisha. Lakini pili, unapanua masoko. Kwa mfano, wale wote waliopata bahati ya kuja pale, vitu vyao karibu vyote vilinunuliwa. Dagaa wa Kigoma wali-*shine* sana, asali kutoka Tabora ndio usiseme, kuna mboga inaitwa Nsansa, Wakenya walikuwa hawajapata kuiona. Basi walinunua karibuni vyote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kwa kweli hali ya soko inaendelea kutafutiwa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha ukosefu wa ajira kinaongezeka mwaka hadi mwaka. Sera ya Ajira ya mwaka 1967 inajaribu kupambanua namna ya kupambana na tatizo hili na tunafahamu kwamba tangu mwaka 1997 mpaka sasa sera hii, kidogo imepitwa na wakati, tunairejea ili kuweza kuboresha hali zaidi. Lakini vile vile ndio maana unakuta Serikali inajaribu kuandaa mazingira ya kuvutia wawekezaji, ndio maana tunasema kila siku Waheshimiwa Wabunge ni vyema tukaenda pamoja kuliko kusema tu kwamba wawekezaji, Makaburu, sasa hao tunapowatia hofu wawekezaji kutoka nje ili waweze kuja kuzalisha ajira zaidi ndani ya nchi, tutakuwa tunalea umasikini, tunapunguza ajira kwetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, hili nalo naomba kulisisitiza.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, alisema Serikali ichukue hatua kuhusu suala la vijana wanaohitaji ajira kutokuwa na uzoefu miaka kadhaa. Hili nadhani Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, amelijibu, lakini nitaliongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba ni kweli suala la kujenga Vyuo vya Uzoefu hilo haliwezekani kwa sababu utajenga Chuo gani ambacho kitajenga watu watakaokuwa na uzoefu kwa kazi ambazo zinategemea kutangazwa bila hata kujua? Lakini tumeanza kuzungumza na baadhi ya Kampuni hizi hasa hizi za kigeni na tumeanza kupata mafanikio katika maeneo fulani. Kwa mfano *Mining Companies,* yale Mashirika ya Madini, kwa mfano kuna ile Kampuni ya Ma-*bulldozer,* wameanza kuchukua vijana wabichi kutoka Chuo Kikuu halafu wanawafundisha wenyewe na kuwajenga. Msingi ambao Vyuo vyetu vinatoa umeonekana kwamba kumbe unafaa kama kianzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *East African Gold Mine* hata wanafunzi wanaotoka *VETA* wameonekana kwamba ni kianzio kizuri. Baada ya hapo wanawapa *specialize training.* Lakini ndani ya Serikali hatuna ubaguzi huo wa kusema kwamba mpaka uwe na *experience* ya miaka mitano, *unless really you are dealing with very specific jobs.* Halafu ndani ya *Parastatals* vile vile tunajitahidi sana kuchukua watu bila kujali kwamba wana uzoefu wa miaka mitano. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kuhamasisha vijana wetu.

Lakini vile vile, ni vyema hawa wanafunzi ambao bado wako Vyuoni watembelee basi Chuo chetu cha Ajira, hapo ndipo utakwenda kujua kwamba ni mapungufu gani ambayo unayapata ili uanze kujiandaa vizuri zaidi na kwa kuunganisha na Mfuko wetu wa *HIPC* ambao unajaribu kuwachukua vijana ambao tayari wanatafuta kazi, unajaribu kuwasaidia kwa kuziba mapengo ya upungufu wa stadi walizonazo, itasaidia sana. Lakini vile vile na Vyuo vyetu navyo vijaribu kutembelea Kituo chetu cha Ajira ili viweze kujua ni stadi gani zinazohitajika katika Soko la Ajira kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Remidius Kissassi, aliongelea kuhusu Kituo cha Ajira kwamba kiongeze bidii katika kujitangaza. Hilo tunalipokea na tunalikubali kwa sababu kwa kweli kujitangaza huku kuchache ambako tumepata kukuona tayari matokeo yameanza kupatikana. Idadi ya watu ambao wanatembelea Kituo hicho imeongezeka sana na idadi ya waajiri wanaotambelea Kituo hicho imeongezeka sana na idadi ya maunganisho kati ya wanaotafuta ajira na wanaotafuta wafanyakazi imeongezeka sana na wanaopata ajira

kidogo kwa mwaka huu alhamdulillah. Kwa hiyo, tunasema tutaendelea kukitangaza sana.

Mheshimiwa Peter Kabisa, alizungumzia kwamba Mkoa wa Dar es Salaam kati ya nafasi 12,000 ni asilimia 33 waliopata nafasi, asilimia 62 walikosa kwa sababu ya kutokuwa na ujuzi. Hili nimelizungumza jinsi ambavyo tunaweza tukaziba mapengo ya ujuzi na kwa kweli tukisaidiana, nadhani tunaweza tukafanikiwa. Lakini key institution ni Kituo chetu cha Ajira, hicho ndicho ambacho kitatusaidia kubaini mapengo ya ujuzi na stadi za kazi.

Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, alisema vijana waliohitimu baada ya kusomeshwa na Serikali hawajaajiriwa na Serikali. Ni kweli kwa sababu Serikali sio mwajiri mkuu, tena na hili Waheshimiwa Wabunge ni vyema mkalifahamu. Sasa hivi Serikali inarudi katika majukumu yake ambayo ni yale ya ki-*traditional* yaani amani, utulivu, *law and order,* suala la ajira ndio maana tunazungumzia habari za kuvutia wawekezaji.

Vile vile tusiwe na tafsiri fupi ya ajira, ndio maana tunasisitiza sana sekta binafsi, sekta isiyo rasmi kwa kusaidiana na Vyuo vyetu ambavyo vinawaandaa vijana hawa, itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kituo cha Ajira huendesha warsha kwa watafuta kazi kuhusu mbinu za kutafuta ajira na namna ya kufanya vizuri katika usaili wa kazi kwa sababu vijana wetu wengine hata namna ya kuingia katika usaili hawajui; Lugha na desturi katika usaili hawajui na kwa bahati mbaya Makampuni mengi haya yanaendesha usaili wao kwa Kiingereza.

Kwa hiyo, hata kile Kiingereza chenyewe kina namna yake ambavyo unaweza ukajipanga vizuri kumfanya huyu mwajiri avutiwe na wewe. Sio unafika tu unasema, *Good morning!* Mimi ndio mwenye kazi, kwa hiyo, vile unavyonisalimia tu najua huyu hana adabu. Wenzetu wamezoea, akifika pale anasema, *Good morning Sir,* anajua naam, tunaanza na *gentleman* hapa. Sasa haya yote tunajaribu kuwaimarisha vijana wetu.

Nashauri Vyuo vya Mafunzo vitoe mafunzo kulingana na mahitaji ya soko la Ajira. Vile vile nawashauri wazazi wawatie moyo watoto wao kufikiria aina za ajira wanazopenda ili waweke mkazo sahihi katika fani zitakazowawezesha kupata ajira hizo.

Kwa mfano, sasa hivi nchi hii tuna nafasi nyingi sana za Walimu, lakini bado mwamko wa Jamii katika kazi ya Walimu haijakaa sawasawa. Watu wengi bado wanakwenda katika kazi ile kama *the last resort* na utakuta vijana hata wanataniana wanasema eeh, wewe umekosa kweli, hata Ualimu! Sasa mwamko namna hii hausaidii.

Mimi nakumbuka tulipokuwa Darasa la Nane, kuna kitabu tulichosoma *chapter* ya mwisho ilikuwa inasema, Mwandishi anawashauri wanafunzi wanaomaliza Darasa la Nane, wakati huo Darasa la Nane ilikuwa ni elimu kubwa sana, anasema: "Mwanangu umemaliza Shule, sasa unapokwenda huko usichague kazi. Unawaona waliofanikiwa,

hawakuanza na kazi waliyoipenda, walianza na kile ambacho mikono yao ilijikuta inafanya." Kwa hiyo, nenda kwanza kwenye kazi ambazo zinapatikana. Sasa hivi kazi zinazopatikana kwa wingi ni ualimu, tunahitaji Walimu kwa maelfu. *(Makofi)*

Eneo lingine ni *OSHA* au Kitengo kile cha Afya na Usalama Kazini. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, anasema hivi Serikali haioni umuhimu wa kitengo hiki? Mbona haitengi fedha za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwanza ni kwa sababu ya umuhimu wake ndio maana tukakifanya Wakala ili kiweze kuwa *autonomous* kiweze kujitafutia njia za kuweza kupata fedha za kuweza kukiendesha. Lakini la pili, bado Serikali kama jinsi ilivyokuwa kwa kurugenzi nyingine, inatoa mishahara ya wafanyakazi wote wa Taasisi hiyo. Kwa mfano, kwa mwaka huu tumetoa shilingi 108,915,900/= kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi.

Kwa hiyo, mishahara ni *guaranteed,* nyenzo nyingine kama ada yao wakiitumia vizuri itakuwa ni vizuri zaidi. Kwa mfano mwaka jana walikusanya shilingi milioni 126, mwaka huu wameongeza wamekusanya shilingi 306,609,000/=. Kwa hiyo, unaweza kuona kasi inavyopanda.

Mheshimiwa William Shellukindo, alisema kuhusu wafanyakazi kutokutumia vifaa vya kujikinga walivyopewa na Waajiri. Anasema yeye alishauri wafukuzwe kazi hawa, kwa nini hawatumii vifaa? Kwa sababu baadaye wakipata ajali itakuwa mzigo kwako. Ni kweli wakati mwingine tuna utamaduni wa aina hiyo, unaweza ukakuta hata *Petrol Station* tu unakuta kuna mahali pameandikwa *No Smoking,* lakini unamkuta mfanyakazi ameshika sigara ndefu, inatoa moshi mkubwa pale na *spark* zinaweza zikatokea saa yoyote. Unamwambia bwana, huoni kuna Petroli hapa? Anakwamba ah, Petroli ya siku hizi mzee haiwaki! Hivi kweli Petroli ya siku hizi haiwaki? Majengo mangapi yameteketea?

Lakini vile vile sio vizuri tu kupitisha *summary decision* kwamba unawafukuza kazi kwa sababu hawakuvaa, pengine kuna sababu. Kwa mfano, kutokufahamu umuhimu wa vifaa hivyo, pengine hawajapewa hata mafunzo ya namna ya kutumia vifaa hivyo. Kwa mfano, vifaa kuwa duni. Kuna vifaa kwa mfano *mask* za kuvaa mdomoni, watu wengine wakivaa inakuwa ni afadhali hata kutokuvaa maana zinateremka teremka. Sasa zikiteremka inabidi asogeze sogeze na wakati mwingine vidole vinagusa midomo, ulimi ukitoka, tayari unachukua ile sumu ambayo ilikuwa imedhamiriwa kukingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upungufu na uchache wa wakaguzi ili kufuatilia utekelezaji wa sheria hii. Kwa kweli tutaendelea kupata wafanyakazi wengi ili kuhakikisha kwamba kaguzi zinafanyika mara kwa mara.

Vile vile kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye aliuliza kama mfanyakazi hakutumia vifaa wakati vipo, anaweza kuadhibiwa? Hili mimi nakubaliana kabisa. Kama anajua na hakutumia, basi anastahili kuadhibiwa. Kwa sababu kutokutimiza matakwa ya Sheria, Mfanyakazi anaweza kupelekwa Mahakamani chini ya Kifungu cha

sheria Na.93 cha Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi ya mwaka 2003. Hiyo *provision* ipo ya kuweza kumpeleka Mahakamani. Unajua kama sheria ipo, ndiyo maana utakuta sisi tunaotoka maeneo ya treni, ukigongwa na treni kwenye reli ile, wewe uliyegongwa hata kama umekufa ndio unayeshitakiwa kwamba wewe ndio umeigonga treni. Sasa na mfanyakazi huyu akiathirika kwa sababu ya uzembe wake, naye pia anastahili kushitakiwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge wengi wamechangia na Kamati imeona bado kuna upungufu wa Watumishi Mahakama ya Kazi. Hoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge wanne wote yanahusu uhaba wa Watumishi na ukosefu wa nyenzo za kutosha katika Mahakama ya Kazi. Ni kweli bado upungufu wa Watumishi na nyenzo za kufanyia kazi katika Mahakama ya Kazi ambayo inasababisha migogoro huchukua muda mrefu. Juhudi bado zinaendelea kwa kushirikiana na Mamlaka husika ili kujaza nafasi zote katika ngazi zote zilizo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nasoma hotuba hapa, nilieleza jinsi ambavyo Mahakama yenyewe imejitahidi kusogeza huduma katika Mikoa mbalimbali kwa kuongeza Vikao. Wafanyakazi wengi wameajiriwa hata Kanda ya Arusha imepata sasa Makamu Mwenyekiti Msaidizi. Mwanza tumeshapata hata Ofisi. Kwa hiyo, juhudi zilizo madhubuti zinachukuliwa. Lakini vile vile kwa sababu tunafahamu kuna tatizo la kesi kuchukua muda mrefu, *DANIDA* wamejitokeza kushirikiana na Mahakama ya Kazi kuweka mradi maalum wa kushughulikia kesi hizi ziishe haraka. Kwa mfano, tangu wameanza wana wiki mbili tu na ndani ya wiki mbili hizo tayari wameshamaliza kesi 30 na bado mradi unaendelea. Kwa hiyo, tunao utaratibu ambao sasa kidogo utapunguza *congestion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyumba za Kinyerezi ni ghali kwa mtu wa kipato kidogo. Nyumba hizo ziko katika mafungu matatu. Fungu la kwanza vyumba viwili shilingi 9,800,000/=, Vyumba vitatu shilingi 12,800,000/=, vyumba vinne shilingi 13,300,000/=. Nyumba hizi zimejengwa kwa matofali, zina choo, bafu, maji na umeme. Kwa hiyo, ni nyumba ya kisasa kweli kweli.

Waheshimiwa Wabunge, tatizo tulilonalo, kama jamii inadhani ni kutaka kupata nyumba kwa mkopo ambao unamaliza haraka, sasa haiwezekani. Sisi ni waoga kukopa na utakuta Watanzania wengi wanataka wajenge nyumba kwa fedha yao mfukoni, kitu ambacho hakiwezekani. Ndio maana tukasema, kwa hawa ambao tunadhani tunaweza tukawasaidia, tujenge nyumba hizi za kisasa. Mtoto anayetoka katika nyumba hii hajisikii mnyonge kama mtoto mwingine anayetoka katika nyumba nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, lazima zitakuwa na gharama zake. Tunafahamu ni walala hoi, hawana uwezo wa kutosha ndio maana tukaweka kipindi kirefu cha kulipa miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* wana mpango gani wa kuendeleza kiwanja chao cha Lindi? Shirika linawekeza katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia *financial viability, economic viability.* Ni kweli Shirika linamiliki kiwanja Mjini Lindi, malengo ya Shirika ni kujenga nyumba za kuishi au hoteli. Hata hivyo tathmini ya awali

inaonyesha miradi hiyo miwili sio *viable* kwa sasa. Hivyo mipango ya kuendeleza kiwanja hicho itafanyika mara mradi utakaobuniwa utakidhi haja ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Shirika la *NSSF* tukiligeuza kwamba na lenyewe ni Shirika la huduma itatuletea matatizo, ndiyo maana sasa hivi ni lazima lijiendeshe kiuchumi na Lindi nadhani baada ya kupata barabara ya lami huenda hali itakuwa nzuri zaidi. Kwa hiyo, watafanya tathmini upya na itakapoonekana kwamba inalipa, basi watajenga na kukamilisha mradi huu. *(Makofi)*

Suala la *VETA* na *NSSF* kushirikiana, tutaangalia jinsi ambavyo inakwenda lakini lazima vile vile tuzingatie tatizo la ile *Procurement Act* kwa sababu inahitaji *tender* zitangazwe, watu waombe ndio uwazi na ukweli ambao tunauzingatia. Sasa kama *VETA* tutaweza kuwasaidia wajiandikishe kama Kampuni ya Makandarasi, wakitenda *competitively* watapata. Sisi kama Serikali tutafurahi kwamba *VETA* ijenge.

Mheshimiwa Sophia Simba alitoa pongezi kwa *NSSF,* hizo tunapokea. Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, pongezi tunapokea, Mheshimiwa Ally Karavina, kujenga Chuo cha *VETA* Urambo Mjini, sasa hivi juhudi zetu tunazielekeza katika kujenga Chuo katika kila Mkoa. Tukimaliza tutajitahidi kwenda katika maeneo ya Wilaya. Lakini kwa Mheshimiwa Ally Karavina, anacho Chuo pale Uliyankhulu ambacho hivi sasa tutakipelekea fedha nyingi kukijenga upya ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi mimi na yeye kama Wabunge wa eneo lile kuhamasisha vijana wetu wakajae pale, ukienda kile Chuo kimejaa wageni, basi. Lakini tunajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, alisema vijana wengi wanazurura tu, Serikali iweke mkakati wa kuweza kuwasaidia vijana. Nadhani hilo nimelisema. Ajira mbaya ya watoto, hilo tumelizungumza.

Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, alisema kuhusu sheria ya nguvukazi. Ni kweli sheria hii imefutwa lakini ikawekwa sheria nyingine ambayo inaitwa *National Employment Promotion Services Act No.9 of 1999.* Sheria hii imeweka taratibu nzuri zaidi ambazo zinahusisha Serikali za Mitaa katika kukuza ajira kwa kushirikiana na Halmashauri. Kwa sababu unajua hii sheria ya nguvukazi ilikuwa inaonekana kama vile tunawalazimisha watu kufanya kazi *(forced labour).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli katika mazingira tuliyonayo ukiwaruhusu watu kuwa wanazagaa tu, tutakuwa tunapiga kelele njaa, njaa. Ardhi tunayo, watu wapo hawafanyi kazi, kwa hiyo, ni *balance* ambayo ilibidi tu-*strike* kati ya mahitaji ya *ILO* na mahitaji ya nchi yetu, ndiyo maana tukaibuni sheria hii. Ukiisoma sheria hii vizuri, inatatua tatizo hilo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Stephen Kahumbi, alizungumzia kuhusu mtumishi wa *TRA.* Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kulifanyia kazi hilo tatizo la

huyo mfanyakazi, kwa sababu mimi naamini Serikali ni moja na Waziri wa Kazi anapoamua, anaamua kwa niaba ya Serikali ile ile. Kwa hiyo, nadhani Mawaziri wengine nao vile vile wanajua kwamba lazima tuheshimiane kwa sababu Serikali ni moja. Tutakachofanya sisi, tutaiangalia hiyo karatasi ambayo mmetupa hivi sasa, tuangalie namna ambavyo tunaweza tukakazia hukumu ili huyo mfanyakazi apate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, yapo mengi ambayo amechangia, hasa la kilimo. Nataka nimhakikishie kwamba sisi kama Serikali tunatambua kilimo ni kazi, lakini vile vile hata katika Vyuo vyetu vya *VETA* vimeshaanza kushughulikia namna ya kufundisha kilimo bora. Kwa hiyo, sio tu kilimo cha kizamani, tunataka watu walime kilimo cha kisasa. Sasa mtazamo wa vijana wetu ndio bado tatizo. Tusaidiane na Waheshimiwa Wabunge kubadilisha mtazamo wa vijana wetu ili nao wajue kwamba kilimo ni kazi. Pamoja na majibu haya, lakini nataka nimhakikishie kwamba ombi lake la kutaka kuonana na mimi niko tayari, tutaonana ili tuendelee kushirikiana zaidi.

Mheshimiwa Venance Mwamoto, alisema *NSSF* ijenge Ofisi za *BMT.* Hizi Ofisi za *BMT* zimezingatiwa katika ujenzi wa uwanja mpya unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ishirikiane na *NSSF* kubuni miradi ya maendeleo na miradi mingine kama vile ujenzi wa Bunge. Shirika la *NSSF* kwa kushirikiana na Mashirika mengine ya Hifadhi ya Jamii kama *PPF, LAPF* na *PSDF* wanaendelea na mazungumzo na Serikali na hivi karibuni pengine ujenzi utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba kama sikuyagusia mengine naomba niwahakikishie tena kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi na tutatoa majibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda tuliopewa, naomba niishie hapo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 60 - Mahakama ya Kazi**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... 428,522,100/=
Kifungu 1002 - *Arusha Zone* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 37,853,200/=
Kifungu 2002 - *Dar es Salaam Zone* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 47,115,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 751,676,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa JAcob Shibiliti na Mheshimiwa Omar Chubi. Tunaanza na Mheshimiwa Margareth Mkanga. Leo nitakuwa pande zote, huku na huku maana jana yalitokea mambo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na kwamba muda ulikuwa mdogo, lakini naomba nifafanuliwe, sina haja ya kutoa mshahara wala nini, naomba ufafanuzi.

Kwanza nipongeze Wizara kwa kukamilisha suala la sera ya maendeleo na huduma za watu wenye ulemavu, lakini sasa ninaloomba ni ufafanuzi, lini basi ukamilishaji wa sera hii kabisa utakuwa ili tugawiwe humu Bungeni kama tulivyogawiwa sera ya Wazee leo?

Pili, kwa masikitiko makubwa, hotuba nzima hii sikuona chochote kilichogusiwa kuhusu Azimio la Muongo la Watu Wenye Ulemavu Barani Afrika, ni miaka mitano sasa imepita na Serikali iliridhia mambo haya, kuna mikakati gani ya utekelezaji ya yale yaliyomo ndani ya Azimio hilo? Hayo mawili naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la sera ya watu wenye ulemavu kuletwa Bungeni kama tulivyogawa hii Sera ya Wazee, hilo litafanyika. Lakini kama tunavyofahamu kwamba sera ikishapitishwa na Serikali ambayo hiyo ya walemavu tayari imeshapitishwa, lazima sasa irudi tena kwa wadau wale wale kwa ajili ya kuchangia namna bora ya kuipangia mikakati, yaani utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba fedha ya wazee ilipigiwa kelele sana hapa na akina Mheshimiwa Peter Kabisa, kwa muda mrefu, lakini tatizo lilikuwa ni la kuwafikia watu katika maeneo mbalimbali. Lazima tukubaliane kwamba watu wenye ulemavu hawapo tu Dar es Salaam, wako maeneo mbalimbali na kila Mbunge anayesimama hapa hutaja habari ya watu wenye ulemavu katika eneo lake.

Kwa hiyo, ningeiomba Mheshimiwa Margareth Mkanga, atustahimilie, maadam Baraza la Mawaziri limeshapitisha, nina uhakika hatua sasa ya kukutana na wadau ni ndogo kuliko pale tulipovuka.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muongo wa Watu Wenye Ulemavu ni kweli mwaka wa tano na kama ukichukua kile kitabu chetu katika ile *section* ya Ustawi wa Jamii, tumeligusia hilo. Hivi sasa tumefikia nusu ya kipindi. Kwa hiyo, moja ya mkakati ni kujaribu kutathmini kitu gani ambacho tumeshafanya ili kiweze kutupa dira namna ya kuendelea katika miaka mitano iliyobaki.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba msaada wa ufafanuzi kwamba ni mangapi haya ambayo yamekwishafanywa kwa miaka mitatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo ya ziada.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kamili hapa siwezi kuwa nayo. Lakini ninachosema ni kwamba sisi wenyewe tunatambua kwamba tumeshafika nusu ya muda unaohitajika na kwa hiyo tunafanya tathmini ya yale ambayo kwa mfano kila mwaka huwa tunafanya sherehe za kuheshimu Muongo huo. Kwa taarifa ninazotoa sasa ni kwamba tumeshaunda Kamati Maalum ya Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa mwongo huo. Sasa kwa hapa kwenda ku-*produce list* kamili sitakuwa na uwezo huo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kwamba kuna hatua ya Kamati kuundwa itakayoanza. Kwa kweli tuseme ndiyo itakayoanza. Lakini kusema kwamba kuna kilichoanza mimi nasikitika kwamba hicho basi hata hatujawahi kuhusika nacho. Kwa hiyo, nashukuru tu kwa hiyo, hatua aliyofikia.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10, *Sub-Vote 1001* Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Mimi tangu mwaka 2001 namwomba huyu bwana aje kule kwangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hakuna Bwana, Mheshimiwa Waziri siyo, kwani unamzungumzia Waziri au bwana nani? *(Kicheko)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, katika kifungu hiki si ndiyo kuna mshahara wa bwana mkubwa? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tumekubaliana kwamba kwa mujibu wa kifungu 49 Kifungu kidogo cha 8 Waziri ataitwa kwa Cheo chake, ndiyo Kanuni inavyotudai.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukazia hapa yaani hoja mimi sina ubaya na hili suala lakini nasema, kwa sababu hapa ndiyo tunapitisha mambo yake, Mheshimiwa Waziri mimi nilimwomba tangu mwaka 2001 kwamba kule kulikuwa na kiwanda cha Wamisionari ambacho vijana ambao hawakupata elimu sawasawa walikuwa wanajiendeleza. Tangu wale Wamisionari wameondoka kile kiwanda kimekufa na mahala ambapo tunaweza kupata vifaa ni kwenye Ofisi yake. Sasa hapa ndiyo niliyoona labda nimwambie, je, lini utatembelea kwa sababu bado miezi 12 tu hizi shughuli zitakwisha. Naomba anihakikishie. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, ni

jirani yangu kwa maana ya majimbo na miezi mitatu tu iliyopita nilikuwa jimboni kwake, kumbe kwa bahati mbaya yeye alitaka hili afike mwenyewe Mheshimiwa Waziri tu, maana tumetembea kweli kweli mpaka usiku. Lakini nataka nimthibitishie kwamba ili chuo kiweze kupata msaada wa *VETA* ni lazima chuo hicho kiwe kimesajiliwa.

Sasa kama kile ni kiwanda *VETA* haiwezi ikaingia kusaidia. Lakini kama ni Chuo, basi *VETA* inaweza kusaidia. Lakini lazima kiwe kimesajiliwa. Sasa ili afahamu taratibu zinazotakiwa mimi ningemwomba Mheshimiwa Omar Chubi baada ya Bunge tukirudi Dar es Salaam Ofisini tuelekezane msaada huu haswa anautaka kupitia Idara ya vijana au *VETA*. Lakini vyote vinahusiana na vijana. Kwa sasa hivi tunaomba utupe hizi pesa basi tuendelee tupate nauli ya kuja huko. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nimeridhika.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Mimi fungu hilo hilo 1001 Mshahara wa Waziri, nilikuwa nataka kuzungumzia kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la *VETA* kujenga katika kila Mkoa katika nchi yetu. Nataka atutamkie hapa Bungeni kwamba katika Mkoa wa Pwani kwa sababu Mkoa wa Pwani mara nyingi miradi inayokuja huwa Mafia tunaisikia tu kwenye redio, kwenye magazeti. Sasa basi kwa upande huu wa *VETA* atamke kwamba wakati ukifika *VETA* kujenga Mkoa wa Pwani basi ije kujengwa Mafia, viwanja vipo, wananchi wapo na wanaotoka Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe, Rufiji na Mkuranga, na sehemu zingine katika nchi hii wataweza kuja kukaa na kupata mafunzo yao kule Mafia. Nataka maelezo hayo.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Tunapoanza kufikiria kujenga *VETA* katika mkoa fulani, kwa kawaida huwa tunawaandikia uongozi wa Mkoa, uongozi wa mkoa ndiyo unatushauri twende wapi. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Abdulkarim Shah, akakae na uongozi wa Mkoa wa Pwani, wajadiliane waamue watakapotupa maelekezo sisi ya kwenda Mafia hatuna tatizo, tutakwenda Mafya.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na taratibu alizotoa Mheshimiwa Waziri, lakini mara nyingi sisi ndiyo wakazi wa pale na sisi ndiyo viongozi wa Mkoa ule, tunaona miradi mingi tunasema inakuja, kwa nini basi kwa mradi huu mmoja yeye kama Waziri unaona, siyo alazimishe. Lakini aseme kwamba basi jamani sisi tunapendekeza kwamba Kitengo hiki cha *VETA,* Idara hii mafunzo haya tunataka yaende pale kwa sababu jamani tuoneeni huruma Mafia, kila kitu tuwe tunakisikia tu tena inaweza hata ikatuletea kule kuna uvuvi, bahari, wanaweza wakaleta hata ile Idara ndogo ya uvuvi ikaletwa pale Mafia na sisi tukapata kufaidika na hii miradi ya kitaifa. Mradi tulioupata sisi ni wa mabusha tu matende pale. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba jitihada kubwa za Serikali katika awamu hii ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Ndiyo maana Serikali Kuu kila inapotaka kufanya jambo lolote inabidi lazima tupate maelekezo kutoka Mkoani.

Naomba kurudia maneno ya Mheshimiwa Waziri, kwamba shilingi bilioni 21 ambazo tumeziomba Korea kwa ajili ya kujenga Vyuo Manyara, Pwani na Lindi maamuzi ya wapi kijengwe kwa kweli yatakuwa ni maamuzi ya Mkoa. Najua uchungu wake, kama mimi kile Chuo cha Lindi ningependa kijengwe Mchinga. Lakini kimejengwa Mitwero kwa Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, kwa sababu ndiyo makao makuu ya Mkoa na ndiyo Mkoa walivyoamua wenyewe, nasema Mheshimiwa Mbunge pamoja na uchungu wote na miradi ya ajabu ajabu uliyoletewa lakini bado turudi katika Mkoa wetu, ninaamini kwamba atakuunga mkono maadam ni swahiba wako na Mheshimiwa Athumani Janguo. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 65, Sub-Vote 1001.* Namshukuru Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kujibu yale niliyoyapeleka kwake lakini kuna jambo dogo ambalo nilikuwa naomba ufafanuzi, ni kuhusu jambo hili la *OSHA.* Hiki Kitengo sasa ni *Executive Agency* lakini Serikali haikipi kitengo hiki fedha ili kiweze kuanza kwa nguvu zote. Mwaka 2003 tumepitisha sheria ya *Occupational Health* ambayo inahitaji fedha za kutosha ili waweze kutekeleza Sheria ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha wanazokusanya kwa ajili ya ku-*charge* huduma wanazotoa kwa kweli fedha hazitoshi, lakini umuhimu wa kazi wanayoifanya ni ya msingi sana. Afya za wafanyakazi viwandani ni jambo la msingi sana na tusilipuuzie. Kuna ajali nyingi zinatokea viwandani, Serikali imeingia hasara kubwa kuanza kulipa fidia na mambo mengine. Lakini Kitengo hiki hakijapewa zana za kutosha, wanasema watumie fedha wanazo-*charge,* kwa kweli fedha wanazo-*charge* ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimetoa *suggestion* kwamba kama *VETA* walivyoingiza, walivyoleta Muswada wa Sheria tukapitisha kwamba hawa watu au *VETA* wachangiwe na waajiri ili kuweza kuimarisha fedha kwa ajili ya *VETA*. *VETA* kwa kweli hawana matatizo ya kifedha. Hii *agency* inahitaji fedha za kutosha, je, si vizuri Mheshimiwa Waziri akaona umuhimu wa kuleta hapa Bungeni Muswada ili waajiri waweze kuchangia fedha za kutosha kwa ajili ya *Occupational Health* ili wafanyakazi wote waweze kufikiwa na Kitengo hiki, ajira itakuwa ya kutosha, wafanyakazi wengi watapatikana, Madaktari watapatikana na *Engineers* watapatikana. Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu suala hili?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza wakati nikihitimisha nilisema yapo mengine ambayo hatukupata muda wa kuyajibu mojawapo lilikuwa ni hilo na jibu ninalo. Tulisema kuhusu kuleta Muswada hapa Bunge ili mwajiri achangie asilimia mbili ya Bajeti ya mishahara ili ziwekezwe kwenye huduma ya afya na usalama wa wafanyakazi

Wizara tayari imeshaliona hilo na kwa sasa inaandaa Sera ya Taifa ya Afya na Usalama wa mahala pa kazi *National Policy and Occupational Health and Safety* ndani ya Sera hii imepangwa kuchangia suala hili la afya na usalama mahala pa kazi litawasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo ndipo Muswada au pendekezo hilo litaletwa hapa Bungeni, kwa sababu lazima kwanza mambo haya yatamkwe katika Sera, halafu Sera ndiyo inazaa Sheria.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda nianze kwa kusema kwamba kifungu 1001 Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Wakati wa majumuisho ya Mawaziri wote wawili wamegusia zaidi michezo, *VETA* na masuala ya wafanyakazi. Suala la makambi ya wazee halikugusiwa. Labda hawa wazee walikosewa kuwekwa katika Wizara hii kwa nini wasirudishwe Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Maana yake naona wamesahaulika hawa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza mambo mengi kuhusu kambi ya wazee Bukumbi ni kambi iliyo na watu wengi zaidi kuliko kambi zote, ina watu 515. Vurugu zote za pale kwenye Jiji la Mwanza kusafisha na kutoa wazee wote waliletwa kwenye kambi hiyo. Hawana mahala pa kulala, wanalala chini. Watoto wanasoma kwa shida. Sikupata jibu. Matibabu ni ya shida. Tumeelezwa kwamba basi Halmashauri itasaidia, tunajua matatizo ya Halmashauri. Napenda nielezwe kwamba wametenga shilingi ngapi, wanasemaje kuhusu maradhi ya wazee hao na watoto wao? Mshahara bado ninao. Naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lakini nadhani hukutoa shilingi, Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mbunge alikuwepo wakati mimi natoa ufafanuzi niliwataja na majina pamoja na la kwake kwamba majibu yao kwa sababu ya muda tutayapeleka kwa maandishi. Lakini tulifanya hivyo kwa sababu ya kukosekana kwa muda na siyo kudharau wazee kiasi cha kutafutiwa Wizara nyingine.

Mheshimiwa Jacob Shibiliti na mimi tumeingia Bungeni kupitia kwenye Chama ambacho moja ya Ilani yake ni kuhudumia wazee. Kwa hiyo, Serikali hii hata kwa bahati mbaya haiwezi ikafikiria kudharau wazee kwa sababu itakuwa ni kudharau Ilani yake yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa fedha za matunzo kwa wazee na watu wasiojiweza kulingana na fungu la bajeti tunalopangiwa humu ndani. Tunafanya ukarabati wa majengo ya makazi hayo vile vile kutegemea na fungu tulilonalo hapa.

Mheshimiwa Jacob Shibiliti, nilizungumza naye juu ya tatizo ya kambi yake na kama mwaka jana nilizungumza naye hivyo hivyo, tukatekeleza aliyoyaomba hata kama hayakuwa yote. Niliamini kwamba kauli yangu niliyompa mwaka huu vile vile ameiamini. Nataka niendelee kumsisitizia kwamba Sera ya Taifa ya wazee inajielekeza

zaidi katika familia na jamii kuthamini wazee wetu. Hili la kukimbilia kwenye makambi liwe ndiyo kimbilio la mwisho. Lakini kwa utamaduni wetu tujenge utamaduni Watanzania wa kuthamini wazee wetu kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Venance Mwamoto na sisi ni wazee watarajiwa.

Kwa hiyo, hili suala la kambi yake Mheshimiwa Mbunge kama alivyoahidi hapa Mheshimiwa Waziri atatembelea Kambi ya Magugu kule kwa Mheshimiwa Omar Kwaangw', atatembelea na hata kambi ya Mheshimiwa Jacob Shibiliti, ili kujionea matatizo kwa sababu matatizo yanapishana kati ya kambi na kambi na ni vigumu kutenga kwa nini *center* itapata kiasi hiki kambi fulani kiasi hiki kwa sababu mlipuko wa watu kuletwa kwenye kambi unategemea na hali halisi. Kwa hiyo, tunaangalia wapi wakati huo wamejaa, tunapeleka kutokana na idadi ya watu. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli alijaribu kutekeleza kiasi mwaka 2003. Lakini baada ya kipindi cha asubuhi kwa leo Mheshimiwa Waziri tulikutana naye akasema wakati wa majumuisho nitakupa jibu la hali halisi ya kwamba nimetenga shilingi ngapi. Si kwamba Naibu Waziri simwamini, kwa vile Waziri yupo labda analo jibu kwa sababu ndiyo Serikali yenyewe. Naomba niishie hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una jibu la ziada?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati wa michango ya Wabunge walitaja kabisa fedha ambayo tumepata kwa ajili ya makambi ya wazee ni shilingi milioni 208 na wakasema kwa kila mzee kwa sshilingi 126/= kwa siku hazitoshi kwamba ni kidogo sana na sisi tunaamini kwamba kwa kweli fedha ni kidogo lakini kwa sababu ndiyo uwezo wa Serikali.

Kwa hiyo, jinsi Serikali inavyozidi kuimarika kiuchumi fedha itaongezeka. Hamna mwenye roho mbaya ndani ya Serikali hapana ndiyo uwezo wenyewe tulio nao. Lakini fedha zilitamka kabisa shilingi milioni 208 ndiyo bajeti ya mwaka huu kwa kuhudumia makambi ya wazee. *(Makofi)*

Sasa ni kiasi gani kwa kambi ya kwake *specifically* hiyo ndiyo siwezi kutaja hapa. Kwa sababu mpaka turudi maofisini labda kama kesho hivi nikipiga *fax* Dar es Salaam nitampa. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona acha achukue mshahara wake nimekubaliana naye, yameisha. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...168,083,200/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 340,106,400/=
Kifungu 2001 - *Labour* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 896,047,100/=

Kifungu 2002 - *Employment* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 527,408,900/=
Kifungu 4001 - *Social Welfare* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...1,937,144,800/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Youth Development* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 709,807,600/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sishiki mshahara wa Mheshimiwa Waziri, wala sishiki mshahara wa wafanyakazi hapa. Mimi ninachoomba baada ya mimi mwenyewe kufanya utafiti, nimezaliwa Dar es Salaam. Naijua Dar es Salaam nimezunguka Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na hapa Dodoma, nimeweza kufika Tanga, Kilimanjaro na Iringa. Hiyo nidyo mikoa niliyofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanaopiga debe, ni *drug addicts.* Vijana hawa ni *drug addicts,* hawa ni wagonjwa. Tukiwaachia wazazi wao hawana utaalam wa kuwaondoa ugonjwa huu. Tukiwaachia Wabunge hawana utaalam wa kuondoa ugonjwa huu ni *drug addicts.* Mheshimiwa Waziri utakubaliana nami au utatoa ushauri gani? Ushauri wangu ni kwamba, je, mnaonaje? Hakuna haja sasa hivi Wizara yako ikawasiliana na *Circuitry Departments* za hospitali mbalimbali na hasa Muhimbili chini ya Profesa Kilonzo na wenzie tuwasaidie hawa vijana na vijana hawa tukiwasaidia wako tayari hata kusema wanauziwa na akina nani dawa hizi. Nilishawahi hata kuzungumza na Profesa Kilonzo lakini kwa sababu ya *funds* hakuna kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kama Waziri unakubali tusaidiane, tuwasaidie hawa vijana ambao tayari ni wagonjwa na watu ambao ni wa kawaida itakuwa ni vigumu.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mchango wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, katika mikoa aliyotaja kwamba amewahi kufika, nilitegemea atataja na Tabora ambako alipata na mume lakini hakutaja. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba nikubaliane naye kwamba tutaendelea kushirikiana na Kitengo cha *Circuitry* chini ya Profesa Kilonzo. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba tunayo *rehabilitation programme* ya Kitaifa ambayo iko chini ya Tume ya Kuzuia Dawa za Kulevya na moja ya kitengo muhimu anachokitumia ni hospitali ya hapa Dodoma ambayo ipo pembezoni mwa Gereza pale. Kwa hiyo, programu imeshaanza. Lakini kuongeza utaalam si vibaya. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali programu imeanza chini ya Kitengo cha Dawa za Kulevya, lakini wanaohusika na wanaoumia sana na wanaoandaa mikakati ni Wizara yako. Ndiyo maana mimi nimesema kwa makusudi ushirikiane nao.

Samahani kwa kutamka hilo, hawako *serious* kwa sababu hawa vijana wanaharibiwa kaka yangu. Nakuomba ushirikiane nao na Kitengo hiki hata ikiwezekana mimi na Profesa Kilonzo tutakusaidia kutoa ushauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri amekubali ushauri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6004 - *Sports Development*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 464,901,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 60 - MAHAKAMA YA KAZI TANZANIA**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... ... 251,815,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 65 - WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... ... 100,620,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...5,236,811,000/=
Kifungu 2001 - *Labour* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 40,675,000/=
Kifungu 2002 - *Employment Division*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 34,870,000/=
Kifungu 4001 - *Social Welfare*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 58,250,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Youth Development*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 50,640,000/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo zaidi kuhusu mambo ya Ukimwi unaowamaliza vijana wetu hasa kwenye kifungu hiki cha 5001 na hasa kwenye barabara kuu ambayo sasa inaanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza katika vituo na vijiji kando kando ya barabara hii ukimwi umeendelea kuzidi na wananchi wana matatizo. Kwa hiyo, naomba nini ambacho Mheshimiwa Waziri ana mipango gani ya kuhakikisha kuwa vituo vya elimu na kutoa tiba kwa wananchi ambao wako kwenye barabara kuu hii inaimarishwa na katika bajeti hii ni kiasi gani kimetengwa katika kuimarisha vituo vya elimu kwa ukimwi katika barabara kuu?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna *specific programme* kwa ajili ya vituo vya barabarani. Lakini kama Wizara tunao mpango wa kudumu au mipango ya kudumu kwanza. Moja ya sababu kubwa ya kutaka kuendeleza mbio za mwenge. Ujumbe wa kudumu katika mbio za mwenge ni jinsi ya kuhamasisha jamii kupambana na ukimwi na wanaohusika walio wengi katika mbio hizi za Mwenge na wanaohudhuria mbio hizi za mwenge huwa ni vijana na tunatumia aina mbalimbali za kufikisha ujumbe pamoja na video pamoja na senema ili kuwatahadhirisha vijana na moja ya sababu ambazo tunazitaja kama vyanzo vya kueneza ukimwi ni vituo vya barabarani hasa madereva wanapolaza magari yao makubwa.

Lakini la pili vile vile tunayo wiki ya vijana ambayo inafanyika wiki moja kabla ya kufikia kilele cha mbio za mwenge. Moja ya maeneo ambayo yanafanyiwa kazi sana wakati wa wiki ile ni elimu juu ya kupambana na ukimwi na vinakuwepo vikundi mbalimbali kutoka nchi nzima ambavyo vinakuja kuzungumza na vijana kwa njia ya redio, kwa njia ya ana kwa ana, jinsi ambavyo wanavyowasaidia vijana kupambana na ukimwi. Kwa hiyo, hatuna kipengele kidogo cha kusema sasa barabara basi. Ni moja katika vitu ambavyo tunavishughulikia katika programu za kudumu.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake. Kwa kuwa sasa mwamko wa mwenge ni mdogo sana, Wizara yake ina mpango gani kwa kuhamasisha mwenge kusudi watu wengi washiriki na wapate kufaidika na elimu ya ukimwi ambayo inaenezwa na mwenge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, si kama umebadilisha hoja tena? Umeshabadilisha hoja. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6004 - *Sports Development* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 49,816,945,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## TAARIFA

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo basi naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.30 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 30 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*